

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Thelathini Na Sita – Tarehe 23 Julai, 2009

(Kikao Kilianza Saa Tatatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, na Kitabu Cha Takwimu Muhimu za Elimu, “*Basic Education Statistics (BEST)*,” kwa Mwaka 2009/2010.

MHE. OMAR S. KWAANGW’ - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii, Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

MHE. NURU AWADH BAFADHIL (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Randama za Makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

NAIBU SPIKA: Leo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hayupo, kwa hiyo tunaenda kwa Mheshimiwa Luhaga Mpina. Swali la kwanza litaulizwa kwa Waziri Mkuu.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa kuwa, watu wote ni sawa mbele ya sheria, na kwa kuwa wanayo haki sawa bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki mbele ya sheria kama inavyoainishwa katika Ibara ya 13 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Sheria namba 15 ya mwaka 1984, Ibara ya 6. Je, Serikali hufanya jitihada gani...

NAIBU SPIKA: Hiyo *Microphone* yako kidogo inaleta matatizo, hatukusikii vizuri. Unaweza kuhama?

WAH. WABUNGE: Hapo hapo!

NAIBU SPIKA: *Commander* ni mmoja, wote mnafanya kazi gani ya kusema? Haya... (*Kicheko*).

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nirudie swali langu. Kwamba, kwa kuwa, watu wote wana haki sawa mbele ya sheria, na kwa kuwa wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.

Kama inavyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 13 (1) na Sheria Namba 15 ya mwaka 1984, Ibara ya 6.

Je, Serikali hufanya jitihada gani za kuhakikisha kwamba Sheria tunazozitunga hapa Bungeni, zinafahamika kwa wananchi ili kuepusha wananchi wasiozijua, kuvunja sheria na kwamba wasionewe kwa kutokujua haki zao? (*Makofi*).

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Ndugu yangu Mpina, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kutoa elimu kwa ajili ya sheria zote zinazotungwa hapa Bungeni, kwa upande mmoja ni jukumu la Serikali yenye na hasa Wizara ambayo inakuwa imeongoza mjadala wa upitishaji wa hiyo sheria. Lakini Vyombo vya Habari navyo vinasaidia sana katika kutoa hiyo elimu. Lakini vilevile Wabunge na ninyi huwa mna fursa kubwa tu ya kusaidia kutoa hiyo elimu. Kwa hiyo, ninachowea kusema tu ni kwamba, ni jukumu la kila mtu kwa ujumla kutambua tu kwamba sheria zikishatungwa, ni juu yetu sisi sote kusaidiana kutoa elimu kwa wahusika wote kwa kadri itakavyowezekana. (*Makofi*)

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakubaliana na ushauri wangu kuwa, kwa kuwa sheria nyingine zinahusu shughuli za kila siku za wananchi. Kwa mfano zile sheria zinazohusu wanyamapori kwa wananchi wanaoishi kandokando. Serikali itachukua jukumu la kutoa semina na kuzitafsiri sheria hizo kwa lugha nyepesi na kuzisambaza kwa wananchi ili wazielewe na wasiendelee kuonewa na wakati mwingine wasivunje sheria bila kujua?

NAIBU SPIKA: Lugha nyepesi, hapo una maana Kiswahili? Au?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wake tunauchukua. Tutaomba Wizara inayohusika ifanye hiyo kazi. (*Makofî*).

MHE. ARCH. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jiji letu la Dar-es-Salaam, ndio kioo cha nchi yetu, ni kitovu cha mapato kwa maana ya kuwa na viwanda vingi na wafanyakazi wengi. Na ili tuweze kuendelea ni lazima tuthamini sana muda na kuutumia vizuri. Kwa kuwa, katika Jiji la Dar-es-Salaam, kuna msongamano mkubwa sana wa magari hasa kwenye makutano ya barabara, *junctions*, ambao unasababisha upotevu wa muda mwingi sana kwenda au kurudi majumbani.

Je, Serikali itakubaliana na mimi sasa, umefika wakati muafaka kabisa wa kujenga barabara za kupishana za juu kwa maana ya *fly-overs*, katika makutano yote makubwa katika jiji la Dar-es-Salaam?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Kimbita, kwamba tunalo tatizo la msongamano wa magari hasa kwenye barabara zetu za Dar-es-Salaam, si katika maeneo ya makutano ya barabara tu. Lakini kwa ujumla wake na sababu zake ni nyingi. Lakini niseme kwamba rai yake Serikali imeshaanza kuifanyia kazi, tuliwaomba wenzetu wa Serikali ya Japan, waweze kutusaidia katika zoezi hili kufanya uchunguzi na kujaribu kutoa mapendekezo Serikalini. Kwa hiyo, hilo ni jambo mojawapo kati ya mambo mengi ambayo yanatazamwa na Serikali katika kujaribu kupunguza msongamano kwenye miji yetu mikubwa. (*Makofî*).

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kufahamu kwamba ule umeme ambaو unatoka Songsongo kwenda Dar-es-Salaam, ambaو uliahidiwa kwamba utapita umeme katika vijiji vya Somanga, Njenga, Njia Nne, Tungi, Nangurukuru, Rufiji na Kilwa Mjini, mpaka sasa haujagawiwa bado; tatizo liko wapi? (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Sijui, lakini lilikuwa swali la kisekta, lakini labda Waziri Mkuu, unaweza kujibu hilo.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema. Kusema kweli ni swali la kisekta zaidi, lakini ninachowenza kumuahidi tu Mama Mikidadi ni kwamba, jambo hili tumekuwa tukilihangaikia kwa muda mrefu kidogo, hatujafikia mwisho kwa maana ya kujaribu kufanya juhudu zile za kutoa umeme kwa maeneo yale ambako *line*

zile zitakuwa zinapita. Lakini ili uweze kupata pengine maelezo ya kina zaidi, ni vizuri basi nikamwomba Waziri wa Nishati na Madini, akakutana na wewe akakupa maelezo kwa kirefu kujua ni hatua zipi mpaka sasa zimefikiwa. (*Makofi*)

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 4 (3) kwene Nyongeza ya kwanza, mambo ya Muungano, jambo la pili ni Mambo ya Nchi za Nje. Lakini katika Katiba hiyo, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, ambayo kinyume na nyongeza ya kwanza. Kwanza hapo anakubaliana na mimi kwamba Ushirikiano wa Kimataifa haumo kwene Katiba? Na kama ni hivyo, haoni kwamba ni uvunjaji wa Katiba ya Nchi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika hasa Ndugu yangu Yahya, anataka kupata nini kwa swali lake hili. Lakini Wizara yetu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kama jina linavyosema, ndio Wizara inayoiwakilisha nchi hii katika masuala yote yanayohusiana na Taifa letu. Sasa kama ndani ya Katiba pengine unaona halimo, na kwa maana hiyo sina hakika ultaka kusema nini. Lakini bado mimi ninasema Wizara hii ndio itaendelea kusimamia mambo yote yanayohusiana na nchi yetu tunapokuwa tunashughulika na mataifa mengine.

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sisi tunafuata Katiba na Katiba ni maandishi, sio maneno. Huoni kwamba hilo ni kosa kwamba, kuweza kuingiza kitu na ndani ya Katiba hamna. Na kama hamna, huoni kwamba Zanzibar inakosa kuingia katika Mashirikiano ya Kimataifa ambayo inakosa haki zake wakati ndani ya Katiba hamna? (*Makofi*).

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Yahya, kama ni hivyo, basi si mjaribu kuingia huko mnakotaka kwenda? Maana kama ni rahisi hivyo, jaribu tu halafu baadaye ndio tutaona kama mko sahihi au hapana. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: *Actually*, jina hilo linajaribu kueleza kazi za Wizara ya Mambo ya Nje, sio kwamba ni jina linalojitegemea. Tunaendelea na Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa.

MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais, alisema mafisadi wafichuliwe. Wafanyakazi wa Maji Mbeya, wamefichua mafisadi, wakamwandikia Mheshimiwa Rais, pamoja na wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa nakala. Je, ni kwa nini mpaka sasa hivi hatua hazijachukuliwa?

NAIBU SPIKA: Enhee! Na wewe walikupa nakala eeh? Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Kicheko*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mnyaa, ungekuwa na nia njema ungekuwa umenipa hiyo nakala na mimi nikaipitia. Mimi sijaiona hiyo barua unayoisema na sina hakika wameituma lini na sijui wamefichua ujisadi gani. Kwa hiyo,

kwa kweli kazi unayonipa sasa ni kukuomba, kama una nakala hiyo, nipe. Ili niweze kufuatilia na kuona ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Nguvu za giza. Mheshimiwa Mnyaa, swali la nyongeza. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. MOHAMMED HABIB MNYAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nitampa hiyo nakala Mheshimiwa Waziri Mkuu.

NAIBU SPIKA: Sasa kama mwenyewe hajapata, tena wewe vipi! Haya, tunaendelea, tunategemea, hii ni ahadi ya ndani ya Bunge. Kwa hiyo, tutapenda kujua hiyo nakala. Mheshimiwa Ali Jacob Shibili, swali linalofuata.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaitwa Jacob Shibili, sio Ali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, lipo tatizo la Madaktari Bingwa, kukimbilia nje kwa sababu ya maslahi, lakini wapo Madaktari Bingwa wengine wanabaki hapa nchini na kutumia uzalendo wao kuwashudumia Watanzania. Wewe Mheshimiwa Waziri Mkuu, tarehe 27/05/2008 uliwatembelea pale Muhimbili – *MOI*, na ulijiona kazi iliyokuwa inafanywa na Madaktari Bingwa kuhusu upasuaji wa moyo, chini ya Daktari Mahalu. Na sasa hivi zaidi ya watu 100, wamehudumiwa hapa Tanzania na hawa wazalendo.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inasemaje kwa uzalendo wa Madaktari hao Bingwa, ambao wameokoa mamilioni ya pesa, badala ya kupeleka watu nje ya nchi, kuwapa motisha? (*Kicheko*).

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Shibili, kwa kuleta swali hili zuri na niharakishe kusema kwamba, mimi ninaomba kwa niaba ya Serikali, kwanza niwapongeze sana Wataalamu wetu wanaotoa tiba katika Taasisi ya Mifupa pale Dar-es-Salam. Wanafanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Shibili, kwamba kwa muda mrefu tumekuwa tunapeleka wagonjwa nje. Hasa tunapozungumza wagonjwa wanaokwenda nje kwa sehemu kubwa ni wale ambao wanahitaji rufaa ya ngazi ya juu zaidi kuliko uwezo tulionao katika hospitali zetu. Na magonjwa makubwa yanayowapeleka nje kundi hili, zaidi ni magonjwa ya moyo na kabla hatujaanzisha Taasisi ya Mifupa, ilikuwa ni pamoja na matatizo ya mifupa. (*Makofi*)

Lakini kwa juhudi za Serikali, kuititia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, suala la matatizo ya mifupa kwa sehemu kubwa sasa yanahudumiwa hapa nchini. Kwa kweli mimi ninawapongeza sana, na nimepata nafasi ya kwenda pale, nimeona kazi ni nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa tumechukua ile hatua ya kwanza, tumekwenda kwenye hatua ya pili ambayo tumeianza mwaka 2006, baada ya kuunda

Kamati Maalum ya Wataalam, Madaktari. Kazi iliyofanyika kwanza ilikuwa ni kujifunza kuona ni namna gani tunaweza tukaanzisha upasuaji mkubwa wa moyo. Tulikuwa tunafanya upasuaji mdogo, lakini mkubwa ilikuwa si rahisi kwa sababu inataka kidogo muwe na Madaktari waliobobea sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ile imefanyika vizuri sana na kuanzia mwaka jana mwezi Mei, tukaanza kutoa kwa mara ya kwanza, upasuaji mkubwa wa moyo. Kwa hiyo, ni kweli kabisa anachokisema Mheshimiwa Shibili, na mpaka mwaka huu ninavyozungumza hapa tayari wameshafanya upasuaji wa wagonjwa 105. Kwa hiyo ni jitihada kubwa na nzuri sana, ingawa kati ya hao 105, 15 walipoteza maisha, jambo ambalo katika mazingira ya fani kubwa kama hizi ni la kawaida.

Kwa hiyo, ninataka nikubaliane naye na nilipofanya ziara nilisema haya, kwamba Serikali itajitahidi kuona ni namna gani tunaweza tukaweka mfumo wa motisha utakaoweza kuwafanya wapende kufanya kazi hii kwa sababu ni kazi ngumu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Shibili, nataka nikuhakikishie kwamba kazi hii tutaifanya. Tumeanza mwezi Mei upasuaji, kwa hiyo sasa ni kama mwaka mmoja na zaidi kidogo na juhud hizi za kujaribu kuona tufanye nini zimeshaanza. (*Makofi*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi imani yangu ni kwamba Serikali imesikia na kwa sababu ilishaanza kulifanyia kazi, tutafika mahali pazuri na tutawaweka watu hawa katika hali ambayo ni ya kuwatia moyo zaidi. Lakini narudia kwa kweli, ninawapongeza sana. Na mimi ninataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, mkipata muda mwende mkaone kazi nzuri inayoendeshwa pale, katika juhud za kujaribu kujitegemea kama Sekta ya Afya. (*Makofi*)

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Sisi wote tunapoapa huwa tunaapa kuilinda na kuitetea Katiba. Naamini kabisa na wenzetu wa Baraza la Wawakilishi nao huapa na kuitetea Katiba. Hivi karibuni kumekuwa na maneno ya kuchokonoa Muungano ambayo yamekuwa yakisemwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na mara nyingine yakiletwa na viongozi Waandamizi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Lakini sio Rais, sio Makamu wa Rais na hata Waziri Mkuu na Rais wa Zanzibar wote wako kimya. Je, Waziri Mkuu huoni haya maneno ni ya uchochezi ya kuashiria kuvunja Muungano?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nalisubiri swali hili lakini nilidhani lingetoka kwa rafiki zangu akina Mnyaa, lakini safari hii wamenyamaza kimya. Kwa hiyo, inaashiria kama walishabikiashabikia yale yaliyotokea. Lakini namshukuru sana Mheshimiwa Selelili kwa kuleta swali hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme kwamba kama watu mlipata nafasi ya kusikiliza hotuba ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 26 Aprili, 2009. Mambo mengine kama haya anayosema Mheshimiwa Selelili, wala hayana sababu yoyote ya kujitokeza. Msingi wa yote mnayoyasikia ni suala la mafuta na gesi asilia. Suala la mafuta na gesi asilia liliridhiwa na pande zote mbili mwaka 1968 na liko kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania. Siku ile Rais alisema: “*Jamani tusizingumze suala la mafuta kama vile mafuta yamepatikana, mafuta hayajapatikana,*” na akasema: “*inawezekana wala yasipatikane*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama ni hivyo kwa nini tuanze kutupiana maneno makali na mengine pengine, hata kuyasikiliza yanatia uchungu sana. Lakini akaendelea kutuasa Watanzania akasema: “*Hili halina tatizo ni moja kati ya mambo ambayo tulikuwa tumesema yaachwe yazungumzwe chini ya Kamati ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na lilishaanza kuzungumzwa.*” Lakini vile vile akasema: “*jambo hili si kwamba limeachwa tu, iko Kamati iliyoundwa kwa ridhaa ya pande zote mbili, tukamteua Mshauri wa kutushauri juu ya jambo hili na tarehe 23 Juni, 2009 taarifa ile imewasilishwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilidhani busara nzuri ilikuwa ni Serikali mbili kupitia hiyo taarifa, tukaona kilichomo, na kwa kweli kama alivyosema Rais, kama hapana budi jambo hili kulinyofoa kutoka kwenye orodha ya Muungano, lina ugumu gani. Kubwa mnakaa mnafuata utaratibu, mnakubaliana kwa dhati kabisa kama mnataka kulitoa, mnalitoa.

Lakini kama anavyoshangaa Mheshimiwa Selelii, hata mimi nilishangaa, maana tumeambiwa huku Wakoloni, tukaitwa wezi wa mchana. Kwa hiyo, mimi nasema haya ni matamshi mengine ambayo yanatia simanzi kusema kweli, hakuna sababu ya kufikishana hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Selelii anasema mbona hamjasema jambo?

Sasa leo umeniambia na mimi nimesema mawazo yangu, lakini ni Kiongozi ndani ya Serikali. Mimi imani yangu ni kwamba Watanzania tutaendelea kuuenzi Muungano huu. Ni Muungano mzuri kwa maana kwamba umeunganisha pande zetu mbili. Na mimi kila siku najiuliza iko siku tutafarakana tuuvunje, lakini tukiuvunja, muwe na uhakika matokeo yake ni wapi kutaathirika zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama yako matatizo kama alivyosema Mheshimiwa Rais, bora kukaa mkaendelea kuzungumza, mtayamaliza, kubwa tuendeleze huu udugu ambao umejengwa kwa kipindi kirefu sana. Mimi matumaini yangu ni kwamba Rais aliyasikia, Rais Mzee wetu wa Zanzibar naye aliyasikia, naamini litapata ufumbuzi kwa maana labda kwenda kwenye Chama, au viongozi hao wawili watakutana watalizungumza, na mimi nina hakika litakwisha vizuri.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, swalii kwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa Mkoo wa Kigoma, Wilaya ya Kigoma Vijijini, ambayo iko katika Jimbo la Kigoma Kaskazini, kuna Vijiji ambavyo viko kando kando ya Ziwa Tanganyika, ambavyo ni Mtanga, Mwamgongo, Kiziba, Zache, Kagunga na vinginevyo.

Kuna watu ambao walihisiwa kuwa ni wakimbizi, wakashikwa wakapelekwa wakawekwa ndani kama miaka miwili hivi, wakati Uhamiaji wanawachunguza kama ni wakimbizi au la. Baada ya muda huo kupita, wale watu wakatolewa ndani, wakaambiwa sio wakimbizi ni Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa hivi ninavyozungumza kadi zao za Chama pamoja na Stashahada za kupigia kura bado ziko Uhamiaji. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, anawaambiaje?

NAIBU SPIKA: Aah! Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hili swali wameshindwa kuongea na Waziri Masha! Haya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa vile dada yangu Nkayamba, acha nijaribu kulijibu. Je, Waziri Mkuu, unasemaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu anasema, lete majina ya hao watu, niambie wako wapi, mimi nitawasilisha kwa Mkuu wa Mkoa, tutalifuatilia na mimi nina hakika tutapata ukweli wa jambo hili ukoje. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ilianza kubinafsisha mali zake mbalimbali tangu miaka ya 1990.

Moja ya mali zilizobinafsishwa ni shamba la Magamba, ambalo liko kule Mbozi na lina ukubwa wa eka 12,051; nimekuwa naiomba Serikali iwape wananchi shamba hilo kwa sababu ya uhaba wa ardhi uliopo Mbozi.

Lakini pia juzi juzi Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, ilishauri Serikali itoe shamba hilo kwa wananchi wa Wilaya Mbozi, hususan wale wa Tarafa ya Igamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba hilo lilitangazwa kubinafsishwa tangu mwaka 1996, mpaka leo hamna hatua zozote za maana zilizochukuliwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, unawaeleza nini wana-Mbozi, kwamba ni nini hatima ya shamba hili?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, labda nimsihi tu Mheshimiwa Zambi Ndugu yangu, kwamba hebu tuonane kati yangu, wewe, tuunganishe na Wizara ya Kisekta inayohusika, tuliangalie suala hili kwa karibu halafu tukubaliane namna ya kufanya. Kwa sababu bado mimi naamini kama limekaa kwa kipindi chote hicho, ipo haja ya kuchukua hatua mapema zaidi. (*Makofi*)

Ni suala la kukubaliana tu kama eneo lote linahitajika kwa matumizi ya wananchi au tungeweza kubakiza eneo fulani kwa matumizi mengine ambayo sasa tunajaribu kutaka suala la Kilimo Kwanza lijikite. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nina uhakika tukikaa pamoja na Wizara ya Kisekta, tunaweza kupata ufumbuzi wa tatizo hilo. Na mimi ninakuahidi tutalishughulikia kwa haraka sana, mara tu tukishakaa pamoja ufumbuzi utapatikana. (*Makofî*)

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nimwulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Bajeti ya mwaka huu wa 2009/2010, Serikali iliridhia misamaha ya kodi kwa Taasisi za dini. Na iliridhia baada ya kupata kilio kutoka kwa jamii na kupata kilio kutoka kwa Taasisi zenyewe.

Lakini kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Taasisi hizi zimekuwa zikitoa huduma za kijamii na zimekuwa zikitoa huduma za kijamii hasa kwa masuala ya afya na elimu, lakini huduma yenye imekuwa ghali sana kwa watumiaji. (*Makofî*)

Sasa naomba niulize kwamba baada ya kuridhia kwamba hiyo misamaha ya kodi, Serikali ipo tayari kukutana na hizi taasisi za dini ili ikashauri zikapunguza gharama za huduma kwa watumiaji ili iwe nafuu kwa watumiaji? (*Makofî*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, tulichofanya kama Serikali na kwa kweli matokeo ya mjadala hapa Bungeni kwa sehemu kubwa ni kwamba vyombo hivi kwa maana ya mashirika yasiyo ya kiserikali Taasisi mbalimbali za madhehebu ya dini wamekuwa wakiendesha shughuli hizi za kutoa huduma kwa jamii kwa mifumo mbalimbali. Na wamekuwa kwa muda mrefu wanapata msamaha katika maeneo fulani fulani.

Sasa Serikali ilibaini kwamba kuna baadhi ya misamaha ambayo inatumiwa vibaya na ndiyo ikaamua kuchukua hatua kwamba tuondoe baadhi ya misamaha ili iwe ni kama fundisho kwao lakini wote ni mashahidi mlisema hapa tutakuwa tunawaadhibu waliowengi na ndiyo maana Serikali ikarejesha tena maamuzi ya awali kwamba tuendelee na misamaha.

Bado, mimi naamini kwa dhati kabisa kwamba unapolinganisha kwa mfano huduma unayoipata kwenye hospitali ya mtu binafsi na huduma utakayokwenda kuipata kutoka kwenye vyombo hivi, gharama zake ni nafuu zaidi kuliko kwa mtu binafsi huo ndiyo ukweli.

Kwa hiyo msamaha si kwamba unawezesha sasa bei ya madawa iweze kushuka kiasi ambacho unadhani tunaweza wote tukaishabikia hapana, mimi ninaamini bado huduma yao nzuri na tuwatie moyo waendelee kuitoa lakini na mimi nitaendelea kuwaasa kwamba wako baadhi yao wachache amba wanaweza kuwa pengine wanafanya mambo kama haya na naamini wanansikia wajaribu kwa kweli kusikiliza kilio chako na kilio cha Watanzania kwa ujumla. Lakini kazi yao kwa ujumla ni nzuri na ni vizuri tukaendelea kuienzi. (*Makofî*)

MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkoo, Mheshimiwa Waziri Mkoo kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kupeleka vituo vya polisi katika karibu maeneo mbalimbali ikiwemo karibu katika kila kata kwa ajili ya kulinda usalama wa raia na mali zao.

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkoo hawa polisi kwa kuwepo kule karibu muda wote yapo mambo migongano midogo midogo inayojitokeza ambayo ni pamoja ambayo ni ya kuwaharasi wale wananchi lakini kubwa zaidi na ambalo ni vibaya ni kwamba inapofika wakati usiku vile vituo vyote vya polisi kuanzia saa moja unakuja vimefungwa, na kwa vimefungwa, uchambazi unatokea uharifu katika ule usiku mzima sasa wananchi wanashangaa kwamba wakati wa mchana polisi wanaonekana sana, lakini wakati wa usiku wanapata matatizo na polisi hawapo.

Sasa ningependa kufahamu Mheshimiwa Waziri Mkoo Serikali yako imejipangaje, kuhakikisha kwamba wale polisi hawawepo mchana tu isipokuwa na usiku vilevile kuhakikisha kwamba ujambazi ule unaondelea kule unaondokana na wananchi waendelee kuishi kwa amani?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Manyinyi kwa swali hili, lakini nafikiri tunganeanzia kwanza kwa kuipongeza sana jeshi la polisi jamani wanajitahidi sana, na hasa katika mazingira ambayo wanafanya kazi. (*Makofit*)

Tatizo ninaloliona kubwa ni kwamba bado ni wachache sana unaweza ukaenda kwenye vituo vingine unamkutana pengine polisi mmoja au wawili kwa hiyo katika mazingira ya aina hiyo ni kweli kabisa anachokisema Mheshimiwa Manyinyi unaweza kupata tatizo la kuwa na uhakika wa kuwepo askari kituoni pale mchana na usiku kucha.

Kwa hiyo katika vituo vidogo vidogo sehemu nyingi ni kweli lipo tatizo, lakini katika vituo vingine vikubwa wilaya hasa tatizo hilo kwa sehemu kubwa halipo kabisa.

Kwa hiyo mimi nikuombe tu Mheshimiwa Manyinyi kwamba kadri uwezo utakavyokuwa unaongeza wa kuongeza idadi ya polisi katika vituo naamini hii rai yako itaendelea kutekelezwa, lakini nataka niwaombe vilevile kupitia Wizara ya mambo ya ndani ya nchi katika maeneo yale ambako inaonekana tatizo hili la ujambazi ni kubwa, tufanye juhudhi tuweze kuongeza askari kidogo katika maeneo hayo ili kuwezesha kuwepo mzunguko wa kutosha wa ulinzi mchana na usiku.

NAIBU SPIKA: Natumia muda wa matangazo wa mwanzo.

MHE. MZEE NGWALI ZUBERI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii, zipo sera za elimu ya ufundi, elimu za juu, hizi ni sera ambazo nataka kuunganishwa sasa hivi na kufanyiwa marekebisho.

Je, hatuoni wakati muafaka hivi sasa na sera ya muungano wa elimu ya juu ikawa pamoja?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi swali kama ifuatavyo, nachelea kulijibu haraka haraka kwamba ndiyo kwa sababu kidogo linahitaji mawazo kidogo ya sekta tuweze kuona uwezekano wake ukoje.

Lakini mimi nadhani ni ushauri wacha tuuchukue namkabidhi Waziri mwenye uhusika aone kama hilo linawezekana na faida na hasara zake zinaweza kuwa ni nini. Kwa hiyo nadhani tulipokee tulifanyie kazi kwanza.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kipindi cha maswali kwa Waziri Mkoo kimekwisha naomba nichukue nafasi hii kwa niaba yenu kumshukuru Waziir Mkoo kwa umakini wa kuulizwa maswali hata mengine yanafanana ya kisekta sekta hivi ambayo kanuni zetu zinasema hayo tuwaacie wenyewe Waziri Mkoo aulizwe ya kisera. Lakini tunakushuru hata hayo umeweza kuyajibu asante sana. (*Makofi*)

MASWALI NA MAJIBU

Na. 267

Kuanzisha Ukanda wa Uchumi Mkoani Kagera

MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MHE. JANETH B. KAHAMA) aliuliza:-

Kwa kuwa, Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) imepanua eneo lake kwa kujumuisha wanachama wapya amba ni Rwanda na Burundi na kwamba Mkoa wa Kagera utakuwa ni kiungo muhimu kati ya nchi wanachama wa *EAC*:

Je, Serikali haioni kuwa itakuwa ni jambo la manufaa kiuchumi kustawisha na kuendeleza *Corridor* ya Kyaka, Bunazi na Mtukula katika mkoa wa Kagera kuwa Ukanda wa kiuchumi (*special Economic Zone*) kwa kuzalisha bidhaa za kuuza kwa nchi jirani hasa za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kongo?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba baada ya nchi za Rwanda na Burundi kujiunga na Jamuiya ya Afrika Mashariki, Mkoa wa Kagera umekuwa ni kituo muhimu katika biashara na nchi zinazopakana na Mkoa huo hususan nchi za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutambua umuhimu huo, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuititia Baraza la Mamlaka ya EPZ ilibainisha mkoa wa Kagera kuwa mojawapo ya Mikoa 14 yenye kipaumbele cha kutenga maeneo maalum ya uwekezaji yaani *special economic zones (SEZ)* na *Export Processing Zones (EPZ)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008, wataalam kutoka Mamlaka ya EPZ kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Kagera walikagua maeneo mbalimbali mkoani Kagera kwa lengo la kupata eneo maalum la uwekezaji la EPZ na SEZ.

Mojawapo ya maeneo yaliyokaguliwa na kuonekana yanafaa kwa uwekezaji huo ni eneo la ukdana wa Kyaka, Bunazi na Mtukula. Hata hivyo, kwa wakati huo eneo lililopendekezwa lilikuwa ni lile la Kitengule wilayani Karagwe. Aidha, ufuatiliaji zaidi ulionesha kuwa eneo hilo la Kitengule lilishamilikishwa kwa kampuni ya Kagera *Sugar Company* hivyo lisingeweza kutumika kwa EPZ na SEZ.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoptaka na hali hiyo, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa kushirikiana na Mamlaka ya EPZ wameomba uongozi wa mkoa wa Kagera kuangalia uwezekano wa kutenga eneo jingine la EPZ na SEZ na mamlaka ya EPZ itakuwa tayari kulikubali eneo la Ukanda wa Kyaka, Bunazi na Mtukula iwapo uongozi wa Mkoa wa Kagera utalipendekeza.

Wizara itaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Janeth Kahama na Wabunge wengine wa Mkoa wa Kagera na Uongozi mzima wa Mkoa wa Kagera kuhakikisha kazi hii inakamilika na kuwezesha mkoa wa Kagera kuwa kituo muhimu nchini na cha kuhudumia nchi jirani.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii, pia nichukue nafasi kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini pia nichukue nafasi kumfahamisha Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba eneo la Kitengule katika wilaya ya Karagwe halimiliwi na kampuni ya Kagera Sugar, bali lilisharudishwa katika mikoa ya Serikali na liko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ambayo iko tayari kutenga eneo hilo kwa ajili ya SEZ na EPZ je, Serikali iko tayari kufuatilia jambo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wa Karagwe na Mkoa wa Kagera kwa ujumla ni wakulima wa zao la kahawa na mara nyingi wamekuwa wakitafuta soko la bei la nzuri katika nchi jirani ya Uganda kwa njia ambayo sio halali. Je, Serikali iko tayari iko tayari kutumia eneo hili kujenga soko kubwa la kimataifa ili wananchi wauze kahawa yao hapo hapo wilayani Karagwe.

NAIBU SPIKA: EPZ mpaka soko la kahawa.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Blandes kwa kutupa taarifa hizi kwamba eneo hilo la Kitengelu, limesharudishwa sasa katika Halmashauri husika na

tumuombe Mheshimiwa Blandes na Waheshimiwa Wabunge wengine wote wa Mkoa wa Kagera watusaidie kuongea na uongozi wa mkoa wa Kagera sasa ili mamlaka ya mkoa ituandikie sisi sasa kwamba lile eneo liko tayari kwa matumizi ya EPZ, namhakikishia kwamba endapo barua hii itakuja na uongozi wa mkoa ukaridhia eneo hilo litumike, Wizara yangu na mamlaka ya EPZ haitasita kulitumia eneo hilo kwa kazi hiyo ambayo ni muhimu sana kama nilivyosema.

Swali la pili nakubaliana naye vilevile kwamba wakulima wale wa Karagwe na mkoa wa Kagera kwa ujumla ambao wamelima kahawa wanahitaji kupata soko. Soko sio tu kwa ajili ya hapa Tanzania lakini vilevile kwa sababu ya maeneo ya mpakani kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanunuzi kutoka nje ya Tanzania wanakuja pale na wanawenza wakanunua na wakalipa kodi sawa sawa.

Ninachopenda kumwambia Mheshimiwa Blandes ni kama nilivyojibu swal la awali endapo Halmashauri husika watakaa wakaona eneo hilo husika wakaliandikia utaratibu ni kwamba Halmashauri ile inaanza kutafuta vyanzo vyake vyenyewe vy a fedha kwa ajili ya ujenzi huo.

Endapo Halmashauri hiyo inaona kwamba haitawenza kujenga soko lile labda kutokana na ukubwa wake, basi wanaleta maombi Wizarani na sisi tunajaribu kuongea na wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba soko hilo linajengwa katika kiwango kinachotakikana.

Na. 268

Kuhusu Sheria Inayosimamia Mifuko ya Pensheni

MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA aliuliza:-

Kwa kuwa sheria zetu zinasimamia mifuko ya pensheni hazina kipengele chochote kinachoruhusu mafao ya wastaaafu kulipwa pamoja na riba pale mafao hayo yanapochelewa kulipwa kwa wakati jambo ambalo linasababisha usumbufu kwa wastaaafu:-

Je, Serikali iko tayari sasa kuleta Muswada wa Sheria Bungeni utakaoruhusu pensheni kulipwa pamoja na riba pale taasisi inayohusika inapochelewesha malipo ya pensheni kwa wastaaafu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR Y. MZEE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonyesha kuwa kuchelewa kulipwa mafao wastaaafu kunatokana zaidi na waajiri kuchelewa kulipa michango ya wafanyakazi wao au kuchelewa kuwasilisha taarifa za wafanyakazi wao wa wakati. Hata hivyo, kufuatia elimu

iliyotolewa kwa waajiri pamoja na agizo la HAZINA, tatizo la kuchelewa kwa michango kutoka kwa waajiri kwa sasa na hasa kwa mashirika na taasisi za umma limepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge sio bayo lakini Serikali haioni haja ya kuwasilisha Muswada wa marekebisho ya sheria, itakayoruhusu mafao kulipwa pamoja na riba pale taasisi inayohusika itakapochelewesha malipo ya wastaaifu. Hii ni kutokana na kwamba, kuchelewa kwa ulipaji wa mafao hakusababishwi tu na mfuko bali ziko sababu nyingine ambazo zinaweza kuchelewesha malipo.

MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua iwapo katika mfuko wa hifadhi kuna sheria inayomlinda mwajiriwa kulipwa mafao yake kwa wakati wakati yeye anakatwa michango yake kwa wakati. Mheshimiwa Naibu Waziri iwapo mafao ya mwajiriwa yatacheleweshwa kulipwa kwa muda mrefu je, pensheni yake itaanza kulipwa wakati gani?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUS MZEE): Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria za mifuko viko vipengele ambayo vinamlinda mwajiriwa kama mwajiriwa imethibitika kwamba yeye analipa michango yake kwa wakati lakini ni mwajiri wake ndiye aliyesababisha michango ile ichelewe. Kwa hivyo huyu mwajiriwa hulipwa mafao yake kwa wakati na kesi inayobakia inakuwa ni baina ya mifuko na mwajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili nataka nimueleze Mheshimiwa Mbunge kwamba pensheni inakokotolewa kutokana na mafao ambayo mwajiriwa analipwa. Lakini mafao yanapochelewa haina maana kwamba ile pensheni yake ndiyo miezi ili itakuwa imeruka, pensheni ile italipwa kuanzia mwezi ule ambaa ameanza kustaafu. (*Makofit*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza ukiangalia kwenye mifuko yetu ya pensheni yote wafanyakazi wako watatu, wanachangia kwenye mifuko tofauti, na walikuwa wanalipwa mishahara sawa lakini wanapostaafu mafao ni tofauti, sasa Serikali haoni imefika wakati wa kuangalia sheria hizi ili kuweza kuona wafanyakazi hao wanalipwa sawa wanapomaliza muda wao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSUS MZEE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nah ii ndiyo kwa maana Serikali imepitisha ile sheria ya kuweka mamlaka ambayo mamlaka hiyo itaangalia hivi viwango ili kila mfanyakazi kwa kila mshahara waweze kulipwa mafao yanayolingana.

Na. 269

Kuandaa Hesabu kwa kiwango cha Kimataifa

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa duniani kote nchi zinatakiwa kuandaa hesabu kwa kiwango cha kimataifa (*IPSAS*); na kwa kuwa mfumo huu ni mpya na hatuna wataalam wa kutosha:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza hili na itachukua muda gani?

(b) Je, tuna wataalam wangapi ambao wamebobea kwenye utaratibu huu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI - MHE. JEREMIA S. SUMARI Alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mohammed Rashid Abdallah, Mbunge wa Pangani lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rished kwa swalii lake zuri. Serikali iliamua mwaka 2004 kuiandaa na kuanza kutumia viwango vya kimataifa vya uandaaji wa Hesabu za Serikali.

Mwezi Julai, 2007 viwango ambavyo vimeainisha kwenye *The International Public Sector Accounting Standards (IPSAS)*, na *International Financial Reporting Standards (IFRS)* vilianza kutumika. Tayari utaratibu wa kuandaa Hesabu za Serikali kwa kiwango cha Kimataifa *Cash basis IPSAS* umeanza kutumika kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008. Hesabu zinazohusika ni za Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, mikoa na Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa mpango huu kutategemea uwezo na kasi itakayowezekana kutokana na ukubwa wa mabadiliko yanayohitajika ambayo ni ya kitaaluma. Baada ya kujenga uzoefu na cash *basis IPSAS* Serikali itaendelea na kuingia kwenye *accruals IPSAS*.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Wahasibu 334 walipatiwa mafunzo kuhusu viwango hivyo vya kimataifa. Idadi hiyo ya wahasibu waliopatiwa mafunzo ni pamoa na wahasibu wakuu wa Wizara na idara zinazojitegemea, wahasibu wawili wawili wanaohusika moja kwa moja na uandaaji wa hesabu katika kila Wizara na idara zinazojitegemea, wahasibu wa Sekretariati za mikoa, wahasibu wa ofisi za ubalozi nje ya nchi na wakaguzi wa ndani wa Wizara na idara zinazojitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuwapatia wahasibu wake mafunzo zaidi, na kuongeza idadi ya kada hii kufuatana na mahitaji.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwanza naomba wanaouzungumza wasiwazidi wanaotoa majibu hatuelewani.

MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawaili madogo ya nyongeza. Kwa mfumo wa sasa na kwa huu mfumo wa *cash basis IPSAS* hutuoni *balance brought forward* katika taarifa ya mahesabu. Je, nitatofauti gani tutakayoiona katika taarifa ya mahesabu kati ya hii tunayoitumia sasa ambayo imepitwa na wakati na hii ya *cash basis IPSAS* katika mwaka unaofuata.

Kwa kuwa pesa nyingi za maendeleo zinakwenda kwenye Halmashauri na accruals basis IPSAS itasaidia sana katika kudhibiti pesa zinakwenda hasa katika miradi ya maendeleo je, Serikali haioni kuna umuhimu wa lazima ili kuokoa fedha hizi zinazokwenda kule katika Halmashauri tuanzishe mfumo huu hata kwa Halmashauri chache kwa kuanzia kila mwaka ili tuokoe fedha hizi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza nia na shabaha ya kuingia katika mfumo huu wa kimataifa ni hilo hilo alilosema Mheshimiwa Rished kwamba taarifa hizi za mahesabu zinapotengenezwa zimekutwa zina mapungufu mengi, ingawaje zinasimamiwa na sheria ya fedha za umma ya mwaka 2001, 2004 na lakini tunategemea mambo matatu ya msingi yatajitekeza.

- (i) Ni kwamba kwa mfumo huu mpya kutakuwa na uwajibikaji zaidi.
- (ii) Kutakuwa na uwazi zaidi na kwa hiyo hata hilo alilosema la *balance brought forward* na kwa mfano *guarantees* zile dhamana zile ambazo hazionekana kwenye vitabu vyta mahesabu sasa hivi tutaweza kuviona na,
- (iii) Tunalotegemea litatokea ni kwamba kwa mfumo huu wa kimtaifa tutaweza kuwa na hali ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni fedha za maendeleo zinazokwenda kwenye Halmashauri, kwamba kwa mfumo huu wa sasa wa Halmashauri ingawaje wanatakiwa kutohakana na sheria ya *the local government finances act* ya mwaka 1982 kutengeneza mizania kwa mfano.

Tunetegemea hata hayo ya fedha za maendeleo na mali za Serikali za mitaa zingeonekana lakini ukitizamana zile hesabu kwa sasa hivi na taarifa zinazotolewa hazionekani. Na kwa hiyo tunagemea kwamba kuanzia mwaka huu wa 2008/2009 na juhudhi zinafanyika sasa hivi na maagizo yameshatolewa hesabu zile za Serikali za mitaa zitakapowasilishwa kwa mdhibiti na mkaguzi mkuu zitakuwa zimtengenezwa kufuatana na *accruals basis IPSAS* ambayo ni *International Public Sector Account Standard* na kwa hiyo zitakuwa zitakuwa wazi zaidi, zitakuwa bora zaidi na tutaweza kupata taarifa ambazo zinaaminika.

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza, kwa kuwa taarifa za *CAG* inaishia June, 300, 2008 na pia kwenye Kamati yetu ya *LAAC* tumeona kwamba mfumo wa *IPSAS* umeshindikana kwenye Halmashauri pamoja na kufungwa kwa mitambo ya *IPCO*.

Je, Serikali iko tayari kufanya tathimini ya kina kuona sababu iliyofanya mfumo huu ushindakane, na kuubadilisha kama itakuwa lazima kwa sababu mfumo wa Serikali Kuu na wa Serikali za Mitaa inaelekea haijaowanishwa bado?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba si kwamba utayarishaji wa taarifa ya mahesabu yalipelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu yalishindikana kutengenezwa.

Isipokuwa ni kweli tunakiri kwamba yaliwapa tabu kutengeneza zile hesabu na kwamba ni kweli vilevile kwamba ziliwu haziko kwenye viwango ambavyo ndivyo hivyo ambavyo tunategemea za kimataifa chini ya *accruals IPSAS* kama ilivyo lakini naomba nitaarifu kwamba hata bodi ya *IPSAS* yenyewe imeomba Halmashauri na Serikali za nchi wanachama na ziko 83 ambazo zimekuwa zimeshaingia kwenye mfumo huu zipeleke kwenye ile bodi mapungufu ambayo yameonekana, matatizo ambayo wamekutana nayo ili sasa yazungumzwe na ili tutafute njia ya kusaidiana.

Lakini nikiri vilevile kwamba tuna tatizo la upungufu wa utaalam hapa na pale tutakapokuwa tumekamilika kwenye mambo haya basi hesabu hizo za Halmashauri pamoja na za Serikali Kuu zitakuwa zinakuwa bora zaidi.

Na. 270

Kujenga Kituo cha Polisi na Kuwapatia Nyenzo za Usafiri Polisi

MHE. GOSBERT B. BLANDES aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Karagwe inakabiliwa na wimbi kubwa la ujambazi hasa katika mapori ya Kimisi, Burigi na eneo la Uzuri na kondoo kata ya Kihanga ambapo juhudzi za polisi zinakumbana na tatizo la nyenzo hasa magari na pikipiki; na kwa kuwa, wilaya hiyo ni kubwa sana na iko mpakani mwa nchi za Uganda na Rwanda jambo linalosababisha muingiliano mkubwa wa wageni.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuipatia idara ya Polisi wilayani Karagwe gari na pikipiki?

(b) Je, kwanini Serikali haijengi vituo vya polisi vya kudumu katika eneo la pori la Kimisi na eneo la Uzuri wa Kondoo kata ya Kihanga ambayo ndiyo maeneo yanayotumiwa na majambazi mara kwa mara?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Gosbert Blandes Mbunge wa Karagwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa wilaya ya Karagwe ina magari moja ambalo ni la Mkuu wa Polisi Wilaya pamoja na pikipiki mbili. Kutokana na jiografia ya Wilaya ya Karagwe ni wazi kwamba wilaya hiyo inahitaji vyombo vya usafiri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge wakati wa Bajeti ya Wizara yangu siku ya tarehe 08 Julai, 2009 niliahidi kwamba mara baada ya kupata magari yalijotengwa katika bajeti 2008/2009 wilaya ya Karagwe itapelekewa gari lingine jipya bila kukosa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hujenga vituo vya polisi katika maeneo ya makazi ya watu ambapo kuna shughuli za kiutawala, kiuchumi na kijamii. Hivyo, Serikali haiwezi kujenga vituo vya polisi katika maeneo yenye mapori ikiwemo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

Aidha, kwa kuthamini usalama wa Raia na mali zao Jeshi la Polisi limeweka Kiteule (*detach*) katika pori la Kimisi ambacho kina usafiri, limeweka vizuizi katika pori la Burigi na Uzuri wa Kondoo. Pamoja na Kiteule na vizuizi hivyo, Jeshi la Polisi pia limeanzisha kituo kidogo cha polisi Kitengule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ulinzi katika maeneo yote ya wilaya ya Karagwe na mkoa wa Kagera kwa ujumla kwa kutumia rasilimali zilizopo. Aidha, ushirikiano wa wananchi ni muhimu sana katika kutimiza azma nzima na usalama wa raia na mali zao.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swal la nyongeza kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu nakuishukuru Serikali.

NAIBU SPIKA: Hivi kwanini hatukusikii vizuri hapa.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Waziri kwa majibu mazuri na pia nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kutupatia gari la polisi wilayani Karagwe ingawa halijafika lakini naamini litafika.

Sasa baada ya hapo niulize maswali mawili ya nyongeza, tatizo la wilaya ya Karagwe kuhusiana na ujambazi ni kubwa sana kiasi kwamba majambazi wamefikia kutumia hata silaha za kivita ikiwemo pamoja na mabomu. Gari moja katika wilaya ya Karagwe, ambayo ina majimbo mawili kusema kweli halitoshi hata kidogo, mahitaji halisi ya wilaya ya Karagwe ni magari yasiyopungua kumi. Sasa nataka niulize Serikali.

Je, iko tayari kuongeza magari hayo angalau yafikie matano?

Swali la pili, Wilaya ya Karagwe imekuwa na upungufu mkubwa sana wa Askari Polisi, sasa hata hayo magari yakija bila kuwa na Askari Polisi hiyo kazi itafafanywa na akina nani? Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongeza Askari Polisi haraka iwezekanavyo?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Gosbert Blandes Mbunge wa Karagwe kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama nilivyoeleza katika jibu langu la awali kwa sasa hivi tayari kuna gari moja katika Wilaya ya Karagwe na nimetambua kwamba hilo gari halitoshi. Lakini kama nilivyoahidi hilo gari ambalo tumemuahidi litafika mwaka huu wa fedha na ninamuomba hasa kutokana na hili gari ambalo atalipata mwaka huu liliahidiwa mwaka jana. Kabla sijaanza kuahidi magari mengine ninaomba avute subira apokee hilo gari ambalo tumeahidi kwa mwaka huu. (*Makofî*)

Lengo la Wizara yangu ni kuhakikisha kwamba kuna vitendea kazi vya kutosha katika Wilaya zote kwa bahati mbaya kutokana na uhaba wa bajeti haitutoshelezi kuweza kuweka magari yote ambayo tungependa kuwa nayo katika Wilaya zetu zote lakini tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kwa kuangalia hali halisi katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba magari ambayo yanapelekwa yanatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza Askari nafikiri Mheshimiwa Blandes alimsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyoongea leo asubuhi, amenielekeza kwamba niangalie hali halisi katika maeneo mbalimbali na kuangalia uwezekano wa kuongeza Askari na kama anakumbuka katika hotuba yangu ya bajeti nilieleza kwamba mwaka huu wa fedha ni nia ya Serikali kuongeza Askari 7000 katika Jeshi la Polisi.

Kwa hiyo, tutaangalia hali halisi katika Wilaya ya Karagwe na kuona ni wangapi ambao tutawapeleka kule Karagwe.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. najua mnapenda sana tuendelee lakini muda haututoshi. Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu swali linalofuatia.

Na. 271

Kujenga Nyumba na Ofisi za Viongozi wa Polisi

MHE. FRED TUNGU MPENDAZOE aliuliza:-

Kwa kuwa, viongozi wa polisi na watumishi wengine katika Wilaya ya Kishapu hawana ofisi na nyumba za kuishi kiasi cha kuwafanya wahangaike kwa kupokezana sehemu za kuishi na kufanya kazi:

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga ofisi na nyumba za viongozi wa Polisi na watumishi wengine hasa ikizingatiwa kuwa viwanja viro?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba watumishi wake wote wakiwemo Askari polisi katika ngazi zote wanafanya kazi katika mazingira yaliyo bora ikiwemo ofisi, nyumba za kuishi na wakiwa na vitendea kazi vya kutosha na vya kisasa. Hata hivyo nia hiyo nzuri ya Serikali inakwamisha na uwezo mdogo wa kiuchumi, hivyo azma hii itaendelea kutekelezwa kwa awamu kadri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa viongozi wa polisi na askari kuwa na ofisi na nyumba za kuishi, Wizara yangu kwa mwaka 2009/2010 imepanga kukamilisha ujenzi wa vituo vya polisi wilaya za Meatu na Bukombe na ujenzi wa kituo cha Polisi Kishapu umepangwa kutekeleza kuititia bajeti ya mwaka 2010/2011. (*Makofî*)

MHE. FRED TUNGU MPENDAZOE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swal la nyongeza.

Kwanza naomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri ya kuridhisha na ya kutia matumaini kwa wananchi wa Jimbo la Kishapu.

Naomba niulize swal dogo tu, kwa kuwa tatizo la nyumba za kuishi Polisi katika Wilaya ya Kishapu ni tatizo kubwa na nila kidharura kama ilivyo katika Wilaya ya Bukombe na Wilaya ya Meatu. Na kwa kuwa, wananchi kwa kuona tatizo hili ni kubwa sana wako tayari kushirikiana na wadau mbalimbali katika Wilaya ya Kishapu ili waweze kujenga kituo cha Polisi.

Je, Serikali iko tayari kuwaunga mkono kwa kuchangia ujenzi huo kwa kutoa vifaa vya ujenzi kwa mfano mabati, *cement* na kadhalika ili tatizo hilo liweze kuisha?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo.

Kwanza, napenda kumshukuru sana yeche pamoja na wananchi wa Kishapu ambao wako tayari kujitolea kutusaidia kujenga nyumba pamoja na kituo cha Polisi.

Napenda kusema kwamba namwomba Mheshimiwa Mbunge aje ofisini kwangu ili tuangalie na tuone Wizara yangu itamsaidia vipi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha na pia muda wa maswali umepita.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuwatambue wageni tulionao katika *Gallery* zetu. Kwanza kabisa, nadhani toka mmeingia mmeona kuna watu wanafanya vitu vyao hapo katika *Speakers Gallery*. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika na ni watoto wa kituo cha Viziwi kilichopo Njombe. Hawa watoto wako 17 pamoja na Walimu wao. Kile kituo kinachukua watoto wa shule ya msingi kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba. Halafu tumeanzisha sasa shule ya sekondari kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne.

Kwa namna ya pekee, tunamshukuru sana Waziri wa Elimu kwa sababu kulikuwa na utata wa kutoa kibali cha kuanzisha Sekondari ya pekee katika Afrika Mashariki. Waziri wa Elimu alitoa kibali hicho na sasa hivi wafadhili kutoka Finland wanajenga Sekondari kubwa kabisa ya watoto wenye ulemavu wa kusikia. Kwa hiyo, naomba wote wasimame pamoja na Walimu wao wakiongozwa na Mchungaji Sabina Luhemwe. Yeye Mchungaji Sabina ni Katibu Mkuu Huduma za Jamii katika Kanisa la KKKT, yuko na Mkurugenzi wa Kituo Mchungaji Alfonse Ngavatula na wako Walimu Benito Mkage na Restituta Mdenye. Karibuni sana. (*Makofi*)

Watoto wa Sekondari pia wasimame, hawa ni watoto wa Sekondari ambao ni viziwi, pia kuna watoto wa shule ya Msingi. Mnakaribishwa sana na Waheshimiwa Wabunge wamefurahi kuwaona. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunatoa wito kwa watu wengine pia kwamba wanaweza kupeleka watoto kule kwani ni shule nzuri sana na si vizuri wazazi au walezi wakawaacha nyumbani watoto kwa sababu wana ulemavu fulani, pale tuna watoto wengi sana. Kwa hiyo, tunaomba kabisa wananchi kwamba watoto walemvu si kwamba wanashindwa bali wanaweza kila kitu. Pale kuna Chuo cha Ufundu pia, kwa wale wanaomaliza kidato cha nne hata wa darasa la saba. Kwa hiyo, mnakaribishwa kupeleka watoto.

Nina wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe ambao ni familia yake ikiongozwa na Mke wake Mrs. Kudra Maghembe, yuko na mtoto wake Ngwali Maghembe. Karibuni sana. (*Makofi*)

Yuko Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundu Prof. Khamis Dihenga na pia Naibu Katibu Mkuu Bwana Selestine Gesimba. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wengine ni Wenyeviti na Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, karibuni sana. Makamu Mkuu wa Chuo cha Sokoine na Mzumbe pia. Yupo pia Makamu Mkuu wa Chuo cha Tiba na Sayansi ya Afya Muhimbili, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo

Kikuu cha Dodoma UDOM na Chuo Kikuu cha Zanzibar. Karibuni sana Bungeni na tumefurahi kuwaona. (*Makofi*)

Lakini pia, kuna Wakuu wa Vyuo vingine, nao ni kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara, Moshi, naona Makamu wake yuko. Chuo Kikuu Huria, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam na Chuo cha Mkwawa Iringa na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Dar es Salaam. Mnaona sasa Sera za CCM vyuo vikuu vyote hivi vimeshaanzishwa nchini. Suali la ubora wa chuo litakuja tu, nasema kweli miaka iliyopita kulikuwa na Chuo Kikuu kimoja tu lakini sasa hivi viko vingi sana. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuna Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundu hapa nchini. Sasa kwa kuwa wako wengi naomba tu wasimame walipo. Karibuni sana.

Tuna wageni wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Philip Marmo ambaao ni walimu wakuu wa shule zilizofanya vizuri katika mitihani ya kumaliza elimu ya Msingi na Sekondari Wilayani Mburu, Manyara. Hawa Walimu wako wa sekondari na pia wa shule za msingi. Kwa kuwa wako wengi sana ninaomba nisiwataje Majina yao. Samahani sana kwani jana tuliwatambulisha lakini kumbe hamkuwa mmeefika. Karibuni na tunawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya ya kufahausha wanafunzi katika shule za msingi na sekondari na huo ndiyo ubora wa Elimu unaotakiwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Kuna Walimu Wakuu wamefuatana na Walimu watatu kutoka shule tofauti ambaao ni Walimu wa Shule nne za msingi ndiyo hao waliosimama.

Halafu tuna wageni wengine ni Walimu Wakuu wa shule sita zinazoongoza kwa ubora Wilayani wakiongozana na Mkuu wa Kituo binafsi cha Elimu. Waratibu wa Elimu wa Kata, Viongozi wa Elimu wa Wilaya na Viongozi Wakuu wa Wilaya akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Mburu na Mkurugenzi wa Halmashauri. Ahsante sana kwa kazi nzuri kwani sasa hivi mambo ya Elimu ya Shule za Sekondari yameachwa mikononi mwenu, tunaamini ninyi mtakuwa mfano wa kuigwa. Karibuni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tuna wageni wa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu Mheshimiwa Mwantumu Mahiza ambaao ni Afisa Elimu wa Mkoa wa Tanga akifuatana na Maafisa Elimu wa Shule za Sekondari na Msingi katika Wilaya za Mkoa wa Tanga. Lakini kati yao yuko Ndugu Mouson Hufin *Director of Solar Aid Tanzania*, karibu sana. Karibuni sana na ahsante sana. (*Makofi*)

Huyu anatoa msaada wa kuweka umemenuru kwa shule za Sekondari za Kata akifuatana na Bi. Beatrice Habadi. Nadhari hiyo teknolojia wengi tutapenda kujifunza jinsi inavyofanya kazi.

Wageni wengine nane ni wageni wa Naibu Waziri wa Elimu na Mfunzo ya Ufundu Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka kutoka Elimu Mkoa wa Mara ambaao ni Afisa

Elimu wa Mkoa. Karibuni sana na ahsante sana kwa kuja na tunafurahi kuwaona ndani ya Bunge hili.

Pia kuna mgeni wa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Margret S. Sitta, Bi. Christa Rweyemamu ambaye ni Meneja wa Shule ya St. Joseph iliyopo Dar es Salaam *Mbezi Beach*, ye ye pia ni Afisa Mwandumizi wa Mfuko wa NSSF Dar es Salaam. Karibu sana Mama.

Tuna wageni wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Menejimenti ya Utumishi wa Umma Mheshimiwa Hawa A. Ghasia. Hawa ni Bi. Salma Mnali Diwani wa Viti Maalum, Bwana Issa Ally Kea Mjumbe wa Baraza la Wazee Kata ya Nanyamba. Karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Nimrod E. Mkono amba o ni Waheshimiwa Madiwani 40 Mbunge wa Musoma Mjini, karibuni sana na tunategemea mnamsaidia Mheshimiwa Mbunge katika shughuli zake. (*Makofit*)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Archt. Fuya G. Kimbita amba o ni Mke wake Bi. Monica na watoto wake. Karibuni sana.

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Goti Eliyah Rais wa ARUSO, naona wamekosa nafasi basi wataingia baadaye.

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mariam Mfaki amba o ni wanafunzi saba kutoka *Mwalimu Nyerere Memorial Academy College* wasimame walipo. Naona hawakupata nafasi ila watapata nafasi mchana.

Tuna Viongozi wa Chama cha Muungano wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania yaani *THTU* wakiongozwa na Ndugu Maswanya Kulu, nafikiri walikosa nafasi watakuwa kwenye basement lakini wataingia mchana.

Tuna wanachuo wa Chuo cha Ualimu cha *Capital* wakiongozwa na Ndugu Pamba, naona nao pia wamekosa nafasi.

Tuna wanafunzi 40 na Walimu wao kutoka Shule ya Sekondari ya Hazina iliyopo hapahapa Dodoma kama wapo naomba wasimame, ooh! Naona hawapo lakini watapata nafasi mchana.

Tuna wanafunzi 50 na Walimu wao kutoka Shule ya Msingi Mbwanga iliyopo hapahapa Dodoma, nadhani watapata nafasi mchana.

Tuna wanafunzi 10 na Walimu wao kutoka Shule ya Sekondari ya Makole iliyopo hapahapa Dodoma. Karibuni sana Walimu na wanafunzi.

Tuna wanafunzi 50 na Walimu wao pia kutoka shule ya Sekondari Kikuyu iliyopo hapahapa Dodoma. Ooh! kumbe nyie mmebahatika kupata nafasi, karibuni sana.

Wanafunzi 40 na Walimu wao kutoka Shule ya Sekondari Nkuhungu iliyopo pia hapahapa Dodoma, hawa ni awamu nyingine. Nadhani wako *basement*.

Tuna wanafunzi 46 na Walimu wao kutoka Shule ya Msingi NARCO iliyopo hapahapa Dodoma, karibuni sana.

Tuna mgeni mwengine ambaye ni Mrs. Grace Chambo kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara, amekuja kwa ajili ya kutembelea Bunge. Huyu nadhani ni Mke wa Makamu Mkuu wa chuo hicho kule Moshi. Karibu sana Mama na tunashukuru kwa kuja kwako. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni pia wa Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi ni Mwinjilisti Laban John wa Kanisa la *Seventh Day International Fellowship Ministry Dar Es Salaam*. Popote ulipo tunakukaribisha sana.

Tunayo bahati kubwa sana kwani leo tuna wageni wengi na kwa hiyo nafasi haitoshi, lakini wengine wanakaa kwenye *basement* ila wakati wa jioni wanawenza kuingiza ndani.

Matangazo ya kazi ni kama ifuatavyo;

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo wakutane nje ya ukumbi wa Pius Msekwa kwa ajili ya safari ya kwenda Chuo cha Mipango saa saba mchana. Kwa hiyo, m Kutane pale mara ifikapo saa saba mchana ili muelekee huko chuoni.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Alhaji Mohamed Hamisi Missanga anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo kutakuwa na kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa saa saba mchana.

Jana nilitangaza kwamba, Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Chama Cha Mapinduzi watakuwa na kikao chao saa saba mchana katika Ukumbi wa Spika.

Hapa nina tangazo lingine kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Zaynab A. Gama linasema kwamba siku ya Jumamosi baada ya swala ya saa saba kutakuwa na Hitma yaani kisomo cha Marehemu Shehe Suleiman Gologosi na Marehemu Prof. Haroub Othman.

Pia anasema kwamba, kuwa kuwa shughuli hii ina gharama tunaomba kila Mbunge atakayeguswa achangie kiasi anachowenza.

Kwa upande wa Mawaziri atapokea Mheshimiwa Hawa A. Ghasia na kwa upande wa Wabunge watakaopokea ni Mheshimiwa Anna M. Komu, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Athumanii

Saidi Janguo na mwenyewe Mheshimiwa Dr. Zaynab A. Gama. Yeye alisema chama tawala na upinzani lakini katika misiba hakuna chama tawala wa upinzani.

Kwa hiyo, hawa watu ndiyo watakaopokea hii michango na mnakaribishwa siku ya jumamosi baada ya swala za saa saba lakini hakusema wapi. Mheshimiwa Zaynab Gama ni wapi?

MHE. DR. ZAYNAB A. GAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema saa saba kwani ningesema baada ya salat la alasiri wengi wasingefahamu, na itafanyika kwenye Msikiti wa Nunge kila mmoja anakaribishwa sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kwa hiyo mahali ni katika msikiti wa Nunge na nyote mnakaribishwa sana.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa George Malima Lubeleje Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 23 saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati na yeye pia hakusema wapi.

Mheshimiwa George M. Lubeleje Wajumbe wako wakutane wapi?

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, ni katika ukumbi namba 219 jengo la utawala.

NAIBU SPIKA: Unajua hawa hawakuandika kwa hiyo nadhani wamefikiria hapahaha ndiyo maana hawakutaja sehemu husika.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hatua inayofuata.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu namba 68 (7) katika kitabu chetu cha Kanuni za Bunge naomba mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Kifungu kinasemaje?

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu namba 68 (7)

NAIBU SPIKA: Kinasemaje?

MHE. DIANA M. CHILOLO: Inasema hivi ‘Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimamia wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na

Taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa.'

NAIBU SPIKA: Haya ni jambo gani limetokea?

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunajadili hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni kubwa sana na ina mambo mengi, kuna chekechea, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, vyuo vikuu na vyuo vya ufundii na mambo mengi sana muhimu nadhani hata wewe mwenyewe utakuwa shahidi hata wageni walioingia leo ni wengi mno na hata nje pia ni wengi mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kulingana na uzito wa wizara hii ninaomba wizara hii ijadiliwe siku mbili badala ya siku moja ili Waheshimiwa Wabunge wengi tuliokuwa tunakimbizana asubuhi kupeleka maombi ya kuchangia tupate muda muafaka wa kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Hakuna hoja hapo, huu ni mwongozo wa Spika kwa hiyo huwezi kuugeuza mwongozo ukawa hoja.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu utaratibu pia ni kwamba ratiba ya vikao vyetu vyote mnayo toka hatujaanza Bunge, kwa hiyo kama mngekuwa na hiyo *contention* basi toka tunaanza Kamati ya Uongozi imesambaza ratiba ya vikao vyetu. Sasa hapa hatuwezi kubadilisha namna hiyo kwa sababu kuna mambo mengi ambayo yanapaswa kuangaliwa.

Kwa hiyo, tunaanza na hiyo kazi na tutaendelea na kushauriana katika Kamati ya Uongozi, kama ikibidi sawa, lakini kama hakutakuwa na uwezekano tutatoa taarifa. Lakini sasa hivi tunaendelea na kazi.

Ila naomba *order* kwa wanaotoka watoke kimya na kuongea Bungeni Kanuni yetu inakataza kwani tunahitaji utulivu ndani ya Bunge.

KAULI YA SERIKALI

UBINAFSISHAJI WA MGODI WA KIWIRA

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima kubwa, naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Serikali kulieleza Bunge lako tukufu na umma wa Watanzania kwa ujumla kuhusu suala la ubinafsishwaji na

umiliki wa Mgodi wa Kiwira na kampuni ya *Kiwira Co. Ltd* (KCML), hatua zilizochukuliwa na uamuza wa Serikali wa kuhakikisha miradi wa uchimbaji wa Makaa ya Mawe na uzalishaji wa Umeme kutoka Kiwira unatekelezwa.

Aidha, maelezo haya ni utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyojatoa kwa Wizara ya Nishati na Madini wakati wa majumuisho ya Mijadala ya Bajeti zake za tarehe 27 Juni, 2008 na tarehe 26 Juni, 2009 na ahadi ya Wizara ya Nishati na Madini niliyoitaoa wakati wa majumuisho ya bajeti ya Wizara yetu tarehe 9 July, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Historia. Ujenzi wa Mgodi wa Kiwira ulianza mwaka 1983 na kukamilika mwaka 1988 kwa ushirikiano kati ya Serikali ya China na Tanzania ambapo gharama halisi za ujenzi wa mgodi huo wakati unakamilika zilikuwa shilingi bilioni 4.29.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni iliyoundwa kuendesha shughuli za kuchimba makaa ya mawe na kuzalisha umeme kutoka mgodi wa Kiwira kwa matumizi yake na Wilaya za Rungwe, Ileje na Kyela Mkoani Mbeya ni Kampuni ya *Kiriwa Co. Mines Ltd.* iliyosajiliwa tarehe 3 Oktoba, 1988 kwa kupitia cheti cha usajili namba 15715 ikiwa ni kampuni tanzu ya shirika la Madini la Taifa yaani *State Mine Cooperation (STAMICO)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa makaa ya mawe na uzalishaji wa umeme ulianza rasmi tarehe 1/11/1988 ambapo makaa yaliyochimbwa yalitumika kuzalisha umeme kwa ajili ya matumizi ya mgodi wenye.

Ziada iliyopatikana iliuzwa kwa kutengeneza saruji cha Mbeya yaani *Mbeya Cement Company*, Kiwanda cha kutengeneza karatasi yaani *Southern Paper Mills* kilichopo Mgololo Mkoani Iringa na ziada nyingine iliuzwa kwa Shirika la Umeme Tanzania yaani *TANESCO*.

Kufuatana na upembizi yakinifu, kiasi cha mashapo ilikadiriwa kuwa tani milioni 35.14 na uhai wa mgodi ulikadiriwa kuwa kati ya miaka 65 kuanzia mwaka 1988 kwa kasi ya uchimbaji wa tani 150,000 na 300,000 kwa mwaka. Hata hivyo, kampuni ya KCML haikuwahi kufikia makadirio haya kwani kiwango cha juu cha uzalishaji kilikuwa tani 80,000 tu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, *KCML* kama mashirika mengine ya umma iliwekwa kwenye mchakato wa kubinafsishwa kupitia *Government Notice No. 543* ya tarehe 22 August, 1997 kwa kuzingatia kifungu namba 48 cha *The Public Cooperation's Act*, Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992. Hadi *KCML* inabinafsishwa ilikuwa inajиidesha kwa hasara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na msimamo wa Serikali kwamba miradi yote iliyokuwa inapata msaada kutoka Serikali ya China, kipaumbele kipewe kampuni za Kichina pale miradi hiyo inapobinafsishwa, mwezi Aprili 1999 katika jitihada za kufufua mgodi huo, Serikali iliingia makubaliano na kampuni ya *China Hunan International*

Economic and Technical Cooperation Corporation (CHITEC) ambapo katika makubaliano hayo, CHITEC ingemiliki hisa asilimia 62 na Serikali asilimia 38 kwenye mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya CHITEC kufanya uchambuzi wa kina kuhusu mradi wa makaa ya mawe wa Kiwira na soko lake, walibaini kuwa mradi wa makaa ya mawe peke yake haukuwa na manufaa kibiashara, hivyo waliazimia kuunganisha na mradi wa kuzalisha umeme. Hata hivyo, mradi ulishindwa kusonga mbele kutokana na kukatishwa tamaa na TANESCO ambao, inasemakana wakati huo, walidai kuwa walikuwa na umeme wa ziada (*excess power*) na hawakuhitaji umeme kutoka mradi wa CHITEC na kusababisha kampuni hiyo kujitoa. Baada ya kampuni ya CHITEC kujitoa, Serikali iliamua kuubinafsisha mradi huu kwa wawekezaji binafsi katika mkakati wa kuukwamua.

Mheshimiwa Spika, wakati kampuni ya KCML inasajiliwa, ilikuwa na mtaji wa Shilingi milioni 30, yaani, hisa 30,000 zenyе thamani ya Shilingi 1,000 kila moja. Kampuni ilimilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 kupitia STAMICO na baadaye mwaka 1997 ilihamia kwa Msajili wa Hazina kupitia GN Na. 547/1997.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa serikali kubinafsisha KCML kwa kampuni ya *Tan-Power Resources Company Limited*. Kama nilivyoleza awali, kampuni ya KCML ambayo ilikuwa chini ya STAMICO, ilishindwa kujiendesha kwa faida kwa sababu ya uzalishaji wa chini wa makaa ya mawe wa kati ya tani 20,000 na 80,000 badala ya kiasi cha tani kati ya 150,000 na 300,000 kwa mwaka ambacho kilikuwa kimeainishwa kwenye upembuzi yakinifu ili kujiendesha kwa faida.

Mheshimiwa Spika, jitihada mbalimbali za kuukwamua mgodi wa KCML zilifanyika kwa muda mrefu na ilipofika tarehe 14 Februari 2005, Serikali iliamua kuongeza mtaji kwa njia ya kuingia ubia na kampuni binafsi bila kuathiri hisa za Serikali kwenye mradi huo (*Subscription and Joint Venture Agreement*).

Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Februari 2004 mtaji wa KCML uliongezeka kutoka Shilingi milioni 30 hadi Shilingi milioni 120, kati ya hizo hisa 90,000 zilihamishiwa kwa Msajili wa Hazina. Tarehe 16 Juni 2005 mtaji wa KCML uliongezwa kutoka Shilingi milioni 120 kufikia Shilingi bilioni 1. Tarehe 16 Desemba 2005 mtaji wa KCML uliongezeka tena kutoka Shilingi bilioni 1 na kufikia Shilingi bilioni 15, yaani, hisa 15,000,000 zenyе thamani ya Shilingi 1,000 kila hisa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Kampuni ya Tan-Power Resources Company Limited (TPR) ilinunua (*subscribed*) hisa 700,000 za KCML kwa bei ya Shilingi 1,000.00 kila hisa moja, sawa na asilimia 70 ya hisa zote na Serikali ilibakia na hisa 300,000 ikiwa ni asilimia 30 ya hisa zote. Malipo hayo yaligawanywa katika awamu mbili, Shilingi milioni 70 zililipwa mara baada ya kusaini mkataba, na salio la Shilingi 630,000,000 lililipwa baada ya TPR kuanza kuendesha mgodi chini ya jina la Kiwira Coal and Power Limited (KCPL).

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *TanPower Resources Company* ilisajiliwa na Msajili wa Makampuni tarehe 29 Desemba, 2004 na kupewa hati ya Usajili Na. 51080.

Mheshimiwa Spika, mtaji wakati kampuni inaanzishwa ulikuwa Shilingi bilioni 2, hisa za kampuni milioni 2 za Shilingi 1,000 kwa kila hisa. Tarehe 9 Julai, 2008 kampuni ya TPR iliongeza mtaji na kufikia Shilingi bilioni 15 na kuwa na hisa 15,000,000 za Shilingi 1,000 kila moja.

Mheshimiwa Spika, wakati kampuni ya *TPR* inaanzishwa wanahisa walikuwa wafuataao, hisa zao zikiwa kwenye mabano:-

1.	<i>ANBEN Limited</i>	(200,000)
2.	<i>DevConsult International Ltd .</i>	(200,000)
3.	<i>Universal Technologies Ltd.</i>	(200,000)
4.	<i>Choice Industries Ltd.</i>	(200,000)
5.	<i>Fosnik Enterprises Ltd.</i>	(200,000)

Mheshimiwa Spika, tarehe 10 Januari, 2005 (siku 13 tangu kuanzishwa kwa *TPR*) *ANBEN Limited* iliondolewa kuwa mionganii mwa wamiliki wa hisa kwa vile haikuweza kulipia hisa ilizokuwa imechukua wakati wa usajili wa TPR. Hivyo, wamiliki wa TPR waliobaki walikuwa ni *DevConsult International Ltd* (Hisa 200,000); *Universal Technologies Ltd* (Hisa 200,000); *Choice Industries Ltd* (Hisa 200,000); na *Fosnik Enterprises Ltd* (Hisa 200,000).

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa kuendeleza mradi wa Kiwira kati ya Serikali na kampuni ya KCPL uliingiwa tarehe 24 Machi 2006 kwa kutia saini makubaliano ya makusudio (*Agreement of Intent – AoI*) na mikataba ya Power Purchase Agreement (PPA); *Implementation Agreement (IA)*; *Escrow Agreement (EA)*; *Transmission Line Facilities Agreement (TLFA)*; na *Facility Transfer Agreement (FTS)* ilitiwa saini mwezi Agosti, 2006.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Kampuni ya KCPL kuendeleza mradi kati ya 2006 – 2008. Kama nilivyosema awali baada ya Serikali kubinafsisha KCML, Kampuni ya KCML ilibadilishwa jina na kuitwa KCPL kwa lengo la kuendeleza mradi iliyoubuni wa kuzalisha jumla ya megawati 400 za umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Kiwira kwa lengo la kuiuzia gridi ya taifa kuititia *TANESCO*.

Pamoja na mikataba iliyoingia na Serikali katika kutekeleza mradi huu, KCPL iliingia mikataba ya usanifu na ujenzi wa mitambo (*Engineering and Procurement Contract – EPC*) na kampuni za Shanghai *Electric Company (SEC)* na *COMPLANT* za China; na wa ujenzi wa njia ya kusafirirshia umeme *Transmission Line Contract* na kampuni ya KALPATARU ya India.

Mheshimiwa Spika, sambamba na maandalizi ya utekelezaji wa mradi mpya wa kuzalisha megawati 400 za umeme, *KCPL* pia ilitumia jumla ya Shillingi bilioni 3.9

kupata ushauri wa kitaalam wa kuwezesha mradi wa awali uliojumuisha uchimbaji wa makaa ya mawe kutoka mgodi wa chini na uzalishaji wa megawati 6 za umeme kwa kuagiza vipuri vya mgodi wa awali na mtambo wa kuzalishia umeme pamoja na kukarabati miundombinu ya juu kwa lengo la kuwezesha mradi wa awali kuzalisha kama ilivyokusudiwa katika upembuzi yakinifu na hivyo kuijendesha kwa faida.

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza mradi wa makaa ya mawe wa Kiwira, kampuni ya *KCPL* tayari imefanya matayarisho ya kupata na kujenga mitambo ya kuzalisha umeme kwa kufanya yafuatayo:-

Tathmini ya mazingira – *Environmental Impact Statement - EIS* kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha megawati 200 za umeme ilifanyika;

Upembuzi yakinifu kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha megawati 200 za umeme ulifanyika na mshauri wa kimataifa, ambayo ni kampuni ya PB Power; Kuingia mkatuba wa usanifu na ujenzi wa mitambo (*Engineering and Procurement Contract – EPC*) na kampuni za Shanghai *Electric Company* (SEC) na *COMPLANT* za China ambapo kampuni ya *COMPLANT* ndiyo ilikuwa mkandarasi katika ujenzi wa mgodi uliopo wa Kiwira;

Kulipa malipo ya awali ya jumla ya Dola za Marekani 6.0 million kwa mkandarasi ili aanze kazi. Usanifu na utengenezaji wa mitambo (turbines, generators na boilers) minne (4) ya umeme ya kuzalisha megawati hamsini (50) kila moja imeanza katika kampuni ya Shanghai *Electric company Limited* (SEC); na Kuchagua na kufanya usanifu wa eneo litakalojengwa mtambo wa kufua umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kujenga njia ya umeme, *KCPL* tayari imefanya yafuatayo:-

Kukamilika kwa usanifu wa njia ya umeme iliyopangwa ya Kiwira – Mwakibete ili kuunganisha kwenye gridi ya Taifa. Hata hivyo kufuatia mabadiliko ya sehemu ya kuunganika na gridi ya Taifa kutoka Mwakibete kuishia Uyole, KCPL ilitafuta washauri wengine kupanga tena njia mpya yaani, njia ya Kiwira – Uyole;

Kukamilika kwa tathmini ya mazingira – *Environmental Impact Statement - EIS*;

Kupatikana kwa Mkandarasi kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa njia ya umeme kuunganisha kwenye gridi ya Taifa;

Matayarisho kwa ajili ya fidia kwa watakaoathirika kutokana na kuhamishwa kupisha njia ya umeme; na

Kuanza kwa tathmini ya kijamii kuhusiana na kuhamisha makazi ya watu kupisha njia ya umeme.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha upanuzi wa mgodi na kuongeza uzalishaji wa makaa ya mawe ya kutosha uzalishaji wa megawati 200 za umeme za awamu ya kwanza ya mradi, kampuni ya KCPL imeishatekeleza yafuatayo:-

Kufanya tathmini ya mazingira (*environment audit*) kwenye mgodi wa awali;

Kufanya tathmini ya mazingira (*environmental study*) katika mgodi mpya wa wazi (open cast mine) unaotegemewa kuanzishwa kwenye eneo la Kabulo;

Mshauri wa Kimataifa aitwaye *Wardell Armstrong* kupewa kazi ya kufanya tathmini ya awali (*scoping study*) kwenye mgodi wa awali; upembuzi yakinifu (*feasibility study*) kwenye mgodi wa awali; na upembuzi yakinifu (*feasibility study*) kwenye mgodi mpya unaotarajiwa kuanzishwa; na

Zabuni ya kimataifa (*International Tender*) kwa ajili ya upanuzi wa mgodi wa awali - Kiwira Coal Mine imetangazwa na inatarajiwa kufunguliwa mwezi huu wa saba 2009.

Mheshimiwa Spika, maamuzi ya Serikali. Kwa kuwa kumekuwepo na kasoro katika uendeshaji wa mradi huu zilizosababisha hisia mbalimbali mionganoni mwa wananchi, na kwa kuwa hisia zilizoibuka kuhusu ubinafsishaji wa kampuni ya KCML zimeathiri sana mazingira ya kampuni kuweza kutekeleza na kutimiza malengo yake kama yalivyoainishwa kwenye mkataba na hivyo kuiathiri nchi (ikiwa ni pamoja na kushindwa kulipa mishahara ya wafanyakazi wapatao 500 kwa zaidi ya mwaka sasa inayofikia shilingi bilioni 1.5), hususan, sekta ya nishati, kwa mashauriano na Serikali, kampuni ya KCPL imeona ni busara irudishe mgodi wa Kiwira na mradi wa kuchimba makaa ya mawe na kuzalisha umeme Serikalini kwa makubaliano kwamba Serikali itarudisha gharama zilizotumiwa na KCPL endapo zitathibitika kuwa za kweli.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza mchakato wa kupata utaratibu muafaka wa kuendesha mradi kama ilivyokusudiwa kwa kuangalia fursa/njia (*options*) mbalimbali. Moja ya fursa hizo ni Serikali kuingia mkataba wa Uendeshaji “*Management Contract*” na kampuni itakayopewa mamlaka ya kujenga na kuendesha mradi huo. Chini ya mkataba wa uendeshaji Mkandarasi atapewa jukumu la kujenga uwezo wa mashirika ya STAMICO na TANESCO ili kuyawezesha kumiliki na kusimamia mradi.

Mheshimiwa Spika, hatua ya awali kabisa ni kwa Serikali kuhakikisha kuwa wafanyakazi waliopo wanalipwa haki zao zote na kuwawekea mazingira mazuri ya kuendelea na kazi kufuatia utekelezaji wa mradi kuanza.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imezungumza na Serikali rafiki ya watu wa China iliyoanzisha na kuendesha mradi huu ili kupata mkopo wa kufufua mradi huu na kuhakikisha mradi wa kuzalisha umeme wa MW 200 unakamilika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

NAIBU SPIKA: Ndiyo, nilikuwa nashangaa maana Kauli za Mawaziri, hatuzijadili labda litokee ombi maalum.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DR. LUKE J. SIYAME: Mwongozo wa Spika!

NAIBU SPIKA: Mwongozo wa Spika, Kifungu gani?

MHE. DR. LUKE J. SIYAME: Kanuni ya 68, Kifungu namba 7.

NAIBU SPIKA: Eleza, yenyewe inasema unaweza kusimama na kusema mwongozo wakati wowote. Sasa wewe unataka kupata mwongozo wa nini sasa?

MHE. DR. LUKE J. SYAME: Nataka kusema hivi, kwa kuwa m,wongozo wako kuhusu kuongeza muda wa kujadili bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis haukuweka wazi; na kwa kuwa kauli ya Serikali ya Serikali kuitia Wizara ya Nishati na Madini tayari imeishachukua muda wa kutosha; na kwa kuwa pia kutakuwa na muda wa kuwasilisha hii Miswada, Je, unaweza kutupa mwongozo wako ni namna gani tutafidia huu muda wa kujadili bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis?

NAIBU SPIKA: Unajua, na kuhusu utaratibu nayo inachukua muda! Waheshimiwa, nilisema hivi, mambo yetu sisi, mimi kama Naibu Spika hapa nikikaa hapa siwezi kuamua kwamba naongeza muda mpaka tarehe fulani, ndiyo maana nimewaambia suala hili tumelisikia. Lakini tuzingatie kwamba suala la ratiba yetu ilikuwa imepangwa toka tunaanza Kikao cha Bunge. Toka mwanzo, hakuna aliye-*call attention* ya Kiti kwamba tubadilishe. Kwa hiyo, nimesema siwezi kujibu hapa, na mimi hayo yote uliyosema naya-*consider*, lakini tuendelee na Waziri aendelee na shughuli wakati Kamati ya Uongozi itakapokaa na kufikiria nini kinaweza kufanyika ama hakiwezi kufanyika. Kwa hiyo, tunaendelea.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo wa Mwaka 2009 (The Constituencies Development Catalyst Fund Bill, 2009).

Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbali mbali wa Mwaka 2009 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2)Bill 2009),

Muswada wa Sheria ya Baraza la Usalama la Taifa wa Mwaka 2009 (The National Security Council Bill, 2009)

(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu Kuhusu

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu; baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningependa kuungana na wenzangu kuzipa pole familia za wenzetu marehemu Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa na Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba Wabunge wenzetu waliotangulia mbele ya haki katika mwaka wa fedha uliopita, 2008/2009. Aidha, natoa pole kwa familia na Watanzania wote kwa kifo cha mwanataaluma mashuhuri Profesa Haroub Othman na kifo cha Sheikh wetu Suleiman Gorogosi ambaye alikuwa Naibu Mufti wa Tanzania, Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. (*Amin*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mheshimiwa Lorensia Bukwimba kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Busanda na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Biharamulo Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Mawaziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, Mbunge wa Viti Maalum Mkao wa Mara na Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, Mbunge wa Viti Maalum Mkao wa Tanga, kwa kazi nzuri, ushirikiano, uaminifu na uadilifu waliouonesha kwangu.

Aidha, nawashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Profesa Hamisi Omar Dihenga, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Selestine Muhochi Gesimba pamoja na Kaimu Kamishna wa Elimu Ndugu Leonard Ryoba Musaroche, Wakurugenzi wa Idara zote, Viongozi wa Vyuo Vikuu, Mashirika na Mabaraza Chini ya Wizara, Walimu, Wahadhiri, Maprofesa na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu na katika maandalizi ya bajeti hii.

Napenda pia kutoa shukrani na pongozi kwa Mwenyekiti Prof. Mayunga Nkunya na Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Elimu la Taifa (*National Education Advisory Council*) kwa ushauri wao. Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru viongozi na wanachama wa vyama vyote vya wafanyakazi wilayani, mikoani na Makao Makuu kwa ushirikiano na ushauri wao katika kushughulikia masuala ya wafanyakazi. Ninaomba ushirikiano huo uendelezwe katika mwaka 2009/2010. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha na Uchumi kwa hotuba zao nzuri ambazo kwa pamoja zilitoa tathmini na mwelekeo wa Bajeti ya Serikali na hali ya uchumi na maendeleo kwa ujumla na utendaji wa kazi za Serikali na mwelekeo wake kwa mwaka 2009/2010. Kwa mwelekeo huo hotuba yangu itatoa ufanuzi wa Makadirio na Matumizi yanayohusu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii ambayo kwa sasa inasimamia Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Elimu ya Ualimu, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, Elimu ya Juu na Elimu ya Ufundii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omari Shaban Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, kwa kuchambua na kujadili utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2008/2009 na Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2009/2010. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu imezingatia mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati na itaendelea leo kupokea mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge ili kuongeza ufanisi na ubora wa elimu inayotolewa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kuishukuru familia yangu kwa upendo na msaada wa pekee katika kazi yangu. Aidha, napenda kuwashukuru wananchi wa jimbo langu la Mwanga kwa kuniunga mkono na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Ubunge na kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii unajumuisha Idara 9 ambazo ni Idara ya Elimu ya Msingi, Idara ya Elimu ya Sekondari, Idara ya Elimu ya Juu, Idara ya Elimu ya Ualimu, Idara ya Ukaguzi wa Shule, Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, Idara ya Elimu ya Ufundii na Mafunzo ya Ufundii Stadi, Idara ya Utawala na Rasilimali Watu na Idara ya Sera na Mipango.

Aidha, Aidha, Wizara inasimamia Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) na Baraza la Taifa la Kusimamia Elimu ya Ufundii (NACTE); Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii Stadi (VETA), Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (IAE), Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB), Kituo cha Maendeleo Dakawa, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na baadaye nitoe mwelekeo wa Mapato na Matumizi kwa mwaka 2009/2010.9.8. Katika mwaka 2008/2009 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ilipanga kukusanya maduhuli ya Serikali ya jumla ya Shilingi bilioni 3.574. Hadi kufikia Juni 2009, Shilingi bilioni 15.01 zilikusanywa na kuvuka lengo kwa asilimia 319.98. Hali hiyo ilitokana na Wizara kutoweka kwenye makisio yake kwa kutegemea kuwa ugatuaji wa Shule za Sekondari kwenda kwenye Halmashauri ungekuwa umekamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 480.475 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (*Recurrent Expenditure*). Kati ya hizo Mishahara (*PE*) ilikuwa Shilingi bilioni 273.504 na Matumizi Mengine (OC) Shilingi bilioni 206.971. Hadi Juni 2009, Mishahara ilikuwa Shilingi bilioni 272.912 (asilimia 99.78) na Matumizi Mengine, Shilingi bilioni 205.887 (asilimia 99.48). Jumla ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo) hadi Juni 2009 ilikuwa Shilingi bilioni 478.799 (asilimia 99.65).

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka 2008/2009 ilikuwa Shilingi bilioni 128.446. Matumizi hadi Juni, 2009 ni Shilingi bilioni 85.064 (asilimia 66.226). Kati ya hizo Shilingi bilioni 57.442 ni Fedha za Ndani na Shilingi bilioni 27.622 ni Fedha za Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo ya jumla ya utekelezaji wa Bajeti niliyoyatoa awali, sasa ifuatayo ni taarifa ya Utekelezaji kwa Ofisi ya Kamishna wa Elimu, kila Idara, na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Idara ya Utawala na Rasilimaliwater inasimamia masuala ya utawala, ajira, maslahi na maendeleo ya watumishi. Aidha, idara inasimamia sheria, kanuni, taratibu za utumishi na uratibu wa masuala ya Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2008/2009 Idara ya Utawala na Rasilimaliwater ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo wa Wizara katika muda mrefu na mfupi kwa watumishi;
- (b) Kutoa mafunzo ya OPRAS kwa watumishi 416 wa Makao Makuu;
- (c) Kuthibitisha kazini watumishi 201 na kuratibu upandishwaji vyeo wa walimu 6,592 na watumishi wasio walimu 124;
- (d) Kufanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja ili kuimarisha utoaji wa huduma;
- (e) Kuajiri watumishi wapya 3,241 kati yao walimu ni 3,217 na watumishi wasio walimu 24 na kutoa vibali 337 vya ajira za wataalamu wa kigeni;

(f) Kupitia muundo wa wizara kwa lengo la kuimarisha utendaji; na;

(g) Kukamilisha Rasimu ya kuhuisha Muundo wa Kada zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu na kuwasilishwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu ilikabiliwa na madeni makubwa ya ndani yaliyojumuisha madai ya walimu, wazabuni na posho za nyumba kwa wahadhiri wa vyuo vikuu. Katika mwaka 2008/2009 Serikali ilifanya marekebisho ya madaraja ya walimu na kulipa malimbikizo ya mishahara ya shilingi 7,564,230,962.91.

Aidha, hadi kufikia mwezi Machi 2009, Serikali ilipitia na kulipa madai 3,202 ya walimu yatokanayo na likizo, matibabu, mafunzo na uhamisho wa walimu wa shule za sekondari, Vyuo vya Ualimu na Ofisi za Ukaguzi wa Shule yenye thamani ya Shilingi 1,175,492,157.

Baada ya hatua hizo, Serikali ilituma timu za wataalamu kutembelea kila shule ya Sekondari ya Serikali, Chuo cha Ualimu na Ofisi zote za Ukaguzi wa Shule nchini na kuzungumza na mwalimu mmoja mmoja ili kupata madai yao. Kazi hiyo ilikamilika tarehe 15 Juni, 2009. Katika zoezi hili madai yaliyokusanywa kabla ya uhakiki yalifikia Shilingi bilioni 22.8. Madai hayo yamewasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa uhakiki kabla ya kuwasilishwa Hazina kwa malipo.

Hadi mwezi Machi 2008 madai ya wazabuni yanayotokana na utoaji wa huduma ya chakula katika shule za sekondari na vyuo vya ualimu yalifikia Shilingi bilioni 11.67. Aidha, madai ya wazabuni waliota huduma za vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya maabara na kemikali yalifikia Shilingi bilioni 3.89. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali ilihakiki madeni ya chakula ya hadi mwezi Machi 2008 na kuyalipa. Madeni ya chakula kuanzia mwezi Aprili hadi Desemba 2008 na madeni ya vifaa vya kufundishia yenye jumla ya Shilingi bilioni 17.69 yamehakikiwa na kuwasilishwa Hazina kwa malipo.

Aidha, Serikali ilitenga Shilingi bilioni 2.03 kila mwezi kuanzia Januari hadi Juni 2009 kwa ajili ya kulipia chakula cha wanafunzi moja kwa moja kwa lengo la kutoendelea kulimbikiza madeni.

Kuanzia mwaka 2005/2006 hadi 2008/2009, ulipaji wa stahili ya posho ya nyumba kwa Wahadhiri na Maprofesa wa Vyuo Vikuu vya Umma haukufanyika kikamilifu kutohana na fedha za matumizi mengineyo zinazotolewa kutokidhi mahitaji ya vyuo vikuu hivyo. Hii imesababisha malimbikizo ya posho ya nyumba kwa Wahadhiri. Katika mwaka 2008/2009 Serikali imelipa malimbikizo yote ya nyuma mpaka Juni 2009. Jumla ya Shilingi 17.05 bilioni zimelipwa katika zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Sera na Mipango inahusika na utoaji wa utaalamu na huduma katika utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 Idara ya Sera na Mipango ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kuratibu mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji ya mwaka 1996 na Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 na kuandaa Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo. Aidha, rasimu inayojumuisha Sera hizo iko tayari kupelekwa kwa wadau wa Elimu kwa ajili ya kupata maoni zaidi;

(b) Kuimarisha ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu na taarifa za elimu (*database*) kwenye Halmashauri 28 kwa majaribio, kununua kompyuta na vifaa vya mtandao, kutoa mafunzo ya kompyuta na “*database*” kwa maafisa vifaa na takwimu wa wilaya na wataalamu wa TEHAMA wa mikoa 14 kwa ushirikiano na *UNESCO*; na;

(c) kufanya mapitio ya matumizi ya fedha katika Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara na kuratibu Mpango wa kazi na Mtiririko wa Fedha za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Habari Elimu na Mawasiliano kina jukumu la kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu habari na mawasiliano na kushirikiana na vyombo vya habari na wadau wengine wa sekta ya elimu katika kuhamasisha ushiriki wa wananchi kutekeleza mipango ya maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutoa elimu kwa umma na kudumisha Utawala bora, uwazi na uwajibikaji, Wizara imeimarisha Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano ili kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu mawasiliano na kushirikisha vyombo vya habari na wadau wengine wa sekta ya elimu katika kuhamasisha ushiriki wa umma katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kuratibu utoaji wa taarifa 85 za maendeleo ya elimu kwa jamii na wadau na kuhamasisha ushiriki wao;

(b) Kuandaa na kutoa matangazo 10 na vipindi 30 vya televisheni na redio kueleza sera na mikakati ya utekelezaji wa mipango ya elimu;

(c) Kuandaa, kuchapa na kusambaza kalenda 50,000 kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa MMEM; na;

(d) Kuandaa na kuchapa nakala 100,000 za Jarida la Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Ed-SDP) na kusambaza kwa wadau katika kanda za elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu kwa ufanisi, Wizara inayo Ofisi ya Kamishna wa Elimu yenye jukumu la kuratibu utoaji wa elimu katika ngazi ya Awali, Msingi, Elimu ya Sekondari, Mafunzo ya Ualimu na Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi. Majukumu hayo ni pamoja na Udhibiti wa ubora wa Elimu, Ukuzaji Mitaala, Uendeshaji Mitihani, Huduma za Maktaba na Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Ofisi ya Kamishna wa Elimu ilitekeleza yafuatayo:-

- (a)Kukamilisha Andiko la Mpango Mkakati wa kupanua na kuimarisha Elimu Maalumu na Elimu Jumuishi;
- (b)Kununua na kusambaza vifaa vyenye thamani ya Shilingi milioni 773.394 vya kufundishia na kujifunzia; na visaidizi katika shule zinazotoa Elimu Maalumu ambazo ni shule za Msingi 228 na shule za Sekondari 24;
- (c)Kusajili Shule 242 za Serikali za sekondari zilizojengwa kwa nguvu za wananchi, shule 132 zisizo za Serikali zikiwemo za Awali 5, Awali na Msingi 61, Sekondari 59 na Vyuo vya Ualimu 7;
- (d)Kuchambua kwa kina taarifa ya utafiti wa Kimataifa kuhusu ubora wa Elimu katika Nchi 15 za Kusini na Mashariki ya Afrika (*SACMEQ Research Project III*);
- (e)Kutoa Leseni 315 za kufundisha kwa wahitimu mbalimbali walioomba kufundisha: Shahada ya Uzamili 65, Shahada ya kwanza 180, Stashahada 39, Cheti cha Ualimu 7 na Kidato cha Sita 24;
- (f)Kugharimia Mafunzo ya Ushauri na Unasihi kwa Wawezeshaji 200 wa Shule za Msingi na walimu wapya 200 wa Shule za Sekondari katika kanda ya ziwa na ya Kati;
- (g) Kutoa mafunzo kwa walimu 76 na wakaguzi wa shule 24 kuhusu Elimu ya Mazingira kwa Maendeleo Endelevu na Utumiaji wa Mwongozo wa Kufundisha Elimu ya Mazingira kwa Shule za Msingi;
- (h) Kutoa mafunzo ya Elimu Rika na Unasihi kwa walimu 300 wanaofundisha masomo yenye mada za Elimu ya UKIMWI;
- (i) Kutayarisha na kutangaza vipindi 52 vya ‘Boresha Elimu’, na vipindi 52 vya Mbinu Shirikishi za Ufundishaji, vipindi 456 vya masomo ya English, Sayansi, Kiswahili Darasa la V, VI na VII; Historia Jiografia na Uraia Darasa la III, IV na V; na Maarifa ya Jamii Darasa la VI na VII; na kutayarisha vielelezo vya picha 50 za TV (VIDEO CLIPS) kwa ajili ya masomo ya sayansi na Hisabati darasa la V na VI;
- (j) Kuandaa Mwongozo wa Elimu Rika kwa shule za sekondari Kidato cha 3 na 4;

(k) Kuratibu uendeshaji wa mitihani ya Taifa ya Darasa la VII, Kidato cha 4, 6 pamoja na Cheti na Stashahada ya Ualimu, (Kielelezo cha 3 kinatoa muhtasari wa matokeo hayo);

(l)Kuratibu maoni na mapendekezo ya kuzuia mimba shulen ikiwa ni pamoja na adhabu kwa wanaowapa mimba wanafunzi na uwezekano wa kuwarejesha shulen baada ya kujifungua wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wanaopata ujauzito; na

(m)Kutoa mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa elimu katika ngazi mbalimbali za elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, wanafunzi wa Elimu ya Awali wa shule za Serikali na zisizo za Serikali wameongezeka kutoka 638,591 mwaka 2005 (wasichana ni 319,974) na kufikia 896,146 (wasichana 450,279 au 50.25%) mwaka 2009 wakiwemo wanafunzi 2,208 wenye mahitaji maalumu.

Wanafunzi wa Elimu ya Msingi wameongezeka kutoka 7,541,208 (wasichana 3,685,496) mwaka 2005 kufikia 8,441,553 (wasichana 4,192,789) mwaka 2009 wakiwemo wanafunzi 27,422 wenye mahitaji maalumu. Walimu wa Elimu ya Awali wameongezeka kutoka 11,148 mwaka 2005 kufikia 17,176 (wanawake 10,477) 2009, Walimu wa Elimu ya Msingi wameongezeka kutoka 135,013 (wanawake 64,707) mwaka 2005 kufikia 153,724 (wanawake 75,534) mwaka 2009. Aidha, idadi ya mikondo ya Elimu ya Awali imeongezeka kutoka 21,607 mwaka 2005 kufikia 41,154 mwaka 2009 na Shule za Msingi zimeongezeka kutoka 14,257 mwaka 2005 kufikia 15,727 mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II) ilianza mwaka 2007 na inatarajiwu kumalizika mwaka 2011. Malengo ya mpango huo ni kuendelea kuimarisha uandikishaji; kuinua ubora wa elimu; kujenga uwezo wa watendaji; kuimarisha taratibu za kitaasisi; kuimarisha elimu ya masuala mtambuka na kufanya ufuatiliaji, tathmini, mapitio na utafiti katika Elimu ya Awali na Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kutekeleza awamu ya pili ya MMEM (2007-2011) kwa lengo la kuhakikisha azma ya serikali ya kutoa elimu ya Awali na Msingi kwa wote inafikiwa. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ilitekeleza yafuatayo:-

(a) kufuatilia uandikishaji wa wanafunzi 824,791 katika Elimu ya Awali wenye umri wa miaka 5 – 6 na wanafunzi 1,166,017 wa Darasa la kwanza ambapo wanafunzi 896,146 wameandikishwa katika Elimu ya Awali na 1,358,790 wameandikishwa Darasa la kwanza;

(b) Kufuatilia matumizi ya ruzuku ya uendeshaji kwa ajili ya ununuzi wa a mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia katika Halmashauri na Shule. Shilingi 45,507,836,450 zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa vitabu, ukarabati wa madarasa na miundombinu mingine, mitihani ya ndani na kuendesha shughuli za utawala;

(c) Kukamilisha miundombinu ya madarasa na nyumba za walimu zilizokuwa katika hatua mbalimbali za ujenzi ambapo jumla ya shilingi bilioni 5 zilitumwa kwenye Halmashauri kwa kazi hiyo. Aidha, Wizara ilitumia shilingi 387,500,000 katika ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa samani kwa shule ya Arusha (Arusha School) na shule zilizo chini ya vyuo vya ualimu Ilonga, Kitangali, Mhonda na Tabora.

(d) Kufuatilia wanafunzi wa MEMKWA kundi-rika la kwanza ili kuingiza kundi hilo kwenye mfumo rasmi wa Elimu ya Msingi ambapo wanafunzi 10,582 (wasichana 4,086) wameingizwa katika mfumo rasmi (darasa la V) mwaka 2009. Aidha, matokeo yalibaini kuwa wanafunzi wa MEMKWA wanaendelea kuandikishwa na kusoma katika madarasa ya MEMKWA;

(e) Kuimarisha vituo vya walimu kwa kuvinunulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vitabu, vibao vya mwandiko, vivunge vya sayansi na modeli za mwili wa binadamu vyenye thamani ya shilingi 8,500,071,000 na kusambazwa kwenye mikoa 14 yenye maeneo ambayo hayakufanya vizuri katika mtihani wa Darasa la Saba mwaka 2008. Mikoa hiyo ni Dodoma, Singida, Kilimanjaro, Tanga, Ruvuma, Rukwa, Mwanza, Kagera, Mara, Kigoma, Lindi, Mtwara, Shinyanga na Pwani;

(f) Kuchapa nakala 240,000 za miongozo ya MMEM II na kuisambaza;

(g) Kufanya tathmini ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi ambayo ilibainisha kuwa asilimia 69 (Hisabati) na 54.7 (English) ya sampuli ya wanafunzi 700 walikosa maswali yote ya mitihani hiyo. Aidha, katika masomo hayo mada zenye matatizo ya ufundishaji zimebainishwa. Baadhi ya mada zenye matatizo katika Hisabati ni Algebra, Mafumbo na Jometri; na kwa English ni *Composition, Tenses, Comprehension na Vocabulary*.

Mafunzo kwa walimu wawezeshaji 30 kwa kila Halmashauri yameandaliwa ili kuwaimarisha walimu katika maeneo hayo. Aidha, tathmini ya Mtihani wa Darasa la IV kwa mwaka 2008, imeonesha kuwa ufaulu umepanda kutoka asilimia 78.5 (2007) hadi asilimia 85.1 (2008). Hata hivyo, maeneo yenye matatizo ya ufundishaji yamebainishwa na maelekezo ya utoaji mafunzo rekebishi kwa wanafunzi wasiofikia viwango vya ufaulu yametolewa;

(h) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Shule Zenye Mazingira Yanayomjali Mtoto katika Halmashauri za Hai, Magu, Bagamoyo, Mtwara (V) na Temeke kwa kushirikiana na UNICEF. Ufuatiliaji huo umeonyesha kuwa uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi ni kati ya 1:3 na 1:8 hasa kwa masomo ya mtaala uliorekebishwa, kamati za shule ni hai bali mikutano ya mabaraza ya wanafunzi haifanyiki mara kwa mara; uhaba wa madarasa, nyumba za walimu na vyoo;

(i)Kununua na kusambaza vifaa vyta kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenyewe ulemavu vyenye thamani ya shilingi 966,980,065;

(j)Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mradi wa Lishe Shulen. Ufuatiliaji ulifanyika katika Halmashauri 13 zinazotekeleza Mradi huu ambazo ni Bahi, Longido, Karatu, Simanjiro, Kiteto, Ngorongoro, Mpwapwa, Singida (V) na Monduli;

(k)Kutekeleza mradi wa BridgeIt ikiwa ni pamoja na kuweka vifaa vyta TEHAMA vikiwemo simu na televisheni katika shule 150 toka Halmashauri 17 za mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Kilimanjaro, Dodoma, Tanga na Mtwara katika shule za msingi pamoja na kutekeleza hatua ya majoribio ya ufundishaji kwa kutumia TEHAMA. Njia hii imeonesha mafanikio kwani inawezesha kuhudumia wanafunzi wengi kwa wakati mmoja, kuvutia na kurahisisha uelewa wa maudhui ya masomo. Awamu ya kwanza ya mradi itakamilika Septemba 2009. Katika Awamu ya Pili, shule zisizo na nishati ya umeme zitajumuishwa kwa kutumia nishati mbadala. Ili kujenga umiliki (*ownership*) na uendelevu (sustainability) awamu ya pili itahusisha zaidi watendaji wa elimu wakiwemo viongozi wasimamizi wa walimu wa darasani; na;

(l)Kuimarisha michezo shulen kwa kujenga uwezo wa wawezeshaji ili kufundisha walimu wa michezo kwa kushirikiana na *Right to Play* na Serikali ya Ujeruman. Aidha, Wizara ilifuatilia utekelezaji wa mtaala wa michezo ambapo jumla ya walimu 148 kutoka mikoa ya Kigoma, Mara, Morogoro na Dar es Salaam wamepatiwa mafunzo ya ukocha na walimu 112 kutoka mikoa ya Morogoro, Ruvuma, Arusha na Mbeya walipatiwa mafunzo ya mchezo wa riadha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Sekondari ni kiungo muhimu kati ya Elimu ya Msingi na Elimu ya Juu. Idara inasimamia uendeshaji na uratibu wa utoaji elimu kuanzia kidato 1 – 6 kwa usawa katika jamii, kuongeza ubora wa elimu na kuimarisha uongozi na usimamizi wa shule katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, wanafunzi wa elimu ya sekondari kidato 1-6 wa shule za Serikali na zisizo za serikali wameongezeka kutoka 524,325 mwaka 2005 (wasichana 244,571) kufikia 1,466,402 mwaka 2009 (wasichana 653,457). Wanafunzi waliojiunga na kidato 1 wameongezeka kutoka 180,239 mwaka 2005 (wasichana 88,559) kufikia 524,784 mwaka 2009 (wasichana 234,088). Aidha, wanafunzi waliojiunga na Kidato cha 5 watakaoingia Kidato cha 6 baadaye wameongezeka kutoka 18,893 mwaka 2005 (wasichana 7,147 sawa na 37.83%) kufikia 43,052 mwaka 2009 (wasichana 17,870 sawa na 41.51%). Walimu wa shule za sekondari wameongezeka kutoka 18,754 mwaka 2005 kufikia 33,954 mwaka 2009. Hata hivyo, mahitaji halisi ya walimu wa sekondari ni makubwa zaidi. Changamoto hii inatokana na ongezeko kubwa sana la shule za sekondari katika kipindi cha miaka 4 cha Serikali ya Awamu ya Nne. Katika kipindi hicho idadi ya shule za sekondari nchini zimeongezeka kutoka shule 1,745 mwaka 2005 kufikia shule 4,102 mwaka 2009. Serikali imechukua hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo hili kama ilivyoelezwa chini ya Idara ya Ualimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) 2004-2009 ili kwenda sanjari na kasi ya uandikishaji na ongezeko la ufaulu uliotokana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM).

Wizara yangu ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) utakaozingatia changamoto zinazotokana na utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya MMES zikiwemo ukamilishaji wa madarasa, kujenga maabara, nyumba za walimu na uanzishwaji wa TEHAMA kama chombo muhimu cha kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kugharimia elimu ya sekondari kwa wanafunzi 11,895 wanaotoka katika familia zenye kipato duni na yatima ambapo Shilingi bilioni moja zilitumika;
- (b) kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 1.8 kuchangia ujenzi wa madarasa 180 ya Kidato cha 5 na 6;
- (c) kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 8.8 kuchangia ujenzi wa nyumba 678 za walimu;
- (d) kutoa ruzuku ya Shilingi bilioni 7.38 kuchangia ujenzi wa maabara 187 kwenye shule za kidato cha 5 - 6;
- (e) Kutoa ruzuku ya Shilingi 3,965,477,360 kwa ajili ya kununulia vifaa vya maabara, maktaba na zana za kufundishia na kujifunzia kwa shule 3,174 za sekondari za Serikali;
- (f) Kutoa fedha za kununua vifaa kwa wanafunzi wa elimu maalumu katika shule 3 kwa gharama ya Shilingi 30,000,000;
- (g) Kugharimia vitabu kwa walimu 500 wanaojiendeleza katika Chuo Kikuu Huria, walimu 71 katika Chuo Kikuu Tumaini na walimu 10 wanaosoma shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (h) Kugharimia matengenezo madogomadogo katika shule 14 za Kidato cha 5-6 ambazo ni Kishoju, Moshi Sekondari, Mara, Iyunga, Kilosa, Ifakara, Bwiru Wavulana, Geita, Kantalamba, Kigonsera, Songea Wavulana, Mwenge, Tabora Wavulana na Usagara kwa gharama ya Shilingi milioni 190; na kuzipelekea shule mpya 13 za kidato cha 5-6 fedha kiasi cha shilingi milioni 10 kila moja kwa ajili ya kununulia vifaa vya kufundishia

na kujifunzia. Shule hizo ni Vudo, Nyerere, Ilaje, Kiwanja, Mwanzi, Ilula, Kisarika, Lukole, Mkugwa, Maji ya Chai, Londoni, Msamala na Kabanga;

- (i) Kupeleka jumla ya shilingi 1,603,136,484 katika shule za Serikali za kutwa zikiwa ni fidia ya ada kwa wanafunzi 994,699
- (j) Kuratibu na kukamilisha uhakiki wa awamu ya pili ya madai ya wazabuni wa chakula na vifaa vya kufundishia na kujifunzia; na;
- (k) Kukamilisha andiko kwa ajili ya ukarabati wa shule 89 za sekondari za bweni na Andiko la mradi wa kujenga maabara ya sayansi katika shule zote za sekondari nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI imeshughulikia suala la ugatuaji wa usimamizi na uendeshaji wa shule za sekondari kwenda kwenye Halmashauri kwa kufanya yafuatayo:-

- (a) kuandaa na kukamilisha andiko la mapendekezo la makabidhiano;
- (b) kuandaa ofisi na kuteua Maafisa Elimu wa Elimu ya sekondari katika Halmashauri;
- (c) kutoa taarifa kwa umma kuhusu utoaji wa huduma kwa watumishi wa shule za sekondari kwenda Halmashauri;
- (d) kuandaa na kupeleka miongozo ya uhamisho wa wanafunzi wa shule za sekondari;
- (e) kukusanya takwimu za walimu na kukabidhi majalada ya shule kwa Wakurugenzi wa Halmashauri; na
- (f) kuteua wakuu wa shule kujaza nafasi za Wakuu wa shule walioteuliwa kuwa Maafisa Elimu wa Elimu ya sekondari katika Halmashauri.

Aidha, kuanzia mwaka 2009/2010 wizara yangu itashughulikia zaidi masuala ya uandaaji wa sera, mitaala, kuweka viwango, usimamizi wa ubora wa elimu itolewayo na kufanya ufuutiliaji na tathmini. Kwa uelekeo huo, wizara yangu itaimarisha shughuli za mafunzo na maandalizi ya walimu, ufuutiliaji, ukaguzi na uandaaji wa mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Ualimu ina jukumu la kuratibu utoaji wa Elimu ya Ualimu ngazi ya Cheti na ngazi ya Stashahada, kutoa na kupitia Sera, Miongozo na Viwango vya Elimu ya Ualimu na kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa

Maendeleo ya Elimu ya Ualimu (*Teacher Development and Management Strategy - TDMS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafunzo ya Ualimu ya Daraja A na Stashahada hutolewa katika vyuo vya ualimu 34 vya Serikali ambavyo vina uwezo wa kudahili wanachuo 17,113 na na vyuo vya ualimu 43 visivyo vya Serikali vyenye uwezo wa kudahili wanachuo 5,169. Hivyo kwa pamoja tumedahili wanachuo 22,282 kwa wakati mmoja. Mafunzo ya ualimu ngazi ya Shahada ya ualimu hutolewa na baadhi ya vyuo vikuu. Vyuo vikuu hivyo ni Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), *State University of Zanzibar (SUZA)*, *Muslim University of Morogoro (MUM)*, *Mwenge University College of Education (MWUCE)*, *St. Augustine University of Tanzania (SAUT)*, Teofilo Kisanji University (TEKU), Sebastian Kolowa University College (SEKUCO) na Tumaini University. Aidha, *Mount Meru University of Arusha (MMU)* hutoa Elimu ya Ualimu katika ngazi ya Stashahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 Idara ya Ualimu ilikamilisha kazi zifuatazo:-

- (a) Kutoa mafunzo ya Ualimu kwa wanachuo 12,784 wa ngazi ya cheti Daraja A na 14,095 wa Stashahada;
- (b) Kutoa mafunzo kwa walimu 4,000 wa Daraja B/C ili kufikia Daraja A kwa njia ya masafa. Walimu hao walifanya mitihani ya kuhitimu mafunzo hayo Mei, 2009;
- (c) Kutoa mafunzo kwa wakufunzi 102 kuhusu mbinu za ufundishaji bainifu;
- (d) Kuhamasisha Wadau wa Elimu kuongeza ujenzi wa Vyuo vya Ualimu vya sekta binafsi;
- (e) Kutoa mafunzo ya awali kwa wakufunzi 80 na kuanza kutumia TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia (*online teaching and learning*) katika Vyuo vya Ualimu 31 na kukamilisha kufunga mtandao katika vyuo vya Shinyanga na Dakawa. Aidha, vyuo vya ualimu vya Ndala, Tandala, Kasulu na Kabanga tayari vimefungiwa umeme wa nishati ya jua (*Solar energy*);
- (f) Kuanza utekelezaji wa baadhi ya shughuli zilizopo katika Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Walimu (*Teacher Development and Management Strategy – TDMS*). Hii ni pamoja na kujenga uwezo wa kufundisha na kujifunza kwa walimu na kutoa mafunzo kabilishi kwa Viongozi Wakuu 62 wa Wizara;

- (g) kuridhia mkataba wa makubaliano kati ya Shirika lisilo la Kiserikali liitwalo Liike la nchini Finland wa kuendeleza michezo katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali;
- (h) kutoa mafunzo ya ufundishaji bora wa Elimu ya Awali kwa walimu 140 kutoka Halmashauri 7 za majoribio Mtwara Vijijini, Makete, Bagamoyo, Temeke, Hai, Siha na Magu;
- (i) kufanya utafiti na kuandaa Mkakati wa Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya elimu ya msingi (*In-Service Training Strategy*);
- (j) kuendesha mjadala kwa kushirikiana na UNESCO katika mradi wa UNESCO–Teacher Training Initiative in Sub-Saharan Africa kuhusu njia bora za kufundishia na kujifunzia kwa walimu na wanafunzi;
- (k) kutoa Mafunzo ya Mbinu za Ufundishaji Bainifu na Elimu ya UKIMWI kwa wakufunzi 36, walimu wa shule za Msingi 190 na Walimu wa Shule za Sekondari 40 wa Mkoa wa Kigoma chini ya Mpango unaogharimiwa kwa pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa (*One UN Joint Programme*);
- (l) kufuatilia mafunzo kwa vitendo kwa wanachuo 5,539 wa Stashahada; na;
- (m) kuratibu utekelezaji wa Mpango wa TEHAMA ambapo vyuo 32 kati ya 34 vya Ualimu vya serikali vimeunganishwa kwenye mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi inabuni, inasimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Serikali imeongeza nafasi na ubora wa mafunzo ambapo vyuo vya ufundi stadi vimeongezeka kutoka 819 mwaka 2005 hadi kufikia 889 mwaka 2008. Katika kipindi hicho (2005-2008) idadi ya wanafunzi wanaosomea mafunzo ya ufundi stadi imeongezeka kutoka 79,031 (wasichana 35,564) kufikia 114,295 (wasichana 43,568). Idadi ya vyuo vya Elimu ya Ufundi vinavyotoa elimu katika ngazi ya Cheti, Stashahada, Stashahada ya Juu na Shahada ni 195 (Katika kuimarisha ubora wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo, Idara imeratibu uanzishaji wa mafunzo yanayozingatia umahiri (*Competence Based*) katika vyuo vya ufundi nchini. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha vyuo vya Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilitekeleza yafuatayo: -

- (a) Kudhamini wanafunzi 600 wa mafunzo ya Ufundi Sanifu katika Chuo cha Ufundi Arusha kwa gharama ya Shilingi milioni 360;

- (b) Ili kupanua mafunzo ya uhandisi, ufundi na teknolojia nchini, Serikali imeamua kuanzisha mafunzo kwa ngazi ya stashahada ya ufundi na teknolojia katika vyuo vya VETA vya mikoa. Katika mwaka 2008/2009 Serikali ilifanya tathimini ya hali halisi ya rasilimali katika vyuo vya ufundi stadi vya mikoa 4 (Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro na Mtwara) kwa lengo la kuviwezesha kutoa mafunzo ya ufundi ngazi ya Stashahada;
- (c) Kuratibu mchakato wa ujenzi wa chuo cha ufundi cha wilaya ya Makete utakaogharimu Shilingi bilioni 3 na ukarabati wa vyuo vya wilaya za Karagwe, Korogwe na Mwanga;
- (d) Kuratibu uchambuzi wa mahitaji ya stadi katika wilaya 6 ambazo ni Geita, Longido, Siha, Bagamoyo, Ludewa na Makete;
- (e) Kudhamini watumishi 2 wa Idara katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili;
- (f) Kukamilisha Andiko la Mradi wa Maendeleo wa Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi katika kila wilaya. Awamu ya kwanza ya vyuo hivyo katika wilaya 28 za Tanzania ipo katika majadiliano na wahisani;
- (g) Kufanya utambuzi wa upungufu (*gaps*) uliopo kati ya ngazi ya III na IV katika program za vyuo vya ufundi stadi zinazohusu uhandisi, teknolojia na sayansi husika (*engineering, technology and related sciences*) ili kuwezesha wahitimu wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi kupata sifa za kuendelea na mafunzo ya ngazi sanifu;
- (h) Kuandaa hadidu za rejea za kumpata Mtaalamu Mwelekezi wa kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (MMEU); na;
- (i) Kuimarisha uhusiano na Serikali ya Canada wa kuendeleza mafunzo ya ufundi na ufundi stadi katika sekta ya madini, kilimo na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Juu ina jukumu la kutunga, kusimamia na kutathmini Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utoaji wa Elimu ya Juu katika vyuo vikuu vyetu. Idadi ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki vya Serikali ni 11 na visivyo vya Serikali imefikia 20 katika mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za msingi zinazofanywa na Vyuo vikuu ni kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Serikali na wananchi kwa ujumla. Katika mwaka 2008/2009, jumla ya wanafunzi 22,350 wanatarajia kumaliza masomo yao ya shahada ya kwanza kwenye vyuo vikuu nchini. Wahitimu hao ambaeo ni wataalamu wa fani mbalimbali wanatarajiwa kuingia kwenye soko la ajira kuanzia mwezi Agosti 2009.

Tafiti zinazofanywa na watafiti vyuoni zimekuwa na manufaa sana kwa kuvipandisha hadhi vyuo vikuu vyetu kitaaluma, kusaidia wananchi kupambana na umaskini pamoja na kuongeza uzalishaji viwandani na mashambani. Aidha, katika mwaka 2009 vyuo vikuu vya Dar es Salaam na Sokoine vimeendelea kushika nafasi za juu za ubora wa vyuo vikuu barani Afrika, Afrika Mashariki na Afrika ya Kati. Kwa upande wa vyuo vikuu vya Afrika Mashariki na Kati Chuo kikuu cha Dar es salaam kimekuwa cha kwanza na chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimekuwa cha nne. Hii imetokana na wahadhiri wengi kufanya tafiti nyingi na kuchapisha matokeo yake kwenye majarida na machapisho ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Sheria ya vyuo vikuu ya mwaka 2005, kila chuo kinatakiwa kuwa na hati idhini. Nafurahi kukufahamisha kuwa mpaka sasa vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki 12 vimeshapata Hati Idhini na vinaongozwa kwa kutumia Kanuni na Miongozo ya Hati Idhini zao. Aidha, nichukue nafasi hii kuvipongeza vyuo vikuu vingine vitano ambavyo vimepata Hati Idhini hivi karibuni baada ya kutunukiwa idhini zao na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vyuo Vikuu hivyo ni Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohane, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Chuo Kikuu cha Tumaini cha Stephano Moshi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara na Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba na Sayansi za Afya cha Weil Bugando.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vikuu vya umma vinafanya kazi kubwa sana ya kutatua tatizo la uhaba wa walimu katika shule zetu za sekondari. Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam na Dodoma vimeongeza sana udahili wa walimu. Udhili wa walimu umeendelea kuongezeka katika vyuo vikuu vishiriki vya Elimu vya Dar es Salaam na Mkwawa.

Pamoja na juhud hizi, vyuo vikuu 10 visivyo vya Serikali yaani University College of Education Zanzibar, Tumaini University Makumira College, Muslimu University of Morogoro, Mwenge University College, St. Augustine University of Tanzania, St. John's University, Sebastian Kolowa University College, Tumaini University Iringa College, Teofilo Kisanji University na University of Arusha vinafanya kazi kubwa ya kusomesha walimu.

Mheshimiwa Spika Katika mwaka 2007/2008 jumla ya walimu 2,843 walihitimu; na katika mwaka 2008/2009 walimu 5,331 wanatarajiwa kuhitimu. Vyuo vikuu visivyo na fani ya ualimu vimehamasishwa kuanzisha vitivo au program za shahada ya elimu na ualimu ambapo Vyuo Vikuu vya Sokoine na Mzumbe vimeanzisha shahada hiyo katika mwaka 2008/2009 na kudahili wanafunzi 153 (Sokoine) na 77 (Mzumbe). Chuo Kikuu Huria kinaendeleza walimu wa leseni 637 walioajiriwa katika programu maalum ili kupata shahada ya elimu baada ya miaka mitatu. Chuo Kikuu Huria kina vituo katika mikoa yote. Aidha, katika kujiimarisha kinamiliki majengo kwenye miji ya Iringa, Mbeya, Songea, Singida, Dodoma na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 Idara ya Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kudhamini wanafunzi 1,532 wa Shahada ya Kwanza ya Udaktari, wakiwemo 16 wa Udaktari wa Meno na 25 Udaktari wa Tiba ya Mifugo;
- (b) kudhamini wanafunzi 82 raia wa Uganda katika utaratibu wa kubadilishana wanafunzi wa Shahada ya Kwanza katika Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Ardhi, Muhimbili na Sokoine;
- (c) kudhamini wanafunzi 4 raia wa China ikiwa ni kutekeleza Mkataba wa Ushirikiano kati ya Tanzania na China katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (d) kudhamini mafunzo ya Shahada za Juu kwa wanataluma 64 wa Shahada ya Uzamili na 16 Uzamivu katika Vyuo Vikuu vya Umma;
- (e) kushiriki kwenye maonyesho ya Taasisi za Elimu ya Juu na wiki ya Utumishi wa Umma pamoja na mahojiano kwenye vyombo vya habari;
- (f) kuratibu uteuzi wa wanafunzi 75 wanaosoma nchini Urusi kwa utaratibu wa mkopo katika Chuo Kikuu cha Urafiki Lumumba;
- (g) kuratibu uteuzi wa wanafunzi 104 kwa ajili ya nafasi zilizotolewa na nchi rafiki ambazo ni Algeria (42), China (22), Cuba (24), Urusi (4), Uingereza (10), Uturuki (1) na Czeck (1);
- (h) kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Sayansi na Teknolojia ya Elimu ya Juu (*Science Technology and Higher Education Project*) unaolenga kuimarisha na kuboresha mazingira ya ufundishaji wa sayansi na teknolojia pamoja na ualimu katika Taasisi za Elimu ya Juu;
- (i) Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu (MMEJU) 2010 - 2015;
- (j) Kuratibu utekelezaji wa mkataba kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Serikali ya Ufaransa wa kufundisha lugha ya Kifaransa kwa shule 3 za Sekondari na vyuo 3 vya ualimu pamoja na kuwasomesha walimu lugha ya kifaransa kwa ngazi za uzamili; na
- (k) Kutayarisha mahitaji ya ukarabati wa miundombinu ya Taasisi na Vyuo Vikuu vya Umma; na
- (l) Wizara ilipokea msaada wa scholarship kwa watoto wa kike 100 wanaotoka kwenye familia maskini kutoka shirika la Shirin Pandu Merali Foundation la California, Marekani ili kufadhili masomo ya shahada ya kwanza na shahada za uzamili hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu sasa, pamekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi wa vyuo vikuu kuhusu mafao na pensheni duni wanayolipwa wastaaifu. Kwa mwaka 2008/2009 Wizara iliunda kikosi kazi kuchambua mfumo wa pensheni na mafao ya uzeeni na kutoa mapendekezo. Hivi sasa Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana zinayafanya kazi mapendekezo hayo ili yaanze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inazingatia sera ya uchangiaji katika kugharimia elimu ya juu. Sera hii inawashirikisha wanaonufaika na elimu ya juu kuchangia gharama za elimu kulingana na hali ya uwezo kama inavyobainishwa katika mfumo wa kutambua uwezo wa kiuchumi wa wanafunzi na mzazi au mlezi wake. Kwa Watanzania walio na uwezo wa kiuchumi, sera inasisitiza kuwa wanapaswa kulipia gharama za elimu ya juu ya watoto wao kulingana na uwezo wao. Kwa wale wenye uwezo mdogo, Serikali huwasaidia kwa kuwapatia mkopo kupitia Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Sera hii imewezesha watanzania wengi kunufaika na elimu ya juu kwa kupata mikopo kama ifuatavyo: Mwaka 2005/06 wanafunzi 42,729 walikopeshwa jumla ya Shilingi bilioni 56.2, mwaka 2006/2007 wanafunzi 47,554 walikopeshwa Shilingi bilioni 76.2, mwaka 2007/2008 wanafunzi 55,687 walikopeshwa Shilingi bilioni 112.5 na mwaka 2008/2009 wanafunzi 58,841 walikopeshwa Shilingi bilioni 140.3;

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vikuu vya umma vinakabiliwa na uchakavu na upungufu wa miundombinu ya maabara, vyumba vya miyahdara, ofisi za wafanyakazi, mabweni ya wanafunzi, maktaba, vitabu na majorida mbalimbali na matumizi ya ICT. Ili kuanza kukabiliana na baadhi ya matatizo haya, Serikali ilizindua mradi wa kuboresha ufundishaji wa Sayansi na Teknolojia katika vyuo vikuu kwa mkopo wa Dola milioni 200 kutoka Benki ya Dunia. Awamu ya kwanza inalenga kuboresha maabara vyuoni, matumizi ya ICT na kusomesha wanataluma wa fani za Sayansi na Teknolojia. Aidha, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU) unaotarajia kuanza mwaka 2010/11 utaibua maeneo mbalimbali ya kufadhiliwa sambamba na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa kuboresha sayansi na teknolojia katika vyuo vikuu;

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna upungufu mkubwa wa wahadhiri katika vyuo vikuu kwa sasa kutoptana na ongezeko kubwa la udahili katika elimu ya juu (Kielelezo Na. 5). Katika kukabili tatizo hili, Serikali inashirikiana na Vyuo vikuu kutafuta wahadhiri kutoka nchi za nje kama vile India, Urusi na Cuba. Kuanzia mwaka 2006/2007 Serikali inatenga fedha za kusaidia vyuo kusomesha Wahadhiri Wasaidizi kwa kutumia Vyuo Vikuu vya ndani. Kuanzia mwaka 2008/2009 Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imeanza kutoa mikopo kwa wahadhiri ili wasome Shahada ya Uzamili na Uzamivu. Aidha, Serikali imeingia ubia na nchi marafiki na Mashirika ya nje katika kusomesha wahadhiri wa vyuo vikuu.

Idara ya Ukaguzi wa Shule

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Ukaguzi wa shule ina jukumu la kuhakikisha kuwa sera, sheria, kanuni na viwango vya utoaji elimu vilivyowekwa vinatekelezwa

ipasavyo katika shule za awali, msingi, sekondari, shule na vitengo vya elimu maalum, vituo vya Ufundu Stadi, Elimu ya Watu Wazima na vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Idara ya Ukaguzi wa Shule kuanzia mwaka 2005 – 2009 imeimarishwa kwa kuongeza wakaguzi 298 wa shule, kukarabati ofisi za ukaguzi wa shule za wilaya 50, kununua samani za ofisi za ukaguzi wa shule katika wilaya 23 kununua kompyuta 88 kwa ajili ya ofisi za Kanda na Wilaya, kununua magari 45 ya ofisi za ukaguzi wa shule za Kanda na Wilaya. Katika kukabiliana na upungufu na uwezo wa utendaji kazi, mafunzo ya awali kwa wakaguzi wa shule 127 na mafunzo ya manejimenti kwa wakaguzi wakuu wa shule wa wilaya 120 yametolewa ili kuwajengea uwezo wakaguzi juu ya mitaala iliyoboreshwa. Aidha, kanda 3 mpya za ukaguzi wa shule za Dar es Salaam, Nyanda za Juu Kusini na Ziwa Magharibi zimeanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Idara ya Ukaguzi wa Shule ilitekeleza yafuatayo: -

- (a) Kukagua asasi 5,610 sawa na asilima 22.3 ya lengo. Aidha, ukaguzi maalum kwa ajili ya uanzishwaji wa shule mpya 194, tuhuma na matukio maalum katika shule za sekondari 88 na vyuo vya ualimu 8 ulifanyika;
- (b) Kukarabati ofisi 20 za ukaguzi wa shule za kanda na wilaya pamoja na kununua samani za ofisi 10 na kununua magari 6;
- (c) Kuendesha Mtihani wa Taifa wa Kidato cha 2 mwaka 2008 katika vituo 3,508; ambapo kulikuwa na watahiniwa 415,303 kati yao wasichana walikuwa 192,694 (46.4%) na wavulana 222,609 (53.6%). Idadi ya waliopata alama ya ufaulu ni 284,167 (73.7%) ambapo 124,400 (32.3%) ni wasichana na 159,767 (41.4%) ni wavulana na waliopata alama chini ya ufaulu ni 101,410 (26.3%) wakiwemo wasichana 54,741 (14.2%) na wavulana 46,669 (12.1%). Hata hivyo watahiniwa wote waliofanya Mtihani huo waliingia Kidato cha 3 ambapo watahiniwa waliopata alama za chini wanapatiwa mafunzo rekebishi; na;
- (d) Kuanzisha kanda mpya 3 za ukaguzi wa shule ambazo ni; Kanda ya Ziwa Magharibi inayojumuisha mikoa ya Kagera na Kigoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayojumuisha mikoa ya Ruvuma na Iringa; na Kanda ya Dar es Salaam yenye mkoa wa Dar es Salaam pekee. Aidha, Kanda ya Mashariki ambayo imehamishia Makao yake Makuu Morogoro inajumuisha mikoa ya Pwani na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ilianzishwa mwezi Julai 2008 kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la watu wazima na vijana wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu ili kuleta maisha bora kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Serikali ya Cuba, imefanya Upembuzi Bainifu na kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Kisomo wa Ndiyo Ninaweza (*Yes, I can*) utakaotekelawa kwa Njia ya Redio na Video katika kipindi cha 2009/2010 hadi 2013/2014. Aidha, katika kuimarisha Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa, Wizara yangu imeandaa Hadidu za Rejea kwa ajili kutathmini utekelezaji wa Mkakati wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na kuandaa Mkakati mpya kwa lengo la kuimarisha MEMKWA na MUKEJA ili kutoa elimu kwa watoto na vijana walio nje ya shule kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Idara ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuandaa miongozo ya wawezeshaji na wasimamizi wa programu za masomo kwa ajili ya kutoa elimu ya watu wazima kwa njia ya redio, televisheni na video kupitia programu ya Ndiyo Ninaweza katika wilaya za Temeke, Ilala, Kinondoni (Dar es salaam), Ilemela (Mwanza), Dodoma Mjini (Dodoma) na Songea Mjini (Ruvuma);
- (b) Kukarabati majengo ya kituo cha uchapaji cha Makao Makuu ambapo kazi imefikia asilimia 75 na Kituo cha Taifa cha Kisomo Mwanza kazi imefikia asilimia 25 na inaendelea;
- (c) Kutoa mafunzo kwa Waratibu Elimu Kata 120 na Maafisaelimu 30 kuhusu ukusanyaji wa data na uingizaji wake kwenye kompyuta kwa kutumia software StatEduc2. Aidha, Kompyuta 12 zilinunuliwa na kusambazwa kwenye wilaya za mradi. Data zimekusanya katika Kata 60 na zinaingizwa kwenye kompyuta katika Halmashauri za Temeke, Ilala, Rombo, Mbulu, Kondoa, Shinyanga (M), Shinyanga (V), Kigoma (V), Makete, Mvomero, Sumbawanga na Mtwara Mikindani;
- (d) Kutoa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa vituo vya MUKEJA katika Halmashauri kwa washiriki 1,427 (Walimu wakuu 940 na Waratibu Elimu kata 487); na
- (e) Kuratibu mafunzo ya ufundishaji bainifu na kufuatilia matumizi ya mbini hiso katika madarasa ya kisomo katika Halmashauri za majaribio ambazo ni Temeke (M), Mvomero, Morogoro (V), Dodoma (M), Igunga, Hai, Iringa (V), Sumbawanga (V), Songea (V) na Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi, Wakala na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yangu yanafanikisha utoaji wa elimu bora.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina jukumu la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu. Aidha, chuo kinasimamia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa na Skuli ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma. Taasisi hiso zina jukumu la

kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaaluma na kitaalam katika masuala mbalimbali yanayofundishwa katika vyuo hivyo. Mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitekeleza yafuatayo: -

- (a) Kudahili jumla ya wanafunzi 6,370 kati yao 3,958 ni wa shahada ya kwanza ambao 2,575 ni wanaume na 1,383 ni wanawake. Wanafunzi wa shahada za uzamili walikuwa 2,218 kati yao 1,567 ni wanaume na 651 ni wanawake; kwa sasa Chuo kina jumla ya wanafunzi 14,203;
- (b) Kuendeleza ushirikiano na Serikali na wafadhili mbalimbali katika kugharamia utafiti na kusambaza matokeo ya utafiti;
- (c) Kuajiri wanataaluma 167 ili kukidhi ongezeko la wanafunzi na kujaza nafasi za kazi zilizoachwa wazi na walioondoka;
- (d) Kuboresha ufundishaji wa Kifaransa kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa, mradi huu umehusu msaada wa vitabu na ufundishaji wahadhiri wa somo la kifaransa;
- (e) Kudhamini mafunzo ya uzamili kwa wanataaluma 84 na wafanyakazi waendeshaji 21 kwa ufadhili wa Serikali ya Norway, Sida/SAREC, Carnegie Corporation, DANIDA na *Rockfeller Foundation*;
- (f) Kuendeleza awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la Skuli ya Biashara na Kitengo cha Ujasiriamali, kumbi 2 za miadhara zenyewe uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kila moja na kukamilisha awamu ya pili ya mradi wa Mlimani City; wenye kujumuisha kumbi za mikutano, majengo ya ofisi na nyumba za kuishi na kukamilisha ukarabati wa awali wa majengo ya kilichokuwa chuo cha TTCL kwa msaada wa Serikali ya Korea (KOICA);
- (g) Kukamilisha andiko la ujenzi wa madarasa, maabara na makumbusho ya Chuo kupitia mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia;
- (h) Kuanzisha mafunzo ya Shahada ya Biashara na Uongozi (BBA) na Stashahada ya Elimu (PGDE) na Menejimenti ya Uhandisi (PGDEM) kwa kutumia mtandao wa kompyuta;
- (i) Kuanzisha muundo mpya wa utawala kwa lengo la kuongeza ufanisi na hivyo kupunguza ngazi za kiutawala kutoka 4 kwenda 3 na kufanya chuo kuwa na vyuo 3 vya kampasi, skuli 5 na taasisi 4;
- (j) Kuendeleza ujenzi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari huko Buyu, Zanzibar; na;
- (k) Kufanya tafiti zifuatazo ambazo nyingine zimeombewa hatazo (*patents*):

- (i) Teknolojia mpya ya kukausha matunda na mboga kwa wingi na kwa muda mfupi ambayo imeanza kutumiwa na wakulima wa Zanzibar, Morogoro na Kibaha.
- (ii) Ugunduzi wa kichocheo (*catalyst*) ambachokinatumika viwandani kuchochea mchakato mzima wa kutengeneza bidhaa na hivyo kupunguza muda wa kutengeneza bidhaa hizo.
- (iii) Teknolojia ya kutengeza juisi ya ndizi ambayo imeombewa Hataza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Skuli ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 273 wa ngazi ya Shahada ya Kwanza, 10 Stashahada ya Uzamili na 38 wa ngazi ya Cheti;
- (b) Kukarabati maabara ya picha, studio za matengenezo na utayarishaji wa vipindi vya televisheni;
- (c) Kugharamia mafunzo kwa wahadhiri 4 katika Shahada ya Uzamili na 2 wa Uzamivu;
- (d) Kujenga uzio wa Chuo ili kuimarisha usalama; na
- (e) Kurusha matangazo ya redio na televisheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Dar es Salaam kina jukumu la kufundisha, kutafiti, kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Ualimu na Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 801 kati ya hao 76 wa masomo ya sayansi na 725 wa masomo ya Sanaa na Sayansi ya Jamii. Kwa sasa Chuo kina jumla ya wanafunzi 3,528;
- (b) Kuendeleza ujenzi wa madarasa, maabara, ofisi za walimu, kumbi 3 za mihiadhara (*Lecture Theatres*) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,000 kwa wakati mmoja na upanuzi wa jengo la utawala;
- (c) Kutoa mafunzo maalum kwa wadahiliwa 35 wa kike wa mwaka wa kwanza kwenye fani ya sayansi;
- (d) Kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa maktaba;

- (e) Kuendelea kuimarisha miundo na matumizi ya TEHAMA;
- (f) Kuendelea kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hasa kwa shahada za Uzamili na Uzamivu. Wahadhiri 36 wako kwenye mafunzo ya Shahada za Uzamili (33 – UDSM, 2-Kenya, 1-Sweden), Wahadhiri 22 wako kwenye mafunzo ya Uzamivu (9- UDSM, 5- Germany, 2- Australia, 1- Ireland, 1- UK, 2- South Africa, 2- Japan); na
- (g) Kujenga kituo cha afya na kutoa elimu ya jinsia, UKIMWI na ushauri na unasihi kwa jumuiya ya Chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kina jukumu la kufundisha, kutafiti, kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Ualimu na Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 650 wa Shahada ya Kwanza. Kwa sasa Chuo kina jumla wanafunzi 1,899;
- (b) Kuendeleza ujenzi wa ukumbi wa miyadhabara wenye uwezo wa kukaliwa na wanafunzi 1000, na kuanza maandalizi ya ujenzi wa mabweni ya wanafunzi;
- (c) Kuendelea na ukarabati wa majengo ya Chuo kwa ajili ya ofisi, maktaba, zahanati na ununuzi wa vifaa vya maabara;
- (d) Kukarabati barabara za ndani ya Chuo;
- (e) Kukamilisha mchakato wa kumpata mkandarasi na kuanza ujenzi wa jengo la utawala;
- (f) Kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la Chuo;
- (g) Kuajiri wahadhiri 42 na wafanyakazi waendeshaji 12;
- (h) Kugharamia mafunzo kwa wahadhiri 20 katika Shahada za Uzamili na Uzamivu; na
- (i) Kuendelea kutumia wahadhiri wa muda kujaza pengo lililopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinatekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya Shahada za Kwanza na za Juu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za Kilimo, Misitu, Mifugo, Wanyamapori, Mazingira, Utalii na fani nyingine za Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kudahili wanafunzi 1,470 wa Shahada za Kwanza na wanafunzi 694 wa Shahada za Uzamili na kuanzisha shahada 5 za BSc. Education, Bsc. Informatics, BSc. Range Management, BSc. Tourism na BMA *Agri-Business*. Kwa sasa Chuo kina jumla ya wanafunzi 3,619;
- (b) kufanya utafiti katika miradi 127 inayolenga kuchangia jitihada za serikali za kuboresha Kilimo, Mifugo, Maliasili na Mazingira na kuendelea kufanya tafiti zaidi 121 zinazolenga kukuza kipato cha mwananchi wa kawaida na kukuza uchumi kwa ujumla; pia kuanzisha na kutekeleza mradi mkubwa wa utafiti juu ya namna ya kujikinga na athari ya mabadiliko ya hali ya hewa;
- (c) kutekeleza program 36 za huduma ya elimu ya kujiendeleza kwa wakulima, wagavi na wataalamu wa sekta za Kilimo, Mifugo, Maliasili, Afya na Serikali za Mitaa kwa washiriki 1,350 ambapo asilimia 37 walikuwa wanawake;
- (d) kimetekeleza Miradi 10 kati ya Miradi hiyo Miradi 4 imegharamiwa na Serikali na miradi 6 imegharamiwa na Wafadhili;
- (e) Kukarabati kumbi za mihadhara na madarasa yaliyopo Solomon Mahlangu na Kampasi kuu ambapo kazi imekamilika kwa asilimia 95;
- (f) Kukamilisha ukarabati wa nyumba za wafanyakazi na mabweni na kukamilisha ukarabati wa barabara za ndani zilizopo Kampasi Kuu zenye kilometra 3.6;
- (g) Kukamilisha ujenzi wa mabweni 2 na kuanza ujenzi wa kumbi 4; na
- (h) Kuendelea kufanya tafiti ambazo zimekuwa na manufaa kwa wananchi na nyingine kupatiwa hatazo. Tafiti hizo ni:-
- (i) Ugunduzi wa mbegu bora za maharage ziitwazo Pesa na Mshindi.

Tayari mbegu hizo zimeshapata hati miliki na mzalishaji wa mbegu hizi kwa wingi ameteuliwa kuwa ni *Tanseed Internaciona*l.

- (ii) Ugunduzi wa mbegu za mpunga zinazostahimili magojwa ya rice *yellow mottle virus* zinazoitwa “Kalahi” na “Mwangaza”.
- (iii) Ugunduzi wa teknolojia ya kukata na kuperua magogo kwenye mashamba ya wakulima bila uharibifu wa mazingira.

- (iv) Ugunduzi wa matumizi ya miti isiyojulikana kuwa ina manufaa kwa matumizi ya mbao.

Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara kina jukumu la kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika nyanja za ushirika, maendeleo ya jamii, biashara, oganaizesheni, ujasiriamali na masuala mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 756 na hivyo kufanya Chuo kuwa na jumla wanafunzi 2,068 ambalo ni ongezeko la asilimia 52.9;
- (b) Kugharamia mafunzo ya wanataluma 24 wanaoendelea na masomo katika ngazi mbalimbali;
- (c) Kuendelea kuboresha shughuli za utafiti na uchapishaji kuitia mpango wa utafiti mdogo unaofadhiliwa na chuo kwa njia ya ushindani, uendeshaji warsha za kujenga uwezo;
- (d) Kuendelea kuimarisha vituo vya mikoani kwa kuviongezea wafanyakazi, kuainisha na kuingiza mahitaji kwenye bajeti ya Chuo. Aidha, vituo vya Mwanza, Tanga na Shinyanga vimefanyiwa ukarabati mdogo;
- (e) Kuimarisha ushirikiano na vyuo vya ndani na nje ya nchi vikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Chuo cha Ushirika cha Uingereza, Chuo Kikuu cha Stirling-UK, Chuo cha Biashara na Teknolojia cha Humber-Canada, Chuo Kikuu cha Makerere, Chuo Kikuu cha Malawi na Chuo Kikuu cha Zambia;
- (f) Kuendesha semina na warsha kuhusu masuala mtambuka kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii na kuyaingiza kwenye mitaala ya Chuo katika ngazi zote;
- (g) Kuendelea na utekelezaji wa masharti yaliyotolewa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu ili kukiwezesha Chuo kupanda daraja na kuwa Chuo Kikuu kamili; na
- (h) kuandaa Mpango Mkakati wa Chuo kwa mwaka 2009/2010- 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Dodoma kinatikeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya Shahada za Kwanza na za Juu, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa

kitaalam katika nyanja za Ualimu, Hisabati, Sanaa na Lugha, Sayansi za Jamii, Sayansi za Kompyuta, Tiba na Uuguzi na Sayansi Asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 Chuo Kikuu Dodoma kilitekeleza yafuatayo: -

- (a) kudahili wanafunzi wapya 5,858 kati ya hao 2,563 ni wanawake na 3,295 ni wanaume. Kwa sasa chuo kina jumla ya wanafunzi 7,337;
- (b) kuendesha programu 52 za Shahada za Kwanza na 10 Uzamili na 1 Uzamivu;
- (c) kuajiri wahadhiri 304 na wafanyakazi waendeshaji 203;
- (d) kujenga vyuo 3 vya Sanaa na Sayansi za Jamii (*Humanities and Social Sciences*), Sayansi za Kompyuta (*Informatics and Virtual Education*) na Chuo cha Elimu (*Education*) katika awamu ya kwanza; na
- (e) kufanya tafiti 9 kwenye maeneo ya usimamizi bora wa maliasili, kupambana na magonjwa, umaskini na kutafuta mbinu za kisasa za kuboresha kilimo na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Mzumbe kina jukumu la kupata, kukuza, kuhifadhi na kusambaza maarifa na stadi za menejimenti kwa njia ya mafunzo, utafiti na huduma za kiufundi na kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu Mzumbe kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kudahili wanafunzi 2,539 kati ya hao 1,520 ni wa Shahada ya Kwanza na 1,019 ni wa Shahada za Uzamili. Jumla ya wanafunzi wote hadi sasa ni 4,068;
- (b) kugharimia mafunzo kwa watumishi 15 wa Shahada ya Uzamili na 9 Shahada ya Uzamivu. Watumishi 72 wanaendelea na masomo kati ya hao 39 Shahada za Uzamivu na 33 Uhahada za Uzamili;
- (c) Kuendelea na ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi wa kike 400 ambapo kazi imekamilika kwa asilimia 65;
- (d) Kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300 kwa wakati mmoja;
- (e) Kununua viwanja 3 Namba 906, 907 na 908 Upanga toka Shirika la Nyumba la Taifa kwa kulipia asilimia 50 ya gharama halisi;

- (f) Kukamilisha tafiti 39 na kuendelea na tafiti 37. Aidha, kazi 19 za ushauri katika maeneo ya menejimenti, uongozi na sayansi ya jamii zimekamilika na taarifa zake kukubaliwa na wateja;
- (g) Kuchapisha vitabu 5, makala 3 za kufundishia na makala nyingine 36; na
- (h) Kuajiri wahadhiri 49 na wafanyakazi waendeshaji 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kina jukumu la kufundisha kwa njia ya masafa na ana kwa ana, kutafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kusambaza maarifa kupitia vituo vya Chuo vilivyopo mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 6,085 wakiwemo wa vyeti 1,812, Shahada za kwanza 3,506 na kozi za Stashahada, uzamili na uzamivu 767. Kwa sasa chuo kina jumla ya wanafunzi 28,935;
- (b) Kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa Makao Makuu ya kudumu Bungo-Kibaha kwa kutengeneza barabara na viwanja vya michezo;
- (c) Kukarabati majengo katika vituo vya Chuo katika mikoa ya Singida, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Dodoma;
- (d) Kuvipatia Maabara za Kompyuta vituo vya Chuo katika mikoa ya Singida, Iringa, Mbeya, Temeke na Ilala;
- (e) Kuanza kutumia platform ya elektroniki ya Moodle kwa ajili ya kuwapa wanafunzi nafasi ya kutumia TEHAMA;
- (f) Kupata viwanja na kuanza maandalizi ya awali ya kujenga vituo vya Mtwara na Manyara; na
- (g) Kukamilisha mpango wa ujenzi wa jengo la Kitivo cha Biashara.
- (h) Kufanya tafiti kuhusu mwongozo wa kitaifa wa kutupa taka za “*e-waste*” na matumizi ya matingatinga kusafisha maji taka vyuoni na shulen.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhibili kina jukumu la kufundisha, kutafiti, kutibu na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya tiba na afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2008/2009 Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 261 wa fani mbalimbali za Tiba na afya na kuweka samani na umeme katika majengo. Kwa sasa Chuo kina jumla ya wanafunzi 2,413;
- (b) Kuendelea kufanya tathmini ya mali za wananchi wa Mloganzila kwa ajili ya kulipa fidia;
- (c) Kuajiri wahadhiri 19 katika idara mbalimbali za kitaaluma zilizopo Chuoni;
- (d) Kukamilisha ujenzi wa ukuta kuzungusha eneo la hosteli, kuendelea na ujenzi wa kantini katika hosteli za Chole;
- (e) Kufungua maabara ya kisasa kwa ajili ya utafiti wa kutengeneza dawa za tiba na uhakiki wa ubora wa madawa yanayotoka nje; na
- (f) Kuendelea na tafiti za magonjwa yanayoathiri jamii yakiwemo malaria, afya ya uzazi, kifua kikuu na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu Ardhi kina jukumu la kufundisha, kutafiti, kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya ardhi na usanifu wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Chuo Kikuu Ardhi kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 1,754 wakiwemo 28 wa Stashahada na 124 wa Shahada ya Uzamilli na Uzamivu. Kwa sasa Chuo kina jumla ya wanafunzi 1,908.
- (b) Kuendelea na zoezi la kuhuisha miongozo na taratibu za uendeshaji wa Chuo ili iendane na hadhi ya Chuo Kikuu kinachojitegemea na kuimarisha utendaji wa Skuli na Idara za mafunzo;
- (c) Kukamilisha taratibu za kuanzisha masomo ya jioni (*evening classes programme*) na utekelezaji wake utaanza mwaka 2009/2010;
- (d) Kufanya tafiti 50 katika maeneo ya maafa, ardhi na makazi;
- (e) Kukamilisha Awamu ya kwanza ya kuweka huduma ya Intaneti katika majengo ili kukuza matumizi ya TEHAMA chuoni;

- (f) Kuanzisha kitengo maalumu cha kitaalamu cha '*Funding Promotion and Investment*' kwa lengo la kutafuta raslimali fedha ili kuharakisha maendeleo ya Chuo;
- (g) Kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa jengo jipywa kwa ajili ya miadhara, madarasa, ofisi za wahadhiri na kuendelea na ukarabati wa miundombinu;
- (h) Kugharimia mafunzo ya wahadhiri 40 katika Shahada za Uzamili na Uzamivu na wafanyakazi waendeshaji 20 kwenye ngazi mbalimbali za masomo na ujuzi; na
- (i) kuajiri watumishi 81 wa kada mbalimbali sambamba na upanuzi wa programu za mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kina jukumu la kuendesha mafunzo katika fani za Sayansi Jamii kwa kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada; kutoa Mafunzo ya Uongozi, kufanya Utafiti na kutoa Ushauri wa kitaalamu kwa sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilitekeleza yafuatayo:-

- (j) kudahili wanafunzi 139 wa Cheti, 334 wa Stashahada na 251 wa Shahada ya Kwanza;
- (k) kuajiri wanataaluma 7 na wafanyakazi waendeshaji 12;
- (l) kuanza kuendesha programu ya Shahada ya Kwanza ya Jinsia na Maendeleo;
- (m) kugharamia mafunzo kwa wanataaluma 12 na wafanyakazi waendeshaji 10;
- (n) kukarabati Jengo la Mihadhara, Jengo la Utamaduni na Hosteli ya Kisota; na
- (o) kuanza maandalizi ya ujenzi wa Tawi la chuo la Bububu kwa kumpata mkandarasi ambaye amekabidhiwa eneo la ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ufundu Arusha kina jukumu la kutoa elimu na mafunzo ya ufundu katika fani za Magari, Ujenzi, Mitambo, Umeme, Barabara, Eletroniki na Mawasiliano Anga kwa kiwango cha Cheti na Stashahada. Aidha, Chuo hufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Chuo cha Ufundu Arusha kilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 167 katika ngazi ya Stashahada;
- (b) Kununua kompyuta 8 na vifaa vya maktaba kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji;
- (c) Kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi;
- (d) Kukarabati madarasa 2 ili kuyageuza kuwa maktaba ya Chuo;
- (e) Kuandaa mitaala mipyta ya Sayansi ya Maabara na Teknolojia; na
- (f) Kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa wanataaluma 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya UNESCO iliundwa mwaka 1962 mara baada ya Uhuru kwa agizo la Bunge Na. 337 la mwaka 1962. Mnamo mwaka 2008, Tume ya Taifa ya UNESCO iliundwa upya kuwa Chombo kinachojitegemea kwa Sheria Na. 7 ya mwaka 2008. Tume ina jukumu la kulishirikisha Taifa katika utekelezaji na uratibu wa kazi za UNESCO nchini kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyanja za Elimu, Sayansi, Sayansi ya Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Tume ya Taifa ya *UNESCO* ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuratibu utekelezaji wa maamuzi yaliyofikiwa wakati wa Mkutano Mkuu wa 34 wa UNESCO: kushiriki katika mikutano, kutangaza nafasi za masomo na kazi, kusambaza kwa wadau taarifa na kupokea madodoso na kuwasilisha kwa wadau husika;
- (b) Kuratibu na kutathmini miradi ya vifaa kwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kuelimisha Waheshimiwa Wabunge kuhusu *UNESCO* na Tume ya taifa ya *UNESCO* na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi minne chini ya ‘*Participation Programme*’ 2008-2009;
- (c) Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuhifadhi Historia ya Ukombozi Barani Afrika kwa kupeleka ujumbe kwenye mkutano wa mashauriano wa nchi wanachama za Windhoek, Namibia na kuandaa mpango wa kazi kwa kushirikiana na wadau;
- (d) Kuratibu utekelezaji wa Programu za Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia na kuandaa mpango wa kazi kwa kipindi cha miaka mitatu;
- (e) Kuratibu uanzishwaji wa Kiti cha UNESCO katika Taasisi ya Sayansi ya Bahari Zanzibar ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

- (f) Kushirikisha wadau katika programu ya Uhuishaji wa Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu na kuandaa Mpango wa Kazi 2009/2010;
- (g) Kuratibu programu ya Mwaka wa Kimataifa wa Astronomia na kuandaa maelezo ya kina (*concept paper*);
- (h) Kuratibu programu ya Mwongozo wa Kimataifa wa Elimu kwa Maendeleo Endelevu na kuandaa taarifa ya utekelezaji ya miaka 5; na
- (i) Kutekeleza Sheria Na. 7 ya mwaka 2008 ya kuunda Tume ya UNESCO huru inayojitegemea kwa kuandaa ikama mpya na kuandaa bajeti ya kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ina jukumu la kutoa ithibati, kuratibu uanzishwaji wa vyuo vikuu, kuhakiki ubora wa elimu na kuidhinisha programu zifundishwazo ili zikidhi mahitaji ya taifa na soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) kuratibu ubora wa programu 21 za masomo ya vyuo vikuu nchini;
- (b) Kuendesha warsha na semina za mafunzo kwa wakuu wa vyuo, wakuu wa menejimenti za vyuo na wadau wengine kuhusu majukumu ya Tume, uongozi katika vyuo vikuu, uhakiki ubora (*quality assurance*), na mfumo wa tuzo zinazotambuliwa kitaifa (*National Qualifications Framework*);
- (c) Kufanya tathmini na kutoa ulinganisho wa vyeti 250 vilivyotolewa kwa Watanzania na vyuo mbalimbali nje ya nchi ili kutambua uhalali wake;
- (d) Kutoa machapisho 6 na taarifa za kuuelimisha umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu vyuo vikuu;
- (e) Kuendelea kutengeneza mfumo wa fomu moja ya kuratibu udahili katika vyuo vya elimu ya juu ambapo software ya mfumo tajwa inaendelea kufanayiwa kazi;
- (f) Kukagua na kutathmini mipango 10 ya kuanzisha au kuhuisha vyuo vikuu kwa lengo la kutoa hati husika;
- (g) Kusimamia udahili wa wanafunzi 35,000 waliojiunga na vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki;

- (h) Kuratibu na kushiriki maonesho ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia; na
- (i) Kuanza mchakato wa ujenzi wa jengo la ofisi za Tume.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania ina jukumu la kutafuta na kubaini vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kugharamia maendeleo ya sekta ya elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wadau wa elimu kuchangia kwa hiari katika miradi ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Mamlaka ya Elimu Tanzania ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuendelea kukamilisha uandaaji wa rasimu ya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu Namba 8 ya mwaka 2001 ilioanzisha Mfuko wa Elimu na Mamlaka ya Elimu Tanzania;
- (b) Kukusanya rasilimali zenyе thamani ya Shilingi billion 6.6 kutoka kwa wadau wa elimu wa ndani na nje ya nchi;
- (c) Kufadhili miradi 187 yenyе thamani ya Shilingi 5,168,822,800. Kati ya miradi hiyo, miradi 149 yenyе thamañi ya Shilingi 1,460,170,400 inalenga kuongeza ubora wa elimu, miradi 16 yenyе thamani ya Shilingi 2,624,560,800 inalenga kuongeza udahili na miradi 22 yenyе thamani ya Shilingi 1,084,091,600 inalenga kuongeza usawa katika upatikanaji wa elimu nchini;
- (d) Kuanzisha ushirikiano na mifuko ya elimu ya wilaya 7 ambazo ni Songea Mjini, Songea Vijiji, Namtumbo, Tunduru, Rufiji na Kiteto na kufanya jumla mifuko ya elimu ya wilaya kuwa 27. Aidha, katika kudumisha ushirikiano wa kimataifa Mamlaka imeanzisha ushirikiano na Mifuko ya Elimu ya Ghana na Nigeria;
- (e) Kutoa taarifa za Mamlaka ya Elimu kwa wadau kwa njia ya taarifa ya mwaka, vipeperushi, jarida na tovuti;
- (f) Kutathmni miradi 98 iliyofadhiliwa na Mamlaka pamoja na programu ya Elimu ya Sayansi kwa shule za Sekondari (*Science Education for Secondary Schools – SESS*);
- (g) Kugharamia mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 15 wa Mamlaka; na

(h) kuendelea na mchakato wa ujenzi wa jengo la ofisi za kudumu za Mamlaka;

- (i) Kukagua miradi 49 inayofadhiliwa na Mfuko wa Elimu; na
- (j) Kuzindua kampeni ya kuchangia wanafunzi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ina jukumu la kutoa mikopo kwa wanafunzi raia wa Tanzania wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi na kukusanya madeni ya mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kutoa mikopo kwa wanafunzi 58,841 kati yao 25,033 ni wa mwaka wa kwanza na 33,808 wanaoendelea na masomo ambapo hadi kufikia tarehe 30, Juni, 2009 jumla ya Shilingi bilioni 140,295,447,086 zilikuwa zimeshakopeshwa;
- (b) Kutoa mikopo kwa kutumia mfumo wa kutambua uwezo wa kiuchumi wa waombaji ambapo waombaji wamekopeshwa kwa madaraja tofauti kulingana na uhitaji wao. Madaraja hayo ni A (100%), B (80%), C (60%), D (40%), E (20%) na F (0%). Mikopo hii imetolewa katika maeneo ya Ada ya masomo, chakula na malazi, vitabu na viandikwa, Elimu kwa Vitendo, mahitaji maalumu ya vitendo na utafiti;
- (c) Kununua magari 2, kompyuta na samani za ofisi;
- (d) Kugharamia mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi 86;
- (e) Kutoa elimu kwa wadau wa mikopo wakiwemo wanafunzi na umma kwa ujumla kuhusu dhana ya uchangiaji katika gharama za elimu ya juu, taratibu za uombaji wa mikopo, vigezo vyta mikopo pamoja na taratibu za urejeshaji mikopo. Hii ilihusisha programu za radio, televisheni, magazeti, vipeperushi, kongamano na maonyesho katika wiki ya utumishi wa umma;
- (f) Kutafuta taarifa za wanufaika wa mikopo iliyotolewa toka Julai 1994 hadi Juni, 2005 ambapo wadaiwa 15,290 kati ya 113,240 wanaodaiwa jumla ya Shilingi bilioni 51.3 wametambuliwa. Aidha, kiasi kilichokusanywa hadi 30 Juni 2009, ni Shilingi bilioni 2,069,134,497.32;
- (g) Kutoa mikopo kwa ajili ya Mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu ndani ya nchi kwa wahadhiri wahitaji 36 wanaofundisha kwenye vyuo vikuu vyta umma;

- (h) Kuongeza kiwango cha mikopo ya elimu kwa vitendo kutoka Shilingi 6,000 hadi Shilingi 10,000 kwa siku, kwa jumla ya siku 56 kwa mwaka; na
- (i) Kukamilisha maandalizi ya awali kuhusu upatikanaji wa ofisi za kanda, Zanzibar na Dodoma ofisi hizo zinatarajiwani kuanza mwezi Julai, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu linasimamia na kuratibu mitaala, ubora wa mafunzo, mitihani, tuzo, usajili na ithibati za vyuo vya elimu ya ufundu vya umma na binafsi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu lilitekeleza yafuatayo: -

- (a) Kukagua vyuo vya ufundu 16 kwa ajili ya ithibati;
- (b) Kuhakiki utekelezaji wa masharti ya ithibati katika vyuo vya ufundu 13 vyenye ithibati kamili;
- (c) Kukagua na kusajili vyuo 21 vyenye uwezo wa kuendesha mafunzo ya elimu ya ufundu;
- (d) Kuratibu na kuidhinisha mitaala 32 yenye kuzingatia umahiri wa mwanafunzi na mahitaji ya soko la ajira;
- (e) Kuratibu mitihani katika vyuo vya ufundu 34 vinavyotumia mitaala mipyaa inayozingatia umahiri wa mwanafunzi na mahitaji ya soko la ajira;
- (f) Kukagua sifa na kusajili walimu 366 wenye sifa za kufundisha katika vyuo vya ufundu;
- (g) kusimamia na kuvizemsha vyuo 25 vya ufundu kuweka mfumo wa kudhibiti na kuhakiki ubora wa mafunzo yatolewayo na vyuo hivyo;
- (h) kuratibu mafunzo yanayohusu ufundishaji katika mfumo wa *Competence Based Education and Training* (CBET) kwa walimu kutoka vyuo 15 vya ufundu;
- (i) kuratibu udahili wa wanafunzi katika vyuo 17 vinavyotoa mafunzo ya Shahada na Stashahada ya Juu; na
- (j) kuimarisha ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi zilizo na majukumu yanayofanana na Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (*ADEM*) una jukumu la kutoa mafunzo ya uongozi wa elimu kwa viongozi mbalimbali katika ngazi ya shule, vyuo na taasisi; kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wakala ulitekeleza yafuatayo:-

- (a) kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa washiriki 276 kutoka ngazi mbalimbali za Elimu;
- (b) kutoa Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Maafisaelimu Taaluma na Maafisaelimu Vifaa na Takwimu 80 kutoka mikoa ya Tabora, Pwani, Morogoro, Mara na Manyara kwa ufadhili wa JICA;
- (c) kutoa Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji Elimu kwa washiriki 95 wakiwemo: wakaguzi wakuu wa kanda na wasaidizi wao, Wakuu wa vyuo na wasaidizi wao, maafisa kutoka makao makuu, wakufunzi kutoka ADEM na kwa wakaguzi wapya 150 kutoka katika Kanda za Elimu;
- (d) kutoa mafunzo ya Cheti cha Uongozi kwa walimu wakuu 127 wa shule za msingi kutoka katika kanda zote za elimu kupitia vyuo vya ualimu;
- (e) Kugharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 12, watumishi 5 wanaoendelea na mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu; na
- (f) Kukarabati majengo ya maktaba, ugavi, mapokezi, kompyuta na kuboresha mazingira ya Wakala.

Mheshimiwa Spika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ina jukumu la kutoa mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya kuijendeleza nje ya mfumo rasmi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Taasisi ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi wa Stashahada ya Juu 352, Stashahada 346 na Cheti cha Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii 12 na Cheti cha Sheria 135;
- (b) Kutoa Elimu Masafa na Ana kwa Ana kwa wanafunzi 30,036 wa elimu ya sekondari;
- (c) Kuandaa na kuchapa moduli za masomo ya Ufundu, Biashara, A-level na Utangulizi;

- (d) Kutoa elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi 137 wa TEWW makao makuu na wafanyakazi 35 wa TEWW kanda ya mashariki;
- (e) Kugharamia mafunzo kwa watumishi ngazi ya Shahada ya Uzamivu 2, Shahada ya Uzamili 5, Stashahada ya Juu 1, Cheti 2, Elimu ya Sekondari 6 na mafunzo ya muda mfupi 20;
- (f) Kuajiri watumishi 21 katika kada za uhadhiri, uhasibu, udereva, uhudumu na ulinzi;
- (g) Kukarabati majengo ya ofisi za mikoa ya Mbeya na Dodoma;
- (h) Kuandaa Mtaala na Mihutasari ya Mpango wa Elimu ya Sekondari Kwa Walioikosa utakaofanyiwa majoribio katika wilaya 7 ambazo ni Temeke, Hai, Siha, Bagamoyo, Makete, Mtwara (V) na Magu;
- (i) Kurekebisha mitaala kuwa katika mfumo wa *Competence Based Education and Training-CBET* na mtindo wa Moduli na kuipandisha daraja Stashahada ya Juu;
- (j) Kuandaa mahitaji ya walengwa wa *Intergrated Post Primary Education-IPPE*;
- (k) Kuandaa, kuchapa na kusambaza majorida ya SAED Na. 64, JAET Na. 16 na Alumni *Newsletter* nakala 500 kila moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania ina jukumu la kubuni, kuandaa mitaala na mihtasari ya elimu ya awali, msingi, sekondari, ualimu na elimu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Taasisi ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuandaa Andiko la Mwongozo wa taifa wa ukuzaji mitaala;
- (b) Kuendesha mikutano 7 ya Paneli ili kupata maoni ya kuboresha masomo ya Uraia, Historia, *Physical Education* na Haiba na Michezo, *Agriculture, Technical Education* na *Economics* na kuboresha mihtasari 26 ya mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti ili iendane na mabadiliko ya mtaala;
- (c) Kuandika mtaala na miongozo ya uandishi wa kiongozo cha kufundisha pamoja na kuboresha mihtasari 25 ya masomo ya kidato cha 5 na 6;

- (d) Kufuatilia utekelezaji wa mitaala katika wilaya 16 na kuandaa miongozo 2 ya uboreshaji wa mihtasari ya masomo ya dini kwa shule za msingi na sekondari;
- (e) Kuhakiki miongozo 21 ya walimu wa kidato cha 1 - 4 na kuandaa chati za somo la sayansi darasa la V – VII kwa shule za msingi;
- (f) Kurekodi vipindi 6 vya redio kwa masomo ya English na Hisabati kwa shule za msingi darasa la III na IV na kurekebisha vitabu 24 vya MEMKWA kundi-rika la 1 na 2 mwaka wa 2;
- (g) Kugharimia mafunzo ya uandishi wa vitabu vya shule na vyuo kwa wakuza mitaala 50 na mafunzo ya kikazi kwa wafanyakazi 42 wa TET;
- (h) Kuendesha mafunzo kwa walimu wawezeshaji 355 kwa shule za msingi kwa wilaya za Kibondo, Kasulu, Kigoma (V), Ngara na Njombe na walimu 324 wa shule za sekondari kuhusu ufundishaji wa masomo mbalimbali;
- (i) Kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji 200 wa MEMKWA katika wilaya za Kibondo na Kasulu chini ya Programu za UNICEF;
- (j) Kuendesha kongamano 2 za kimataifa: moja kwa nchi 8 kuhusu mitaala chini ya Mpango wa Elimu Msingi katika Afrika (*BEAP*) na pili kwa nchi 12 (*ESACO*) kuhusu mchango wa mitaala na maendeleo endelevu;
- (k) kuendesha bonanza kwa wanafunzi 1,000 wa mkoa wa Mtwara na 500 wa mkoa wa Ruvuma kuhusu stadi za maisha chini ya ufadhilli wa watu wa Marekani(USAID); na
- (l) kuendesha mafunzo kwa walimu wawezeshaji 38 na waelimishaji rika 190 kuhusu ushauri na unasihi na njia zifaazo kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI katika mikoa ya Mtwara na Ruvuma chini ya ufadhilli wa watu wa Marekani.

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ina jukumu la kutoa na kusambaza huduma za maktaba kwa watu wote nchini, kuanzisha,kuendesha,kuongoza, kuboresha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma kuanzia ngazi za Mikoa, Wilaya hadi Vijiji na kutoa mafunzo na kuendesha mitihani ya Taaluma ya Ukutubi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Bodi ilitekeleza yafuatayo: -

- (a) Kuongeza machapisho 52,484 ya vitabu, magazeti na majarida 37,845 na kurakai vitabu 78;

- (b) Kuanzisha matumizi ya teknolojia ya kisasa ya utoaji habari katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro;
- (c) Kukamilisha ujenzi wa madarasa 2 ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi wa Nyaraka Bagamoyo;
- (d) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi 162 Cheti, 70 Stashahada na 30 mafunzo ya muda mfupi;
- (e) Kukamilisha ukarabati wa jengo la maktaba ya mikoa wa Morogoro na kuendelea na ukarabati wa maktaba za mikoa ya Tanga na Mbeya;
- (f) Kuandaa tamasha la kujisomea katika mikoa 10 na kuandaa hema za jumuiya za kujisomea katika mikoa wa Pwani ambapo wanachama 20,096 waliongezeka kati ya hao 5,146 watu wazima;
- (g) Kuimarishe huduma za Maktaba za watoto kwa kununua vifaa vya multi-media kwa ajili ya kujifunzia katika mikoa ya Mtwara, Tabora na Ruvuma; na
- (h) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa shule 32 juu ya uanzishaji, upangaji na uendelezaji wa maktaba za shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Maendeleo Dakawa kina jukumu la kutoa Mafunzo ya mchepuo wa Sayansi na Hisabati kwa vijana wa Kitanzania ili kuwezesha Taifa kupata watalaan wa aina mbalilmbali wa fani hizo na kupunguza ubaba wa walimu na kupanua wigo wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Kituo hicho kilitekeleza yafuatayo: -

- (a) kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati wa kuendeleza kituo; na
- (b) kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya kituo ikwa ni pamoja na ukarabati wa visima vya maji, pampu za kusukuma maji safi na maji taka na ukarabati wa bomba kuu la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani la Tanzania lina majukumu yafuatayo: kuweka sera ya mitihani kwa kuzingatia Sheria ya Elimu, Sera ya Elimu pamoja na miongozo mbalimbali itolewayo kuhusu masuala ya kielimu, kuwa na mamlaka juu ya mitihani katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuidhinisha vituo vya mitihani, kupokea na kuchunguza, kutoka kwa watu wengine au mashirika mengine, taarifa au mambo mengine yanayoathiri sera ya mitihani na kuirekebisha kulingana na hali ilivyo, kushirikiana na watu wengine na/au mashirika mengine katika kuweka utaratibu mzuri wa kuendesha mitihani katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na

kuendesha mitihani na kutunuku Stashahada mbalimbali na Vyeti kwa wale wanaofuzu na kufaulu mitihani iliyo chini yake kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Baraza la Mitihani la Tanzania lilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi, Mitihani ya Kidato cha Nne na Mtihani wa Maarifa, Mitihani ya Kidato cha Sita na Diploma ya Ualimu, Cheti cha Ualimu Daraja la A na Mitihani ya Ufundi;
- (b) Kusimamia uendeshaji wa mitihani itolewayo na Bodi za Nje ya Nchi inayofanywa na watu binafsi hapa nchini;
- (c) Kukamilisha kazi ya upanuzi wa jengo la Kitengo cha Chapa na Uchapishaji, kununua mashine ya kupooza hewa na mashine ya WEBB GOSS kwa ajili ya uchapaji wa mitihani ya taifa;
- (d) Kufanya ukarabati wa majengo ya ofisi za Baraza la Mitihani la Tanzania;
- (e) Kuendesha warsha za utunzi wa maswali ya mitihani kwa lengo la kuongeza ubora wa maswali;
- (f) Kuandaa fomati za Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa kuzingatia mabadiliko ya mtaala yaliyofanyika mwaka 2006;
- (g) Kuandaa mfumo wa kisasa wa usajili, uchambuzi na utoaji wa matokeo;
- (h) Kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Usahihishaji Mitihani, “Mbezi Wani”; na kufanya ununuzi wa samani kwa ajili ya kituo hicho; na
- (i) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi yenye lengo la kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI ambapo wafanyakazi 227 walinufaika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mtihani wa Kitaifa wa Kumaliza Elimu ya Msingi, watahiniwa waliofanya mtihani mwaka 2008 walikuwa ni 1,017,967 ambapo wasichana walikuwa 503,800 sawa na asilimia 49.49 na wavulana walikuwa 514,167 sawa na asilimia 50.51. Jumla ya watahiniwa waliofaulu walikuwa 536,672 sawa na asilimia 52.73 ambapo wasichana waliofaulu walikuwa 229,476 sawa na asilimia 45.55 ya wasichana waliofanya mtihani huo na wavulana waliofaulu walikuwa 307,196 sawa na asilimia 59.75 ya wavulana waliofanya mtihani huo. Mwaka 2007 jumla ya watahiniwa 773,499 walifanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi ambapo waliofaulu walikuwa 419,094 sawa na asilimia 54.18, wakiwemo wasichana 170,906 sawa na asilimia 45.39 na wavulana 248,186 sawa na asilimia 62.52.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mtihani wa Kitaifa Kidato cha Nne mwaka 2008, jumla ya watahiniwa 233,848 walifanya mtihani wakiwemo watahiniwa wa shule 163,855 na wa kujitegemea 69,993. Waliofaulu Mtihani kwa kupata Daraja I-IV walikuwa 168,420 sawa na asilimia 75.82. Kwa upande wa watahiniwa wa shule, waliofaulu katika Daraja I - IV walikuwa 126,617 sawa na asilimia 83.69 wakati watahiniwa wa kujitegemea waliofaulu Mtihani huo walikuwa ni 41,803 sawa na asilimia 59.01.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uendeshaji wa Mitihani ya Kidato cha Nne 2008 ilijitokeza changamoto ya uvujaji wa mtihani wa somo la '*Basic Mathematics*'. Mitihani huo uliokuwa umepangwa kufanyika tarehe 6/10/2008 ulahirishwa hadi tarehe 27/10/2008 ili kutoa fursa ya kuandaa na kusambaza mtihani mwingine. Kufuatia uvujaji huo, Wizara yangu iliunda Tume ya kuchunguza chanzo cha tukio hilo. Kutokana na matokeo ya uchunguzi, hatua stahiki zimechukuliwa dhidi ya wahusika ikiwa ni pamoja na kuwaachisha kazi wafanyakazi wawili na kuwahamisha wengine wawili nje ya Baraza la Mitihani la Tanzania. Aidha, wafanyakazi wengine 79 wamehamishiwa katika vituo vingine vya kazi Serikalini ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa Baraza la Mitihani. Hatua zaidi za kuimarisha Baraza la Mitihani la Tanzania zitaendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja kuboresha maslahi ya wafanyakazi, kuimarisha usalama wa mitihani na vyeti vinavyotolewa na Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mtihani wa Kidato cha Sita mwaka 2009, jumla ya watahiniwa 51,563 walifanya mtihani. Watahiniwa waliofaulu katika Daraja I – IV walikuwa 45,716 sawa na asilimia 89.64. Wasichana waliofaulu walikuwa 17,152 sawa na asilimia 90.92 ya wasichana wote na wavulana walikuwa 28,564 sawa na asilimia 88.89 ya wavulana. Ubora wa ufaulu kwa kuangalia idadi ya watahiniwa wa shule waliopata madaraja I – III umeongezeka. Idadi ya watahiniwa waliopata madaraja I – III imepanda kwa watahiniwa 8,608 kutoka 23,415 waliopata madaraja hayo mwaka 2008 hadi 32,023 waliopata madaraja I-III mwaka 2009. Aidha, asilimia ya waliopata madaraja I – III imeongezeka kutoka 72.55 hadi 82.86 ambapo wasichana walikuwa 12,053 sawa na asilimia 31.19 na wavulana 19,970 sawa na asilimia 51.67

Mheshimiwa Naibu Spika, Mitihani ya Cheti na Diploma ya Ualimu mwaka 2009, ilifanyika mwezi Mei, 2009. Mitihani iliyofanyika ni ya Ualimu Daraja la A (*Grade A Teachers' Certificate Examinations – GATCE*), Kozi Maalum ya Ualimu Daraja la A (*Grade A Teachers Special Course Certificate Examinations – GATSCE*), Stashahada ya Ualimu (*Diploma in secondary Education Examinations – DSEE*), Cheti cha Ufundi Sanifu (*Full Technician Certificate Examinations – FTCE*) na Stashahada ya Juu ya Uhndisi (*Advanced Diploma in Engineering Examinations – ADEE*). Jumla ya watahiniwa 12,502 waliomba kusajiliwa ili wafanye mtihani wa Cheti cha Ualimu Daraja la A, watahiniwa 9,081 sawa na asilimia 72.64 walisajiliwa na 3,421 sawa na asilimia 27.36 hawakusajiliwa kutokana na kukosa sifa za kufanya mtihani huo.

Aidha, kati ya watahiniwa 5,809 walioomba kusajiliwa kufanya mtihani wa Stashahada ya Ualimu, watahiniwa 5,436 sawa na asilimia 93.62 walisajiliwa na 373 sawa na asilimia 6.42 hawakusajiliwa kwa kukosa sifa za kufanya mtihani huo. Watahiniwa

waliokosa sifa walikuwa ama hawajafikisha kiwango cha ufaulu wa pointi angalau 28, au wamewasilisha vyeti vya kughushi au vyeti vya bandia na wengine walikuwa wanatumia vyeti vya watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha utendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania, jumla ya wafanyakazi 17 walijiriwa kwa mwaka 2008/2009. Aidha, Baraza limefanya mapitio ya mfumo wa usambazaji na usimamizi wa mitihani kwa lengo la kuimarisha usalama wa mitihani. Kutokana na mapitio hayo na ili kukabiliana na tatizo la udanganyifu katika vyumba vya mitihani, Baraza la Mitihani liliongeza idadi ya wasimamizi ili kuwa na uwiano wa msimamizi mmoja kwa watahiniwa 40 (1:40) badala ya uwiano wa sasa wa 1:50. Utaratibu huo utaanza kutumika kuanzia Oktoba 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (VETA) ina jukumu la kuratibu, kudhibiti, kugharamia, kutoa na kukuza elimu na mafunzo ya ufundu stadi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuongeza nafasi za mafunzo kwa wanafunzi 2,600 baada ya kukamilika kwa upanuzi wa vyuo vya Shinyanga, Tabora, Dakawa, Mikumi, Kagera, Mara na Songea;
- (b) Kutoa mwongozo kwa ajili ya kukasimu madaraka Mikoani na Vyuoni kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utoaji wa mafunzo;
- (c) Kuboresha karakana za mafunzo kwa vitendo na kuongeza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya Songea, Mara, Kagera, Oljoro, Mikumi, Dakawa na Kigoma;
- (d) Kukuza na kurekebisha mitaala ya fani 16 ya masomo ya ufundu stadi kwa lengo la kuongeza ubora wa mafunzo yatolewayo;
- (e) Kuanza ujenzi wa chuo cha ufundu stadi cha wilaya ya Makete;
- (f) Kukamilisha ukarabati wa vyuo vya Tabora na Shinyanga;
- (g) Kutoa ruzuku ya Shilingi 474,712,049 kwa vyuo vya ufundu stadi vya asasi zisizo za Serikali kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na kutoa mafunzo kwa walimu wa vyuo hivyo kwa lengo la kuongeza ubora wa mafunzo yatolewayo;
- (h) Kutoa mafunzo kwa walimu 255 katika Chuo cha Ualimu wa Ufundu Stadi Morogoro na wengine 82 mafunzo ya muda mfupi nchini Korea, China na India; na

- (i) Kukamilisha utafiti wa utaratibu utakaowezesha wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya III kuendelea na mafunzo ngazi ya IV kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo, mipango na programu 2009 ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- (a) Upungufu wa walimu na wakaguzi wa shule;
- (b) Upungufu mkubwa wa wahadhiri katika vyuo vikuu vya umma;
- (c) Upungufu wa maabara za masomo ya Sayansi na Lugha;
- (d) Upungufu wa vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia na huduma za maktaba;
- (e) Ufaulu mdogo katika masomo ya lugha (Kiswahili na Kiingereza), Hisabati na masomo ya Sayansi katika shule za msingi na sekondari;
- (f) Utoro wa wanafunzi hasa katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari pamoja na mimba kwa wanafunzi;
- (g) Madeni ya walimu, madai ya wazabuni wa chakula, vifaa na stahili za watumishi;
- (h) Kupanua elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa kujenga chuo kimoja cha ufundi stadi katika kila wilaya na kukamilisha ujenzi wa vyuo vya ufundi vya mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Manyara na Lindi;
- (i) Mazingira magumu katika baadhi ya maeneo husababisha watumishi kutopenda kufanya kazi katika maeneo hayo;
- (j) Udogo na uchakavu wa miundombinu katika vyuo, vyuo vikuu na Taasisi nyingine za umma;
- (k) Kuongezeka fedha ili kukidhi mahitaji halisi ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi wanodahiliwa katika vyuo vya elimu ya juu; na
- (l) Mafao duni kwa wastaifu wa Vyuo Vikuu vya umma.
Malengo na Bajeti ya Mwaka 2009/2010

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa malengo ya mwaka 2008/2009, sasa yafuatayo ni malengo ya mwaka 2009/2010 ya ofisi ya Kamishna wa Elimu, Idara, na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Idara ya Utawala na Rasimaliwatu itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuajiri watumishi wapya 472, kuidhinisha vibali vya ajira za wataalamu wa kigeni 800, kuthibitisha kazini watumishi 150 na kuratibu upandishwaji vyeo watumishi 906;
- (b) Kutekeleza Mkataba Mpya wa Huduma kwa mteja na kuratibu tathmini ya utendaji kazi wa watumishi kwa njia ya *OPRAS*;
- (c) Kufanya majoribio ya awali katika vyuo 5 vya ualimu kwa lengo la kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma za usafi, mapokezi na ulinzi;
- (d) Kutekeleza muundo mpya wa Wizara kwa lengo la kuimarisha utendaji;
- (e) Kuanza kutekeleza Muundo mpya wa Utumishi wa Kada zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii;
- (f) Kuondoa kero ya madai ya walimu kwa kulipa madeni yao na kuweka mikakati ya kuepusha malimbikizo ya madeni;
- (g) Kushughulikia mapendekezo ya kuboresha mishahara na maslahi ya viongozi wa elimu;
- (h) Kuendeleza majadiliano juu ya mapendekezo ya kuundwa kwa chombo maalumu cha kushughulikia ajira ya walimu; na
- (i) Kuandaa mapendekezo ya kuundwa kwa chombo cha walimu cha kitaalamu na kitaaluma (*Teachers Professional Board*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Idara ya Sera na Mipango itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuendelea na mazungumzo na Washirika wa Maendeleo ya Elimu ili kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa maabara za Sayansi na TEHAMA katika shule za sekondari za Serikali nchini ili kuboresha ufundishaji na utekelezaji wa mitaala iliyopangwa. Aidha, Serikali imeandaa mradi wa e-learning wa kufundisha wanafunzi kwa kutumia Tayari wizara imebaini aina ya kompyuta ambazo zitatumia betri kavu (dry cell) za AA na majoribio ya ufundishaji huu wa masafa utaanza kabla ya mwisho wa mwaka huu;

- (b) Kuendelea kukarabati miundombinu ya shule na vyuo ili kutoa mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia;
- (c) Kukamilisha maandalizi ya Sera mpya ya Elimu na Mafunzo na kuratibu uandaaji wa mkakati wa utekelezaji;
- (d) Kuendelea kuimarisha mfumo wa usimamizi wa takwimu na taarifa za elimu (*database*) katika Halmashauri 105 zilizobaki kwa kushirikiana na UNESCO kupitia programu ya ESMIS;
- (e) Kuendelea kufanya mapitio ya matumizi ya fedha katika Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara na kuratibu Mpango wa kazi na Mtiririko wa Fedha za Wizara;
- (f) Kuandaa Mpango Mkakati wa utekelezaji wa *TEHAMA* kwa Wizara; na
- (g) Kuratibu na kufanya tafiti kuhusu Mipango, Miradi na Programu za Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kitakeleza yafuatayo:-

- (a) Kuratibu utoaji wa habari za maendeleo ya elimu kwa jamii na kuhamasisha ushiriki wao kupitia vyombo vyta habari na kujibu hoja kutoka tovuti ya wananchi (www.wananchi.go.tz);
- (b) Kutayarisha vipindi 40 vya Redio na Televisheni ili kuifahamisha na kuihamasisha jamii kuhusu mikakati, changamoto na mafanikio ya sekta ya elimu katika kutekeleza mipango ya elimu;
- (c) Kuandaa, kuchapa na kusambaza nakala 300,000 za Jarida la *EdSDP* kwa kanda za elimu ili kuhamasisha jamii kushiriki katika kutekeleza mipango ya Elimu;
- (d) Kuandaa, kuchapa na kusambaza nakala 100,000 za kalenda na vipeperushi 5,000, mabango 500, vijarida 500 kwa ajili ya kuelimisha jamii kuhusu mafanikio na changamoto za utekelezaji wa mipango ya elimu; na
- (e) Kuandaa mkakati wa utoaji wa habari na mawasiliano juu ya programu za elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha, Wizara yangu inakusudia kuboresha utaratibu wa kuandaa na kusambaza vitabu vyta kiada na ziada katika shule za msingi na sekondari. Utaratibu uliopo sasa wa kila shule kununua vitabu vyta kiada na ziada kwa kutumia kamati au bodi za shule. Kwa kutumia utaratibu huu kila shule

imekuwa ikitumia vitabu tofauti na shule nyingine katika kutekeleza mtaala mmoja. Katika kutekeleza azma hii, wataalamu waliobobea katika kila somo watashirikishwa kikamilifu katika kuchagua vitabu bora vinavyofaa kutumika kama vitabu vya kiada na ziada.

Aidha, kamati ya kupitisha vitabu vya shule (*Educational Materials Approval Committee-EMAC*) itaendelea kupitisha vitabu vilivyo bora vinavyotungwa na kuchapishwa na wachapishaji mbalimbali. Vitabu vitakavyopendekezwa na jopo la wataalamu vitachaguliwa kuwa vitabu vya kiada.

Vitabu hivyo vitanunuliwa na kusambazwa na kutumiwa katika shule zote nchini (kama *standard Textbooks*,). Vitabu vingine vitanunuliwa kuwa vitabu vya rejea na kuwekwa katika maktaba za shule. Lengo la hatua hii ni kuwafanya wanafunzi kuwa na uelewa mmoja, kujenga utaifa na kuondoa tofauti baina ya shule na shule, wilaya na wilaya katika kutekeleza mtaala mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Ofisi ya Kamishna wa Elimu itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuijengea uwezo Taasisi ya Elimu Tanzania ili iweze kuandaa mitaala na kuchapa vitabu kwa ajili ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu;
- (b) Kuweka mazingira mazuri ya kisheria na kiutendaji kwa wadau ili washiriki kupanua elimu katika ngazi zote pamoja na kuimarisha uendeshaji na kukuza utamaduni wa Taifa;
- (c) Kuendelea kutoa mafunzo ya walimu kazini kwa walimu 43,000 katika masomo ya Hisabati, Sayansi na *English*;
- (d) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na viwango vya elimu vilivyowekwa na kuandaa na kuratibu mitaala na mitihani;
- (e) Kuendelea kuratibu utoaji wa elimu katika ngazi ya Awali, Msingi, Sekondari, Elimu ya Ualimu, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi;
- (f) Kuandaa utaratibu wa kuwawezesha wanafunzi wanaopata ujauzito kuendelea na masomo baada ya kujifungua;
- (g) Kuratibu na kufanya tafiti kuhusu fursa, usawa na ubora wa elimu katika sekta ya elimu;
- (h) Kuendesha mafunzo ya Elimu Jumuishi kwa walimu 384, wakufunzi 56, na wakaguzi wa shule 70;

- (i) Kununua na kusambaza vifaa maalumu vya kufundishia na kujifunzia; na visaidizi kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu;
- (j) Kufanya ufuatiliaji wa utoaji wa elimu na uanzishaji wa Shule/Vitengo vya Elimu Maalumu/Elimu Jumuishi katika Halmashauri 16;
- (k) Kutoa mafunzo elekezi kwa Waratibu wa Elimu Maalumu (W) 76 na mafunzo maalumu kuhusu matumizi ya vifaa maalumu kwa walimu wataalam 240;
- (l) Kusajili shule 120 zisizo za Serikali na shule 220 za sekondari za zinazojengwa kwa nguvu za wananchi;
- (m) Kuchambua maombi 200 ya vibali vya kujenga shule zisizo za serikali na kuthibitisha wamiliki na mameneja wa shule;
- (n) Kuchambua na kutoa leseni za kufundisha kwa walengwa 500;
- (o) Kufuatilia utekelezaji wa masharti ya usajili wa Shule katika mikoa 5 ya Shinyanga, Mara, Ruvuma, Rukwa na Kilimanjaro;
- (p) Kuandika na kusambaza matokeo ya utafiti wa Kimataifa kuhusu ubora wa Elimu katika Nchi 15 za Kusini na Mashariki ya Afrika SACMEQ *Research Project III*;
- (q) Kuandaa na kutangaza vipindi 52 vya Boresha Elimu, vipindi 52 vya redio vya ufundishaji kuhusu mbini shirikishi na vipindi 528 vya masomo ya English, Sayansi, Kiswahili Darasa la V, VI na VII; Historia, Jiografia na Uraia Darasa la III, IV, V na VI na Maarifa ya Jamii Darasa la VII;
- (r) Kuandaa, kuchapa na kusambaza nakala 397 za Mpango Mkakati wa Ushauri na Unasihi katika Shule na Vyuo vya Ualimu, nakala 40,000 za mwongozo wa Ushauri na Unasihi, nakala 1,000 za Mpango Mkakati wa Elimu ya UKIMWI wa mwaka 2008 – 2012 na nakala 20,000 za Mwongozo wa utoaji wa huduma na faraja kwa wafanyakazi
- (s) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya UKIMWI shulenii, vyuoni na mahali pa kazi katika mikoa 5 yenye kiwango cha juu cha maambukizi ya VVU na UKIMWI ambayo ni Iringa, Dar es Salaam, Mbeya, Mara, Shinyanga na 5 yenye kiwango cha chini ambayo ni Manyara, Arusha, Kigoma, Kilimanjaro na Singida;

- (t) Kukamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa utekelezaji wa masuala ya kielimu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia na kuandaa na kusambaza vipeperushi vya kuhamasisha usawa wa kijinsia katika elimu;
- (u) Kugharamia Mafunzo ya Ushauri na Unasihi kwa Wawezeshaji 200 wa Shule za Msingi na walimu wapya 200 wa Shule za Sekondari;
- (v) Kutoa mafunzo ya Elimu Rika na Unasihi kwa walimu 300 wa shule za msingi wanaofundisha masomo yenye mada za UKIMWI na kuandaa Mwongozo wa Elimu Rika kwa shule za sekondari Kidato cha 3 na 4;
- (w) Mafunzo ya Utetezi wa Ushauri na Unasihi kwa Maafisa 300, mafunzo kwa walimu 800 katika shule mpya za sekondari kuhusu stadi za ufundishaji wa Elimu ya UKIMWI, Stadi za Maisha na Unasihi na mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa taasisi za elimu kwa ngazi ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu;
- (x) Kuelimisha na kuhamasisha elimu ya Mazingira; kutayarisha mwongozo wa kufundishia elimu ya mazingira kwa shule za sekondari pamoja na kuchapa na kusambaza nakala 6,000 za vitini vya kufundishia mada ngumu za elimu ya mazingira kwa somo la stadi za kazi katika Shule za msingi;
- (y) Kuhamasisha wafanyakazi 300 wa makao makuu ya wizara kuhusu kupima afya kwa hiari hususan VVU na kushiriki mafunzo ya unasihi mahali pa kazi;
- (z) Kufuatilia utekelezaji wa utumiaji wa Mwongozo wa kufundishia elimu ya mazingira katika shule na vyuo; na

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kutekeleza awamu ya pili ya MMEM (2007-2011) kwa lengo la kuhakikisha kwamba azma ya serikali ya kutoa elimu bora ya awali na msingi kwa wote inafikiwa. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na wadau wengine itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Uandikishaji wa wanafunzi 1,399,100 katika Elimu ya Awali wenye umri wa miaka 5 – 6, wanafunzi 1,232,570 wa darasa la kwanza na wanafunzi wa MEMKWA Kundu Rika la kwanza ili waingizwe kwenye mfumo rasmi;
- (b) Kugharamia ujenzi wa shule za msingi za mfano zikiwemo zile zinazolenga kuimarisha ushiriki wa jamii za wafugaji katika Elimu ya Msingi na ukarabati wa shule kumi;

- (c) Kuandaa machapisho ya MMEM, miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa MMEM II, kuchapa na kusambaza kwa watendaji wa ngazi zote na kufuatilia matumizi yake katika kutoa huduma bora za elimu;
- (d) Kufanya ufuatiliaji, tathmini na ukaguzi wa fedha za MMEM na mapitio ya MMEM ikiwa ni sehemu ya mapitio ya Sekta ya Elimu kwa lengo la maandalizi ya MMEM awamu ya tatu;
- (e) Kuratibu utoaji wa mafunzo kazini kuhusu ufundishaji unaolenga ujuzi na maarifa kwa walimu mabingwa 3,000 na wengine 40,000 wakiwemo wa masomo ya Hisabati, Sayansi na lugha ya Kiingereza kuititia vituo vya walimu vinavyoimariswa mwaka hadi mwaka;
- (f) Kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya vituo vya walimu, shule za mazoezi na shule za mfano; na shule za msingi za wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu;
- (g) Kujenga uwezo wa wataalam 10 wa Idara, viongozi na wasimamizi wa elimu 494 wa ngazi mbalimbali wakiwemo Maafisa Elimu wapya;
- (h) Kufuatilia matumizi ya ruzuku ya uendeshaji ya shilingi bilioni 80 sawa na shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwa ajili ya uboreshaji wa elimu. Fedha hizi zinalengwa kutumika kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vitabu vya kiada, ukarabati, utawala na mitihani katika Halmashauri;
- (i) Kuwezesha utoaji wa elimu ya masuala mtambuka katika shule za msingi;
- (j) Kufuatilia ulipaji wa madeni ya walimu;
- (k) Kuratibu uandaaji na uendeshaji mitihani ya darasa la IV na VII na kufanya tathmini zake;
- (l) Kufuatilia utekelezaji wa mradi wa BridgeIt awamu ya pili itakayoanza Oktoba, 2009;
- (m) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Mpango wa Shule Zenye Mazingira yanayomjali mtoto, Mradi wa Lishe Shulenii, BridgeIt na Mpango wa pamoja wa kutoa huduma za makuzi, malezi na maendeleo ya mtoto (*Joint Integrated Early Childhood Development Service Delivery*);
- (n) Kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa mashindano ya michezo shulenii kwenye ngazi ya taifa; na
- (o) Kufanya utafiti wa hali halisi (*School Mapping*) ya shule za msingi kwa lengo la kujua uwepo na mahitaji muhimu yakiwemo umbali kati ya shule na makazi, uendeshaji na mahusiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, kwa kushirikiana na wadau wa elimu, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanza utekelezaji wa matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji katika shule za sekondari. Mradi huu unalenga kupunguza tatizo la upungufu wa waalimu shulenii kwa mwalimu mmoja kufundisha wanafunzi wengi katika shule nyingi kwa wakati mmoja.

Mazungumzo yanaendelea na asasi mbalimbali za nje ya nchi ili kuanza majaribio ya mradi huo (*Pilot Project*) wa matumizi ya TEHAMA katika shule chache mwaka huu na kisha kuona namna ya kusambaza teknolojia hiyo kwa shule zote za sekondari nchini kwa awamu kuanzia mwaka 2010. Kupitia mradi huo serikali inakusudia:-

- (i) Kumpatia kila mwalimu wa sekondari kompyuta ya kufundishia;
- (ii) Kuwa na maktaba ya digital katika shule zetu yenyeye rasilimali za vitabu vyote vya kiada;
- (iii) Kuwa na mada za masomo yote na (iv) kuunganisha kompyuta ya kila mwalimu na maktaba hiyo ya shule. Mradi huu utaongeza ufanisi wa mwalimu na kuwaongezea wanafunzi hamasa ya kujifunza;
- (b) Kuhamasisha upanuzi wa nafasi za kidato cha 5 na 6 kwa kusajili shule zaidi za ngazi hiyo zinazojengwa na Halmashauri baada ya kutimiza vigezo muhimu vinavyotakiwa. Upanuzi wa nafasi hizo utapewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari awamu ya II;
- (c) Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa wahisani mbalimbali ili kujenga maabara 3 za masomo ya sayansi (*Phyisics, Chemistry and Biology*) katika kila shule ya serikali kuanzia mwaka 2010. Wahisani ambao wameonyesha utayari kuhisani Mradi huu ni Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) na Benki ya BADEA;
- (d) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mitaala ya Elimu ya Sekondari;
- (e) Kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari wa awamu ya I na kukamilisha utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya II. Wadau mbalimbali wakiwemo Benki ya Dunia wameonyesha nia ya kuhisani mpango huo kuanzia mwaka 2010;
- (f) Kutoa mafunzo kazini kwa walimu 3,000 wa masomo ya Hisabati na Sayansi kupitia mradi wa kuwajengea uwezo walimu wa sayansi unaotarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka huu baada ya mradi kusainiwa kati ya serikali yetu na Shirika la Maendeleo JICA;
- (g) Kuandaa kambi za masomo ya sayansi na programu za TUSEME ili kuwajengea uwezo wanafunzi wa kike katika masomo ya sayansi;

(h) Kuendelea kugharimia walimu 40 wa Hisabati mwaka wa 3 wa Shahada ya Kwanza Chuo Kikuu Tumaini; (i) kufanya mapitio ya kitabu cha Kiongozi cha Mkuu wa Shule;

(j) Kutoa mafunzo kwa wawezeshaji 480 wa masomo ya Sayansi na Hisabati katika ngazi ya taifa na mikoa;

(k) Kukamilisha masuala yote ya ugatuaji wa uendeshaji na usimamizi wa shule za sekondari kwenda Halmashauri. Miongozo na taratibu na mafunzo kwa wahusika wote vinaandalialiwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI. Fedha za uendeshaji wa shule za sekondari zikiwemo za ujenzi, chakula, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ufadhilli wa wanafunzi kutoka familia zenye kipato duni zimetengwa kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu itatekeleza yafuatayo: -

(a) Kuandaa walimu 12,560 wa ngazi ya Cheti, 9,286 wa Stashahada na 320 wa fani maalum za michezo, muziki, sanaa za maonesho/ufundi, kilimo, biashara, ufundu na sayansi kimu ngazi ya Cheti na Stashahada. Katika mwaka 2009/2010 kutakuwa na wahitimu 6,946 wa ngazi ya Cheti na 7,656 wa Stashahada. Aidha, walimu 5,331 wenye Shahada ya ualimu watahitimu katika Vyuo Vikuu nchini na kufanya jumla ya wahitimu wa ualimu wenye sifa ya kufundisha Shule za Sekondari kufikia 12,987 katika mwaka huu wa fedha;

(b) Kutoa mafunzo kazini kwa walimu 1,500 ya ufundishaji wa masomo ya Hisabati, Kiswahili, Kifaransa, Kiingereza na Sayansi kwa shule za Msingi na Sekondari;

(c) Kuboresha mazingira ya kutolea mafunzo katika Vyuo vya Ualimu kwa kutoa vifaa bora vya kufundishia na kujifunzia;

(d) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza katika Vyuo vya Ualimu pamoja na kuunganisha mtandao wa TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu vya Shinyanga na Dakawa. Aidha, wizara itaunganisha maabara za TEHAMA za Vyuo vya Ualimu 34 vya Serikali ili kurahisisha mawasiliano, kuwajengea uwezo wanachuo ili waweze kufundisha kwa TEHAMA na kuwawezesha wakufunzi na wanachuo kuchangia makala mbalimbali kulingana na michepoo ya masomo yao;

(e) Kutekeleza Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Walimu (*Teacher Development and Management Strategy-TDMS*) na kujenga uwezo wa watendaji katika ngazi ya mikoa 21 na wilaya 131 pamoja na Vyuo vya Ualimu vya serikali 34 na visivyo vya Serikali 43;

(f) Kutekeleza Mradi wa Elimu ya Michezo (Januari 2009 hadi Desemba 2011) katika Vyuo vya Ualimu 12 vya Serikali kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali liitwalo Liike la Finland;

(g) Kutayarisha vigezo vya ubora wa walimu (*Teacher Competency Framework*) pamoja na kuendesha mafunzo ya walimu kazini katika wilaya 7 za majoribio Mtwara Vijijini, Makete, Bagamoyo, Temeke, Hai, Siha na Magu kwa kushirikiana na UNESCO pamoja na UNICEF;

(h) Kutoa mafunzo kwa wakufunzi 240 kuhusu uwezeshaji wa masuala ya Afya ya Uzazi, Elimu ya UKIMWI na Stadi za Maisha;

(i) Kushirikiana na mpango wa pamoja wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa katika kuendesha mafunzo ya mbinu za Ufundishaji Bainifu na Elimu ya UKIMWI kwa Wakufunzi 36, Walimu wa shule za Msingi 190 na Walimu wa shule za Sekondari 40 wa Mkoa wa Kigoma;

(j) Kugharimia mafunzo ya walimu wa leseni 637 wanaosomea ualimu Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na watumishi wengine 295 (Shahada ya Uzamivu 4, Uzamili 21, Shahada ya Kwanza 270); na

(k)Kushirikiana na shirika la USAID katika kukamilisha maabara 3 za Lugha katika vyuo vya Butimba, Morogoro na Mtwara (U).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Idara ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi itatekeleza yafuatayo: -

(a)Kudhamini wanafunzi 650 wa mafunzo ya Stashahada katika Chuo cha Ufundu Arusha wakiwemo 50 wa fani mpya ya maabara;

(b)Kuratibu upatikanaji wa rasilimali watu kwa ajili ya vyuo vya ufundu stadi vya mikoa 4 vitakavyoanza kutoa mafunzo ya Stashahada na kuvitayarisha vyuo vingine vya mikoa minne kwa ajili ya kutoa masomo hayo katika mwaka 2010/2011;

(c) Kuratibu maandalizi ya ujenzi wa vyuo vya ufundu stadi katika wilaya 28 na kukarabati vyuo 3 vinavyoendeshwa na wilaya;

(d) Kuendelea kudhamini watumishi 2 wa Idara katika mafunzo ya Shahada ya Uzamili na watumishi 8 katika mafunzo ya muda mfupi;

(e)Kuendelea kufanya uchambuzi wa mahitaji ya stadi katika wilaya 15;

(f)Kuratibu ujenzi wa vyuo vya ufundu stadi vya Mikoa ya Lindi, Manyara, Pwani na Dar es Salaam;

(g) Kuimarisha Chuo cha Ualimu cha VETA Morogoro ili kuongeza walimu katika vyuo vya mafunzo ya ufundi Stadi;

(h) Kuratibu na kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimatafa katika ufundi na teknolojia;

(i) Kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (MMEU);

(j) Kuendeleza mashauriano na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto juu ya kuviongezea uwezo vyuo vya maendeleo ya wananchi 35 ili vitoe mafunzo ya ufundi stadi; na

(k) Kupanua Elimu ya Ufundi ngazi ya cheti na stashahada.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Idara ya Elimu ya Juu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudhamini wanafunzi 1,700 wa Shahada ya Kwanza ya Udaktari, kati yao madaktari wa binadamu 1,614, meno 36 na tiba ya mifugo 50 katika Vyuo Vikuu nchini;

(b) Kudhamini wanafunzi 90 raia wa Uganda katika utaratibu wa kubadilishana wanafunzi wa Shahada ya Kwanza katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki na wanafunzi 5 raia wa China ikiwa ni kutekeleza mkataba wa Ushirikiano kati ya Tanzania na China katika Vyuo Vikuu nchini;

(c) Kuendelea kuelimisha Umma kuhusu dhana ya uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu na fursa za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi kupitia vyombo vya habari, maonyesho ya Taasisi za Elimu ya Juu na kutembelea wadau wa elimu;

(d) Kuratibu utoaji wa mikopo kwa wanafunzi 69,442 wa elimu ya juu kwa mwaka huu ambapo Serikali imetenga Shilingi bilioni 117 na Shilingi bilioni 80.3 zitatolewa katika nusu ya pili ya mwaka 2009/2010 wakati wa mapitio ya Bajeti (*Budget Review*);

(e) Kudhamini mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu kwa wanataluma 100 kutoka vyuo vikuu vya umma;

(f) Kudhamini mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu kwa wanataluma 20 kupitia mradi wa DAAD;

(g) Kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kulingana na Mpango wa Maendeleo wa Chuo hicho;

(h)Kuratibu uteuzi wa wanafunzi 100 kwa nafasi zitakazotolewa na nchi rafiki ambazo ni Algeria, Poland, China, Cuba, Urusi, Uingereza, Malasyia, Pakistani, Uturuki, Misri na New Zealand;

(i) Kuratibu mafunzo na ufadhilli wa wanafunzi 100 wa kike wanaofadhiliwa na Shirika la Shirin Pandu Merali Foundation la Marekani;

(j)Kukamilisha Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu (MMEJU); kwa sasa Serikali iko kwenye majadiliano na wahisani mbalimbali ili kupata fedha za utekelezaji wa mpango huo. Lengo la mpango huu ni kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu ya Vyuo Vikuu vya Umma, kujenga kumbi za kufundishia, maabara na karakana, mabweni mapya, maktaba na miundombinu za TEHAMA ili kuboresha elimu ya juu na kuongeza udahili;

(k)Kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Sayansi na Teknolojia katika Elimu ya Juu (*Science, Technology and Higher Education Project*) unaodhaminiwa na Benki ya Dunia na unaolenga kuimarisha ufundishaji wa sayansi na kusomesha wahadhiri katika Elimu ya Juu. Mradi huu wa miaka mitano utatumia Dola za kimarekani milioni 200;

(l) Kuratibu ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vikuu vya umma wenyе lengo la kuboresha mazingira ya kufundishia;

(m) Kufanya mapitio ya gharama halisi za kumsomesha mwanafunzi wa Elimu ya Juu (*Unit Cost review*) kutokana na mabadiliko ya gharama za uendeshaji;

(n) Kuratibu utekelezaji wa mikataba ya kuendeleza, kuimarisha na kuboresha Elimu ya Juu nchini;na

(o) Kutafuta njia mbadala ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, idara ya ukaguzi wa shule imeongezewa bajeti kwa ajili ya kuimarisha kazi ya ukaguzi wa shule kwa lengo la kuhakikisha kwamba azma ya Serikali ya kutoa elimu bora inatekelezwa. Hatua hii itawezesha kuanza kazi rasmi kwa kanda tatu mpya, kuboresha mazingira ya wakaguzi kwa kununua magari, vitendea kazi na kuongeza idadi ya wakaguzi wa shule. Hivyo, idara ya ukaguzi wa shule itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukagua jumla ya asasi 20,094 sawa na asilimia 43 ya asasi 46,614 zilizopo kwa kufanya ukaguzi wa jumla, wa kufuutilia na maalum (Kielelezo cha 2);

(b) Kukarabati ofisi 20 za wilaya, kununua samani za ofisi 10 za wilaya na magari 27 ya ofisi za kanda na wilaya;

(c)Kuteua na kutoa mafunzo ya awali kwa wakaguzi wa shule wapya 150;

(d) Kufanya tathmini ya ubora wa ufaulu katika mitihani ya Taifa ya Elimu ya Msingi Darasa la IV,

(e)Kugharamia mafunzo kazini kwa watumishi 70 wa idara;

(f)Kugharamia posho ya vitabu kwa wakaguzi wa shule 100 wanaojiendeza Chuo Kikuu Huria;

(g)Kusimamia na kuendesha mitihani ya kidato cha 2;

(h)kufanya ufuatiliaji wa asasi/vituo vinavyotoa elimu ya awali, msingi, sekondari na elimu ya ualimu bila kufuata taratibu na kutoa mapendekoz stahili; na

(i) Kuandaa utaratibu mpya wa kufanya ukaguzi wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi itatekeleza yafuatayo: -

(a) Kununua na kusambaza vifaa vya kuwezesha kufundisha na kujifunza ambavyo ni televisheni, kanda za video, kaseti za redio, kamera na paneli za Sola kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya Ndiyo Ninaweza inayoendeshwa katika Halmashauri za majaribio za Temeke, Ilala, Kinondoni, Ilemela, Dodoma (M) na Songea (M); kuandaa filamu za masomo ya programu ya Ndiyo Ninaweza na kutoa mafunzo kwa wawezeshaji 122 wa programu ya Ndiyo Ninaweza katika wilaya za majaribio;

(b) Kuchapa vitabu vya wawezeshaji 122, wasimamizi 24, wanakisomo 1,840 na kuandaa mada (*scripts*) kwa ajili ya vipindi vya redio, televisheni na video;

(c) Kufanya ufuatiliaji wa programu za MEMKWA, MUKEJA na Ndiyo Ninaweza pamoja na programu ya menejinenti ya data za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo rasmi;

(d)Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi;

(e) Kufanya utafiti wa kisomo ili kubaini hali halisi ya kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu nchini;

(f) Kutoa mafunzo kwa watendaji 15 wa Idara kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi;

(g)Kutekeleza Mpango Mkakati wa Elimu kuhusu Haki za Binadamu katika Kanda ya Ziwa kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; na UNESCO; na

(h) Kuratibu ukarabati wa majengo ya Kituo cha Taifa cha Kisomo Mwanza na kituo cha uchapaji makao makuu ya Wizara (*Press A*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi, Wakala na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yangu yanafanikisha utoaji wa elimu bora. Wakala, Taasisi na Mabaraza yatakeleza kazi zilizopangwa kwa kuzingatia malengo na mipango ya elimu kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitakeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 6,850 kati yao 4,200 ni wa shahada ya kwanza na 2,650 shahada ya uzamili;
 - (b) Kuendeleza ushirikiano na serikali na wafadhili mbalimbali katika kugharamia utafiti na mafunzo;
 - (c) Kuendeleza na kukamilisha ujenzi wa madarasa, maabara na makumbusho ya Chuo kupitia mradi wa Benki ya Dunia;
 - (d) Kuendeleza ujenzi wa makao makuu mapya ya Taasisi ya Sayansi za Bahari (*Institute of Marine Science - IMS*) sehemu ya Buyu, Zanzibar;
 - (e) Kukamilisha ujenzi wa kumbi 2 za mihadhara zenyet uwezo wa kuchukua wanafunzi 1000 kila moja;
 - (f) Kukarabati mabweni 6 ya wanafunzi, madarasa na nyumba za wafanyakazi;
 - (g) Kukamilisha makabidhiano ya majengo ya Chuo cha Bima Mikocheni kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
 - (h) Kufuatilia ujenzi wa awamu ya tatu ya mradi wa Mlimani City utakaojumuisha hoteli ya kitalii na bustani ya wanyama;
 - (i) Kuajiri wafanyakazi 380 ili kukidhi ongezeko la wanafunzi na kujaza nafasi zilizoachwa wazi na waliostaifu na walioondoka; na
- (j) Kuanza awamu ya tatu ya ujenzi wa jengo la Skuli ya Biashara;
Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Skuli ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma itakeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 100 wa ngazi ya Shahada ya Kwanza, 20 Stashahada ya Uzamili, 20 Shahada ya Uzamili, 40 wa ngazi ya Cheti na 30 Cheti cha Awali;

- (b) Kujenga madarasa mawili (2) na ukumbi mmoja (1) wa mihadhara;
- (c) Kuajiri wataalamu 5 na wahadhiri 10;

- (d) Kuongeza masafa ya utangazaji kwa Redio Mlimani na Televisheni Mlimani;
- (e) Kuanzisha Shahada ya Uzamili ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma; na
- (f) Kufanya utafiti wa kitaaluma na kitaalamu katika nyanja za mawasiliano ya umma na matangazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2009/2010 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 1,150 kati ya hao 150 wa fani ya sayansi;
- (b) Kukamilisha ujenzi wa kumbi 3 za mihadhara (*Lecture Theatres*);
- (c) Kununua vifaa vya maabara na vifaa vya kufundishia na kujifunza kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu;
- (d) Kununua samani za maktaba na vitabu zaidi vya kufundishia;
- (e) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA;
- (f) Kutoa mafunzo maalum kwa wadahiliwa wa kike 50 kwenye fani ya sayansi kwa lengo la kuongeza wahitimu wa kike kwenye fani hiyo;
- (g) Kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hasa kwa shahada za uzamili na uzamivu; na
- (h) Kujenga kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi wapya 800 wa Shahada ya Kwanza na hivyo kufanya idadi ya wanachuo kufikia 2,200;
- (b) Kuanza mchakato wa ujenzi wa mabweni ya wanafunzi;
- (c) Kuendelea na upanuzi wa maktaba awamu ya pili ambao utaongeza nafasi 960 za wasomaji ili kufikia hitaji la msingi la asilimia 60 ya wanafunzi kuweza kutumia maktaba;

- (d) Kuanza ujenzi wa ukumbi wa miadhara ambao utakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000;
- (e) Kununua vifaa vya maabara na magari 3 kwa ajili ya Wakuu wa Vitivo;
- (f) Kuendelea kukarabati barabara za Chuo;
- (g) Kuanza ujenzi wa jengo la utawala ambalo litaongeza nafasi za ofisi;
- (h) Kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la Chuo;
- (i) Kuajiri wahadhiri 92 na wafanyakazi waendeshaji 40; na
- (j) Kugharamia mafunzo kwa wahadhiri 20 (Shahada ya Uzamili16 na Uzamivu 4).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 1,571 wa shahada ya kwanza na 513 wa shahada ya uzamili;
- (b) Kuanzisha ufundishaji wa kutumia TEHAMA na kuongeza upatikanaji wa vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia;
- (c) Kuongeza pato la ndani kutoka shilingi 4,512,628,391.00 kufikia shilingi 7,347,618,851.85;
- (d) Kujenga kumbi nne (4) za miadhara zenyе uwezo wa kukaa wanafunzi 250 kila moja, maabara tatu (3) zenyе uwezo wa kukaa wanafunzi 60 kila mmoja, kukamilisha ujenzi wa mabweni mawili (2) ya wanafunzi zenyе uwezo wa kulaza jumla ya wanafunzi 1,320 na kuanza mengine mawili zenyе uwezo unaofanana; na
- (e) Kuendelea kutoa elimu na ushauri kwa wakulima kwa kutumia semina, warsha na kozi fupi na kuanza ujenzi wa Kitivo cha Sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 2,186 mwaka 2008/2009 hadi kufikia wanafunzi 2,450 mwaka 2009/2010;

- (b) Kuendeleza mafunzo ya wafanyakazi, hususani Wahadhiri 20 katika kiwango cha Shahada ya Uzamivu;
- (c) Kuboresha utafiti na uchapishaji wa makala mbalimbali ili kusambaza elimu inayokidhi mahitaji ya sasa ya jamii, ikiwa ni pamoja na vyama vya ushirika vya akiba na mikopo, (SACCOS), maendeleo ya ushirika;
- (d) Kuimarisha Matawi manne ya kanda: Mtwara, Iringa, Mwanza na Tanga ili kuielimisha jamii katika masuala ya vyama vya ushirika vya akiba na mikopo na maendeleo ya ushirika katika sekta za kilimo, Madini, uvuvi na huduma;
- (e) Kuimarisha na kuongeza kiwango cha huduma za utafiti na ushauri kwa kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi;
- (f) Kuimarisha mipango ya uenezi wa elimu ya ushirika kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, COASCO na Muungano wa Vyama vya Ushirika (TFC);
- (g) Kuchukua hatua za makusudi kushughulikia mahitaji ya jamii katika masuala mtambuka, kama jinsia, UKIMWI, walemavu, mazingira na wastaaifu;
- (h) kukamilisha utekelezaji wa masharti yaliyotolewa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu ili kukiwezesha Chuo kupanda daraja na kuwa Chuo Kikuu kamili (*Fully Fledged University*); na
- (i) Kukamilisha maandalizi ya Mpango Mkakati wa Chuo kwa mwaka 2009/2010 - 2014/2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Chuo Kikuu Dodoma kitakeleza yafuatayo:-

- (a) Matarajio ya kudahili wanafunzi 9,810 wa Shahada mbalimbali; na hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 17,282 katika mwaka 2009/2010. Aidha, Chuo kitaanzisha Shahada mpya 28;
- (b) Kuendeleza ujenzi wa Chuo cha Tiba na Chuo cha Sayansi Asili na Hisabati na kuanzisha Skuli ya Tiba, Skuli ya Uuguzi, Skuli ya Sayansi za Asili, Hisabati na Skuli ya Sayansi za Ardhi;
- (c) Kuandaa mkakati wa Mawasiliano na Taarifa kwa mbinu za kisasa;
- (d) Kuajiri wanataaluma 300 kati yao 80 kutoka nje ya nchi na wafanyakazi waendeshaji 260;

- (e) Kuendeleza ujenzi wa jengo la utawala, ofisi na barabara mzingo pamoja na mtandao wa maji safi na maji taka; na
- (f) Kuendelea kufanya tafiti 14 kwa kushirikiana na watafiti wengine wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Chuo Kikuu Mzumbe kitakeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 2,310, kati ya hao 1,215 katika Cheti, Stashahada na Shahada ya Kwanza na 1,095 katika Shahada za Uzamili;
- (b) Kugharamia mafunzo kwa watumishi 15 katika ngazi ya Shahada za Uzamivu na wengine 38 katika ngazi ya Shahada za Uzamili;
- (c) Kukamilisha ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 400 katika Kampasi Kuu Mzumbe;
- (d) Kukamilisha ujenzi wa ofisi za wahadhiri zenyne uwezo wa kuhudumia wahadhiri 100 na maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wasomaji 400 kwa wakati mmoja kwenye Kampasi ya Mbeya;
- (e) Kukamilisha malipo ya viwanja 3 vilivyopo Upanga, kwa ajili ya upanuzi wa Skuli ya Dar es Salaam;
- (f) Kukamilisha tafiti 20 na kutoa ushauri katika maeneo 35 ya menejimenti, uongozi na sayansi ya jamii;
- (g) Kuchapisha vitabu 6, makala za kufundishia 6 na makala nyingine 30; na
- (h) Kuajiri wahadhiri 37 na wafanyakazi waendeshaji 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimejizatiti kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 3,000. Kwa sasa chuo kina jumla ya wanafunzi 28,935;
- (b) Kufanya ukarabati wa majengo ya vituo vilivyopo Kilimanjaro, Zanzibar, Njombe na Mpanda;
- (c) Kukarabati na kumalizia ujenzi wa majengo ya TUFTA katika mikoa ya Tanga na Kagera ili yaweze kutumiwa kwa ubia;

- (d) Kuendelea kushirikiana na Vyuo Vikuu Huria vya Africa (ACDE) katika shughuli za kitaaluma;
- (e) Kufungua vituo vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania nchini Rwanda na Uganda;
- (f) Kutoa mafunzo ya awali ya kompyuta kwa wanafunzi wanaojiunga na Chuo;
- (g) Kufanya ukarabati wa majengo ya PEHCOL mkoani Kilimanjaro;
- (h) Kuanza ujenzi wa ofisi za kituo cha mkoa wa Mtwara kwa mkopo uliotolewa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA);
- (i) Kuanza kutoa mafunzo ya Shahada mpya ya Uzamili ya Sheria (LLM) kwa kutumia Teknolojia ya Mawasiliano na Simu; na
- (j) Kuanza ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya Chuo Bungo wilayani Kibaha kwa kuanza na Ofisi ya Mapokezi, Bohari na madarasa mawili ya kufanyia mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2009/2010 Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 350 wa fani mbalimbali za tiba na afya na kuweka samani na umeme katika majengo;
- (b) Kukamilisha tathmini na kuwalipa fidia wananchi wa eneo la Mloganzila, kujenga barabara na kupeleka umeme na maji katika eneo hilo;
- (c) Kuajiri Wahadhiri 59 katika idara mbalimbali za kitaaluma zilizopo chuoni;
- (d) Kuendeleza ujenzi wa kantini katika hosteli za Chole na kujenga ukuta kuzungukia enelo la hosteli; na
- (e) Kuendelea na tafiti za magonjwa yanayoathiri jamii yakiwemo malaria, afya ya uzazi, kifua kikuu na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2009/2010 Chuo Kikuu Ardhi kitatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 883 wa Shahada ya kwanza 200 wa Shahada za Uzamili na Uzamivu, kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike kufikia asilimia 30 ya wanafunzi wote;

- (b) Kukamilisha zoezi la kuhuisha miongozo na taratibu za uendeshaji wa Chuo ili iendane na hadhi ya Chuo Kikuu kinachojitegemea na kuimarisha utendaji wa Skuli na Idara za mafunzo;
- (c) Kugharamia mafunzo ya wahadhiri wapya 25 na wafanyakazi waendeshaji 16. Wahadhiri 10 watasomeshwa kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia;
- (d) Kuboresha huduma za utafiti na ushauri wa kitaalamu ili kuboresha maisha ya jamii na maendeleo ya taifa kwa ujumla;
- (e) Kuanzisha mafunzo ya shahada za Uzamili za Makazi; Menejimenti na Athari za Maafa (*Disaster Risk Management*); Shahada za Kwanza za Usimamizi wa Biashara, fedha, uhasibu, benki na masoko; Shahada za Kwanza za Sayansi za Kompyuta na Mawasiliano; Teknolojia na Usimamizi wa Mfumo wa Mawasiliano; Uchoraji na GIS; Uhandisi Ujenzi; Uchumi na Taaluma za Maendeleo (*Development Studies*); na Stashahada ya Uzamili ya Makazi;
- (f) Kukamilisha Awamu ya Pili ya kuweka huduma ya Intaneti katika majengo ili kukuza matumizi ya TEHAMA chuoni;
- (g) Kukamilisha awamu ya 4 na ya 5 ya ujenzi wa jengo jipya kwa ajili ya mihadhara, madarasa, ofisi za walimu na kuanza awamu ya kwanza na ya pili ya ujenzi wa jengo jingine jipya (*Observation Hill Building*) kwa ajili ya shughuli za kitaaluma;
- (h) Kufanya ukarabati wa mabweni, ofisi, madarasa, nyumba za wafanyakazi, barabara na njia za watembea kwa miguu na miundo msingi ya usambazaji wa maji, umeme na huduma nyingine muhimu;
- (i) Kufanya tafiti 65 katika maeneo ya maafa, ardhi na makazi kutohana na shughuli za uchimbaji madini na kuainisha mikakati ya kupunguza athari zake; na kufanya tafiti juu ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi pembezoni mwa miji;
- (j) Kukamilisha zoezi la ununuzi wa ekari 2,000 (hekta 810) katika Kijiji cha Kikongo Mlandizi, Mkoa wa Pwani kwa ajili ya upanuzi wa baadaye wa shughuli za Chuo; na
- (k) Kununua vifaa vya upimaji, ujenzi wa maabara ya gesi ya kinyesi cha wanyama, vitabu, vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano, kujenga miundombinu kwa ajili ya ufundishaji kwenye Skuli ya Sayansi ya Mazingira, kujisajili kwenye majorida ya kitaaluma na kununua *hardware* kwa ajili ya uchapishaji kupitia mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kitatkeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 130 wa Cheti, 300 wa Stashahada na 129 wa Shahada ya Kwanza;
- (b) Kuajiri wanataaluma 15 na wafanyakazi waendeshaji 10;
- (c) Kugharamia mafunzo kwa wanataaluma 10 na wafanyakazi waendeshaji 10;
- (d) Kukarabati Mabweni ya Azimio na Mwongozo na kujenga uzio eneo la Chuo - Dar es Salaam; na
- (e) Kuanza ujenzi wa Tawi la Chuo eneo la Bububu – Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Chuo cha Ufundii Arusha kitatkeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi 205 katika ngazi ya Stashahada; katika programu 7 za Cheti cha Ufundii na Stashahada katika fani za Uhandisi za Magari, Ujenzi, Mitambo, Umeme, Barabara, Elekroniki na Mawasiliano Anga;
- (b) Kuanzisha programu mpya ya Sayansi ya Maabara na Teknolojia;
- (c) Kununua vifaa na zana za kisasa za kufundishia katika maabara na karakana ili kuboresha ufundishaji na kujifunza;
- (d) Kukarabati bweni moja la wavulana na baadhi ya nyumba za wafanyakazi;
- (e) Kuboresha na kuimarisha masomo ya jioni pamoja na part time courses ili kuongeza udahili wa wanafunzi;
- (f) kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya Chuo ikiwa ni pamoja na kupata hati miliki;
- (g) Kujenga maabara 3 za kozi ya Sayansi ya Maabara na kuendeleza ujenzi wa hosteli ya wanafunzi 200;
- (h) Kuajiri wanataaluma 20 na wafanyakazi waendeshaji 16;
- (i) Kuendesha kozi ya awali ya kuijunga na chuo kwa wasichana;
- (j) Kugharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wanataaluma 25 na wafanyakazi waedeshaji 15; na

- (k) Kuhuisha mitaala 18 iliyopo na kuandaa mitaala mipyä 9 kwa programu 3 tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Tume ya Taifa ya *UNESCO* itatekeleza yafuatayo: -

- (a) Kuratibu ushiriki wa Taifa katika kuandaa Programu na Bajeti ya *UNESCO* kwa kipindi cha 2010-2011 na kuandaa ujumbe wa Serikali kwenye Kikao cha 35 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO*;
- (b) Kutathmini miradi ya *UNESCO* chini ya Participation Programme kwa kipindi cha 2008-2009 na kuratibu na kutathmini miradi itakayoidhinishwa kwa kipindi cha 2010-2011;
- (c) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuhifadhi Historia ya Ukombozi Barani Afrika;
- (d) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa miradi chini ya programu ya Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia itakayopata fedha;
- (e) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa wa mkataba wa ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Bangor, Uingereza na *UNESCO* unaohusu uanzishaji wa Kiti cha *UNESCO* (*UNESCO Chair*) katika Taasisi ya Sayansi ya Bahari Zanzibar ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (f) Kuendelea kuratibu maandalizi ya uzinduzi wa programu ya Uhuishaji wa Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa kushirikiana na *UNESCO* na wadau wengine;
- (g) Kuendelea kuratibu miradi chini ya programu ya Mwaka wa Kimataifa wa Astronomia itakayopata ufadhili;
- (h) Kutoa elimu kwa wadau na watendaji kuhusu utekelezaji wa programu ya Mwongo wa kimataifa wa Elimu kwa Maendeleo Endelevu;
- (i) Kukamilisha uundaji wa Bodi ya Tume ya Taifa ya *UNESCO* na kuajiri watumishi wapya wa kada mbalimbali;
- (j) Kuwapatia watumishi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ya kuwaongezea ujuzi na ufanisi kazini;
- (k) Kuendesha mafunzo kwa watumishi kuhusu mfumo wa wazi wakupima utendaji kazi kwa watumishi wa umma (*Open Performance Review and Appraisal System - OPRAS*);

- (l) Kutoa mafunzo ya elimu dhidi ya UKIMWI kwa watumishi wa Tume;
- (m) Kutayarisha vipindi nya redio na televisheni na makala na kuchapisha Jarida la Tanzania na *UNESCO* kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu kazi za *UNESCO* na Tume ya Taifa ya *UNESCO*;
- (n) Kutoa elimu kuhusu masuala mtambuka ya jinsia, rushwa na haki za binadamu; na
- (o) Kuimarisha mtandao wa *Associated Schools* na *Club za UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kutathmini ubora wa programu 20 za masomo ya vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki nchini kwa lengo la kuziidhinisha;
- (b) Kuendesha warsha na semina za mafunzo 10 za uelimishaji umma kuhusu majukumu ya Tume;
- (c) Kukamilisha mchakato wa kuandaa mfumo wa tuzo zinazotambuliwa kitaifa (*National Qualifications Framework*);
- (d) Kutathmini vyeti 200 nya wahitimu vitakavyowasilishwa ili kutambua uhalali wake;
- (e) Kuendelea kuratibu na kutathmini mradi wa majoribio ya udhibiti ubora wa vyuo vikuu 7 vinavyotekeleza mradi chini ya IUCEA;
- (f) Kutoa machapisho 10 yenye taarifa za kuelimisha umma kuhusu majukuku ya Tume, ufanisi wake, na kutoa miongozo kwa vyuo vikuu nchini kuhusu uthibiti wa ubora wa elimu ya juu;
- (g) Kukagua na kutathmini mipango ya kuanzisha/kuhuisha vyuo vikuu 5 kwa lengo la kutoa hati husika;
- (h) Kuendelea kusimamia udahili wa wanafunzi wapatao 40,000 ili kufikia lengo la kuwa na wanafunzi wapatao 300,000 kwenye taasisi za elimu ya juu nchini ifikapo mwaka 2015;
- (i) Kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi za kudumu za Tume;
- (j) Kuendelea kuratibu maonesho ya Elimu ya juu, Sayansi na Teknolojia;

na

(k) Kuendelea kuhamasisha wafanyakazi kuhusu masuala mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Mamlaka ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kutafuta rasilimali kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vyatapato ikiwa ni pamoja na wadau wa elimu walio ndani na nje ya nchi;
- (b) Kuendelea kutoa ufadhilli wa miradi ya elimu inayolenga kuongeza udahili na ubora wa elimu na kuleta usawa katika upatikanaji wa elimu katika ngazi zote;
- (c) Kuendeleza ushirikiano na Halmashauri zilizopo chini ya Muungano wa Serikali za Mitaa (*ALAT*) na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ikiwemo mifuko ya Elimu ya Wilaya ili kutekeleza miradi mbalimbali ya elimu;
- (d) Kukamilisha uandaaji wa rasimu ya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Elimu Na.8 ya mwaka 2001 iliyoanzisha Mfuko wa Elimu na Mamlaka ya Elimu Tanzania;
- (e) Kuelimisha na kuhamasisha umma kupitia majorida, vipindi vyatapato, televisiuni na tovuti ya Mamlaka ili kuhamasisha jamii kushiriki katika kuchangia miradi ya elimu;
- (f) Kuendelea kukagua na kufanya tathmini ya miradi ya elimu iliyofadhiliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania ili kubaini kama malengo tarajiwani yamefikiwa;
- (g) Kununua magari mawili (2) na vifaa vyatapato ofisi; na
- (h) Kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa jengo la ofisi za kudumu za Mamlaka ya Elimu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inathamini na imeweka kipaumbele cha pekee katika kuwapa mikopo wanafunzi wote wanaostahili kwa kuwa na sifa za kujiunga na elimu ya juu na kupewa mikopo. Katika mwaka 2009/2010, wanafunzi watakaopewa mikopo ni 69,442 ambao (i) wamefaulu kwa daraja la I-II katika mtihani wa taifa wa kumaliza Kidato cha Sita; na (ii) wamedahiliwa kusomea Shahada za ualimu au sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchaguliwa, wanafunzi wote 69,442 watapewa mikopo na Serikali. Jumla ya Shilingi 197,348,958,875 zimepangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia mikopo hiyo. Malipo hayo ni kwa ajili ya kulipia gharama za chakula na malazi (*Meals and Accommodation*), vitabu na viandikwa (*Books and*

Stationery) na utafiti (*Research*) kwa asilimia 100; na gharama za mafunzo (*Tuition Fees*), mafunzo kwa vitendo (*Field Practicals*) na mahitaji maalumu ya vitivo (*Special Faculty Requirements*) ambazo zitatolewa kwa kuzingatia matokeo ya upimaji wa uwezo wa mkopaji kiuchumi (*Means Testing*). Aidha, katika mwaka 2009/2010 mikopo wa vitabu na viandikwa umeongezwa kutoka Shilingi 120,000 hadi 200,000. Gharama anazochangia mwanafunzi katika Vyuo Vikuu vya umma ni kati ya asilimia 40 na 50 ya gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi. Gharama nyingine hugharimiwa moja kwa moja na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwavutia vijana kuchukua masomo ya sayansi; katika mwaka 2009/2010 wanafunzi wote watakaosomea masomo ya sayansi watapewa mikopo kwa asilimia 100. Taarifa za wanafunzi wengine zitahakikiwa kutumia vyombo vya serikali katika ngazi ya vijiji, kata na wilaya ili kuwapa mikopo kulingana na uwezo wa kiuchumi wa kila mwombaji. Katika mwaka 2009/10, madaraja ya mikopo yameongezwa kutoka madaraja 6 hadi 11; yaani A (100%), B (90%), C (80%), D (70%), E (60%), F (50%), G (40%), H (30%), I (20%), J (10%), na K (0%). Hatua hii inalenga kuongeza ufanisi na kupunguza malalamiko ya wanafunzi kwa kuongeza usahihi wa *Means Testing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 mahitaji halisi ya mikopo kwa wanafunzi 69,442 ni shilingi 197,348,958,875. Katika bajeti tunayojadili sasa shilingi bilioni 117 zimetengwa wakati shilingi bilioni 80.4 zitatolewa baadaye na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa mikopo ya elimu ya juu imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na kuwa mzigo mkubwa sana katika bajeti ya Serikali. Hivyo, Serikali inaangalia njia mbadala na endelevu ya kushughulikia mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Kazi hii inafanywa sasa na itakapomalizika Bunge lako tukufu litaarifiwa. Aidha, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya wajibu wa kila mmoja wetu kuchangia elimu ya juu, taratibu za utoaji mikopo pamoja na urejeshwaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundililatekeleza yafuatayo: -

- (a) Kukagua vyuo vya elimu ya ufundi na kutoa ithibati kwa vyuo 20;
- (b) Kukagua na kusajili vyuo 20 vya elimu ya ufundi vyenye uwezo wa kutoa mafunzo ya ufundi;
- (c) Kuhakiki na kutathimini utekelezaji wa masharti ya ithibati katika vyuo 20 vya elimu ya ufundi vyenye ithibati kamili;

- (d) Kuratibu na kuandaa mtaala wa elimu ya ufundi katika programu 25 zenyenye kuzingatia umahiri wa mwanafunzi na mahitaji ya soko la ajira;
- (e) Kukagua, kutathimini na kuwasajili walimu 500 wenye sifa za kufundisha katika vyuo vya elimu ya ufundi;
- (f) Kusimamia na kuviwezesha vyuo 20 vya elimu ya ufundi kuweka mfumo wa udhibiti na uhakiki wa ubora wa mafunzo yatolewayo;
- (g) Kuratibu mitihani ya elimu ya ufundi katika vyuo 30 vinavyotumia mtaala mpya unaozingatia umahiri wa mwanafunzi na mahitaji ya soko la ajira;
- (h) Kuratibu udahili wa wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi 17 vinavyotoa mafunzo ya elimu ya ufundi ngazi ya Shahada na Stashahada ya Juu;
- (i) Kuratibu mafunzo ya ufundishaji katika mfumo wa *Competence Based Education and Training* (CBET) kwa walimu kutoka vyuo 20 vya elimu ya ufundi; na
- (j) Kuimarisha ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi zenyenye majukumu kama ya Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu utatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kutoa mafunzo ya stashahada ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa viongozi 300 wa ngazi mbalimbali za Elimu;
- (b) Kutoa mafunzo ya cheti cha Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa walimu wakuu wa shule za Msingi 500 kwenye vyuo vya Ualimu;
- (c) Kutoa mafunzo ya mwezi mmoja ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Maafisa Elimu Taaluma Wilaya na Maafisaelimu Vifaa na Takwimu 120 kwa ufadhili wa JICA;
- (d) Kutoa mafunzo ya awali ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakuu wapya wa shule za sekondari 550;
- (e) Kutoa mafunzo ya mwezi 1 ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakuu wa Shule za Sekondari 240;

- (f) Kutoa mafunzo ya mwezi 1 ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakaguzi wapya Shule 200;
- (g) Kutoa mafunzo kwa maafisa 194 wakiwemo wa ngazi ya shule, kata na wilaya juu ya utayarishaji wa Mipango ya Jumla ya Maendeleo katika wilaya sita zinazofadhiliwa na UNICEF ambazo ni Bagamoyo, Makete, Temeke, Siha, Hai na Mtwara (V);
- (h) Kufanya tafiti 2 za kielimu kwa kushirikiana na nchi za Malawi, Uganda, Msumbiji na Afrika Kusini chini ya mradi wa LEAD Link; na
- (i) Kufanya ukarabati wa majengo na kuanza ujenzi wa hosteli na ukumbi wa mihadhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza yafuatayo: -

- (a) Kutoa mafunzo kwa walengwa wa Cheti 40, Stashahada 359, Stashahada ya Juu 355 na Cheti cha Sheria 200;
- (b) Kutoa mafunzo ya namna ya kufundisha kwa kutumia mtindo wa CBET kwa wakufunzi na wahadhiri;
- (c) Kutoa *Alumni Newsletter* Na. 4, kuandika na kuchapa masomo ya Ufundu na Biashara ya Kidato cha 5 na 6;
- (d) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana;
- (e) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Elimu ya sekondari kwa Masafa na Ana kwa Ana, kutoka 30,036 na hadi 50,000;
- (f) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera ya utafiti, ushauri na machapisho ya TEWW;
- (g) Kuzindua utekelezaji wa programu ya *Intergrated Post Primary Education-IPPE* katika wilaya saba za majaribio: Siha, Same, Makete, Bagamoyo, Temeke, Mtwara Vijijini na Magu;
- (h) Kuandaa mfumo wa ukusanyaji wa takwimu na taarifa za TEWW;
- (i) Kuanzisha na kuratibu mfumo wa ufuutilaji na tathmini ya maendeleo ya shughuli za TEWW;

- (j) Kugharamia watumishi 2 mafunzo ya Shahada ya Uzamivu, na 4 Shahada ya Uzamili, Sekondari 30 na 40 mafunzo ya muda mfupi;
- (k) Kuajiri watumishi 7 katika fani za Studio na Ufundu umeme wakiwamo na wahadhire;
- (l) Kununua magari 3 kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Elimu Masafa na masomo ya Ana kwa Ana;
- (m) Kukarabati jengo la Elimu kwa Njia ya Posta Makao makuu na ofisi za mikoa ya Kilimanjaro, Ruvuma na Morogoro;
- (n) Kuunganisha makao makuu TEWW na vituo vitano katika mtandao wa mawasiliano ya kompyuta kwa ajili ya kuboresha utoaji Elimu Masafa;
- (o) Kuandaa na kuchapa Mpango Mkakati wa UKIMWI;
- (p) Kuzindua studio kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kote nchini juu ya masuala mtambuka, Haki za Binadamu, utunzaji wa mazingira, Afya bora, umaskini na elimu ya kujikinga na UKIMWI; na
- (q) Kuendesha mafunzo ya uratibu, usimamizi na menejimenti ya vituo vya MEMKWA na MUKEJA katika wilaya 75 zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Taasisi ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kufanya tathmini ya njia za kufundishia na kujifunzia, matumizi ya maabara na kuendesha mikutano ya paneli za masomo 15 ya mtaala ya shule na vyuo ili kupata maoni ya kuboresha elimu ikiwemo mihtasari;
- (b) Kuandika moduli za wanachuo kwa masomo 26 ya mtaala wa mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti na miongozo ya walimu ya kufundishia masomo 25 ya mtaala wa sekondari kidato cha 5 na 6;
- (c) Kuchapa na kusambaza vitabu 24 vya MEMKWA vya kundi-rika la 1 na 2 mwaka wa 2 pamoja na miongozo 3,000 ya kufundishia masomo ya shule za sekondari kidato cha 1-4;
- (d) Kurusha vipindi 13 vya redio na televisheni kwa masomo ya Hisabati na Kiingereza darasa la III na IV;

- (e) Kuandika vitabu nya shule kwa masomo ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kidato cha 1-4 na kuandaa vivunge nya kufundishia na chati 500 za somo la Sayansi, Stadi za Kazi na Hisabati kwa darasa la I-VII;
- (f) Kuandaa andiko la mradi wa ujenzi wa kituo cha mafunzo, kiwanda cha uchapishaji wa vitabu na ukumbi wa mikutano;
- (g) Kununua magari 4, samani, vifuasi nya kompyuta na ‘software’ mpya na vifaa nya usalama;
- (h) Kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji ngazi ya kitaifa na ngazi ya wilaya na kwa walimu 2,000 wa shule za Awali na Msingi, 1650 wa shule za sekondari na wakufunzi 11,000 wa vyuo nya ualimu;
- (i) Kutayarisha programu za kielektroniki kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia kwa vyuo nya ualimu; na
- (j) Kufanya majoribio ya miongozo ya kufundishia na kujifunzia elimu ya UKIMWI katika shule za awali na msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuimarishe na kuboresha huduma za maktaba kwa watu wazima na watoto katika mikoa 19 ikiwa ni pamoja na kuongeza machapisho 60,000;
- (b) Kuanzisha matumizi ya TEHAMA kwa kufunga mtandao katika maktaba za Mwanza, Tanga na Songea;
- (c) Kuendeleza ujenzi na kuimarishe Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi wa Nyaraka Bagamoyo hasa ujenzi wa hosteli za wanachuo;
- (d) Kutoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi wa Nyaraka kwa walengwa 160 Cheti, 80 Stashahada na 120 mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wa maktaba nchini;
- (e) Kukarabati majengo ya maktaba na kununua samani katika mikoa ya Mara, Mtwara na Tabora;
- (f) Kuhamasisha wananchi katika mikoa 21 ili wajenge utamaduni wa kusoma; na
- (g) Kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa maktaba za shule, vyuo na taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010 kituo cha Maendeleo Dakawa kitatekeleza kazi zifuatazo:-

- (a) Kutoa huduma ya maji safi/taka kwa wakazi kituoni;
- (b) Kuhakikisha wakazi wanaishi katika hali huru bila ya magonjwa;
- (c) Kuhakikisha kituo na makazi ya wana kituo yanafikiwa; na
- (d) kuendelea na utekelezaji wa Mpango Mkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Baraza la Mitihani la Tanzania litatekeleza yafuatayo:-

- (j) Kuweka mitambo maalumu (CCTV) ya uangalizi katika maeneo nyeti ya Baraza la Mitihani na kununua mashine bora zaidi ya kuchapa mitihani ili kuimarisha usalama wakati wa kuchapa na kufunga mitihani;
- (k) Kununua magari 4 kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usambazaji Mitihani na ufuatiliaji wa shughuli za Mitihani;
- (l) kuimarisha utendaji wa Baraza kwa kuajiri wafanyakazi wapya 65;
- (m) Kuendesha Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi; Kidato cha 4 na 6; Ualimu Daraja la A, Stashahada ya Ualimu na Mtihani wa Maarifa;
- (n) Kusimamia mitihani ya nje inayofanywa na watahiniwa binafsi hapa nchini;
- (o) Kukamilisha ukarabati wa majengo na kuanza ujenzi wa ofisi za Baraza ili kukabiliana na ongezeko la wafanyakazi;
- (p) Kukamilisha mfumo wa uchambuzi wa taarifa za Mitihani inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania;
- (q) Kukamilisha ujenzi wa kituo cha kusahihishia mitihani cha Mbezi Wani na ukarabati wa majengo ya ofisi za Baraza;
- (r) Kufanya upanuzi wa bohari ya kuhifadhia vifaa vya mitihani na skripti za watahiniwa ili kukabiliana na ongezeko kubwa la watahiniwa linalotokana na upanuzi wa elimu ya sekondari na;
- (s) Kutoa mafunzo yenye lengo la kupunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI pamoja na kubaini na kuwahudumia wafanyakazi wenye maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi itatekeleza yafuatayo: -

- (a) Kujenga na kukarabati vyuo vya ufundı stadi nya wilaya;
- (b) Kuendeleza ujenzi wa chuo cha ufundı stadi wilaya ya Makete;
- (c) Kukamilisha upanuzi, ukarabati na ufungaji wa vifaa katika vyuo vya Mpanda, Singida, Tabora, Shinyanga na Ulyankulu na kukamilisha ujenzi wa chuo cha ufundı stadi cha Njiro, Arusha;
- (d) Kuendeleza ujenzi wa vyuo vya Lindi, Pwani, Manyara na Dar es Salaam;
- (e) Kuendelea kutoa ruzuku kwa vyuo vya ufundı stadi vilivyoandikishwa ili kuongeza nafasi na ubora wa mafunzo yanayotolewa;
- (f) Kutoa mafunzo kwa walimu 260 wa elimu na mafunzo ya ufundı stadi nchini;
- (g) Kutoa mafunzo kwa Walimu watakaoweza kufundisha kozi za ngazi za III na IV katika Chuo cha Ualimu wa Ufundı Stadi Morogoro;
- (h) Kuandaa *Bridging Course* katika fani za Ujenzi, Umeme na Mitambo;
- (i) Kutoa mafunzo ya ufundı stadi viwandani kwa majaribio katika viwanda 10;
- (j) Kuendelea kuimarisha ushirikiano na Tanzania *Chamber of Minerals* ili kukuza mafunzo yanayolenga sekta ya madini yanayotolewa na chuo cha ufundı stadi Moshi ili yatolewe na vyuo vya ufundı stadi nya Mwanza na Shinyanga; na
- (k) Kuanza kutoa mafunzo katika sekta ya kilimo baada ya kukamilisha utayarishaji wa utaratibu wa utoaji mafunzo katika sekta hiyo ikiwemo kilimo, ufgugaji na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lituwezeshe kutekeleza hayo yote niliyoyaeleza kwa kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı ya Jumla ya Shilingi 507,492,983,000 kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani za pekee kwa wananchi, viongozi na Wahisani mbalimbali kwa kuchangia utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Baadhi ya Wahisani hao ni Wananchi mmoja mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Halmashauri zote za Wilaya, Manispaa na Majiji na Serikali Kuu.

Wahisani wenginwe ni Serikali ya Sweden, Uingereza, Ufaransa, Ireland, Japan, Norway, Finland, Canada, Uhlanzi, Ujerumani, China, Cuba, Jamhuri ya Watu wa Korea, Uturuki, Algeria, India, Poland, Egypt, Pakistan, Ubelgiji na Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*). Aidha, mashirika yaliyochangia ni pamoja na Benki ya Dunia (*WB*), *WFP*, *UNICEF*, *UNESCO*, *ILO*, *UNFPA*, *UNDP*, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), *NORAD*, *GTZ*, *DFID*, *Sida(Sweden)*, *CIDA(Canada)*, *JICA*, *USAID*, *JOVC*, *VSO*, *ZAIN*, *CBP*, *OPEC*, *DANIDA*, *Barclays Bank*, *NMB*, *CRDB*, *NBC*, *KOICA*, *Peace Corps*, *Book Aid International*, *Aga Khan Education Foundation*, *Plan International*, *Sight Servers International*, *UNAIDS*, *World Vision*, *Irish Aid*, *Care International*, *Oxfam*, *Children International* na *International Reading Association*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lituwezeshe kutekeleza hayo yote niliyoyaeleza kwa kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Jumla ya Shilingi 507,492,983,000 kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kama ifuatavyo:-

- (a) Shilingi 377,691,167,000 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ambapo Shilingi 153,249,075,200 zinaombwa kwa ajili ya Malipo ya mishahara na Shilingi 224,442,091,800 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na
- (b) Shilingi 129,801,816,000 zinaombwa kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge Wote kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI NA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa hotuba yangu kuna masahihisho ya uchapaji kwenye Kitabu cha Hotuba ukurasa wa tisa jedwali la 5 (3) naomba lifutwe na lingine jipya limegawanywa halafu vilevile kuna kosa la data ni ya 2008 badala ya 2007. Vilevile niseme kwamba Wizara hii ilipokuwa Wizara ya Elimu na

Utamaduni ilikuwa inapewa kujadiliwa na Wizara ya Elimu ya Juu ilikuwa inapewa siku moja. Kwa hiyo kwa ujumla tulikuwa tunapata siku tatu lakini leo tunapata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja iliyotolewa hapa. Baada ya kusema hayo naomba hotuba yote ichapwe kwa sababu hakuna uwezekano wa kumaliza. Kama Waziri aliweza kuongezewa muda sijui Mwenyekiti ataongezewa ngapi leo. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundikwa Mwaka wa fedha 2008/2009, na malengo ya Mwaka wa fedha 2009/2010 kwa Mujibu wa Kanuni za Bunge Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11).

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Lolensiia Bukwimba Mbunge wa Jimbo la Busanda na Mheshimiwa Oscar R. Mukasa Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi, kwa kuchaguliwa kwao kuwa wabunge. Tunawatakia kila la kheri katika kuwakilisha wananchi wa Majimbo yao na Watanzania wote kwa ujumla. Kamati yangu ilipata muda wa kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundikwa mwaka wa Fedha 2008/2009 na pia kupitia malengo na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunaelewa kuwa elimu ni haki ya kila mtu na ndio Msingi wa maendeleo kuanzia kwa mtu binafsi, familia na hatimaye nchi, kama inavyozingatiwa katika dira ya Taifa ya kutoa Elimu inayolenga kujenga jamii iliyoelimika na kuwa na tija hususan katika masuala yote ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa. Katika kuandaa Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundikwa Serikali inapaswa kuzingatia yafuatayo:-

- (i) Nafasi ya Elimu katika maendeleo ya Taifa.
- (ii) Nafasi ya Elimu katika jamii yetu na ya Kimataifa.
- (iii) Mfumo wa Elimu Tanzania.
- (iv) Changamoto za Elimu Tanzania.
- (v) Mchanganuo na bajeti ya programu za Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na Mipango ya kuendeleza Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Juu kwa kuwa inalenga kufikia malengo ya Millennia na Dira ya Taifa ya 2025 pamoja na Malengo ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Hivyo ni jukumu la Serikali pamoja na Wananchi kushirikiana na kuunga mkono mipango hii ili ifanikiwe na kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Elimu bado inakabiliwa na changamoto zinazosababisha kutokufanikiwa vizuri kutekeleza mipango ya elimu. Baadhi ya changamoto ambazo Kamati imebaini ni kama ifuatavyo:-

- (i) Upungufu wa fedha za kutosha kuendeshea shughuli za Wizara.
- (ii) Kutoeleweka vizuri kwa Sera ya uchangiaji kwa Wazazi/Walezi wa Watoto/Wanafunzi.
- (iii) Ufutiliaji dhaifu wa shughuli za elimu kwa viongozi na wakaguzi wa elimu.
- (iv) Uaminifu dhaifu kwa baadhi ya viongozi wa Shule, Vyuo, watendaji wa elimu katika Halmashauri za Wilaya na baadhi ya Waalimu.
- (v) Matumizi mabaya ya fedha zinazotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya elimu.
- (vi) Maadili ya Wanafunzi, Walimu na Wafanyakazi.
- (vii) Utaratibu wa utoaji Mkopo kwa wanafunzi wanaostahili na wanaohitaji mikopo ya Elimu ya Juu.
- (viii) Fedha za Bajeti kutopatikana kama ilivyopangwa na kwa wakati.
- (ix) Ujenzi na Ukarabati wa majengo ya Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu.
- (x) Kutokuwa na uwiano mzuri kati ya Walimu na Wanafunzi, upungufu wa madarasa, maabara, madawati, vyoo na nyumba za walimu. Aidha miundombinu ya Vyuo na Shule ni duni na haikidhi mahitaji ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuimarisha elimu ni lazima Serikali itenye bajeti ya kutosha kuwezesha vyombo vinavyosimamia ubora wa elimu kutekeleza kazi zake. Vyombo hivyo ni pamoja na:-

- Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania – *TCU*.
- Baraza la Elimu ya Ufundsi – *NACTE*.
- Baraza la Taifa la Mitihani – *NECTA*.
- Mamlaka ya Elimu Tanzania – *TEA*.
- Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu – *HESLB*.
- Maktaba ya Taifa - *NL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya msingi Fedha za kuendeshea Shule- (*Capitation Grant*). Katika bajeti ya 2008/2009 Serikali iliendelea kutenga dola 10 za Marekani ambazo ni sawa na Sh.12,000/= za Tanzania kwa kila mwanafunzi katika Shule

za Msingi. Hadi Juni 4, 2009, Serikali ilikuwa imetoe Shilingi. 6,000/= tu kwa kila mwanafunzi. Kamati inashauri Serikali izingatie na itekeleze ahadi yake na itafakari kwa nini imeshindwa kupeleka dola 10 za Marekani kwa kila mwanafunzi ili wananchi wafahamu sababu zilizoifanya ishindwe kutimiza ahadi yake. Pia Serikali ifuatilie kwa karibu matumizi ya fedha hizi kwa sababu fedha hizi hutumika kununua vifaa vya kufundishia, vitabu, ukarabati mdogo na shughuli za utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi mafanikio ya elimu hutegemea sana upatikanaji wa Walimu wenye sifa. Upungufu wa walimu katika Shule za Msingi bado ni tatizo katika maendeleo ya Sekta ya Elimu. Upungufu huu huathiri kiwango na ubora wa elimu. Jedwali lifuatalo linaonyesha upungufu wa walimu katika Shule za Msingi:-

Jedwali Namba 1, Mahitaji ya Walimu wa Shule za Msingi Nchini, 2008.

MKOA	WANAFUNZI 2008			
MAHITAJI YA WALIMU 2008 WALIMU WALIOPO 2008 UPUNGUFU/ ZIADA				
Arusha	305,779	7,644	7,155	489
Dar es salaam	444,709	11,118	11,064	54
Dodoma	371,176	9,279	7,288	1,991
Iringa	386,675	9,667	8,536	1,131
Kagera	518,646	12,966	9,740	3,226
Kigoma	355,813	8,895	6,815	2,080
Kilimanjaro	333,374	8,334	8,915	+580 (ziada)
Lindi	175,022	4,378	3,548	828
Manyara	269,194	6,730	5,537	1,193
Mara	429,445	10,736	8,053	2,683
Mtwara	248,482	6,212	5,076	1,136
Mwanza	839,708	20,993	15,585	5,404
Pwani	224,137	5,603	5,516	87
Rukwa	299,940	7,499	5,500	1,999
Ruvuma	293,710	7,343	6,098	1,245
Shinyanga	705,290	17,632	12,629	5,003
Singida	264,152	6,604	5,366	1,238
Tabora	389,344	9,734	7,341	2,393
Tanga	462,765	11,569	9,726	1,843
Jumla	8,296,608	207,415	170,039	37,957

Chanzo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, June 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali hili linatoa pitcha halisi ya usambazaji wa walimu katika shule za msingi nchini. Ni vema Serikali ifanye juhudzi za makusudi kuandaa na kusambaza walimu wenye sifa na kuondoa upungufu uliopo. Aidha kwa Mikoa yenye walimu wa ziada kama Kilimanjaro (+580), Serikali ifanye utaratibu wa kuhamisha walimu kwenye Mikoa yenye upungufu mkubwa kama Mwanza (-5,404), Shinyanga (-5,003) Kagera (-3,226), Mara (-2,683), Tabora (-2,393) na Kigoma (-2,080).

Vilevile kwa tarakimu hizi, tunashauri Serikali isiendoolee kupeleka Walimu zaidi kwenye Mikoa yenyne upungufu mdogo wa walimu Mfano, Dar es Salaam (54) na Pwani (87).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa Walimu. Kamati ubora wa elimu huchangiwa na mambo makubwa matatu ambayo ni Walimu, vitendea kazi (vitabu, maabara) na Wanafunzi. Kwa jinsi hamasa ya elimu inavyoongezeka, ndivyo idadi ya Walimu hupaswa kuongezeka pamoja na kasi ya ujenzi wa shule. Hata hivyo ongezeko la idadi ya Wanafunzi haviendo sambamba na ongezeko la Walimu. Ni vema Serikali na jamii kujiuliza, je Walimu wanaomaliza mafunzo katika Vyuo vya Ualimu baadhi yao huwa wanaishia wapi? Tafiti zinaonesha kuwa katika shule za Msingi na Sekondari Walimu wanaopangwa kazi maeneo ya vijijini na hasa mikoa ya pembezoni, wengi wao huwa hawaendi katika vituo vyao vya kazi kutokana na mazingira halisi na ugumu wa maisha.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu ndio nyenzo muhimu ya kuinua ubora wa elimu nchini, hivyo Serikali ina wajibu wa kulipa suala hili umuhimu wa pekee, na kuhakikisha kuwa shule za vijijini zina mazingira mazuri ya kuishi kama nyumba, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na huduma nyingine maalum za kijamii zinapatikana vijijini. Hata ikibidi kuweka motisha maalum kwa walimu wanaopangwa maeneo haya, wapate mikopo ya vifaa vya usafiri kwa masharti nafuu kama namna ya kuwawezesha walimu kuwafikia na kuwafundisha vizuri Wanafunzi walio katika maeneo yenyne mazingira magumu.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa kusambaza walimu kwenye maeneo ya vijijini, pia inatoa wito kwa wananchi kuunga mkono mpango huu ili wanafunzi wanaosoma katika shule zilizopo pembezoni mwa nchi wapate elimu bora. Mpango huu uende sambamba na motisha kama Kamati ilivyoshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachelewa sana kufanya maamuzi ya kutoa motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoro shule za msingi. utoro shulen ni moja kati ya matatizo yanayokabili mafanikio ya Sekta ya Elimu nchini, pamoja na takwimu kuonesha wingi wa watoto wanaosajiliwa Darasa la Kwanza, wapo ambao hawahitimu darasa la saba. Tatizo la mdondoko wa wanafunzi katika Elimu ya Msingi ni kubwa na linaleta maswali kuwa watoto hawa huenda wapi na kwa nini kuwe na mdondoko mkubwa?

Kuna sababu nyingi zinazotolewa kuhusu midondoko ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Wanafunzi kutembea mwendo mrefu.
- (ii) Kutokuwepo na chakula cha mchana shulen.
- (iii) Kutokuwepo Walimu wa kutosha.
- (iv) Ukosefu wa vifaa kama sare za shule, madaftari, vitabu n.k.
- (v) Kuacha shule (*truancy*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina nyingine ya utoro ni ule unaosababishwa na ujauzito. Jedwali lifuatalo linaonesha hali halisi ya tatizo la utoro na mimba shulenii.

Jedwali Na, 2. Matukio ya Utoro na Mimba kwa shule za Msingi Mwaka 2008.

SABABU	IDADI	%
Utoro	50,401	69.54
Mimba	3,370	4.64
JUMLA	53,771	74.18

* *Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji, June 2009.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Inaonekana utekelezaji wa Kanuni ya Uandikishaji na Mahudhurio shulenii ya lazima ya mwaka 2002 “*The Primary School Compulsory Enrolment and Attendance Rules 2002*” haitekelezwi ipasavyo na Maafisa Watendaji wa Kata ambao kimsingi ndio watekelezaji wakubwa wa Kanuni hii. Kamati inahitaji takwimu za utekelezaji wa kanuni hii.

(ii) Ni muda muafaka sasa tatizo la mimba shulenii lipate mjadala wa kitaifa na kuhusisha wadau wote wa elimu na hatimaye Serikali ilete Muswada Bungeni ili Sheria itungwe itakayodhibiti tatizo hili vizuri zaidi na hatimaye Sheria ielekeze namna bora ya kuwasaidia wanaoathirika zaidi (wasichana) na tatizo hili.

(iii) Iwapo tatizo hili litaachwa liendelee ni wazi kuwa lengo Namba 2 la Malengo ya Millenia la Elimu kwa wote halitafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utoro Shule za Sekondari. Pamoja na Serikali na wananchi kutekeleza Mpango wa Maendeleo Elimu ya Msingi (MMES) kwa mafanikio makubwa na kwa lengo la kuongeza idadi ya Wanafunzi katika elimu ngazi ya Sekondari, kumeshamiri vitendo vya utoro kutokana na sababu mbalimbali. Wanafunzi wapatao 48,217 walitoroka Shule mwaka 2008 kutokana na sababu mbali mbali kama inavyoonekana kwenye Jedwali lifuatalo:-

Jedwali Na. 3, Utoro katika Shule za Sekondari mwaka 2008.

Sababu (Reasons)	Form I	Form II	Form III	Form IV	Form V	Form VI	Jumla
Kuacha (Truancy)	4,478	11,264	14,001	3,270	78	29	33,120
Mimba	429	1,588	2,177	747	21	3	4,965
Vifo	68	234	228	125	5	4	664

Kukosa								
Mahitaji	1,105	1,414	1,533	332	27	3	4,414	
Maradhi	87	154	176	60	16	7	500	
Wazazi								
kuugua	93	74	99	25	-	-	291	
Sababu								
zingine	968	1,256	1,397	460	132	50	4,263	
Jumla	7,228	15,984	19,611	5,019	279	96	48,217	

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, June 2009

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo Serikali itaachia utoro uendelee bila kuchukua hatua za kudhibiti na kukomesha matukio haya, itakuwa vigumu sana kufanikisha Malengo ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) tukizingatia kuwa Elimu ni Ufunguo wa Maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahitaji ya Walimu wa Shule za Sekondari. utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo Elimu Sekondari (MMES), umefanyika kwa mafanikio makubwa na Shule nyingi za Sekondari zimefunguliwa hadi ngazi ya Kata. Ni muhimu sana Serikali ieleze mikakati ya kupata Walimu wenye Sifa kutokana na upungufu mkubwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali 4 lifuatalo,

Jedwali Na. 4, Mahitaji ya Walimu Mwaka 2008.

NA.	IDARA	MAHITAJI WALIOPO UPUNGUFU		
1.	Elimu ya juu (vyuo vya umma)	4,200	2,255	1,845
2.	Elimu ya Ualimu (Wakufunzi)	1,636	1,465	168
	Shule za mazoezi za Sekondari kwenye vyuo vya ualimu	192	132	60
	Shule za mazoezi za Msingi kwenye vyuo vya ualimu	1,021	946	75
3.	Elimu ya Sekondari	58,642	26,432	32,210

Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, June 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahitaji ya Walimu wa Masomo ya Sayansi upungufu wa walimu wa sayansi unachangia katika sababu zinazofanya wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi kutokufanya vizuri katika masomo yao. Jedwali Na. 5 linaonesha upungufu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maabara Serikali ina wajibu wa kuweka mazingira sahihi ya kuwezesha masomo ya sayansi kufundishwa kwa mafanikio katika shule za Sekondari. Kuwepo kwa maabara zenyе vifaa na walimu wenyе sifa ni muhimu ikizingatiwa kuwa dunia ya sasa ni ya sayansi na teknolojia. Ukosefu wa maabara na walimu wenyе sifa hizi ni moja ya sababu zinazofanya wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi wasifanye vizuri katika masomo yao, au wanafunzi wengi wachukie kusoma masomo ya sayansi. Jedwali lifuatalo linaonyesha hali ya maabara katika shule za sekondari nchini.

Jedwali Na. 6, Hali ya Maabara za Sekondari za Serikali Tanzania, Desemba, 2008

Shule Jumla shule Hali ya Maabara

Shule zenyе Maabara Hali nzuri Ukarabati Pungufu

Shule za Kitaifa	89	89	—	89	—
Shule za Jumuiya	3,051	639	36	603	2,412
JUMLA	3,340	728	36	692	2,412
Asilimia	23%	1%	22%	77%	

* *Chanzo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji, June 2009*

Kamati inaishauri Serikali kujenga na kuimarisha maabara katika kila Sekondari, kwani itasaidia kukabiliana na tatizo la upungufu wa wataalam wa Sayansi.

Aidha Kamati inaishauri kuwa, Maabara zenyе vifaa liwe ni sharti la lazima kabla ya kutoa vibali vyа kusajili Sekondari zinazofunguliwa na tunashauri Serikali yenye we ndio ijenge kwanza maabara wakati Wananchi wakijenga Madarasa na Nyumba za Walimu na baada ya shule kufunguliwa, Mpango wa MMES uendelee kuimarisha ujenzi wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi za Shule za Sekondari. Wajumbe wa Bodi za Shule ndio nguzo ya mabadiliko na maendeleo ya elimu katika shule na hatimaye Taifa

zima. Kwa umuhimu huo Kamati inashauri mamlaka inayohusika na uteuzi wa Bodi hizo kuwa waangalifu sana na kuteua watu makini, wenyewe uwezo, waadilifu na wanaoheshimika katika jamii.

Aidha, Kamati inashauri kuwa majina ya wajumbe wa Bodi yachujwe kwa taratibu za kiserikali ili kuwapata wajumbe wenyewe sifa stahili. Kwa hali ya sasa, na hasa baada ya Kamati kufanya ziara Mikoani/Wilayani, imebainika kuwa Bodi nyingi zimeteuliwa kutokana na utashi wa wakuu wa shule. Hivyo Kamati inashauri Wizara ifanye utafiti wa Bodi zote za shule za sekondari na kuona kama sifa zimezingatiwa na taarifa iletwe mbele ya Kamati. Usimamizi na Uendeshaji wa Shule za Sekondari kuwa chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali la kuhamisha uendeshaji na usimamizi wa shule za Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kusogezza huduma karibu na wananchi na kuzifanya jamii kuwajibika zaidi katika maendeleo ya shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa angalizo kuwa, kuhamisha shule hizo ni lazima kuambatane na ongezeko la mambo mbalimbali kwa Mamlaka za Halmashauri ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Kuongezeka kwa majukumu.
- (ii) Kuongezeka kwa mahitaji ya taaluma na kitaalam.
- (iii) Kuongezeka kwa rasilimali watu hasa idadi kubwa ya watumishi na majukumu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa muda mfupi.
- (iv) Uwezo wa Serikali kutoa fedha za kutosha kukidhi mabadiliko wakati huu wa mtikisiko wa uchumi ni jambo la kuangalia kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Athari za Mipango hii ya Serikali ni pamoja na ;-

- (i) Mwingiliano wa upangaji mipango kutokana na baadhi ya shule kuwa chini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis na zingine chini ya Halmashauri.
- (ii) Wanafunzi wa ngazi ya kawaida (*O-level*) watakosa kujifunza kutoka kwa wenzao wa ngazi ya juu (*A-level*) watakapotenganishwa.
- (iii) Walimu wenyewe uzoeufu katika ufundishaji na Taaluma maalum watakosa nafasi ya kuwasaidia wanafunzi wa ngazi ya kawaida (*O - level*).

Kutokana na kugawanyika kwa elimu ya sekondari ya kawaida na ya juu, kutakuwa na ongezeko kubwa la mahitaji ya vitabu, madarasa, malazi na kadhalika. Serikali iliwhi kutoa majibu mepesi na rahisi katika kufuta baadhi ya michepuo ya masomo pamoja na tahadhari zilizotolewa na wadau wa elimu na kwamba kulikuwa na mikakati lakini matokeo yake tumeyaona tena kwa muda mfupi na kulazimika kurudisha michepuo ya masomo, lakini wakati huo huo, Walimu wataalam wa masomo hayo tayari wengine walikwishaondoka. **TUSIRUDIE TENA MAKOSA, TUCHUKUE TAHADHARI KUBWA.** Vinginevyo Sekta nzima ya elimu itayumba na likitokea hilo, Taifa litadidimia na hatutakuwa na nafasi ya kurekebisha kwa sababu haya ni maamuzi makubwa na yakikosewa katika mikakati ni vigumu sana kurekebishwa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi. Kumekuwepo ahadi ya Serikali ya kujenga Vyuo vya Elimu ya Ufundi – VETA katika kila Mkoa. Aidha Serikali iliahidi kuwa Mikoa ya Pwani, Lindi na Manyara ingejengewa Vyuo hivyo. Ni muhimu Bunge likaelezwa hatua iliyofikiwa kuhusu mradi huu unaofadhiliwa na Serikali ikishirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa Korea Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya VETA vikianzishwa kila Mkoa na hatimaye kila Wilaya vitasaidia Taifa kuondokana na tatizo la ajira kwa vijana kwani wataweza kuujajiri wenyewe. Ni vyema kwa Serikali kuendelea kuhamasisha wanafunzi pamoja na wazazi kuhusu umuhimu na manufaa ya elimu hii ya ufundi kwa kuwa bado kuna mwamko mdogo katika jamii. Kuhusu elimu ya ufundi. Aidha, Serikali iendelee kuboresha Vyuo vya Ufundi Stadi kwa kuweka mazingira mazuri na vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Juu. Elimu ya juu ndio chimbuko la maendeleo na mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa katika jamii. Pamoja na juhudi za Serikali kuongeza idadi ya Vyuo vya Elimu ya Juu, na vile vya binafsi bado idadi ya wanafunzi katika nchi yetu ni ndogo ikilinganishwa na nchi zinazotuzunguka. Pamoja na uchache huo bado mazingira ya vyuo si mazuri kuanzia miundombinu chakavu, upungufu wa vitendea kazi, upungufu wa Wahadhiri, uhaba wa Maktaba, vitabu, madarasa na Hosteli za Wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazingira ya Vyuo vya Elimu ya Juu kutokidhi mahitaji yote, wanafunzi wengi wanategemea kusoma baada ya kupata Mkopo kuititia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mara nydingi wanafunzi wamekuwa wakilalamika kuwa hawapati mikopo kwa wakati, suala ambalo hupelekea wanafunzi kupoteza muda wa masomo na kujishughulisha na migomo jambo ambalo husababisha baadhi ya wanafunzi kukosa baadhi ya vipindi na hatimaye kufanya vibaya katika mitihani yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa masomo wa 2009/2010 Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iliweka malengo ya kuwakopessa Wanafunzi 65,000 kwa kuweka vipaumbele kuwa wanaosomea kozi za Sayansi na wanaosomea Shahada za

Ualimu wakopeshwe kwa asilimia 100. Aidha wanafunzi wa kozi nyingine wakopeshwe kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa baada ya tathmini ya uwezo wa familia ya mwanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka miwili mfululizo 2007/2008 na 2008/2009, Serikali ilitenga kiwango cha juu (ceiling) cha fedha za mikopo ya Elimu ya Juu kuwa kiasi cha Tsh.117 bilioni. Kiasi hiki ni kidogo na hakikidhi mahitaji halisi ya mikopo ambayo imeongezeka kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi katika Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza azma hiyo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iliomba kutengewa Tshs. 197 bilioni, lakini bado imeendelea kutengewa Tshs. 117 bilioni kwa mwaka wa tatu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari inayojitokeza ni kwa Bodi ya Mikopo kushindwa kutoa mikopo kwa wanafunzi watakaodahiliwa mwaka wa kwanza wa 2009/10 kutokana na pengo la Sh. 80.4 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitafakari suala hili lenye maslahi ya Taifa na ilishauri Serikali kutafuta fedha za kuziba pengo la Sh. 80.4 Bilioni ili kuwakopesha wanafunzi kama Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilivyoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeona na imekubali kutafuta fedha za kuziba pengo la Sh. 80.4 bilioni kwa barua yenye Kumb Na. ED/WEL. 10/III/GEN/12 ya tarehe 15 Juni 2009 kama ilivyowasilishwa mbele ya Kamati na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufund. Kamati inashukuru kwa usikivu wa Serikali katika suala hili muhimu lenye maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kukubali kutafuta fedha za kuziba pengo la Sh. 80.4 bilioni, fedha hizo kwa sasa hazimo kwenye bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge hili tarehe 18/6/2009. Kamati inasisitiza kuwa, baada ya Serikali kukamilisha taratibu za kuziba pengo la Bilioni 80.4, kama alivyoahidi Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufund baada ya mashauriano na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Kamati ya Uongozi na hatimaye Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali itekeleze mambo 3 yafuatayo:-

- (i) Kama fedha hizo Sh.80.4 bilioni zitapatikana kwa kurekebisha mafungu ndani ya Bajeti iliyopitishwa 18 /6 /09, Kamati ipewe taarifa wakati inatekeleza kazi yake kwa niaba ya Bunge ya kusimamia na kushauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba.

- (ii) Kama fedha zitapatikana nje ya Bajeti iliyoidhinishwa ni muhimu zikawekwa ndani ya (Supplementary Estimates) wakati wowote ambapo Serikali italeta makisio ya ziada ili Bunge liidhinishe fedha hizo Sh.80.4 bilioni.
- (iii) Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuweka mtizamo mpya wa namna ya kuendelelea kutoa mikopo kutokana na idadi kubwa ya waombaji inayoongezeka kwa kasi, badala ya utaratibu wa sasa wa kibajeti.
- (iv) Kwa mantiki hiyo, Kamati inaamini kuwa Wanafunzi wote watakdahiliwa Mwaka wa masomo wa 2009/2010 wanaostahili kupata mikopo watapewa pasipo usumbufu kwa kuzingatia kuwa mikopo hiyo hutolewa kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa mbali na tatizo la uchumi ambalo nchi yetu inakabiliwa nalo kwa sasa, Serikali ijithahidi kutoa fedha zilizoainishwa katika bajeti kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa wakati pamoja na kufuatilia matumizi yake ili kuona kuwa yanatumika kama yalivyoainishwa.

Aidha, Kamati inashauri Serikali iendelee kutoa elimu kwa wadau wote kuhusu sera ya uchangiaji wa elimu kwa wananchi ili kuepukana na lawama wakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Mitihani - NECTA linapita katika wakati mgumu katika kutekeleza majukumu yake. Kamati inaamini kuwa Baraza hili ni chombo nyeti na mboni ya Taifa kinachoipatia nchi yetu uhalali wa viwango vyta elimu wanayopata watu wake katika kupima na kusimamia ubora wa viwango vyta Elimu vilivyokubalika kitaifa na hatimaye kukubalika kimataifa. (*Ma kofi*)

Kamati inaona kuwa Baraza linahitaji kuimarishwa katika ngazi zote ili kuepukana kabisa na uvujaji wa mitihani, Kamati inashauri kuwa hatua kali zichukuliwe kwa wote wanaohusika na uvujaji na wizi wa mitihani. Aidha ni muhimu kuitia muundo wa Baraza kama unakidhi mahitaji ya kukabiliana na changamoto za mabadiliko mengi ya kiteknolojia ambayo yanatoa nafasi katika uvujaji wa mitihani na kughushi yeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu ya Tanzania (TEA). Mamlaka ya Elimu Tanzania ilianzishwa kuhamasisha wadau kuchangia mfuko maalum wa kuendeleza elimu na pia kwa kutoa Mikopo kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya Shule, Vyuo na Taasisi mbalimbali za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Sheria ya mfuko huu kutamka wazi kuwa Serikali itachangia kiasi kisichopungua aslimia mbili (2%) ya pato la Taifa baada ya kutoa gharama za madeni ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitika kuona jinsi mchango wa Serikali kupitia bajeti yake unavyoendelea kushuka kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 7

Jedwali Na. 7, Tengo la Bajeti kwa Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA

Mwaka wa fedha	Bajeti ya Serikali (bilioni)	Tengo la fedha kwa TEA (bilioni)	Asilimia %
2001/2002	1,079.6	4.9	0.45
2002/2003	1,175.6	4.9	0.40
2003/2004	1,391.2	5.4	0.39
2004/2005	1,757.8	4.4	0.23
2005/2006	2,262.7	6.8	0.30
2006/2007	4,348.7	4.7	0.17
2007/2008	7,216.1	4.5	0.12
2008/2009	4,095.0	4.5	0.11
2009/2010	9,513.68		4.5
0.087			

**Chanzo, Mamlaka ya Elimu Tanzania June 2009.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tunashauri Bunge lako Tukufu litoe azimio la kuifanya Serikali irekebishe mwenendo huu ambao kwa viwango vyovyyote hauoneshi ufanisi wa sheria iliyounda mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadili ya wanafunzi na jamii kwa ujumla. Ni jukumu la kila raia mwema kupambana na mmomonyoko wa maadili katika jamii yetu. Mfano, kuna ukiukwaji mkubwa katika uvaaji wa mavazi na jinsi yanavyobana. Aidha maadili mema ya Wanafunzi kusalimia waliowazidi umri yanazidi kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapenda kuunga mkono Maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anahitimisha hoja kwa kusema,

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wote pamoja tufanye kazi, wazazi, Waheshimiwa Wabunge, tujitahidi wote kwa pamoja kuendelea kulikemea jambo hili na tuone namna bora zaidi ya kuimarisha utamaduni wenye heshima, utamaduni wa kitanzania ambao kweli ukijitazama, unasema, naam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa ni muda muafaka sasa wa kutafsiri maneno yetu kwenye vitendo kwa kuchukua hatua za kupambana na mmomonyoko wa maadili. (*Makofi*)

Tunashauri Wakuu wa Shule/Vyuo wanaoshindwa kuchukua hatua za kisheria au kurekebisha hali hii kwenye Shule/Vyuo vyao waondolewe madarakani kwa sababu ni Taifa gani linaloona vijana wakivaa nguo fupi za kubana na wengine kuvali chini ya makalio halafu litazamie kujenga maadili ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Naomba kuchukua fursa hii kukupongeza wewe kwa jinsi unavyoendesha Vikao vya Bunge kwa umahiri na busara kubwa. Aidha, nampongeza Naibu Mwenyekiti na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge ambao ndio msingi wa mafanikio ya Bunge katika shughuli zake za kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, (Mb), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu akisaidiwa na Manaibu wake Mheshimiwa Mwantumu Mahiza,(Mb), na Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka, (Mb), pamoja na Watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu Profesa Hamis Dihenga na Naibu Katibu Mkuu Ndgg. Selestine Gesimba kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati kutoa majibu ya hoja za Wabunge kuhusu utekelezaji wa Wizara kwa Mwaka 2007/2008, na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninamshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashililah na Ofisi yake kwa kutuhudumia vyema kipindi chote Kamati ilipokuwa kazini. Nawapongeza Katibu wa Kamati hii Ndugu Hosiana John na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Theonest Ruhilabake kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nisiwasahau wananchi wangu wa Jimbo la Babati Mjini naomba pia niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu wa Babati Mjini kwa imani yangu katika kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 13(5) ya Kanuni za Bunge (2007), naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kwa majina:-

Mheshimiwa Omari S. Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati wakati Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati hii ni Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M. hemed na Mheshimiwa Janeth B. Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Omari A. Mzee, Mheshimiwa Usi Amme Pandu, Mheshimiwa Mch. Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii ahsante sana. (Makofi)

MHE. SUSAN A. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi naamini kwa busara zako utaniongezea dakika chache ili niweze kumaliza kama ambavyo umemuongezea Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri hasa ukizingatia unyeti wa Wizara yenyе.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mafunzo na Ufundi kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 99(7) toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mhe. Hamad Rashid Mohamed (Mb) na Naibu wake Dr. Willibroad Peter Slaa (Mb) kwa kuendelea kuwa na imani nami kushikilia wadhifa huu wa mse maji mkuu wa wizara hii.

Vilevile napenda kuwashukuru kwa kunipatia msaidizi mahiri, Mheshimiwa Nuru Bafadhili (Mb) kama Naibu Waziri wangu. Hotuba hii imefika hapa kwa msaada wake mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Napenda kuishukuru kambi ya Upinzani, kambi makini kabisa chini ya Uongozi wa Mhe. Hamad Rashid na Mhe. Dr. Slaa kwa uongozi wao madhubuti unoijenga kambi ya Upinzani na kuifanya kuwa kambi imara na isiyotetereka, na hivyo kuweza kufanya kazi yake ya kuikosoa serikali bila woga wowote. Ninauhakikishia uongozi wa kambi ya Upinzani Bungeni na Watanzania wote wazalendo kuwa nitafanya kazi hii, kwa uwezo wangu wote kwa lengo la kusaidia maendeleo ya Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kuendelea kunipa ushirikiano ndani na nje ya bunge, nami naendelea kuwaahidi kuitunza imani ya chama changu na kuendelea kukitangaza kwa watanzania wote. Baada ya kusema hayo, Mhe. Mwenyekiti sasa naomba nitoe maoni ya kambi ya Upinzani katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tokea miaka ya mwanzo ya Uhuru wa nchi yetu, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alitutaka tushirikiane na tutumie nguvu za pamoa

kupigana vita dhidi ya maadui wetu ujinga, maradhi na umaskini. Miaka 48 sasa, tukiwa katika vita hivyo hatujawea kumshinda angalau adui mmoja kati ya hao watatu. Hapana shaka tuna udhaifu mkubwa sana katika mapambano yetu, na udhaifu upo hasahaha katika sekta ya Elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama elimu yetu isingekuwa na matatizo mbona tungeushinda ujinga, kwa Elimu tukaushinda umaskini na maradhi; kwa Elimu tukafikia kiwango kizuri cha maendeleo kama tulivyoshuhudia katika nchi za wenzetu (mathalani Singapore, Malaysia, China Japan na nchi za Scandinavia) waliotumia raslimali watu vizuri, wakawekeza katika elimu na sasa wako mbali sana kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tumekosea sana katika elimu kuanzia nini tunachokiamini, na tunachokitekeleza kupitia sera zetu na mipango mbalimbali ya elimu. Tumeshindwa kuwathamini askari wa mstari wa mbele katika vita vyetu (Walimu). Tumeendelea kutenga kiasi kidogo sana cha fedha kwa ajili ya sekta hii. Tumechezea mitaala na kuiyumbishayumbisha kana kwamba taifa hili halina dira wala mwelekeo.

Mara kwa mara kumekuwa na mabadiliko ya nadharia za sera na mipango ya elimu isiyo endelevu na sera zisizoendana na ukweli wa kiutafiti ambazo mara zote zimefanya ubora wa elimu uzidi kuperomoka. Kwa mtindo huo taifa linaangamia kwa kupelekwa hatua moja mbele kisha hatua mbili nyuma ilihali ulimwengu wa utandawazi unasonga mbele kwa kasi, hautungojei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ni vyema tujitathmini sisi wenywewe, tutambue madhaifu yetu, tujirekebishe, tukubaliane njia sahihi za kutupeleka mahali sahihi tena kwa haraka. Hakika tunahitaji kwanza kujadiliana kwa pamoja, tuangalie pamoja na mambo mengine, lile ambalo wadau mbalimbali wa elimu wametoa wito tulifanye, yaani “Mjadala wa kitaifa kuhusu elimu” mjadala wetu uangalie ni nini tulipanga kufanya kama nchi, kitu gani kinatekelezwa katika sekta ya elimu na ni kipi kilicho bora zaidi ambacho tungepaswa kufanya. Kwa maana hiyo mjadala huu uwe sehemu ya kutathmini mipango na utekelezaji wake kisha uibue mapendekezo yatakayoliokoa taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya 2009/ Bajeti ya Kawaida Kama ilivyotegemewa sehemu kubwa ya bajet ni ile ya matumizi ya kawaida inayofikia 65.64%. Katika matumizi ya kawaida Personal Emoluments (mishahara n.k) inafikia 40.58% na matumizi mengineyo ie Other Charges ni 59.42%. Lakini bajet ya OC inagusa sana masuala ya ubora.. Kwa mfano tukirejea kasma ya 7001 (Elimu ya Juu). Jumla ya OC ni 139,864,971,100. Bado, 119,100,000,000 (85.15%) zitapelekwa kwa Board ya Mikopo ya Wanafunzi waElimu ya Juu na 4,500,000,000 (3.22%) zitaenda Mamlaka ya Elimu Tanzania (*Tanzania Education Authority*).

10. Mheshimiwa Mwenyekiti, Hii inamaanisha kwamba ni 11.63% (16,264,971,100) tu ambazo zitatumiwa na vyuo vyote vya elimu ya Juu! Kwa hali hii ni wazi kwamba ni kiasi kidogo kitatumika katika masuala ya taaluma na hivyo kutoleta tija katika matokeo mazuri ya kitaaluma kwa wanafunzi (*very small impact on the cognitive outcomes of students*) kama vile vifaa vya kujifunza na kufundishia. Suala la kujiuliza ni nini

vipaumbele veya serikali katika kuongeza ubora wa waufundishaji na kujifunza kupitia matumizi mengineyo ya bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Maendeleo. Katika Bajeti ya Maendeleo ni sh (129,801,816,000) ambayo ni asilimia 34.36%. Kati ya asilimia 48.87 inategemewa kuwa msaada/mchango kutoka nchi rafiki (43,963,626,900/= 69.30%) kutoka Benki ya Dunia na 30.70% kutoka kwa wafadhili wengine. Kwa maneno mengine 33.86% ya bajeti ya maendeleo iiategemea Benki ya Dunia. Je serikali inajipangaje kujikwamua na tishio hili la kutokutabirika kwa upatikanaji wa fadha hizi kutoka kwa wafadhili hasa tukizingatia mtikisiko wa uchumi duniani?(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika fedha za maendeleo, sh.82,857,617,700 (63.83%) zitatumika kwa shughuli za ujenzi na ukarabati wa majengo na vifaa; ambapo sh. 3,010,578,850 (2.32%) zitatumika katika kuwajengea uwezo wafanyakazi.. kiasi cha sh., 43,933,619,450 (33.85%) cha bajet kitatumika katika shughuli nyingine ambazo hazina uhusiano na ujenzi au ukarabat au ujengaji uwezo, kutokana na hali mbaya ya uchumi duniani ni kwa nini zitengewe fedha?na ziachwe shughuli ambazo zingekuwa na tija katika kuboresha elimu kwa muda mfupi na mrefu?kwa mfano kasma ya *1003: Sub-vote 4312; 4397; 6404; 6571; See Vote 2002: Sub-vote 3001; (ii); (iii) etc.*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Msingi elimu ya msingi ni roho kwa taifa lolote. Maendeleo yote ya elimu huanzia hapo. Msingi wa elimu ukijengwa vizuri bila shaka ngazi zote za elimu za juu zitaendelea vizuri. Wote tunaelewa kwamba elimu ni ufunguo kwa mtu binafsi na kwa maendeleo ya Taifa.

Lengo kuu la elimu ni kuinua utu wote wa kila raia, kuboresha ustawi wa binadamu na kumwandaa mtu binafsi kwa ajili ya uanachama halisi na kushiriki katika maisha halisi, katika kazi na shughuli katika ngazi za familia, jamii na taifa.Elimu bora inachochea ukuaji haraka na endelevu wa uchumi na kukuza uchumi ambaa unaboresha utoaji wa huduma nyingine za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na umuhimu huo, serikali kwa kushirikiana na nguvu za wananchi pia imefanikiwa kuongeza idadi ya shule za msingi, ambazo zimeongezeka kutoka 14,700 mwaka wa 2006 hadi 15,624 mwaka 2007. Hili ni suala la kujipongeza na kupongezana. Lakini tunashauriwa kutodanganyika na taaswira ya takwimu tu. Na tujiulize je ni kweli elimu inayotelewa inawiana na nguvu inayowekezwa na wananchi? Bado tuna tatizo kubwa la uhaba wa walimu.

Pamoja na kusomesha walimu kwa wingi bado walimu hawa hawaendi kufundisha kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kutokulipwa kwa wakati nk. Hili ni suala ambalo wizara ya elimu inatakiwa kulipatia majibu ambayo yanalandana na uzito wa jambo hili na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kuwa ubora wa elimu haupimwi kwa wingi wa shule wala idadi ya wanafunzi, la hasha, ingawaje mjadala wa kitaifa kuhusu

uboreshaji wa elimu umejikita na kuelekezwa zaidi katika wingi wa vitendea kazi hii inashangaza ingawaje sote tunatambua kuwa ubora ni tofauti na uwingi. Kambi ya upinzani inasikitika sana kuona ubora wa elimu katika shule zetu za msingi kutetereka. Tafiti nyingi zilizofanywa na taasisi tofauti zinadhahirisha hilo. Hii inatisha na kukatisha tamaa. Kwa sababu kama hatujengi msingi mzuri maana yake tunajenga taifa la wasomi wasio na uwezo kushindana katika ulimwengu huu wa utandawazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ulimwengu wote unatambua ukweli kwamba hakuna nchi yoyote iliyoendelea bila wananchi wake kuelimika au kuwekeza katika elimu. Maendeleo yote hutokana na elimu sahihi iliyojaa maarifa, ubunifu, uwezo mkubwa wa kufikiri na kuvumbua dhana mpya.

Elimu inayojenga ujuzi na ufundi wa aina mbalimbali, inayojenga kujiamini, kudadisi na kutumia fursa zilizopo kutafuta masuluhisho ya matatizo. Hii ndiyo nguvu ya elimu inayoleta maendeleo katika jamii. Ni mantiki hii suala la kuwekeza katika elimu bora na sahihi haliepukiki hata kidogo na linapaswa kutiliwa mkazo na kila mtu kwa kuzingatia umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo, kambi ya upinzani inaitaka wizara husika kutoa majibu katika masuala yafuatayo:-

- (a) Je, nini hasa, kiini cha poromoko hili katika elimu?
- (b) Je, serikali inafanya nini ili kuweza kukabili tatizo hili ambalo limeikumba sekta ambayo inajenga taifa la kesho?
- (c) Tatizo la walimu linashughulikiwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtaala wa shule ya msingi. Mtaala ni msingi wa elimu ya mahali popote kwani bila mtaala wanafunzi wasingekuwa na cha kusoma.

Katika dunia ya sasa ya habari na mlipuko wa Maarifa, nchi nyingi zinafikiria ni mambo gani yakamilishwe (*covered*) ili kutosheleza mahitaji muhimu ya wanaomaliza elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala wa shule ya msingi. Mtaala ni msingi wa elimu ya mahali popote kwani bila mtaala, wanafunzi wasingekuwa na cha kusoma. Katika dunia ya sasa ya habari na mlipuko wa maarifa, nchi nyingi zinafikiria ni mambo gani yakamilishwe (*covered*) ili kutosheleza mahitaji muhimu ya wanaomaliza elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala wa elimu ya msingi Tanzania, umeparaganyika ukiwa na maeneo mengi mno (*content areas*). Wanafunzi wanachukua hadi masomo 11! Kiswahili, *English*, Hisabati, Sayansi, Stadi za Kazi, Haiba na Michezo, Maarifa ya Jamii, Teknohana, Dini, French, Civics na kadhalika. Hili ni tatizo kubwa hasa katika

mazingira ya kutokuwa na Walimu wa kutosha. Labda hii ndio sababu wanafunzi hawafanyi vizuri katika yale masomo muhimu ya lengo la elimu kwa wote, yaani kusoma na kuhesabu. Madhara ya mkanganyiko huu katika hatua za awali, ni kutokuwa na umakini na uelewa mzuri wa masomo hali inayopeleke baadhi ya wahitimu wa darasa la saba kushindwa kusoma au hata kuandika. Sisi tunajiuliza, iweje mtoto akae darasani kwa miaka saba na ashindwe kuandika au kusoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala isiyoelekeza wala kukazia kumjenga mwanafunzi kupata maarifa, ujuzi na stadi za aina mbalimbali zitakazowasaidia wanafunzi kuishi pindi wamalizapo shule. Mitaala ya sasa, imebuniwa kufanya uzoni, ni mitihali na kukumbuka dhana rahisi tu. Haiwafundishi au kuwapa vijana uwezo wa kutatua matatizo ili kujenga nguvu ya kupambana na changamoto zinazoikabili jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitaala isiyohamasisha uelewa wa rasilimali za taifa na matumizi ya rasilimali, ni kumfanya mwanafunzi asiwe Mzalendo wa nchi yake. Mara nyingi mada zifundishazwo, hazina msingi. Mfano wanafunzi hapati ziara za mafunzo na kazi za nje zinazokazia maarifa kama kutembelea maeneo ya kihistoria na mbuga za wanyama. Hii inafanya wanafunzi wajazwe vichwani nadharia zisizo hai wanazoshindwa kuzipa tafsiri halisi za uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitabu vyta kiada shulen, Wizara ya elimu mwaka 1992 ilitoa tamko kwamba Serikali itajitoa katika kuchapisha vitabu. Pia mwaka 2004, Kamati ya Kuthibitisha Vifaa vya Elimu, iliundwa ili kuwezesha uwepo wa vitabu vyta aina mbalimbali, lengo likiwa ni wachapishaji waweze kuwa na ushindani wa kuchapisha na kusambaza vitabu shulen ili mradi wapate vibali kutoka *EMAC* (*Educational Materials Approval Committee*), wanaoangalia ubora wa vifaa husika kwa ajili ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005, Wizara ikapeleka madaraka ya kununua vitabu shulen. Tunaamini kuwa utaratibu wa kupeleka madaraka ya kununua vitabu shulen, ni mzuri na ni njia mojawapo ya kuboresha ubora wa elimu na kuboresha usomaji. Ni masikitiko makubwa kuona Wizara ikilipia gharama za uchapishaji wa vitabu na kuvipeleka shulen. Hii ni kinyume na Sera ya mwaka 1992. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kutoa maelezo ya kina juu ya utaratibu huu ambao ni kinyume na Sera ya Elimu ya mwaka 1992 na Wizara inatueleza nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sera inayopendekezwa ya kitabu kimoja kwa kila somo kwa nchi nzima, kuna taarifa kwamba Taasisi ya Ukuzaaji Mitaala (T.I.E), inatayarishwa kuchukua jukumu la kuchapisha na kupiga chapa vitabu vyta kiada. Kutokana na historia ya tasnia hii muhimu kwa Taifa, naishauri Serikali kulitazama upya jambo hili kama nilivyoshauri mwaka jana wakati nasoma bajeti ya Wizara hii hasa ikizingatiwa matatizo makubwa yaliyoikumba tasnia hii wakati tulipotumia kitabu kimoja. Kambi inahoji nini kimetokea hadi Serikali itake kubadili mfumo uliopo wakati ule wa awali ulishindwa ndio ukaja huu mfumo wa *multi -text books*? Ni lazima Serikali ije na maelezo ya kina uamuvi wake huu. Kwa hiyo, mfumo wa kitabu kimoja unapingana kabisa na Malengo ya Mtaala Mpya wa Elimu wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukiritimba, hakuna ushindani. Mchapishaji pekee, huwa hana sababu ya kuzingatia ubora au unafuu wa bei. Ni kujidanganya kuwa mchapishaji akipewa mitambo ya kupiga chapa basi vitabu vitakuwa nafuu. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (*TIE*), ina jukumu zito la ukuzaji mitaala ambayo ndio chimbuko la ubora wa elimu. Kazi hii ni nzito na nyeti sana. Hivyo wajikite katika kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali imeshindwa hata kulipa wazabuni fedha za chakula na kuwalipa Walimu, je, wataweza kununua vitabu? Kwa kuwa bado tuna tatizo kubwa la Walimu, vitabu vinaweza sana kusaidia mtoto kujisomea bila hata Mwalimu. Hivyo ni vema Serikali ilione hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya makubaliano ya Nchi tano zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni kuwa na mtaala mmoja kwa nchi zote (*Harmonisation of Curricula*). Kwa sasa, nchi zote zinatumia mfumo wa ‘Multi Textbook’ na tasnia ya uchapishaji katika nchi hizi inakuwa siku hadi siku. Ikiwa Tanzania pekee itarejea kwenye mfumo wa ‘Single Textbook’; basi kuna hatari ya wachapishaji wa Tanzania kufilisika na siku za usoni vitabu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki zikatolewa na wachapishaji wa nchi za jirani tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa vitabu, kwa sasa kuna maeneo mawili ya kuchunguza, eneo la mahitaji na eneo la utoaji (*demand and supply*). Tatizo la uwiano duni linatokana na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitabu. Ni asilimia 40% ya \$10 inayotengwa kwa mwanafunzi kwa vifaa vyta elimu na inayofika shuleni ni kidogo zaidi ya hizo \$4. Hii ndiyo sababu kubwa ya uhaba wa vitabu shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa vitabu vingi vyta kiada kwa somo moja, ni kutoa nafasi ya kufanya uchaguzi. Uchaguzi wa vitabu bora kutokana na mahitaji ya watumiaji ili mradi vitabu vilivyopo ni vile vilivyopewa ithibati ya ubora kutoka mamlaka yenye uwezo wa kisheria ya kutoa ithibati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani kuwa vitabu vyta kiada kwa shule za msingi na sekondari viandikwe na Maprofesa, haina msingi wowote wa hali halisi. Hata vikiandikwa na Maprofesa lazima vihaririwe na wachapishaji. Vitabu hivyo huandikwa kwa ufanisi zaidi na Walimu waliofundisha kwa muda mrefu katika shule hizo na wenye usoefu mkubwa wa kufundisha darasani

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hakika kuwa mpango wa kukabidhi jukumu la upatikanaji wa vitabu vyta shule kwa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (*TIE*), hautafafulu kwani ni njia iliyokwishajaribiwa ikashindwa na matokeo yake yakawa na athari mbaya kwa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa *TIE* kupatiwa mashine za kupiga chapa ili wachape vitabu vyta nchi nzima, unapaswa uangaliwe kwa makini, kwani uchapaji vitabu ni fani ya kiutaalamu ambayo inahitaji wataalamu waliobobe, mamia ya wafanyakazi wa shifti, miKataba madhubuti ya kuhakikisha uwepo wa karatasi za kupiga chapa, wino na

vipuri kwa nyakati zote, maghala makubwa ya kuhifadhi karatasi na vitabu nya nchi nzima. Mabilioni ya pesa yatahitajika kuendeleza uchapaji huu hata kama mashine zitakuwa zimetolewa bure. Pia ina maana Serikali inaingia upya kwenye kufanya biashara na kuendesha viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inajiuliza na kuiuliza Serikali, ni kwa nini Wizara na Taasisi wanataka kurudisha uchapishaji na urudufu (*printing*) wa vitabu kwa Taasisi ya Elimu? Kambi ya Upinzani, inahoji pia ni kwa nini hakuna program za kujisomea Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa chakula shulenii. Ukosefu wa chakula shulenii, ni tatizo kubwa nchini na linaletelea adha kubwa kwa wanafunzi wetu. Kuwepo kwa chakula cha kutosha katika shule zetu, itahakikisha kuwa watoto wetu wanapata elimu inayotakiwa, bila kuwa na fikra kuhusu chakula. Hii inatokana na ukweli kwamba watoto wanahitaji chakula kwa kiasi kikubwa kutokana na sababu nyingi zikiwemo za kibaiolojia ambazo zinahusiana na makuzi yao. Siku za nyuma, watoto walipenda shule kwani walijua watapata mlo. Hali halisi ya uchumi wetu, inaonesha Watanzania wengi huishi chini ya dola moja kwa siku. Kama hali ni hii, ina maana watoto hawawezi kupata mlo na hivyo tegemeo lao lingekuwa shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni jambo la ajabu na la aibu kwa kuwa na matembezi ya hisani ya kutunisha Mfuko wa Chakula. Haieleweki mfuko huo umekusanya kiasi gani na ni shule zipi hupata chakula kitokanacho na fedha hizo. Kwa maana nyingine, ni vigezo gani vinatumika? Je, zoezi hili ni endelevu? Kwa nini pasitengwe bajeti ya chakula shulenii? Kama zamani iliwezekana, tatizo leo linatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti tofauti zinaonesha kuwa ukosefu wa chakula shulenii husababisha wanafunzi wengi hasa katika shule za kawaida kuwa na uelewa mdogo darasani kutokana kutokuwa na lishe bora inayomwezesha kutulia darasani hadi mwisho wa masomo. Njaa imekuwa ni tishio kubwa shulenii kwani ndio kimeonekana chanzo cha kushusha taaluma. Watoto wengi wamekuwa hawahudhurii darasani kwa kushindwa kupata mlo utakaomwezesha awepo shule hadi mwisho wa vipindi hivyo kuamua kushinda nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa chakula kwa maendeleo ya afya na taaluma watoto wetu, Kambi ya Upinzani, inahitaji ufanuzi unaojitosheleza, ni kwa nini Serikali inafanya matembezi ya kutafuta fedha za chakula na, je, zoezi hili ni endelevu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya michango ya wananchi. Wote tunajua ni jinsi gani wananchi wameshiriki katika ujenzi wa shule za msingi na sekondari. Bado haijulikani ni kiasi gani wananchi wamechangia shule hizi. Tunajiuliza, ni nani mwenye

mamlaka ya kuhakikisha kuwa hizi pesa za wananchi zinatumika kama ilivyopangwa? Pia ni nani mwenye jukumu la kuhakiki pesa hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutofanya tathmini ya pesa za wananchi, madhara yake hayaishii tu kwa wananchi bali hii inadhihirisha ya kuwa Serikali iliyoko madarakani haijui hata thamani ya rasilimali zake wenyewe. Hii ni hatari, kwani watu wachache wasio na mapenzi na maendeleo ya Watanzania wote kwa ujumla na waliojawa na tamaa watatumia nafasi hiyo. Hivyo kujilimbikizia mali na hivyo ni ufisadi usioepukika kwa sababu, Serikali haitaweza kumkamata mtu huyu kwa sababu haijui hata wananchi walichangia kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hilo, Kambi ya Upinzani, inahitaji ufanuzi wa kutosha ni kwa nini hakuna tathmini ya nguvu za wananchi katika ujenzi wa shule. Hivyo kuweza kuwahakikisha wananchi juu ya matumizi ya fedha zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya Ualimu, ni taaluma pekee katika jamii inayogusa na kuzaa taaluma nyingine zote. Upekee huu, unatokana na kutoa maarifu na binadamu ana saikolojia ya kuwalea na kuwakuza binadamu wenzie wenge tabia na sifa tofauti ili wawe watu muhimu katika jamii tofauti na Mhandisi anayeshughulika na mitambo au majengo yasiyosema wala kubadili tabia na hisia. Upekee wa Mwalimu unakuja katika kazi kubwa ya kutafsiri falsafa na sera ya nchi ili kuzifikisha kwa wanafunzi na jamii. Mwalimu anajishughulisha na mambo makubwa matatu kwa binadamu nayo ni akili, hisia na maadili au mwenendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya Walimu. Hali ya mvutano wa Walimu na Serikali, ni kiashiria cha hatari kwa mwelekeo wa elimu hapa nchini. Watoto watakosa haki ya kufundishwa kutohana na mvutano huu. Lakini kibaya zaidi, watakaoadhidiwa/kuathiriwa, ni watoto wa wananchi wa kawaida ambao ndio wengi hapa nchini. Hawa ni wale wa wakulima na wafugaji na wafanyakazi wa kipato cha chini wanaofikia 80% tu ya Watanzania wote. Hili ni kundi kubwa na tusipochukua hatua za haraka tutadidimiza Taifa letu. Kwa takwimu hizi, ina maana watoto wachache wanaosoma Shule za Watakatifu (St.) na zile nyingine za binafsi (*academy*) kama 4% ya watoto wote wa Watanzania walioko shulenii, hawa hawana shida ya Walimu wala vitendea kazi. Hawa ni watoto wa viongozi. Labda hii ndio sababu ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la Walimu linasuasua. Watanzania wenge uwezo, wanajua maana ya elimu na umuhimu wake na wanaigharamia sana. Hofu yangu ni pale nchi hii itakapokuwa inaongozwa na idadi hii ndogo ya 5%. Pamoja na matatizo makubwa ya uendeshaji wa Shule za Serikali ikiwemo uhaba wa Walimu, bado Walimu hawa wachache wanashindwa kuthaminiwa na hivyo kugoma. Hii ni sawa na kumsukumiza mtu anayening'inia shimonii badala ya kumpa kamba ili umvute atoke shimonii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, ingependa kujua, ni kwa nini viongozi hatuoni fahari kusomesha watoto wetu shule za Serikali kama ilivyokuwa wakati wa enzi za Mwalimu? Kwa nini hatujivunii shule zetu za Serikali? Ni lini Serikali itawalipa Walimu madai yao ya bilioni 40? Kama Bodi ya Mikopo ilikosa shilingi bilioni 80 na Serikali ikasema itazitafuta, kama barabara ya Dodoma – Babati

ilipigiwa kelele kwa kutotengewa fedha mwaka huu lakini Serikali ikasema itatafuta shilingi bilioni 40, iweje suala la Walimu liendelee kujadiliwa bila ufumbuzi huku tukjua umuhimu wa pekee wa Walimu? Au tunataka kuwa na taifa la wajinga? Lakini kuna msemo usemao, ‘kama elimu ni ghali, jaribu ujinga, *if education is expensive, try ignorance*’. Naona Watanzania tunaujaribu ujinga. Ni vema Serikali ifanye uamuzi wa kuwalipa mapema Walimu hawa ili tuokoe Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Walimu Tanzania (*CWT*). Ni ukweli usiopingika kuwa Walimu ndio watekelezaji wakuu na muhimu katika utoaji wa elimu bora na sio bora elimu. Kama Walimu hawakuandaliwa vizuri kimaisha, katika mazingira yao ya kazi na pia mahali wanapoishi, hata kama Serikali itajenga madarasa na shule nyingi kwa kutumia almasi na dhahabu, bado elimu itakayotolewa haitakidhi viwango vya Kimataifa katika ulimwengu huu wa utandawazi. Kwa kuzingatia hilo, ni jambo la kushangaza kuona tatizo la malimbikizo ya mishahara, fedha za likizo na uhamisho, likichukua muda mrefu jambo linalofanya fani hii ya Ualimu idharauliwe na hata kukimbiwa. Kilio cha Walimu ni cha muda mrefu lakini bado Serikali imeziba masikio. Leo Kambi ya Upinzani inataka matatizo ya Walimu yatatutiwe ufumbuzi wakudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijui sababu ya msingi ni nini hasa, lakini kila mwaka tunaongelea suala la kupunguza madeni ya Walimu kwa Wizara husika lakini ulimbikizaji wa madeni unendelea, pamoja na kuwa Serikali iliahidi kutolimbikiza madeni baada ya Tume ya Waziri Mkuu ya 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za Walimu sio katika upande wa malimbikizo tu, bali moja katika matatizo sugu ambayo huwapata Walimu, ni katika suala la kupandishwa madaraja. Hali hii inakatisha tamaa na inasababisha Walimu waendelee kuwa wanyonge kama vile raia wasio na haki na taaluma ya kujivunia. Kambi ya Upinzani, inamtaka Mheshimiwa Waziri mhusika, atueleze sababu za msingi hasa ni zipi zinazosababisha kero hii iendelee kukomaa? Je, Wizara inasubiri nini ili iweze kuchukua hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wa elimu Tanzania, wamekuwa wakiishauri Serikali uwepo wa Bodi ya Walimu, itakayoangalia pamoja na mambo mengine kudhibiti nidhamu, ubora wa Walimu, maadili na taaluma yao n.k. Ni lini Serikali itakubali ombi hili ili Walimu wawe na bodi yao? Kambi ya Upinzani inaungana na Walimu wote Tanzania na inapenda kuwatanabaisha kuwa iko nao siku zote. Kwa kutumia nafasi yake, itaendelea kuikumbusha Serikali juu ya matatizo yanayowakuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni haki ya kila mtu. Elimu ni stahili ya msingi ya kila binadamu. Elimu ni kipimo cha utu na utashi wa maamuzi sahihi. Elimu ndiyo daraja la maendeleo au ndio ukombozi wa mwanadamu. Pamoja na umuhimu wa elimu kwa kila mtu na kwamba elimu ni haki ya msingi, bado haki hii kwa baadhi ya makundi haipatikani au inapatikana kwa shida sana. Makundi ya wanawake, wenye ulemavu na maskini yamesahaulika. Watoto wa maskini pamoja na kuwa wameenda shule lakini wanakaa chini na hawana Walimu. Kutwa nzima hawaelewi lolote hadi wanamaliza shule hakuna maarifa kichwani, japo wameva sare za shule kwa miaka saba na

kuzipamba nyaraka za Serikali kuongeza idadi ya takwimu za uandikishaji. Kuna haja gani kukaa darasani miaka saba unaondoka hujui hata kusoma wala kuandika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere alijua sana umuhimu wa haki hii ya elimu ndio maana aliwapatia elimu Watanzania wote bure, kuanzia elimu ya msingi hadi Vyuo Vikuu. Leo hii elimu kwa watoto wa kimaskini imekuwa hadithi kwa madai kuwa Serikali haina pesa. Pamoja na ukweli kwamba elimu ndilo daraja la maendeleo au ndio ukombozi wa mwanadamu, bado kwa watu wenye ulemavu kupata elimu ni kama hisani au msaada, badala ya haki ya msingi. Takwimu za Taifa zinaonyesha kuwa ni asilimia moja tu ya wenye ulemavu wako katika shule za msingi (BEST 2007), je, wengine wako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuna mtizamo hasi kuwa watu wenye ulemavu, kwamba hawawezi chochote hivyo hakuna haja ya kuwapeleka shule. Hii si sahihi kwani takwimu ulimwenguni zinaonyesha kuwa karibu kila taasisi kubwa zina wataalamu au Profesa mwenye ulemavu na hawa wala hawakughushi vyeti. Ushahidi wa uwezo wa walemovu uko wazi japo jamii inaendelea kuwatenga na kuwabagua katika nyanja nyingi za maisha ya kila siku. Mfano, hivi ni kweli mtu mwenye ulemavu wa ngozi (albino), mikono yake haiwezi kufanya kazi kama kutumia kompyuta, kufuma, kupaka rangi, udereva na kadhalika? Mlemavu wa miguu, hawezi kufanya shughuli kwa mikono yake na kadhalika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kasumba na mtazamo dhaifu wa jamii na watunga sera ndio unaodidimiza haki za wenye ulemavu, ikiwemo elimu na kudumaza maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Kutengwa huko, kunawanyima fursa nyingi za kimaendeleo kwa sababu wanakosa maarifa yanayotakiwa, ambayo kwa kiwango kikubwa yangewasaidia kutumia fursa zilizopo na kubuni fursa mpya zitakazowawezesha kuishi maisha yenye ustawi wa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu, imekumbwa na changamoto nyingi kwa muda mrefu sana. Hii inatokana na sababu nyingi ikiwamo wananchi kuhamasika kupeleka watoto shulen. Hali iliyopelekea ujenzi wa shule nyingi na hivyo uhaba wa Walimu na vitendea kazi kama vile, vifaa vya kujifunzia na kufundishia, upungufu wa maabara za masomo ya sayansi, ufaulu mdogo katika masomo ya lugha, hisabati na masomo ya sayansi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati huwa na matokeo ya muda mrefu katika ubora wa elimu, kwa mfano, kuongeza nafasi za mafunzo ya Ualimu katika Vyuo vya Ualimu, Vyuo Vikuu na kadhalika. Mikakati hii huchukuwa hadi miaka 4-5 ili kuweza kuonekana matunda yake katika jamii kinamba. Swali la kujiuliza hapa ni kwa jinsi gani ubora wa elimu ulivyowekwa rehani kutokana na upungufu wa Walimu utashughulikiwa katika muda mfupi? Kwa maneno mengine, mikakati yote hii haielezei suala la kupambana na kutatua madhara ya changamoto za ubora wa elimu na mafunzo ambayo tumekuwa nayo kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu vinaweza sana kuongeza ufanisi wa kujifunzia kwa wanafunzi. Hata hivyo, hii inaathiri sana uwezo wa Walimu wa kutumia vitabu kama kigezo muhimu katika mchakato wa kufundishia na kujifunzia. Suala la kujiuliza hapa ni, je, kuna taratibu za ubora na uhalisia wa matumizi ya vitabu na majarida mengine ya kujisomea darasani na hata nje ya darasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii, Wizara imejitahidi sana kuelezea ongezeko la madarasa, maabara ya sayansi na vifaa vyake, maktaba, kufundisha na kuajiri Walimu na kadhalika. Pamoja na umuhimu wa vigezo hivi, kilicho muhimu zaidi, ni kile kinachoendelea darasani na hiki ndicho kitakachojibu kama kweli elimu yetu inaenda sawasawa. Kwa mfano, ni kwa nini wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wanafanya vibaya katika masomo ya sayansi, lugha na hisabati? Kati ya viashiria vya darasani, ubora wa ufundishaji darasani katika utaalamu na ufundishaji (*pedagogical skills*), ndio kiashiria pekee kinacholeta tofauti. Katika hili, je, kuna mikakati yoyote ya kitaalamu ya kusaidia katika ngazi za shule kama vile ukaguzi yaani *clinical supervision?* Jibu sio Vituo vya Walimu yaani *Teachers' Resource Centres* kwa kuwa ushahidi uliopo unaonesha kwamba vituo hivi hutumika kwa Walimu kujiendeleza kitaaluma kama kujisomea kwa mitihani yao ya Kidato cha Nne na cha Sita na si kwa kujiendeleza kitaalamu yaani *professional support*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa mitihani. Wimbi la kughushi vyeti na udanganyifu kwenye mitihani, limezidi kuwa mwiba mkali kwa Serikali ingawa ahadi nyingi na mikakati ya kupambana na kudhibiti wizi huu, bado tatizo linaendelea tena kwa kasi zaidi. Kila sehemu ya nchi hii, jambo linalosikika ni vyeti bandia, kughushi nyaraka, udanganyifu kwenye mitihani kuanzia ngazi ya msingi hadi vyuo vikuu. Mbaya zaidi wahusika ni watu wa tabaka zote kuanzia walinzi, maafisa na kadhalika. Kama litaachwa, kutamalaki nchi hii itakuwa ya wasomo bandia, hii ni hatari kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya sababu ya wizi huu ni:-

- Viongozi wengi wanaghushi vyeti, wanatumia majina yasiyo yao au walidanganya wakati wa mitihani, Kiongozi wa aina hii, kamwe hawezikukosoa tabia ya kughushi vyeti. Kama kughushi, ni kosa la jinai, kwa nini viongozi wanaopatikana na kosa hili, hata wale wa kisiasa, kama Wabunge, wasishtakiwe kwa kosa la jinai? Kughushi vyeti, ni sawa na ubakaji wa ajira, ifike mahala sasa kuwe na Muswada wa Kisheria dhidi ya Wizi wa Mitihani na Kughushi Vyeti.

- Mtazamo hasi wa viongozi na wananchi wengi ulioifanya elimu kuwa ni cheti na kufaulu mitihani na si uelewa na maarifa. Ni watu wachache sana wanatambua kuwa elimu ni maarifa na uwezo ambao mtu anaupata baada ya kuingiza maarifa kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti , mtu anayetambua kuwa elimu ni cheti, hatahangai ka kutafuta maarifa. Yeye atahangaika kupata cheti hata cha kughushi au aibe mitihani maana yake hiyo ndiyo elimu. Hakuna kamusi au kitabu chochote duniani kinachoeleza maana ya elimu kuwa ni cheti au kufaulu mtihani. Je, kwa mtazamo huu, udanganyifu katika mitihani na kughushi vyeti utaisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini viongozi hawana dhamira ya dhati ya kumaliza tatizo hili kwani limeanza zamani na vyombo husika vinawajua wahusika na mbinu zitumikazo. Bila utashi wa viongozi na dhamira ya uzalendo, Taifa hili litaangamia kwa kuwa na wasomi bandia, wasiojua lolote, watakaoliangamiza Taifa letu kwa kuza rasilimali za nchi yetu kwa miKataba mibovu. Kambi ya Upinzani, inataka kujua ni mikakati gani Wizara imepanga ya kumaliza kabisa tatizo hili ikiwa ni pamoja na kuwafikisha Mahakamani wale wote waliogushi vyeti hata kama ni wanasiasa i.e. Wabunge na Mawaziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Baraza la Mitihani la Taifa. Hatuwezi kuongelea wizi/uvujaji wa mitihani na vyeti bandia, bila kugusia Baraza letu la Mitihani (*NECTA*). Kwa muda mrefu, tatizo la wizi limekuwepo na kubwa zaidi lilikuwa lile la mwaka 1998 ambapo Serikali ilifuta mitihani yote na kutunga upya. Baadaye Tume iliyoundwa, ilipendekeza mitihani itungwe nje ya nchi. Mwaka jana tena 2008 tatizo limejitokeza tena baada ya somo la hisabati kuvuja katika hatua za awali. Lakini taarifa zinaonesha hata mitihani ya masomo mengine ilivuja. Kinachoshangaza Tume iliyoundwa kuchunguza uvujaji huo chini ya Prof. Maboko Makenya bado hajatoa ripoti yake kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza pamoja na Tume kutotoa ripoti yake, uongozi wa Baraza umewahamisha wafanyakazi 80 wiki iliyopita bila hata kushirikisha Chama cha Wafanyakazi. Vile vile uhamisho huo wa tarehe 11/7/2009, ulifanywa kwa ubabe na mabavu kwa kusimamiwa na Walinzi Binafsi, Polisi na Usalama wa Taifa, kwa kupewa barua na kulazimishwa watoke nje ya geti kama vile ni wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atoe majibu ya kina, ni kwa nini watumishi hawa wanyanyaswe kiasi hicho na kwa makosa yapi? Ni lini Tume itatoa ripoti ya yaliyojiri kwa uvujaji wa mitihani mwaka 2008? Ni nini mkakati wa Serikali kumaliza kabisa tatizo la wizi wa mitihani? Je, kuwaondoa wafanyakazi wote waliokuwepo kabla ya mwaka 2006, ndio suluhu? Kwa kuwa Tume zote zilizochunguza wizi huo, ni za Serikali, tunaomba Bunge liunde Tume huru kuchunguza uvujaji wa mitihani na ripoti hiyo itolewe hadharani kama ilivyofanyika kwa Kamati Teule ya Bunge ya Kuchunguza Kampuni ya Richmond.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Ugatuaji yaani *D by D*. Usimamizi na uendeshaji wa shule za awali, msingi na sekondari, umepewa Wizara ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa katika kile kiitwacho ugatuaji yaani *D by D*, hii ikimaanisha (Ugatuaji kisiasa, kiutawala, kifedha yaani, *Political Decentralization; Fiscal Decentralization; Administrative Decentralization and Central-Local Intergovernmental Relations*). Hii inamaanisha kuendesha shule za msingi za Serikali 15,257 na shule za sekondari za Serikali 3,039 (i.e 18,296 kwa takwimu za mwaka 2008 *Basic Education Statistics Data*) na zaidi ya wanafunzi 9,000,000 na Walimu na wafanyakazi 220,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinacholeta mtafaruku na kutoingia akilini ni kwamba kabla hata ya ugatuaji madaraka kwenda TAMISEMI kulikuwa na kilio kwamba shule za msingi hazikuwa zinafanya vizuri, kwa kutokuwa na uwezo kwenye Halmashauri zetu hususan katika utawala, uendeshaji na utoaji wa fedha kwa huduma za jamii. Katika ngazi za shule za msingi, kuna tatizo bado la kuwa na uelewa mdogo wa wajumbe wa Kamati za Shule kuweza kuendana na mabadiliko kama vile Mipango ya Maendeleo ya Shule (*School Development Planning*), bajeti za shule (*school budgets*), *capitation fee/development grants*, taratibu za manunuzi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili litaongeza urasimu wa zoezi zima la utoaji huduma nzuri kwa sababu ya miundo isiyoltinganifu (*parallel*) wa kiutawala iliyowekwa katika elimu ya sekondari. Hii si tu kwamba itawaondoa Walimu shulenii na Wakuu wa Shule kushika nyadhifa za Afisa Wilaya na Maafisa Waandamizi wa Elimu ya Sekondari bali watahitaji ofisi, vitendea kazi na mafunzo ya kujengea uwezo. Gharama zote hizi zikibebwa na walipa kodi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya juu ni muhimu sana kwani mbali na kutoa wafanyakazi kwa sekta mbalimbali nchini na nje, pia inajenga uwezo wa kushiriki katika dimbwi linalokuwa la dunia ya maarifa na kuweza kupokea na kutumia maarifa hayo hapa nchini. Ni dhahiri elimu ya juu, inaweza kulingana na kugundua (mbinu) katika nyanja zote za maendeleo nchini. Katika nchi maskini kama yetu, elimu ni lazima (sharti) kama mabadiliko ya kudumu na kwamba kukua katika uchumi wote, haitaweza kutumika bila kujengwa uwezo katika mfumo wa elimu ya juu. Hivyo ni muhimu sana kutegemeana na kuimarisha mahusiano kati ya elimu katika ngazi zote, uchumi na maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akili za kawaida na tafiti zilizofanywa katika jamii mbalimbali, zinaonyesha kwamba umuhimu wa elimu ya juu katika nyanja zote za uchumi na maendeleo ya watu kwani inasaidia:-

- Kukua kwa uchumi, inaboresha mapato na kipato, inaongeza uzalishaji, ujasiriamali, inaongeza pia kukua kwa jamii, ushiriki katika siasa na utawala wa kidemokrasia, kuondoa umasikini na uboreshaji wa umri wa kuishi na ubora wake.
- Uongofu kwa viongozi, elimu inawapa ujasiri kuongoza kwa uadilifu na maarifa ya teknolojia na pia kutengeneza kada za Walimu bingwa katika ngazi zote za elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo makubwa manne yanayohitajika katika mfumo wa elimu yaani kupata elimu hiyo kwa watoto wengi bila kujali rangi, dini, jinsia na utaifa, umuhimu wake kwa mahitaji ya watoto, familia na mahitaji ya uchumi; ubora wake kwa maana ya kupata maarifa na mtazamo. Mfumo wetu wa elimu unahitaji uwazi/unyofu na uainisho wa uhakiki (*intrical analysis*) ili kuwa na elimu bora na si bora elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikiwa na elimu kuna mambo mawili. Kwanza, kuwepo kwa sehemu za kutolea elimu na pia uwepo (*availability*) na upatikanaji yaani (*affordability*) ya gharama za huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la huduma kwa wanafunzi kwa ujumla, ukianzia na malazi, huduma za chakula, vyoo, maji na mabafu, ni kero kubwa na haivumiliki kwa jamii yoyote ile ya wasomi. Wanafunzi wengi wanakosa mahala pa kulala, kwa sababu mabweni ni machache sana ukilinganisha na idadi ya wanafunzi, hivyo hali ambayo inapelekeea wanafunzi kulazimika kubebana yaani kitanda kimoja wanafunzi wawili na hata wakifanya hivyo bado mabweni yanakuwa hayatoshi, kwamba bado idadi kubwa ya wanafunzi wanabaki hawana mahala pa kulala, hali hii inaambatana na pia kwamba vyumba ni vidogo sana, kwa hiyo chumba kidogo kimoja chenye vitanda viwili kinabeba wanafunzi nane, hali ambayo kiafya na kitaaluma siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na sehemu za kulala, pia kuna tatizo kubwa la vyoo vilivyopo ni vile vya kukaa (*European Type*), ambavyo ukiangalia viliwekwa vikilenga wanafunzi wawili ama wanne choo kimoja, lakini kwa staili ya vyoo vya kukaa kwa idadi kubwa ya wanafunzi wote kukalia choo hicho na ukichukulia hali ya magonjwa ya siku hizi, ni hatari kwa afya za wanafunzi. Mfano wa vyoo vya staili hiyo, ni mabweni yote ya *Campus* ya Mlimani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hali ya maji inatisha sana, kwani hakuna maji ya uhakika, hali ambayo inamfanya mwanafunzi kushuka kutoka ghorofa ya II, mpaka chini kufuata maji ama ya chooni ama kuoga na vyoo vyenyewe ni vya kukaa na maji ni shida, hivyo inapelekeea hata hali ya vyoo vinavyohitaji maji mengi, kwa sababu maji yanakuwa ya shida hata hali ya vyoo inakuwa inatisha kupelekeea hatari ya magonjwa ya milipuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa mtandao wa komputa. Hivi karibuni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundis, ametangaza kuwa kila Mwalimu wa shule ya sekondari ya Serikali atapewa kompyuta kwa ajili ya kufundishia wanafunzi kwa kutumia teknolojia ya habari kama njia ya kukabiliana na uhaba mkubwa wa Walimu unaoikabili sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huo utaanza kwa majaribio mwezi Oktoba mwaka huu katika baadhi ya maeneo na kuenea nchi nzima baadaye mwakani. Hii ni habari njema sana kama kweli uwezo huo tunao na shule zetu zote zitakuwa na mtandao huo. Lakini ni wazi kuwa, ubora wa elimu kuanzia shule ya msingi hadi chuo kikuu umeshuka sana Tanzania. Kushuka huku kwa ubora wa elimu, kunatokana na kuwa na mitaala isiyoendana na wakati, Walimu wasio na sifa za kufundisha, ukosefu wa vifaa vya kufundishia, miundombinu mibovu ya madarasa na kushuka kwa ari na mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaamini kuwa kutumia kompyuta kufundishia sio kipaumbele “*priority*” kwa sasa. Ingefaa tuenze kuboresha elimu katika

shule za msingi kwa mfano bado tuna shule zisizo na madawati, watoto wanakaa chini, bado tuna majengo ya udongo na hatuna Walimu. Vile vile hao Walimu watakaopewa hizo kompyuta, wamepewa maandalizi gani ya kuzitumia? Je, tumeandaa mitaala ya kutumika kwenye mfumo wa mawasiliano ya kompyuta? Kambi ya Upinzani, ina wasiwasni na mradi huu mkubwa wa manunuzi na tunahoji fedha hizo zimetoka wapi na tunaamini kabisa hautekelezeka na kubwa zaidi haulengi kuinua ubora wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migomo vyuo vya elimu ya juu. Kwa muda mrefu sasa, vyuo vya elimu ya juu, vimekuwa vikikumbwa na migomo ya mara kwa mara. Sababu kubwa imekuwa ni suala zima la mikopo kwa wanafunzi hawa. Kinachojitokeza waziwazi, ni fedha za mkopo kutofika kwa wakati lakini kubwa zaidi ni vigezo vilivyotumika kuwaweka katika makundi ya kupata mikopo hiyo. Pamoja na kwamba wengi waliwekwa kwenye kundi *D*, bado wazazi walishindwa kulipia gharama hizo za asilimia 40. Kambi ya upinzani, inaamini pamoja na madaraja ya wanafunzi kupata mikopo imeongezeka hadi 10 bado mchakato wa kupanga madaraja hayo hayana uhalisia. Hali hii bado itaendelea kuwabagua wanafunzi hawa na hivyo kuendeleza migongano. Kambi ya Upinzani, inashauri Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ifanye kazi ya kuhakiki hali za uchumi za wazazi/walezi wa vijana hawa ili isije ikawa mwenye nacho anaongezewa na asiye nacho anakosa kabisa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na migomo hii, imekuwa ni jambo la kawaida kabisa kwa viongozi halali wa wanafunzi kusimamishwa/ au kufukuzwa vyuoni kwa kuwa tu wanafunzi wamegoma kwa sababu za msingi kabisa. Tujuavyo sisi, viongozi hawa ndio daraja kati ya wanafunzi na utawala na Serikali. Nyakati zote, hawa ndio wanaowasiliana na utawala kwani wanafunzi wote hawawezi kuwasiliana na utawala. Kinachosikitisha, panapotokea matatizo, viongozi hawa ndio wanawajibishwa. Je, hii ni halali? Mara nyingi au zote, viongozi hawa wanakuwa si chanzo cha mgomo. Serikali haioni kuwafukuza ni kuwaonea na kuwafanya hata wale wenye sifa za uongozi kuhofia kugombea nafasi hizo? Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri atuambie, ni nini hatma ya viongozi wa *DARUSO* wakiongozwa na Antony Machibya ambao hadi leo hawajarudi chuoni na hawapaswi kutoka nje ya Dar es Salaam. Lakini vile vile, ni nini hatma ya wanafunzi wa *UDOM* waliosimamishwa bila hata kuitwa na kusikilizwa. Hivi siku hizi hata Kamati za Nidhamu zinazopaswa kuwasikiliza vijana wanapokuwa na matatizo, zimevunjwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Wafanyakazi wa Elimu ya Juu (*THTU*), kuhusu mishahara ya wafanyakazi waendeshaji. Utekelezaji wa maboresha ya mishahara ya wafanyakazi waendeshaji, bado haujafanyika kama Serikali ilivyoahidi kupitia mapendekezo ya Kamati ya Rais ya mwaka 2005. Licha ya viongozi wa wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu kulifutilia suala hili kwa makini na licha ya Serikali kutoa maelekezo na ahadi mbalimbali, utekelezaji wake haujafanyika kama ilivyopasa tangu mwaka 2006. Ucheleweshwaji huu, umejenga taswira mbaya mionganoni mwa wafanyakazi wa taasisi husika na unaweza kuathiri imani ya wananchi katika Serikali yao. Kambi ya Upinzani, inamtakwa Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake atueleze sababu za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Rais ya 2005 kuchukua

muda mrefu jinsi hii na hali ikoje sasa. Ni lini basi watatendewa haki kama walivyowafanya wanataaluma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya mafao ya uzeeni (Mifuko ya Hifadhi Jamii). Mafao ya ustaafu yatolewayo kwa wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, ni duni mno. Tunayo taarifa kuwa, hoja ya kuboresha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, imefikishwa mikononi mwa Serikali na kwamba Serikali imebaini ukweli wa hoja hii na kuahidi kuifanya kazi. Hata hivyo, kasi ya utekelezaji wa mchakato wa mabadiliko yake hauridhishi, hasa ukizingatia kuwa kundi kubwa sana la wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu wapo njiani kustaafu katika kipindi kifupi kijacho. Tunaiomba Serikali iongeze kasi ya kufanya marekebisho ya mafao ya mifuko ya *PPF* na *NSSF*, ili tofauti kubwa iliyopo kati ya mafao ya wafanyakazi wa shule za elimu ya sekondari na msingi na zile za Taasisi za Elimu ya Juu, ipatiwe ufumbuzi. Serikali iharakishe pia kuwahamisha wafanyakazi wa taasisi husika walio kwenye muundo wa *SSSS (Senior Staff Superannuation Scheme)* inayohudumiwa na *NIC* katika mifuko iliyobora. Tunaamini kwa kufanya hivyo, Serikali itatoa haki na kutambua mchango mkubwa wa wafanyakazi wa taasisi husika katika kuandaa wataalamu na rasilimali watu bora kwa ajili ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya matibabu kwa wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu. Matibabu, ni haki ya msingi ya watumishi wa umma inayolindwa na Katiba na Sheri za nchi. Hivi karibuni, Taasisi za Elimu ya Juu, zimepokea agizo, kutoka kwa Msajili wa Hazina, la kutekeleza mara moja makato ya ada ya Mfuko wa Bima ya Afya kwa mujibu wa sheria husika. Wawakilishi wa wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, hawakuhusishwa katika mchakato wa kutunga/kurekebisha sheria husika kama Katiba ya nchi inavyoagiza. Hivyo, utekelezaji wa agizo hilo unaweza kuleta mtafaruku usio wa lazima maana agizo hilo linakinzana na Sheria za Kazi, Sheria za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (ambayo inajumuisha fao la matibabu), Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria Mama ya nchi. Ili kuzuia mgogoro usio na lazima, tunaomba Serikali isitishe agizo hilo na kutoa nafasi na kuziwezesha taasisi husika kutekeleza mipango ya tiba kwa wafanyakazi wake kwa mujibu wa taratibu na sera zake kwa mujibu misingi ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo lisilopingika kwamba elimu katika ngazi ya juu ni gharama kubwa na sio jambo la kubishana ya kwamba elimu ya juu inahitaji kupanuliwa. Hili ni jambo muhimu na la haraka ambalo ni kipaumbele. Ni dhahiri kabisa pia kwamba uchumi wetu unaweza kulipia gharama zitakiwazo kwa elimu hiyo. Kusema tu hakuna fedha, hilo si jibu la kweli. Ukweli ni kwamba fedha zipo. Suala hapa ni namna gani tunagawa fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali na kama kweli tunajali maendeleo ya wananchi wetu na ya nchi yetu. Jambo hasa, ni namna tunavyochagua vipaumbele na kwa hiyo, ni lazima kujua kwamba ipo haja ya kuacha mengine kwa ajili hiyo. Kwa hiyo, kama tunajali na tunaamua kuwa elimu ni kipaumbele, basi bajeti itatengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ya elimu nchini ni lukuki, ni vyema wote tuyaaangalie si yale tu niliyoyataja katika hotuba hii bali elimu kwa ujumla

wake, ili hatima yake iwe kuibuliwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo yenye ubora wa kipekee, tunayoikubali wote na tena inayoteklezeka. Tutumie fursa hii kuwataka watekelezaji katika sekta ya elimu, wazingatie dira yetu inayobainishwa katika sera zilizo rasmi na iwe mwiko kuchukua maamuzi yanayoliondoa Taifa katika mwelekeo unaokubalika na ulio sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti , vile vile, tuzingatie kuwa ni kazi bure kuongelea elimu bora bila mitaala bora tena inayozingatia wakati tulionao na ujao. Tufikie mahali sasa ambapo tunaweza kusema kumdhailisha Mwalimu na taaluma ya Ualimu sasa basi. Mathalani, tuwe na sheria inayouhesabu ucheleweshaji wa mishahara na maslahi mengine ya Walimu kwamba ni udhalilishaji, ni kunyume cha haki za binadamu na ni kosa la jinai. Pia tuwe na utaratibu unaompa heshima ya pekee Mwalimu. Kama tunadiriki kuwaambia Walimu kila mara kwamba kazi yao ni ya wito, basi tusione taabu kuwapa heshima ileile ya kijamii wanayopewa watumishi wengine wa wito, mathalani viongozi na watumishi wa dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ukosefu wa nyumba za Walimu, iwe marufuku kufungua shule mpya ambayo haina nyumba za Walimu, nyumba zenyen hadhi tena kwa idadi inayoendana na ikama itakiwayo. Aidha, iwe haki ya Mwalimu kupewa nyumba ya kuishi na mwajiri (*entitled*) na Mwalimu asipelekwe katika shule fulani bila mwajiri kumhakikisha nyumba ya kuishi na familia yake. Katika kumwendeleza Mwalimu kitaaluma, uwe wajibu wa mwajiri (Serikali au binafsi) ndani ya mKataba wa kazi kumwendeleza Mwalimu kila baada ya muda uliotajwa wazi, kupitia njia ya mafunzo kazini na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na tatizo linalojitokeza la matumizi mabaya ya rasilimali watu, mjadala wa kitaifa utusaidie tuwapange Walimu wetu (askari wetu dhidi ya ujinga) katika mstari wanapostahili kuwa. Vile vile, tujadiliane tupate ufumbuzi ambao ungefaa kwa matatizo ya maktaba na wananchi kutopenda kujisomea. Suluhu yaweza kuwa ni pamoja na kuwafundisha Walimu hata wa shule za msingi ukutubi ili waboreshe huduma za maktaba kwa wanafunzi mashulen. Hili liendane pamoja na kuzitaka mamlaka husika kuhakikisha kila shule ina maktaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri uwepo wa Sera ya Elimu inayotaja bayana maadili ya kufundishwa kupitia elimu. Isiishie tu kuyataja bali itaje na njia za kuyafundisha. Wataalamu wanataja njia tano za ufundishaji maadili ambazo tunaweza kuziingiza katika sera yetu na kuwafundisha Walimu wetu kuzitumia, nazo ni kufunda (*inculcation*), kukuza mwenendo (*moral development*), kuchambua (*analysis*), kufafanua maadili (*value clarification*) na mafunzo vitendo (*action learning*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatubidi tutambue umuhimu wa kupanua elimu ya lazima kwa kila Mtanzania, iwe si chini ya Kidato cha Nne, ili kulipatia Taifa watu wenyewe ujuzi na uwezo kushiriki barabara katika miradi ya kuondoa umaskini na maradhi na wenyewe uwezo wa kuhoji na kuwajibisha viongozi. Pasipo kupanua elimu ya lazima (ya msingi), tutajikuta hatuna uwezo wa kupanua elimu ya juu na hivyo hatutapata nguvu kazi ya kutosha yenye taaluma za kati na za juu kiteknolojia. Vivyo hivyo, ikiwa tunasita

kuwekeza ipasavyo katika elimu ya juu kwa kuwapa mikopo wahitimu wote wenye sifa za kudahiliwa, maendeleo ya Taifa letu yatabaki kuwa ndoto ya mchana. Hatuna budi kusahihisha makosa yote tuliyyafanya katika sekta ya elimu, vinginevyo tusilie tukiona kuwa soko la ajira la Jumuiya ya Afrika Mashariki linatawaliwa na Wakenya, Waganda, Warundi na Wanyarwanda walioamua kuelewa nini maana ya kuwapa elimu bora raia wote, tusilalamike iwapo tutalazimika kuambulia kazi duni tu katika Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutumie akili zetu na tafiti za wataalamu wetu kutafuta na kutumia ipasavyo vyanzo vyote veya fedha vinavyowezekana kwa ajili ya kugharimia elimu. Vinginevyo, mipango yetu itaendelea kupendeza kwenye karatasi na elimu bora itabaki njozi. Miiongoni mwa vyanzo vinavyoweza kufaa, ni fungu kubwa zaidi kutoka bajeti ya Serikali, kodi maalum ya elimu, ushuru maalum mathalani katika vinywaji vikali, michango ya kila mwezi ya makampuni au mashirika yanayozalisha faida kubwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umekwisha wa kuendelea kuwa mashuhuda wa kuditidimia kwa sekta ya elimu nchini bila kufanya jitihada za maksudi tena madhubuti sote kwa pamoja kuliokoa taifa letu Tanzania. Hatuna budi kutafuta haraka ufumbuzi wa matatizo yote ya elimu kama tunalitakia Taifa letu mema. Tujadiliane kwa nia njema, tuitathmini Sera yetu ya Elimu kwa kina. Tuangalie wapi tunakosea, wapi tunafanikiwa, nini kinatukwamisha na nini tufanye. Hatimaye tuibuke na dira moja madhubuti itakayotuhakikishia kufika salama kwenye bandari ya maendeleo tunayoyatamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudhi mbalimbali zilizosomwa na Waziri za kuboresha mazingira ya elimu hapa nchini kama vile mradi wa komputa yaani *e-learning*, fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa veya maabara, Kambi ya Upinzani, inasisitiza kuwa kama Walimu hawatapatiwa mazingira mazuri ya kufanya kazi zao ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya madai yao, haya yote ni bure kwani Walimu ndio wanaotakiwa wasimamie *computers* hizo na ni wao watakaotumia maabara hizo. Pamoja na Kauli Mbiu ya Kilimo Kwanza, sisi tunasema Walimu Kwanza mengine yatafuata. “*If education is expensive try ignorance*” (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa makini na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Susan Lyimo kwa kuchangia hotuba hii kama mwakilishi wa Kambi ya Upinzani. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda bado unaturuhusu, kwa hiyo, sasa nitaanza kuwaita wachangiaji na kama nilivyosema tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Getrude RwaKatare, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatma Fereji na baadaye kama muda utaendelea kuturuhusu Mheshimiwa Abdul Marombwa ajiandae. Mheshimiwa Dkt. RwaKatare.

MHE. MCHUNGAJI DKT. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Elimu ambayo kwa hakika mimi ni mdau mkubwa.

Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa rehema na fadhili ambazo anatumwagia usiku na mchana. Nimshukuru pia Mungu wetu kwa msamaha wa maovu yetu tunayomuudhi hapa na pale, hakika Mungu wetu ni mwema. Daudi amesema kama Mungu angehesabu makosa yetu, ni nani angesimama? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba niishukuru Serikali yangu ya CCM, kwa kutekeleza Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi kwa asilimia mia moja (100%). Hakika wamejitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukurani za kipekee, naomba zimwendee Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa upendo mkubwa alionao kwa Watanzania wenzake. Mimi ni shuhuda, tumesafiri naye Wilaya hadi Wilaya akishukuru Watanzania wenzake, akiwajulia hali na hata akiuliza kero na tabu zao na pale alipoweza, mara moja aliweza kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi za tofauti kabisa kwa Mheshimiwa Rais, kwa Mabilioni ya JK. Ni wazo zuri na hakika wengi wamefaidika na tunatarajia watafaidika zaidi. Pia kwa jitihada yake ya kuboresha na kuinua kiwango cha michezo Tanzania na hasa Kandanda na vilevile Riadha. Pongezi kwa *UDOM* na mengine mengi lakini zaidi sana pongezi kwa Rais wetu kwa kuifanya Tanzania ijulikane ulimwenguni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu aliiweka Tanzania kwenye *CNN* mwaka mzima na nina hakika kabisa watalii wengi wanakuja nchini kwa sababu ya hatua hiyo. Ahsante pia kwa ujio wa Rais Bush, hakika ilikuwa ni kitu kizuri kwa Rais wa nchi kubwa kama ile kuja kutembelea Tanzania. Pongezi pia kwa yeye kuwa wa kwanza kuweza kumuona na kumpongeza Rais Obama kwa kuwa Rais wa kwanza mweusi katika Bara la America. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kwenye Wizara ya Elimu, kwani hayo yote yamekwisha maana nilikuwa na hamu niyaseme ili watu wayajue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Waziri wa Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Jumanne Maghembe na Manaibu wake, Waziri Mwantumu Mahiza na Gaudentia Kabaka, Katibu Wakuu wake, Wakurugenzi wote na Watendaji wote ambao wameweza kutuletea leo hotuba nzuri ya bajeti ambayo tunaenda kuijadili sasa hivi. Pongezi zenu kwa kutekeleza *MMEM*, *MMES* na mengine mengi na hata sasa hivi kwa percent mia moja (100%) ya mikopo kwa Vyuo Vikuu vyetu, tunashukuru hiyo kwa sababu ni kazi nzuri. Poleni kwa misukosuko pia hongereni kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo na maoni yangu, namba moja, naomba ijulikane kwamba, shule ni Walimu na wala sio majengo mazuri na kama shule ni Walimu basi tujitahidi kuboresha maslahi yao. Kilicho chao tuwape, tusiwakope Walimu kwa sababu mishahara yao ni midogo na wao pia wana mahitaji na pia wanafamilia. Kwa hiyo, tujitahidi na maadamu Waziri amesema pesa zipo basi mimi napendekeza kwamba, malimbikizo ya Walimu, yalipwe mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itawatia moyo Walimu, hii pia itaipa hadhi *profesion* ya Ualimu. Sasa hivi ukiuliza wanafunzi, wangapi wanaotaka Ualimu, wengi wanasema, mimi sitaki kuwa Mwalimu, naogopa, lakini hebu tuiboreshe *profession* ya Ualimu ambayo ni nzuri sana ili iweze kuwavuta vijana wengi ili waweze kujunga nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha Ualimu, si lazima iwe tu kwa kuongeza mishahara, japo mishahara ikiongezwa ni vizuri, lakini pia tunaweza kuanzisha *schemes* mbalimbali za kuwapa uhakika wa maisha yao ya baadaye. *Scheme* kama kuziwezesha *SACCOS* zao, au labda kuwajengea nyumba hata zile za *low costing housing* ili mradi mtu akistaafu anajua kwamba, mimi nina nyumba yangu, watoto wangu hawatapata shida kwa hivyo Mwalimu atafanya kazi kwa moyo zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa katika ziara kule Ulanga, tulivyokwenda Ulanga, Rais alizindua *SACCOS* ya Walimu. Hiyo *SACCOS* ni kubwa sana, mimi sijawahi kuona, ni *SACCOS* ya Kiwanda cha Kukoboa na Kusaga mahindi ambayo wanawenza kupeleka hata nchi za nje na vile vile kukoboa mchele. Ni jengo kubwa, mashine kubwa ambazo wamewezeshwa na Serikali milioni 40. Je, *SACCOS* nyingi za Walimu zikiwezesha itakuwaje? Walimu watakuwa na moyo wa kufanya kazi na watafurahia kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, niongelee kidogo kuhusu somo la Kiingereza. Somo la Kiingereza, naomba litiliwe mkazo tangu shule za awali kwa maana, hakika ndio msingi wa elimu yote ya kila mwanafunzi. Usipojua Kiingereza ukienda *Form One* unashindwa kufanya vizuri, si kwamba huna akili, lakini kwa sababu ni lugha nyingine. Kwa hiyo, ni muhimu tuzingatie Kiingereza kuanzia shule za awali, shule za msingi na hata tukienda kwenye sekondari, basi tuzingatie kwa sababu Kiingereza hakikwepeki, hatuwezi kuishi ndani ya chupa ya chai, wote sisi ni lazima tujue ili na sisi tuweze kuchangia, tukienda nchi za nje, tuweze pia kuwa na nafasi nzuri ya kupata kazi za Kimataifa na watoto wetu pia waweze kuingia Chuo Kikuu moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi, ukienda katika Vyuo vingine vya nje, utakuta mtoto wa Kitanzania anarudia mwaka kwa ajili ya kujifunza Kiingereza, jambo ambalo linasikitisha, linapoteza pia pesa za wazazi. Lakini, kama wakijua Kiingereza na tunachosema siyo kile tu cha kuandika, lakini pia *fluency*. Watu waweze kuongea wakaeleweka, siyo mpaka utafsiri kutoka kwenye Kiswahili, baadaye ndiyo uweke kwenye Kiingereza, baadaye ndio useme neno moja moja, inachukua muda. Hiyo itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe ni shuhuda, nilienda kule kwetu, nilikuwa napita nikasikia Mwalimu anasema “*this is a kinife*” anamaanisha *knife*. Nikaingia darasani, nikamsaidia nikamwambia hiki kinatwa *knife* usiseme “*kinife*”. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, au mtoto wa *Form Six*, anakwambia “*my phone is crying*”. *Your phone is not crying, is ringing!* Ni kwa sababu ya vitu vidogo, kwa sababu hatuko *fluent*, tujitahidi, tusione aibu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaosoma Kiingereza tusione wako *anti-Tanzania*, hapana! Kama kweli tunaamua kwamba Kiingereza hapana, sisi tuingie kwenye Kiswahili, basi hata vitabu vyta *Chemistry, Geography, Biology* vyote vibadilike viwe Kiswahili, hapo ndio tutaweza ku-*argue* ukweli *otherwise* jamani, hatuwezi kuwa nusu Kiswahili, nusu Kiingereza, nusu kila kitu, mwisho tunakuja kujuta. Fikiria Wanyarwanda wao ni *Francophone*, lakini wanajifunza Kiingereza kusudi wawe *Anglophone*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu kodi kwa shule za *private*. Shule za *private*, ni shule zinatoa huduma kama shule zingine zozote lakini unatozwa kodi kama vile una Hoteli ya Shelaton kwa sababu eti umeandika *English Medium* au umeandika *International School*, ukiandika *Trust*, basi kodi inafutwa. Jamani mimi naona kwamba shule ni shule maadamu inatoa elimu kwa watoto wetu wa Tanzania. Tuwasaidie watu wanaojitoa ili waweze kufundisha watoto wengi zaidi na Tanzania iweze kuondoa ujinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ule mfumo wa *Form Five na Six*. Mfumo huu ni mzuri, lakini unaacha wengi hawawezi kwenda Chuo Kikuu. Katika nchi jirani, kuna *Bridge Course* au *Pre-University Course*, hiyo inaweza kumsaidia mtoto aliyeshindwa *Form Four* kuingia *Form Five* na ana uwezo, akaingia kwenye kozi ya mwaka mmoja, baadaye na yeye akaingia Chuo Kikuu. Hii pia tungeschukua wengi zaidi katika Vyuo vyetu ili tuweze kuwa na wasomi wengi kwa sababu kukosa tu *Division One* au *Division Two*, basi mtoto anaKata tama, kuliko kurudia mitihani mwaka hadi mwaka, mtoto anarudia mpaka anaKata tamaa, anajiingiza kwenye makundi mabaya. Tuwasaidie watoto wetu ili wengi zaidi waweze kufikia malengo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Walimu wa nje. Walimu wa nje wanasaidia kwa sababu Walimu wa Tanzania hawatoshi. Kwa hiyo, ninaomba tunapopeleka maombi au tunapojaza *form* zao, wapewe *Teaching License* kusudi wasaidie. Hii ni nzuri kwa sababu kuliko wote kunyang’anyana Walimu na kwa kweli Walimu hawatoshi, ni vizuri pia tuongezee na Walimu wengine ambao wana uwezo wa kutusaidia. Kwa mfano, shule ya Chekechea huwezi kusema mpaka Mwalimu awe na Digrii kwa sababu mpaka awe na Digrii, atakuja kufundisha chekechea! Chekechea ni elimu ya kawaida ambayo watu wamesomea, kwa hiyo tuwape *chance* Walimu hawa wa nje na wao waweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nafikiria kwenye mtaala wetu, tuongezee na somo la ujasiriamali. Chimbuko la ajira isiwe tu Serikali. Chimbuko la ajira liwe zaidi sana, kama vile wanavyosema kwenye *private sector*. Sasa *private sector* ni vizuri hata kama mtu ni Daktari, lakini hakupata kazi, basi aweze kujajiri. Hata kama mtu ni Injinia hakupata nafasi ya kuajiriwa, aweze pia kujajiri. Hili somo litawajengea ile roho ya kuthubutu, vile vile litawajengea kujiamini na vile vile watakuwa wakakamavu na wakiwa hivi, hata wakianza biashara zao, wataweza kuendesha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Herbert Kairuki *University*, wana somo hili la ujasiriamali kwa Madaktari, jambo ambalo ni zuri kwa sababu hata kama utakosa kuajiriwa, bado unaweza kuanzisha hospitali yako ukaiendesha vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nikushukuru wewe Mwenyekiti, niwashukuru pia viongozi wangu, Spika wa Bunge, Naibu wake, Wenyeviti wote na Walimu wote maana mimi nilikuwa bado *Form One*, lakini wako watu walionisaidia hapa mpaka na mimi sasa naweza kusimama nikasema vizuri. Namshukuru jirani yangu Mheshimiwa Manyinyi ambaye amekuwa Mwalimu mzuri kwangu. Mungu awabariki. Naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude RwaKatare. Lakini labda niseme shukrani za pekee ni kwa kuwa umeanza kwa kutuombea humu ndani, ni tofauti kabisa na anavyoanza Askofu Mpesya, ye ye huwa anaanza tu bila hata sala yoyote. Kwa hiyo, kwa kweli umetusaidia sana, tunakushukuru sana. Tumshukuru Mheshimiwa Manyinyi kwa kukusaidia hapo, nadhani itabidi tu uende mpaka Jimboni kwake kusudi mpeane miongozo zaidi. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami asubuhi hii niweze kuchangia katika hoja ya Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kutujalia kutuamsha na afya na uzima ili kuweza kuendelea na shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya na katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitambue na kushukuru jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali, mamlaka mbalimbali za elimu pamoja na taasisi nyingine binafsi, kwa kutambua kwamba elimu ni muhimu na ni jambo la msingi sana katika kutuondo katika umaskini na kutuwezesha kujenga uchumi ambapo ndipo tunapolenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kuititia mpango wa MMEM na MMESS, Serikali imeweza kutanua elimu kuanzia ngazi ya awali yaani elimu ya msingi na sekondari kama ambavyo tumeonyeshwa katika taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kuanzia mwaka 2005 hadi 2008. Katika ukurasa wa 22 hadi 23, naomba kidogo ninukuu kuonyesha ongezeko la elimu lenyewe.

Katika elimu ya awali, wanafunzi wameongezeka, mwaka 2005 walikuwa laki sita thelathini na nane elfu, mia tano na tisini na moja hadi kufikia laki nane sabini na tatu elfu, mia tisa na themanini na moja kwa mwezi wa Desemba 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madarasa katika elimu hiyo ya awali, yameongezeka kutoka 21,607 hadi kufikia 28,048 mwaka 2008 wakati elimu ya msingi mwaka 2005 wanafunzi walikuwa milioni saba laki tano na arobaini na moja elfu mia mbili na nane hadi kufikia tumefikia milioni nane laki nne elfu kumi na tisini na nne mwaka 2008. Katika elimu ya sekondari, kuna mchanganuo tu unaonyesha idadi ya shule za Serikali toka mwaka 2005 zilikuwa 1,202 lakini kufikia mwaka 2008 tunazo shule za Sekondari za Serikali 3,114.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ongezeko la *quantity* tumefanya vizuri, tumefanya vizuri kwa sababu tumeweza kuwachukua wanafunzi ambao walikuwa wako nje tayari tumewaleta katika shule *otherwise* wanafunzi hawa na watoto wengi wangekuwa wako nje ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na changamoto nyingi ambazo zimeelezwa, changamoto kubwa tunayoiona kwetu, ni ubora wa elimu yenye. Katika kitabu cha hotuba ya Waziri, nimefurahi sana kuna mchanganuo hapa katika ukurasa wa 158, unaoonyesha asilimia ya watahiniwa waliofaulu mtihani wa Kidato cha Nne katika madaraja ya kwanza hadi daraja la nne na daraja la kwanza hadi la tatu kwa mwaka 2001/2008 huo ni ukurasa 158. Ni jambo la kusikitisha sana kwamba tunajivunia kiwango chetu cha elimu kimepanda lakini kwa kweli ukiangalia kile kiwango chenyewe unawenza kusema hakikupanda sana badala yake kwa mwaka 2007 na 2008 unakuta kwamba kina shuka. Hasa ukiangalia hasa wale waliopata daraja la kwanza hadi daraja la tatu, ni wachache mno, asilimia inaonekana pale, lakini wengi ni waliofaulu katika daraja la nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo utaona kwamba mwaka 2007, waliopata daraja la kwanza mpaka la nne ni 85.9% lakini uki-*compare* la kwanza mpaka la tatu ambao hawa ndio tutasema wame-*pass* kwa sababu hata mwanafunzi mwenyewe zinapotoka *results* ukimuuliza vipi ume-*pass* akiwa amepata daraja la nne anakwambia sijafanikiwa kwa maana kwamba hawezi kuendelea na elimu yake ya juu, Kidato cha Tano na cha Sita, sisi tunawa-*consider* hao kama bado hawajafanya vizuri. Kwa hiyo, ni changamoto ambayo Wizara inayo kuona kwamba viwango hivi vyta ubora wa elimu vipande sasa kutoka daraja la kwanza hadi la tatu na kuondosha kutoka daraja la kwanza na la nne bila hivyo tutajidanganya oh, tunafanya vizuri kumbe kwa kweli hatujafanya kama ambavyo tunatakiwa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyeki, katika miaka hiyo miwili, ukiangalia watahiniwa wote ambao walifanya mitihani katika Kidato cha Nne, theluthi mbili chini ya tatu ya watahiniwa hao wote walipata *division four* na *zero* yaani wamefeli kabisa. Kwa kweli, hiyo si hali nzuri na inapaswa tutafakari badala ya kujipa moyo tu kwamba tunafanya vizuri kwa sababu daraja zuri ambalo linamwezesha mwanafunzi kuendelea ni la

kwanza, la pili yaani kwa vyuo vingine na sehemu zingine anayokwenda hata la tatu kama hana *combination* nzuri, inakuwa ni tabu kwa mwanafunzi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya yanatokana na sababu nyingi ambazo zinasababisha matokeo haya ya sekondari yasiwe mazuri. Kwanza, maandalizi kutoka shule ya msingi siyo mazuri sana kutokana na shule zenyewe zilivyo, zinakosa vifaa, lakini kubwa zaidi unapofika sekondari sasa na hata huko msingi tatizo la ukosefu wa Walimu ni kubwa mno. Tumesikia hapa juhudzi za Serikali lakini kwa kweli bado inatakiwa tukimbiye sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Walimu ni kubwa kiasi ambacho siku nyingine unasiakia vitu ambavyo kwenye akili yako ukivisikia huwezi kuamini kwamba shule nzima ina Walimu wawili. Hayo yapo na tumeyasikia na hali bado siyo nzuri. Tatizo lililotokea ni kwamba ongezeko lile la shule na wanafunzi ambalo tumelipata kutokana na *programme* ya MMEM na MMES, halikuenda sambamba na ongezeko la Walimu yaani *Training* ya Walimu imekuwa *slow*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameelezea jitihada za Serikali katika kuongeza Walimu kwamba sasa hawa watakaokwenda Chuo Kikuu kusoma, watakaosomea Ualimu na Sayansi watapata mkopo wa 100%, ni nzuri na ametuelekeza kuwa tutafika pahala lakini napenda tu nim-*caution* kwamba bado tuna Walimu wa Daraja la Cheti na Stashahada hawa wamewafikiriaje? Hawa pia wanatakiwa wasome lakini bado wanatakiwa walipe karo na michango mbalimbali katika vyuo hivi nya elimu. Mimi nashauri Serikali ifikirie sana kuondosha ada hii kwa wanafunzi wa Ualimu ili wanafunzi wengi wavutike kwenda kujunga na Ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa RwaKatare alipomaliza, amesema kwamba kwa sasa kazi ya Ualimu haiwavutii wengi kinyume na ambavyo sisi wengi tulivutika na kazi ya Ualimu wakati ulikuwa na hadhi ya kweli kweli. Mwalimu alikuwa anathaminiwa lakini kwa sasa unamsikia mwanafunzi analenga kwenda kwenye Uhasibu na mambo mengine lakini hataki Ualimu. Kwa hiyo ni vizuri kwanza tukaona kwamba ada hizi zinapunguzwa sana na hatimaye kuziondosha kabisa ili wanafunzi wengi waweze kujiunga na vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna shule ambazo zilikuwa zinafundisha Walimu, Vyuo nya Ualimu lakini vilikuja mara moja tu vikaondoshwa kama vile Ndwiwa ambacho iko Mtewa na Urambo Tabora. Basi ni vizuri Serikali ikafikiria kuvirudisha tena vyuo hivi ili kuweza kuandaa Walimu zaidi na zaidi ili kukabiliana na upungufu huu mkubwa ambao unatusababishia kuwa na matokeo ambayo si mazuri kwa wanafunzi wetu na kurejesha nyuma jitihada zetu za kupata rasilimali watu walio bora ambao watatusaidia katika kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninapenda kugusia katika hili ambalo linahusiana moja kwa moja na kushuka kwa kiwango cha elimu, ni lile la Idara ya Ukaguzi wa Shule. Shughuli ya ukaguzi katika elimu, ni ya muhimu sana lakini kwa

kweli ninavyoionna, kadri bajeti zinavyokuja, ni kwamba Idara hii ya Ukaguzi wa Shule haipewi umuhimu, bado bajeti yake ni ndogo sana, haitoshi hata kwa yale mahitaji ya kazi zake za kila siku. Hali hii inasababisha Walimu wakae muda mrefu bila ya kukaguliwa na hiyo pia inasababisha viwango vyetu vya elimu viweze kushuka. Ni bora kuweza kufikiria sasa kwamba wale Wakaguzi Wakuu wa Shule amba wako katika ngazi ya Wilaya, wawezeshwe kukagua shule za msingi na sekondari badala ya kutegemea Ukaguzi wa Kanda tu kukagua shule za msingi na sekondari, hii itatusaidia lakini vilevile hawa wakaguzi nao walipwe yale madai yao ili kuwapa motisha kuweza kufanya le kazi yao vizuri ili wasivunjike moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa haraka ambalo ninapenda kugusia, ni elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu. Nilifurahi leo tulikuwa na wanafunzi hapa amba wana mahitaji maalumu na Mheshimiwa Naibu Spika alituelezea jinsi gani ambavyo wamepigana kuwapatia sekondari *school*. Kwa kweli Wizara bado inatakiwa ivute soksi zake juu ili kuona kwamba Serikali nayo inabeba jukumu hili ambapo kwa sasa inaonekana bado tunategemea zaidi taasisi hasa Mashirika ya Dini katika kuwapa watoto wetu hawa amba kwa bahati mbaya hawako sawa na wenzao kielimu, lakini zaidi pia ni wale Walimu amba wanafundisha wanafunzi hawa. Walimu wanaofundisha watoto wenye mahitaji maalumu, wenyewe wanakuwa wameandaliwa kwa hiyo wanakuwa wana elimu ya ziada ya zaidi ya Ualimu katika kuweza kuwashughulikia wanafunzi wale na kuweza kufanya kazi zao. Lakini wanavunjwa moyo, hawapewi posho kwa ajili ya kazi ya ziada ambayo wanafanya. Tunashauri Walimu hawa wapewe posho ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Walimu hawa wengine wanazimika asubuhi kuwaafuata watoto nyumbani kwao na kuwarejesha baada ya saa za kazi kwa jinsi watoto wenyewe walivyo na baadhi ya wazee kuKataa jukumu la kuwapeleka shule na kuwarudisha. Kwa hiyo, ili kuwapa moyo na kuwathamini Walimu hawa, ni vizuri sana Wizara ikashughulikia kuona kwamba wanapewa posho ya ziada kwa sababu kazi wanayofanya ni ngumu na inahitaji kuthaminiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo kama sikulisema sitakuwa nimewatendea haki Walimu, tutakumbuka kwamba mwaka huu wa 2008, kulikuwa na tafrani kubwa ambayo ilikuwa inaongozwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa upande mmoja na upande wa pili ikiwa Serikali. Walikuwa na madai na tumeyasikia sana humu ndani ya Bunge, mimi nafurahi kuambiwa kuwa sasa tayari fedha hizo zimepatikana na ziko kwenye bajeti hii. Ushauri ni kwamba tusizidi kuwabeza hawa Walimu wenye madai yao, kama kweli fedha hizi zipo basi bajeti hii ikipitishwa tu, fedha hizi zilipwe mara moja na kwa sababu tumeambiwa uhakiki nao umekamilika, tafrani zile zinapotokea na msuguano kati ya Walimu na Serikali inaaathiri jamii kwa ujumla ambapo watoto wetu wanaathirika ndani ya shule, Walimu wanapoteza hamu ya kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri sana Serikali, ikaliangalia mara mbili na tatu suala hili, kama kweli fedha hizi zimetengwa, wale wote wanaohusika, fedha za waliopandishwa mishahara amba hawakulipwa, tofauti zao walipwe, waliokuwa na

malimbikizo ya likizo hawakulipwa, waliokwenda matibabu na mambo kama hayo, kazi yoyote inahitaji motisha bila motisha mfanyakazi yoyote hufa moyo wa kufanya kazi yake kwa bidii na kwa kweli Walimu lazima tuwashukuru sana kwa sababu wanafanya kazi ya kusomesha pamoja na kuwalea watoto wetu. Kwa hiyo, ni lazima tuwathamini, tuwaone kwamba katika jitihada zetu nzima za kupigana na umaskini, wao ni namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru, ahsante sana. (*Makofî*)

MWENYEKTI: Nakushukuru Sana Mheshimiwa Fatma kwa mchango wako na hasa kwa kuzingatia hoja nzito ya wale mavu, ni hoja ya msingi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilisema nitamwita Mheshimiwa Abdul Marombwa, nafikiri yeeye atakuwa msemaji wetu wa mwisho asubuhi hii mpaka tutakapofuatalia Mwongozo wa Naibu Spika kuhusu suala zima la uchangiaji wa hoja yetu.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri na Manaibu Mawaziri wote, kwa kazi kubwa sana wanayoifanya katika Wizara hii kubwa na hata kutupatia ufanisi mkubwa katika Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu katika maeneo mbalimbali wanayoshughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hao tu, niwashukuru sana Walimu wote wa nchi yetu, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya usiku na mchana, kazi ambayo imesababisha Walimu hawa kutuletea ufanisi mkubwa wa ufundishaji katika shule za msingi, sekondari hata na Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nawapongeza sana Walimu? Nawapongeza Walimu kwa sababu inafikia muda hata wakati ule wa likizo zao, Walimu hawa wanabakia shuleni wanaendelea kufundisha madarasa ya nne na saba bila kuchoka, wanawafundisha vijana wa *Form Two* hata na vijana wa *Form Four* wanafanya wakati wa likizo na Serikali haiwalipi hata senti tano, ni kujitolea kwao na uchungu wao wa elimu, ndio kunawafanya wafanye kazi hiyo. Kwa hiyo, ni lazima niwapongeze sana Walimu kwa kuwa wanafanya kazi kubwa ya kuendeleza elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa kwa Serikali kuthamini mchango mkubwa ambao Walimu wanautoa. Malalamiko yao yote yaweze kulipwa kwa wakati. Tusiwatumie Walimu hawa kama punda, tuwatumie Walimu vizuri, malalamiko yao yaweze kushuhulikiwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linguine, nimshukuru sana Mama Salma Kikwete pamoja na Mama Shein, kwa kazi kubwa ya kuchangia elimu katika Wilaya ya Rufiji. Mimi ni mwenyeji wa Wilaya ya Rufiji, michango yao ambayo wameitoa kule kwetu, ni mikubwa sana. Nina ombi moja tu hasa kwa Mama Kikwete, kwa shule yake ya

Sekondari ya Nyamisati chini ya WAMA, kwa kuwa Wilaya yetu ya Rufiji ina matatizo makubwa sana ya elimu, wengi hawakusoma, basi tunaomba angalau 30% ya wanafunzi watakaoingia pale kila mwaka watoke katika Wilaya ya Rufiji ili tuweze kuinua elimu Wilaya ya Rufiji, hilo ni ombi maalumu tunalipeleka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa matokeo ya mitihani mbalimbali ambayo inafanywa hapa nchini, nianzie mitihani ya elimu ya msingi. Kama nilivyosema, Walimu wetu wanafanya kazi kubwa sana ya kufundisha, lakini pamoja na kufanya kazi hiyo kubwa ya kufundisha, kuna matatizo mengi ambayo yanajitokeza. Kwa mfano, katika mitihani ya mwaka 2007 na ile ya mwaka 2008, kutokana na kitabu cha hotuba ambacho tulipewa na Mheshimiwa Waziri, mwaka 2007, jumla ya wanafunzi 354,417 walifeli mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na mwaka 2008 jumla ya wanafunzi 480,902 walifeli mitihani ya kumaliza elimu ya msingi. Ukiangalia ule mwaka 2007, ni sawa na 46% na mwaka 2008 ni sawa na 47%. Hiki ni kiwango kikubwa sana, kwa miaka miwili tu wanafunzi ambao wamefeli elimu ya msingi ni 835,319, idadi hii ni kubwa sana. Wanafunzi hawa wamebakia vijijini, wanafunzi hawa hawana kazi yoyote, wanafunzi hawa wako kwenye umri wa miaka kati ya 12 na 13 hata ukiwaambia waende kulima hawana uwezo, hivi Wizara ina mpango gani? Wanafunzi zaidi 800,000 kwa miaka miwili ni Wanafunzi wengi mno, hawa watatupa shida sana hapo baadaye kwa sababu hawajapata elimu ya kutosha na hivyo kuona Taifa lao limewatelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kama kuna uwezekano, ni lazima tuanze mpango wa kuwasaidia wanafunzi hawa kwa sababu umri wao ni mdogo. Ukiwapeleka kulima, kama nilivyosema hawawezi, ukiwapeleka kufanya kazi yoyote, hawawezi, wengi wao wanakuwa ni wauzaji maandazi mitaani, kutokana na shughuli ambazo wanazifanya mama zao. Sasa ni vizuri kungekuwa na *Post Primary Education* kwa watoto wetu, elimu ambayo itawasaidia hawa watoto waweze kujitegemea. Tuelewe wazi katika mitaala yetu ya shule ya msingi hakuna elimu ya kujitemea. Sasa mtoto wa miaka 13 unamtelekeza mitaani, atafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, naiomba tena Serikali iangalie, tuna malengo ambayo tumejiwekea, tulisema kuwa ifikapo mwaka 2010, watoto wetu wanaomaliza shule ya msingi angalau 80% waende sekondari. Ilikuwa ni kama *transition period*. Tunachokihitaji sasa, tutoke kwenye 80% twende kwenye 100% kwamba elimu ya msingi ianzie darasa la kwanza mpaka darasa la 12. Mchakato huu uweze kufanyika kwa sababu ya umri wa watoto wetu, watoto wetu wengi wanamaliza darasa la saba wakiwa wadogo mno wengine wana miaka 12, wanafeli, ni vizuri tuwapeleke mpaka wamalizie darasa la kumi na mbili, ndio iwe elimu ya msingi kwa sababu tumetoka kwenye 80% kwenda kwenye 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nitalizungumzia, ni kuhusiana na elimu ya sekondari. Mheshimiwa Fatma, amezungumzia vya kutosha katika ukurasa ule 158 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini pamoja na maelezo yale yote, shule zetu za Jumuiya, daima maendeleo yake ni duni sana hata *statistics* zenu za Wizara zinaonyesha hivyo. Kwa mfano, katika kitabu cha *BEST (Basic Education Statistics in Tanzania)* cha

mwaka jana, ukurasa wa 65, kulikuwa na matokeo ya mitihani wa Kidato cha Nne, naomba kunukuu maelezo ambayo Wizara imetoa kutuarifu Watanzania wanasema:-

“Regarding to the performance of division one to three, candidates from Seminary Schools performed better followed by Goverment and Non-Goverment Schools while, Community Schools experienced the worst performance over the period under SEDEP 2004 up to 2009”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, shule zetu za Jumuiya *performance* yake ni mbovu sana “*the worst performance*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani Waziri atakuja na mikakati mingine ya kuboresha elimu yetu hasa kwa shule hizi za jumuiya. Katika shule za jumuiya, kuna matatizo mengi, matatizo makubwa ni upungufu wa Walimu. Tunashukuru Serikali kwa mkakati waliouweka lakini tatizo kubwa ambalo linatukabili, ni mazingira magumu kwa shule zetu za kwenye Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata nyingi ziko vijiji na ziko katika mazingira magumu sana. Ukiwahi kuambiwa kwenye Kata tu, basi hizo Kata ziko vijiji na Walimu wengi hawapendi kwenda kufundisha kwenye Kata zile. Kwa mfano, mwaka jana tuliletewa Walimu wengi Wilaya ya Rufiji, matokeo yake, wale Walimu wote waliondoka na mpaka kufika mwezi wa kumi mwaka jana, shule zetu nyingi za Sekondari zilikuwa na Walimu wawili au watatu, wengi wameondoka kutokana na mazingira ya vijiji kuwa ni magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali ikaangalia upya suala hili. Mwaka huu, Serikali imeingiza kwenye mpango wake, kusaidia watumishi wanaoishi katika mazingira magumu kuweza kuwapatia *Hardship Allowance*, naomba Wizara ya Elimu ianze kwa kutoa *Hardship Allowance* kwa Wilaya zilizokuwa *identified*, zimetangulia Wilaya zote ili ziweze kusaidia watumishi hawa kuweza kuishi katika mazingira mazuri kinyume cha hivyo, hata kama tutapeleka maabara katika shule zetu zote vijiji wakuzitumia maabara hizo hakuna!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wengi wa Sekondari, ni Walimu wa *Arts*, hakuna Walimu wa *science*, peleka maabara kila shule, nani atakayeziongoza hizo maabara zenyewe? Kwa hiyo, ni vizuri kwa Serikali kuangalia *Hardship Allowance* kwa Walimu ambao wanafundisha maeneo hasa ya vijiji na hasa Walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mishahara kwa Walimu. Bado mishahara yao ni midogo na mishahara hii inaleta matatizo mengi lakini hata viwango vingine vya mshahara havijawekwa sawa. Kwa mfano, Maafisa Elimu, wanakazi nyingi sana ambazo wanazifanya katika nchi hii. Wao ndio waratibu wa elimu wa Mkoa lakini mshahara huu wa Afisa Slimu wa Mkoa haujulikani kama ni wa Mkuu wa Idara wa sehemu hiyo. Kwenye Wilaya, mishahara ya Maafisa Elimu wa Wilaya pamoja na Maafisa Elimu wanaoratibu elimu ya sekondari, wanaanza mshahara wa shilingi milioni moja na kama laki mbili hivi lakini mshahara wa Afisa Elimu wa Mkoa ambaye ana *Masters*, anapewa kulingana na daraja lake wakati ye ye anaratibu elimu ya Mkoa mzima

elimu ya msingi, elimu ya sekondari, elimu ya vyuo na elimu ya awali. Naiomba Wizara, iwatambue hawa kwa kuwapatia mishahara kama vile Wakuu wa Idara kwenye sekretarieti ile ya Mkoa badala ya kuwaacha holela tu kwa kuwapatia mishahara yao kulingana na madaraja waliyosomea.

Mhweshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tena suala la vitabu vya ziada na kiada. Niishukuru sana Serikali kwa maamuzi yake ya kuamua kuwa na mlango mmoja tu wa kutoa vitabu vya kiada. Tuelewe wazi kwamba kitabu cha kiada kinaandaliwa na taasisi ya ukuzaji wa mitaala ambayo, ndiyo inayoandaa muhtasari hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miaka ya nyuma kulikuwa na mchanganyiko mkubwa mashulen. Mimi nilikuwa huko, unakwenda kwenye shule moja kitabu cha hesabu Darasa la Tano, ni cha *MC Millan*, shule ya pili, kitabu cha Darasa la Tano, ni cha Mtire, unakwenda shule nyingine kitabu kingine ni cha mtu mwengine, tutakuwa na vitabu vingapi? Ni vizuri vitabu hivi vya kiada vitungwe na taasisi moja ya ukuzaji wa mitaala lakini hawa *publishers* wengine waruhusiwe kutoa vitabu vijulikane kama ni vitabu vya ziada, wavitungwe hivyo ili kuongeza *material* lakini kitabu cha kiada kiwe kimoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Abdul Marombwa, lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na hasa kwa kuwasemea sana Walimu. Lakini niseme tu kwamba asubuhi Mheshimiwa Diana Chilolo aliomba Muongozo wa Kiti, nina uhakika, majibu ya hoja ya mwongozo wa Kiti, yatatolewa ufanuzi tutakaporudi hapa saa kumi na moja jioni kwa sababu sijapata lolote kutoka kwenye ofisi ya Naibu Spika. Ninaamini kwamba kikao alichokiitisha cha Kamati ya Uongozi, huenda pia ajenda mojawapo ni kujadili mwongozo huo. Kwa hiyo, sina neno la kusema mpaka sasa mpaka hapo nitakopopata maelezo kutoka kwenye ofisi ya Mheshimiwa Naibu Spika.

Waheshimiwa Wabunge, tutakaporudi mchana, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Rosemary Kirigini, atafuatiwa na Mheshimiwa Thomas Mwag'onda na Mheshimiwa Margreth Mkanga naye nitaomba ajiandae na tutaendelea na orodha hii kwa wachangiaji ambao hawakuchangia hata mara moja na tutaingia katika orodha ile nyingine inayofuata. Lakini bado tutaendelea kuzingatia Kambi ya Upinzani, tutaendelea kuzingatia jinsia, tutaendelea pia kuzingatia mambo mengine yatakayojionyesha.

Waheshimiwa Wabunge, ninafikiri sasa muda wetu wa kusitisha shughuli hizi umefika na nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, baada ya mapumziko ya mchana tunaendelea na kikao chetu tena jioni hii ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na kama nilivyosema wakati tunasitisha shughuli zetu mchana, tutakaporudi ndani msemaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mara na ninamwona yupo hapa ndani kwa hiyo nitampa nafasi na Mheshimiwa Thomas Mwang'onda ajiandaye.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu sana iliyopo mbele yetu leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwashukuru wapiga kura wangu, wanawake wa Mkoa wa Mara na wananchi wa Mkoa wa Mara kwa ujumla, kwa namna ambavyo wanani pa ushirikiano katika kuhakikisha natekeleza majukumu yangu ya Ubunge vizuri sana na mimi naahidi nitaendelea kuwa mwakilishi mzuri kwao, wao wanachotakiwa kufanya ni kunipa tu ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa hii, kumpongeza Waziri na Manaibu Mawaziri wote, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Elimu, kwa hotuba hii nzuri sana ambayo imeeleza mikakati mizuri sana katika kuhakikisha inaongeza ubora wa kiwango cha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, naomba nitumie fursa hii, kwa niaba ya Walimu wa shule ya msingi Mwisenge, niipongeze Wizara na hasa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, kwa namna alivyonisaidia na kuweza kupata ile ahadi iliyokuwa imetolewa miaka mitatu nyuma ya shilingi milioni tatu kwenda kwenye shule hii ya watoto walemovu wa kuona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua kwamba Wizara hii ni muhimu sana na hata jana tulipokuwa tunajadili Wizara ya Kilimo na hatimaye kuelekea kwenye ile kauli mbiu ya kilimo inayosema Kilimo Kwanza, mimi nilikuwa najiuliza kwamba kilimo kinawezaje kikawa kwanza na elimu isiwe kwanza? Kwa sababu ninaamini hata wale watalaaam wanaoweza kukiwezesha kile kilimo kikawa Kilimo Kwanza, ni lazima wapitie kwenye elimu! Kwa hiyo, kwangu mimi nasema Wizara hii, ni muhimu sana na hatunabudi sote kwa pamoja kwa kushirikiana na watalaaamu wa Wizara kuweza kuisaidia Wizara hii na kuhakikisha inatekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia, kuipongeza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kwa zoezi zima walilolifanya mwaka 2007/2008 la kuhakiki watumishi. Katika zoezi lile, ofisi hii ya Rais ilitumia kiasi cha shilingi milioni mia mbili na nane tu, lakini kilichopatikana kwenye zoezi lile zima, ni mambo ambayo yamekuwa dira kubwa na hasa katika Wizara hii ambayo tunaizungumzia leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili lilifanyika katika Wizara tatu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara hii ya Elimu na

Mafunzo ya Ufundu. Nitoe tu masikitiko yangu kwamba, wakati Waziri alipokuwa akitoa hotuba humu ndani, nilitegemea angetueleza yale yote yaliyobainishwa kwenye zoezi hili la uhakiki kwa sababu kutoka kwenye zoezi hili pamoja na kwamba Serikali imepata hasara ya shilingi bilioni tatu, lakini kiasi cha shilingi bilioni moja milioni mia nne zimetokana na Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, kwa kulipa watumishi hewa. Kwa hesabu zangu za haraka haraka, nikichukulia wastani wa kila mtumishi kwa maana ya kwamba kila Mwalimu labda anapata shilingi laki mbili na nusu, ninaona watumishi hao hewa ni Walimu wapatao 4,500 idadi hii ni kubwa sana na nilitegemea Waziri wakati anatoa hotuba yake hapa ndani angetueleza ana mikakati gani ambayo anategemea kuifanya ili kuondokana na tatizo hili la kulipa watumishi hewa na kuipa Serikali yetu hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nkinukuu kitabu cha ukaguzi wa fedha kilichotolewa na CAG cha tarehe 26 Machi, 2009, tunaona pia CAG ameelekeza upungufu kwenye Wizara hii kwamba kulikuwa na ulipaji wa Walimu 100 kwa shilingi milioni mia moja na tano laki tano sabini na tisa. Walimu hawa wapo lakini hawajulikani vituo vyao viko wapi, lakini malipo yao yamekuwa yakiendelea kuelekezwa benki zao lakini cha kusikitisha mpaka leo hii hawajulikani vituo vyao vya kazi ni vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi hili zima, mambo ambayo yamebainishwa ni mawili. Kuna matatizo kwenye Wizara kama Wizara, kwamba hawaweki rekodi zao vizuri kiasi kwamba hawajui wana watumishi wangapi na hawajui ni watumishi wangapi wanalipwa na Serikali na hivyo Serikali inaendelea kupata hasara kwa kulipa watumishi ambao hawapo au wamekufa ama wamehama katika Wizara hii wameingia kwenye *private sectors* lakini bado Serikali inaendelea kuwalipa Watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo nimeligundua ni tatizo la udanganyifu wa watumishi. Humu ndani tunasema kwamba Walimu wana matatizo mengi sana lakini pia Walimu hawa hawa wamekuwa ni wadanganyifu wakubwa sana. Zoezi hili zima limebainisha ni kwa jinsi gani Walimu walivyofanya walivyoidanganya Serikali yao wenye na nchi yao wenye na wamesomesha na Serikali lakini hawakwenda kufanya kazi kwenye shule za Serikali badala yake wengi wamefanya kazi kwenye shule za watu binafsi. Sawa tunaelewa mishahara ni midogo lakini naiomba Wizara na Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, atuambie ni hatua gani amechukua dhidi ya hao Walimu ambao wameonekana ni wadanganyifu dhidi ya Serikali yao, dhidi ya nchi yao na kuipatia hasara nchi yetu ya Tanzania kiasi cha shilingi bilioni moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri, ametuambia kwamba ifikapo mwaka 2012 atakuwa ameongeza kiasi cha Walimu wapatao 15,000. Mimi nampongeza sana kwa mikakati hii lakini kama nilivyosema hapo awali, mikakati hii itakuwa ni sifuri kama tutakuwa tunasomesha Walimu halafu wanatoroka kwenye shule zetu wanaenda kufanya kazi kwenye shule za *private* au wanabadilisha kabisa mfumo, wanaenda kufanya kazi ambazo hawajazisomea na hawaajaagizwa kuzifanya. Kwa hiyo, kiwango hiki cha Walimu elfu kumi na tano, tungependa tu Waziri atuambie ana mikakati gani ya

kuhakikisha Walimu hawa ifikapo mwaka 2012 kweli wote wataingia kwenye sekta hii ya elimu na kutupa ongezeko hili la Walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia malimbikizo ya madeni ya Walimu, naweza kusema hii pia inaweza kuwa ni sababu mojawapo inayowafanya Walimu watoroke kwenye hizi shule. Kumekuwepo na malimbikizo makubwa sana yanayotokana na mishahara, kupanda kwa madaraja, kupandishwa vyeo, malimbikizo ya likizo, malimbikizo ya matibabu, yote haya hayajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti mimi najiuliza ni sababu zipi zinafanya Serikali yetu na hasa Wizara hii ishindwe kulipa mishahara ya Walimu, wapo walimu ambao walajiriwa mwaka 2008 lakini wamekaa mwaka mzima hawajalipwa mshahara. Hebu fikiri mwaka mzima unafanya kazi, hujalipwa mshahara, unakula nini? Walimu hawa wana hali ngumu sana na hata walipolipwa mshahara, walilipwa mshahara wao wa kwanza tu hawajalipwa malimbikizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuamua kulipa katika mwaka huu wa fedha. Mwaka jana wa fedha walilipa shilingi bilioni 7.6 na wafanyakazi wengine wa Wizara hii walilipwa kiasi cha shilingi bilioni moja na milioni mia mbili sitini, lakini bado madai ya Walimu ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ametuambia kwamba madeni yaliyohakikiwa tu ni shilingi bilioni 22 lakini hayo ni madeni ya zamani, ukichanganya madeni ya mwaka jana, miaka miwili iliyopita, madeni haya tayari yameshafikia shilingi bilioni 53 na nimefanya uchunguzi na ninazo taarifa kabisa, siongei tu kutoka kwenye kichwa changu, Walimu hawa wanadai shilingi bilioni 53 ambapo kwa shule za msingi pekee yake, Walimu wanadai shilingi bilioni 35, Waziri hapa anatuambia ni shilingi bilioni 22. Ninamwomba ajaribu kukaa na wataalamu wake ajaribu kuangalia, Walimu wa shule za msingi wanadai shilingi bilioni 35 na wale wafanyakazi wengine wanaohudumiwa na Wizara hii wanadai shilingi bilioni 18. Kwa hiyo, tunaona kwamba bado madai kwenye Wizara hii ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kinachonisikitisha zaidi ni kwamba yamekuwa yakifanyika majadiliano mengi tu, Waziri amefanya majadiliano na Walimu, Waziri Mkuu kama yupo, ananisikia naye amefanya majadiliano na Walimu na yeze alitoa tamko kabisa kwamba ifikapo tarehe 30 mwezi wa tano mwaka huu, madai yote ya Walimu yatakuwa yamelipwa. Waziri akafuatia nyuma naye akasema kwamba ifikapo tarehe 15 Juni, Walimu hao watakuwa wamelipwa bila kujali Waziri Mkuu amesema nini mpaka leo hii tunavyoongea hapa ndani, Walimu hawa hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachojuiliza, tunapokuwa tunafanya mazungumzo haya kama viongozi, ni vizuri kabisa tukawa tunatoa kauli ambazo ni za uhakika kuliko kutoa kauli ambazo zinakuwa ni za kuwakatisha tamaa Walimu. Kauli kwamba tarehe 30 mwezi wa tano, kauli hiyo inakuwa hewa, anakuja Waziri tena tarehe 15 Juni, sasa hao Walimu wamekuwa ni watu wa kupigwa danadana tu? Leo Waziri tena ametuambia kwamba katika mwaka huu wa fedha, zimeshatengwa kabisa pesa na Walimu watalipwa

lakini nina uhakika hizi ni kauli tu. Nimwombe tu Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, atueleze humu ndani kwa uwazi kabisa bila kuficha hata kama kuna kuchelewa basi Waziri aweze kutuambia kwa ukweli kabisa ili yale matumaini ya Walimu waweze nao kujiwekea malengo, kwa sababu unapomwambia utalipa mwezi wa nane hulipi, ni bora ukasema utalipa mwaka 2010 ili Mwalimu akae asubiri malipo yake mwaka 2010. Waziri atuambie ni lini Walimu hao watalipwa mafao yao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kidogo kuhusiana na suala zima ya Idara ya Ukaguzi. Mimi nilipokuwa nikifuatilia sana suala la elimu, niliona kwamba Idara ya Ukaguzi, ni idara muhimu sana.

MWENYEKITU: Mheshimiwa una dakika mbili za ziada, kwa bahati mbaya saa ilidondoka kwa hiyo, malizia.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Idara hii iangaliwe kwa umakini mkubwa. Idara hii haina magari, sisi Waheshimiwa Wabunge tunatembea sana vijijini, kuna matatizo mengi sana kule vijijini, kuna mdondoko mkubwa wa watoto wa kike kule vijijini, kwa mfano katika Wilaya zangu, nimesema mara nyingi hapa Bungeni, katika Wilaya ya Serengeti na Wilaya ya Tarime, kuna mdondoko mkubwa sana wa watoto wa kike unaotokana na masuala mazima ya mila na desturi, vile vile suala la uolewaji wa watoto wadogo na mimba za utotonii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni kubwa sana na Idara pekee ambayo inaweza kutuletea mchanganuo mzima, ni Idara hii ya Ukaguzi. Sasa kama Idara hii haijangaliwa kwa umakini, tutajuaje taarifa hizi za mdondoko? Tutakaa hapa tunajidanganya kwamba hali ya elimu ni nzuri lakini kwa kweli hali ya elimu kwa watoto wa kike bado si nzuri katika nchi yetu na ninapenda Idara hii ya Ukaguzi iweze kufanya ukaguzi na kubaini ni mdondoko kwa kiasi gani umetokea na ni hatua gani ambayo Wizara inatakiwa ichukue ili kupunguza mdondoko huu wa watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ni-declare interest*, mimi ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huria, nitumie fursa hii kumwuuliza Waziri wa Elimu, kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukifuatilia kupata *guarantee* ya Serikali kuhusiana na suala zima la mikopo kwenye mifuko ili chuo hiki kiweze kujenga Makao Makuu, pale kilipo eneo limeshakuwa dogo lakini *guarantee* hii imekuwa ni ngumu sana kupatikana. Namwomba Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho atueleze, je, ni ugumu gani unapelekeea Chuo hiki Kikuu Huria kishindwe kupata *guarantee* hii ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniongezea hizo dakika mbili na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITU: Nakushukuru sana Mheshimiwa Rosemary Kirigini, kwa mchango wako mzuri kabisa. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Thomas Mwang'onda atafuatiwa na Mheshimiwa Margreth Mkanga.

MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe, kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangaji wa pili jioni hii, katika hotuba ambayo ni muhimu sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa, kwanza kwa kushukuru kutokana na imani kubwa niliyonayo ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu katika suala zima la usimamizi wa Ilani nzima ya uchaguzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkubwa siku zote ni jalala, yatasemwa lakini kwa kweli viongozi wetu hawa wanafanya kila wanaloweza kuhakikisha kwamba ile Ilani yetu ya Uchaguzi inakwenda vizuri na hasa katika hii sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nisiwe mwizi wa fadhila, Mheshimiwa Waziri Maghembe nimeisikiliza sana hotuba yake na kwa kweli sina namna yoyote ya kusita kumpongeza. Nimeridhika sana na kusuuzika na roho yangu kutokana na kazi kubwa uliyofanya, tukizingatia hivi sasa dunia ipo katika mtikisiko wa uchumi. Mimi niliposikia kwamba umeweza kukusanya fedha zisizopungua shilingi bilioni 500/- na ndizo unazoomba kama sehemu ya bajeti hii, nilipata mshangao mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi mbalimbali za kimataifa zimeonekana kushawishika. Naamini katika uwezo wa Serikali yetu ya CCM itahakikisha kwamba zinatupatia fedha za kuendeleza sekta yetu hii ya elimu. Si kazi ndogo ndugu zangu katika muda huu amba tuko nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani siku zote huwa tunapongeza viongozi. Mimi hii sekta ya elimu, nadhani bila kusomeshwa na nyie wenzangu wote mliokuwa humu, nadhani tusingekuwa humu ndani na nadhani sikosei katika hilo. Kwa hivyo leo kwa nafasi ya pekee kabisa, naomba nichukue nafasi hii kupongeza Walimu wote walionifundisha mimi na nyie wazee wengine na vijana humu ndani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nipeleke shukrani za pekee kabisa kwa Mwalimu mmoja ambaye amenisaidia, sasa nikikutana na Wazungu angalau Kiingereza cha kuombea maji naweza kuongea. Mwalimu huyu si mwingine, ni Georgia Dianna Cornel Apson. Nakushukuru sana Mwalimu wangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niache hizi blaa blaa. Mchango wangu naomba nianzie kutoka juu kwenda chini. Maana yangu ni kwamba Wizara hii inahusisha vyuo vikuu, vyuo vya ufundi, shule ya sekondari, shule za msingi na vilevile chekechea.

Lakini kwanza nimpongeze tena Rais wetu kwa kuhakikisha tunajengewa Chuo kizuri na cha kisasa hapa Dodoma *UDOM*. Hili jambo, nakumbuka mwaka 2005 tukizunguka na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kuhakikisha anashinda na kuwa Rais wetu na ikawa hivyo, aliwahi kulisemea kule Mbeya na mimi nakiri leo humu ndani niliona ni la ndoto tu lakini ndoto ile naona kila siku inazidi kukamilika mpaka sasa hivi

tunao wanafunzi na Mkoa huu wa Dodoma unazidi kuneemeka kiuchumi kwa uwepo wa hawa wanafunzi. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nadhani tutakubaliana, hasa kwa wenzangu mimi ambao wana asili kidogo ya Mikoa ya Pwani kwa sababu tupo karibu hapa; kwamba siku zote usiache mbachao kwa msala upitao. *University of Dodoma* tutaijenga vizuri na kisasa lakini tunavyo vyuo vikuu vingine ambavyo leo nimemsifu Waziri maana nimesikia kwa Afrika Mashariki *University of Dar es Salaam* ndiyo imekuwa ya kwanza kama sikosei kiubora na mtanisaidia na Sokoine University imekuwa nafasi ya nne kwa Afrika Mashariki na Kati lakini bado wanafunzi wetu wale, sisi wengine tumeshamaliza huko vyuoni ingawa elimu haina mwisho, tunaendela kusoma bado, wanasoma katika mazingira magumu sana, bado kuna wanafunzi wanapanga uswahilini. Sasa

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama milifuatilia vyombo vya habari, mlisikia shughuli ya Ubungo kule, kuna kijana mmoja akaishia kumuua dada mmoja. Ni habari ya kusitikisha na ni mambo haya haya ya mitaani. Mimi nadhani kwa sisi tuliosoma shule za *boarding kwa Form Five* na *Six* ilitusaidia sana unapokuwa katika mazingira ambayo ni ya kitaaluma. Hawa wanafunzi tungehakikisha pamoja na hiki kipyta kinachokuja au kilichopo na hivi na viliwyokuwepo nyuma tuviboreshe. Maana inaweza ikasaidia hawa wanafunzi nao wakaweka mtazamo wao zaidi kwenye masuala yale ya kitaaluma kuliko yale ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale tuna *Sokoine University, Mzumbe University*, tuna *University of Dar es Salaam* yenye inayosifika, bado kuna wanafunzi wanapanga uswahilini. Hili jambo linasikitisha sana. Hebu tutafute mkakati unaoleweka na wakati Waziri unapoenda kujiandaa kwa majumuisho; sijapata taarifa kama ni leo au kesho, unatuambia nini kuhusu kuhakikisha kwamba tatizo hili tunalitatu na wanafunzi wanasoma katika mazingira ya *ki-academic* zaidi na wajengewe mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo mimi nakereka nalo, mfano mzuri uko *Tumaini University* pale. Chuo cha Tumaini kimepandisha ada yake kwa asilimia 60 kutoka shingili milioni 1.5 mpaka shilingi milioni 2.5. Sasa labda kwa Waheshimiwa Wabunge, maana si wote wenye uwezo huo mnaweza mkamudu gharama zile lakini wengi wa wanafunzi pale Chuoni hizi gharama zinawapa tabu sana. Kuna wanafunzi 1,000 ambao wanategemea fedha za mikopo kutohana na upandishaji huu inasemekana wanafunzi wale 1000 hawatalipiwa. Kweli tupo tayari hili litokee? Halafu kibaya zaidi kushinda yote ile asilimia 60 ya nyongeza imefanyika bila taarifa ambayo imetoa muda wa kutosha ili wazazi wajiandae. Sasa siku zote tunasema nchi yetu maskini, nchi ya wakulima na wafanyakazi, mimi bado naamini hivyo lakini tunavyoindesha mbona haiendeshwi katika *style* hiyo? Nadhani Waziri, hili hebu jaribu kuli-*address*, jaribu kukaa na uongozi na wenzako kwenye Wizara muonge tunawasaidiaje wale wanafunzi. Wengi wana uwezo wa kiakili, kitaaluma lakini fedha hawana na hatuwezi kuwaacha vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pamoja na haka kakitambi haka kanakoonekana, ni mdau katika michezo na nilikuwa mchezaji wa mpira wa miguu na Kapuya anajua ni

mshabiki mzuri wa *Simba Sports Club* na *Manchester United*. Kama kuna washabiki wengine huku sijui lakini wakati wangu mimi, kwa uchezaji wangu mpira, nilipata fursa ya kujenga mwili wangu na akili yangu na mpaka nikaelimika nilivyoelimika kupitia mashindano ya UMISHUMTA na UMISETA. Nimecheza timu za shule katika madaraja yote ya shule za msingi na sekondari lakini haya mashindano yameyeyuka na uyeyukaji wake bado siuelewi. Kwa sababu bado naamini kwamba *healthy body* inakupa *healthy mind*. Ukiwa mkakamavu wa mwili na akili zako zinakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo hii kuna Wabunge wengine huwa tunakutana nao tunaenda kuangalia *Taifa Stars* pale Dar es Salaam. Tunakwenda kwa ufahali na *Taifa Stars* tumeshaitela humu ndani lakini jamani msidhani kwamba kila kinachoelea hakikuundwa. Vinavyoelea vimeundwa na muundo wake unaanza chini na chini kwenyewe ndiyo shule za msingi na shule za sekondari. Kwa hiyo, naomba Wizara ifanye kila linalowezekana, turudishe mashindano ya UMISHUMTA na UMISETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina la muhimu sana na hili naomba niliseme kwa ajili ya Walimu wa Mbeya. Nina Walimu 450 ambao wamekuja kunipa kilio chao kutoka Mkoa wa Mbeya na Mheshimiwa Kyendesya shahidi yangu. Lakini kilio hiki naona kimeakisiwa, *reflected* humu humu ndani ya Bunge hasa katika suala zima la malimbikizo ya mishahara lakini vilevile kukosekana uwiano ama usambamba wa upandishaji wa madaraja na mishahara. Jamani ndugu zangu Walimu wanafanya kazi kwa taabu sana. Mimi naongea kama mtoto wa Mwalimu na aliyenitangulia katika kusema jioni hii ya leo ni mtoto wa Mwalimu tunalielewa hili na tunalielewa kwa matendo. Kwa hiyo, ninaposema sisemi kwa blaa blaa ninasema kitu kinachotoka kwenye sakafu ya moyo wangu. Kwamba jamani mishahara yenyewe midogo halafu unampandisha mtu daraja mshahara wenyewe humpi, ni sawasawa na kuchukua tonge la pilau halafu ukamnusisha mtu kwenye pua ukamwambia hili huli. Ukachukua kachumbari tena ukampa mtu puaní ukamwabia na hii huli! Ni mateso makubwa sana ya kiakili hayo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hili Serikali isinielewe vibaya. Nia yangu si kusema vibaya ila ni kuweka jambo ambalo linakera watu kwa muda mrefu. Lakini vilevile Rais alitoa maagizo na huu mfano ninao pale Kinondoni Dar es Salaam, mimi ni Mbunge wa Kitifa zaidi Jimbo sina bado, kwa hiyo, naomba nisemee na Dar es Salaam vile vile lakini linahusika sehemu nyingi sana, kwamba Rais aliagiza usifanyike uhamisho mpaka kuwe na pesa ya kulipia uhamisho huo. Matokeo yake Walimu wanahamishwa hovyo hovyo tu na kule Kinondoni ni mfano mzuri zaidi lakini fedha hawana. Sasa anaenda kujitegemea, anajitegemea vipi huyu? Ndiyo inayofanya sasa Mwalimu labda aanze kuwa mtoro ama atengeneze *tuition* zake, sasa hili si zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linanifanya nikumbushie pia suala zima la *teaching* au posho ya kufundishia na posho ya kufanya kazi katika mazingira magumu (*Hardship Allowance*) vilikuwepo! Nchi hii tangu lini tumekuwa matajiri, tuviondoe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya sababu tunakuwa na hizi tunaita *tuition* ambazo watoto wenyewe uwezo ndiyo wanakwenda kusoma na wale ambao baba kidogo

hali siyo nzuri wanaishia kusoma soma kwa kubabaisha, ni kukosekana kwa haya, Mwalimu kila akijaribu mkono huu na mkono huu kukutana haukutani. Njia pekee ya kumsaidia akaweza kumudu maisha yake, ni kurudisha tena *Teaching Allowance* na *Hardship Allowance*. Nawaomba sana Serikali, kwa kuwa dume mimi tu, ningekuwa mwanamke ningetoa kilio mnaniruhusu?

MBUNGE FULANI: Lia!

MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA: Hapana hatulii Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo la mdondoko, wengine tunaita *drop outs* kwa lugha ya kigeni. Midondoko hii, ina sababu nyingi sana. Kwenye hotuba imesemewa na mimi bahati nzuri nimezunguka na viongozi kwenye ziara wakija Mkoani Mbeya, Mheshimiwa Rais alipokuwepo pale na wakati ule Waziri Mkuu aliyeppita tumelikuta hili ni tatizo. Kule kwetu Mbeya ni hatari suala la mimba. Hivi kwa nini hatutafuti mkakati unaoeleweka kwa Walimu hawa wanaowapa watoto wetu mimba ili tatizo likaeleweka na kuisha? Kwa sababu zamani tungeweza kusema labda lingekuwa ni mimba tu lakini sasa na gonjwa hilo la UKIMWI. Kwa hiyo, nasema kwamba Walimu wengi, kama wengine wanatilea kama mama yangu, ni watu wazuri lakini kuna wengine kidogo wanateleza. Kwa hiyo, naomba hili tusaidiane kurekebisha kwa kukaa nao vizuri kuona linakwenda vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimejaribu kukaa na Walimu ikaonekana wanapoanza kazi ...

*(Hapa kengele ililia Kuashiria
kumalizika kwa muda wa Mzungumzaji)*

MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, kuunga mkono hoja, mengine nitachangia kwa maandishi, ahsante. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Thomas Mwang'onda, kwa mchango wako na nakushukuru sana kwa kitendo chako cha kutokulia ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa sababu ingekuwa ni tatizo lingine jipyä hapa. (*Makofî*)

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii muhimu iliyo mbele yetu.

Kwanza, naipongeza Wizara na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wasaidizi wake, Wakurugenzi, Wakuu wa Vyuo na wote kabisa ambao wanahangaika katika sera na kupanga mipango kama hivi walivyotuandikia. Ninawatachia heri, ni utekelezaji sasa. Mipango kwenye vitabu humu nimeona ni mizuri kweli kweli lakini basi Mungu atujalie kuweza kuitekeleza sawa sawa. (*Makofî*)

Baada ya hayo, kwa dhati kabisa natoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge wote humu ndani kwa mchango tuliyotoa kuchangia jitihada ya kampeni ya TEA ambayo kwa wakati huu, wamebuni mkakati wa kukusanya vifaa kwa ajili ya kusaidia watoto wenyе ulemavu katika shule 280 na kitu hivi kwa nchi nzima. Kwa kweli, kwa niaba ya watoto hawa watakaopata vifaa hivi, mimi natanguliza shukrani za dhati kwa sababu ni mdau kabisa kama siyo *number one* basi wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizi, nianze sasa kusema machache kuhusu hotuba hii ambayo kwa kweli ni nzuri. Mambo mengi yanaonyesha mwelekeo mzuri, fedha zimeongezeka kidogo pamoja na kwamba Wizara yenyewe hii ni kubwa sana, ina maeneo mengi ya kuzungumzia. Lakini mimi kama kawaida, najikita kwanza na elimu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu, ninazungumza na nitaendelea kuzungumza mpaka Mungu atakaponipa uwezo wa kuendelea kusema, Wizara imeeleza kwamba kutakuwa na mafunzo ya Walimu wataalam wenyе ulemavu. Lakini niseme mpaka sasa hivi katika eneo hili kuna upungufu mkubwa Walimu wa kuhudumia watoto wenyе ulemavu wa aina aina, bado ni wachache kwa sababu aina moja ya ulemavu inahitaji Mwalimu mmoja, mwanafunzi mmoja, utatosheleza lini mambo hayo? Kwa hiyo, bado hapa tunahitajika kuongeza jitihada ili tuweze kupata Walimu hawa wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani nilishauri, ili tatizo hili tuweze kulipunguza basi kozi hii ya elimu maalum iingizwe kwenye dozi ya mitaala ya wote wanaokwenda kusomea Ualimu kama ilivyo kwa Madaktari kwamba wanapata dozi ile, sasa baadaye kama anakwenda *ku-specialize* sawa, ili angalau kuweza kusaidia vinginevyo tatizo hili bado litaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naisihi Serikali, Patandi ndiyo Chuo pekee angalau kinachoandaa watu wa Cheti mpaka Stashahada, kipanuliwe hiki na kiimarishe ili nacho basi kiweze kutoa hata Shahada kwa elimu maalum kama ilivyo na kama nitakavyoendelea kupongeza Chuo Kikuu cha Sebastian Koloa kilichopo kule Lushoto ambao kweli kwa kozi ya kwanza ya Shahada, wao walisema sisi ni walimu watakaohudumia watoto wenyе ulemavu, ndiyo Shahada yao ya kwanza. Ya pili, wataongeza lakini wao wameweka kwamba hili eneo la elimu maalum na mambo ya watu wenyе ulemavu watayafundisha kwa kozi zao zote, iwe sheria wataingiza hicho kitu, iwe sijui *theology*, wataingiza hicho kitu. Kwa hiyo, jamani mimi ninaomba haya yaweza kufanyika, hayahitaji hela kutoka nje ni mabadiliko yetu wenywewe ambao tunaweza tukayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo, Walimu hata hawa wachache waliopo pamoja na kwamba wengine wana mazingira magumu ya kazi, hawa ndiyo wana mazingira magumu zaidi. Unapohangaika na mtoto mwenye ulemavu, yule anayetoa udenda, wewe peke yako tangu asubuhi, ukambebe nyumbani, umrudishe, ni kazi kubwa.

Naiomba Serikali iwaongezee angalau motisha ya posho, jamani wanafanyakazi ya Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa vifaa na nyenzo, nashukuru *TEA* na Wizara imesema mwaka jana ilitenga fedha kiasi Fulani lakini kwa mwaka jana fedha zilizotengwa zilitumika zaidi kununua vifaa vya watoto viziwi na *autism, autism* Kiswahili chake sikijui labda tutaelimishwa hapo baadaye, kwingine sikuona. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba hizi zilizotengwa, tujitahidi kuongeza *braille machines*, vifaa vya kusikilizia viziwi, vitabu vya maandishi makubwa makubwa kwa *albino, Perkins Brailler*, yote haya wana watalaan pale kwenye kitengo wanayajua. Fedha hizi zitumike sasa kwa kusambaza, najua kwa nyongeza ya *TEA* inavyofanya kazi huenda *alhamdulillah*, mambo yataendelea kuwa mazuri katika sehemu hii ya vifaa vya kujifunzia na kusomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu jumuishi, mimi bado unanichanganya. Sasa kama mimi nikichanganyikiwa hata wapiga kura wangu wanaponiuliza namangamanga hivyo hivyo. Mfumo huu bado unalalamikiwa na wanafunzi viziwi na wasioona hasa kwamba inawezekanaje moja bila kuwa hata na mtalaam wa lugha ya alama, Mwalimu akanifundisha mimi kiziwi nikaelewa Mheshimiwa Mbunge, wananiuliza hivyo. Kwani jibu ninakuwa nalo, sina! Nnao ushauri kama ni mfumo ambao tumeamua kwamba ni mzuri na nadhani mengine tunaiga kutoka huko nje, *Finland* ambao wameshajitosheleza kwa kila kitu basi tuseieneze mfumo huu kwa nchi nzima mpaka maandalizi kamili kabisa yawe yamekamilika. Walimu, vifaa, vyumba zinazohitajika, mashine zinazotakiwa, ndiyo itatusaidia, vinginevyo bado tutaaendelea kufanya *programs* ambazo watoto wetu tena wengi wataendelea kuwa nje ya *system* ya elimu na elimu ni haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu maalum, sijaona kwamba katika ukaguzi kuna angalau hata wakaguzi waliosomea masuala haya. Kinachotokea ni nini, wanapokwenda kukagua shulen, wale Walimu kwa sababu wakati mwingine wanatumia njia zingine walizofundishwa jinsi ya kumsaidia mtoto mwenye ulemavu, wao wanaona kama vile haipo kabisa. Kwa hiyo, wananyanyasika, wanapata *marks* za ovyo ovyo kwamba hawatimizi kazi yao sawa sawa. Sasa naomba wakaguzi nao wakasomee haya ili waweze kuwakagua watoto, maeneo na Walimu wanaofundisha kwa haki bin haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninaomba Halmashauri zote ziwe na Maafisa Elimu Maalum kwa sababu tuna Maafisa Elimu Taaluma, Vielelezo, Michezo, sijui vitu gani sanaa, mbona hili eneo halina? Niliambiwa kwamba kibali kimetolewa lakini kwa sababu ni jambo geni, Halmashauri zingine wala hazijaajiri wala hazijali. Kwa hiyo, masuala ya watoto wenye ulemavu katika maeneo hayo, ina maana basi hayana mwenyewe kama hayana mwenyewe tutafika wapi? Naomba hili litekelezwe kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho siku zote nimeendelea kusema na sitalia kwa sababu sasa nikilia itanisaidia nini, jamani ni ukosefu wa miundombinu, rafiki

kwa wanafunzi, kwa Walimu, kwa wafanyakazi wenyewe ulemavu wa aina aina. Hili nalo wala halihitaji wafadhili wala fedha zao, mimi ndiyo maana wakati mwingine kinaniuma, ni mipango yetu na dhamira ya dhati ya kubadilisha mambo haya. Nimeambiwa siku zote kuna ramani inayo-guide ujenzi hata huu wa sasa hivi sijui wenzengu humo mnamatembea hata kama mmeona mabadiliko. Hivi hili nitalisema mpaka lini? Tatizo hasa ni nini, basi mimi leo naomba zile ramani nipewe nitaziposti kwa gharama yangu katika Halmashauri zote za nchi hii. Maana haiwezekani sasa ni jambo la kawaida kabisa lakini hakuna kinachoendelea. Mimi kinanisikisha kwa sababu hapa wala tusingepata gharama yoyote tuna ma-engineer kwenye Halmashauri zetu, kuna engineer sijui wa kitu gani inakuwaje wasitumie nafasi ile kuweza kulikamilisha hili kila siku niwe ninasemasema tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kukosa miundombinu rafiki, nikueleze kwamba watoto wengine wanakata tamaa kwenda shule. Akibahatika kuandikishwa leo, kesho akiona choo cha kutumia chenyewe hawezi, watoto wa Tanga walitueleza hawaendi maliwato akija asubuhi mpaka nyumbani jioni kwa sababu hakuna kwa kwenda. Vitu vidogo vidogo kama hivi ni vikwazo kwa watoto wenyewe ulemavu kuweza kuzingatia masomo, tatizo ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la wazazi na walezi kuwaficha watoto hawa wasiende shule, mwenzangu amesema kwamba hata wanaona kazi kuwapeleka shuleni wanangoja Walimu waje wawachukue. Kwa hiyo, naomba hapa Serikali iendeleze ile sheria kali ya wazazi wote ambao hawaandikishi watoto wao wenyewe ulemavu wawachukulie sheria hasa inavyostahili hasa hawa wenyewe ulemavu kwa sababu sasa maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo watoto wasioona hawasomeshwi Hisabati wafikapo Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne lakini darasa la kwanza mpaka la saba wanasoma Hisabati. Sasa kinachonisikitisha mimi ni kwamba wale wa sekondari ambao hawasomi Hisabati wanapofanya mitihani, madaraja yao ya ufaulu yanashushwa kwa sababu hakufanya hesabu kana kwamba hesabu hizo aliacha mwenyewe kusoma, hili lirekebishwe. Nataka taarifa, mambo yanakuwaje kwa sababu wanaweza wakasoma hesabu. Kama ni vitabu kuna mashine iko pale Uhuru Mchanganyiko inayoweza kuandaa vitabu kwa lugha ya wasioona wakaelewa, hilo lirekebishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shule za *boarding* za watoto wenyewe ulemavu ambazo Serikali inapaswa kupeleka chakula na nauli za kutosheleza kuwarudisha nyumbani na wakati wa likizo kuwarejesha, hili limekuwa tatizo. Halmashauri nyingi MA-DEO, sijui zinatoka wapi sijui hawazipeleki huko shuleni kiasi kwamba wanafunzi wanaweza wakajikalia na njaa zao na wala kwenda nyumbani hakuwezekani mpaka Walimu wajitolee hela yao. Hii tunaiyosema haitoshi Mwalimu ajitolee kumrudisha mtoto nyumbani, Serikali kazi yake ni nini? Elimu ni moja ya haki ya watoto hawa kuipata na ni huduma kutoka Serikalini pamoja na kwamba wadau wengine wanaweza wakasadidhia hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napongeza sana *University* ya Sebastian Koloa, kama nilivyosema, wamejitoa kusaidia Taifa hili kuanzisha elimu maalum kwa ngazi ya Shahada. Walimu hawa wakihitimu ndio watakaowasomesha watoto hata watakaoweza kwenda vyuo vikuu wenye ulemavu kwa kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze mfano wa leo asubuhi, Kituo cha Njombe ambacho Serikali imekubali waanzishe Sekondari, wamekuja hapa mimi nilitembelea kituo hiki, nao watatusaidia hasa kwa wale wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa tatizo kwa Walimu wenye ulemavu, wanaopata ulemavu ukubwani, wanaweza wakasaadiwa kwenda kutibiwa kama ni nje kama ni hapa hapa, lakini stahili zile za matibabu hawalipwi. Mifano ninayo mkitaka nitaisema, hawalipwi, wanahangaika mpaka wanakata tamaa na haki ile basi inapotea mtu anasema basi Mungu atayajua. Mungu atayajua na mtu anateseka! Kwa hiyo, Walimu hawa waangaliwe wanapolalamikia vitu vyao jamani wapeni kwa sababu ni haki yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya Walimu na matatizo yao, mimi ni Mwalimu *ni-declare interest* kabisa, nilikuwepo huko, nayajua, naungana mkono na wengine waliosema malimbikizo, vyeo, madaraja yanabebana tu mpaka sasa hivi na ndiyo tunawazalisha wengi, sijui itakuwaje tutakapowapata hao mia ngapi elfu huko, sijui mambo yatakuwaje. Lakini nina hakika kwa sababu kuna mambo ya kompyuta siku hizi labda mambo yatakaa sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo lililotokea *Iringa Girls* na *Lugalo Secondary School*, kulikuwa na Walimu wanaowasaidia watoto wasioona *Lugalo Girls* na *Iringa Girls*, viziwi, *alhamdulillah* wamepata *promotions* wamekwenda kwingine lakini pengo lile bado halijazibwa tangu mwaka jana na Waheshimiwa Viongozi humu waliahidi kwamba pengo hili la Walimu hao litazibwa mpaka leo. Mpaka saa nane hii, nimepigwi simu wanauliza mama sasa tufanyeje, mimi siyo ninaowagawa Walimu wala siyo ninaowafundisha lakini lazima niseme hapa. Kuna matatizo kule watoto viziwi hawana msaada, wasioona hawana msaada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, huwa sipendi kugongewa kengele, mengine mengi yaliyobaki hapa nitayachangia kwa maandishi. Lakini ninaomba haya niliyoyaeleza basi mwendelee kunipa imani kubwa kwamba yatawezekana pamoja na kwamba mengine yameanza kuwezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja lakini Mheshimiwa Waziri unahitajika Sebastian Koloa University, uende ukawatembelee ukaona walivyo-furnish maabara zao, wanavyofundisha wale Walimu wengi tu, wanakuhitaji ili ukayajue yaliyoko kule kwa sababu Walimu wanaofundisha mnasema wa *PhD* kumi kumi, kule wanashindwa kuwapata kwa sababu ile ni shule ya taasisi ya dini. Nenda walinituma na ninakuomba uende. Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Margreth Mkanga kwa mchango wako mahiri na mara zote kwa kweli umekuwa mstari wa mbele sana kutetea maslahi ya watu wenye ulemavu. Hongera sana.

MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Awali ya yote, nitoe pungezi kwa Profesa Maghembe, Waziri, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Katibu Mkuu, Dihenga, Wakurugenzi wote na wafanyakazi wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kumsaidia Waziri kuandika hoja nzuri. Naanza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kuhusu mfumo wa elimu katika Tanzania na baadaye nitakwenda kwenye matatizo yaliyoko katika Wilaya ya Ngara kuhusu Wizara ya Elimu na nitahitimisha kwa kueleza changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mfumo wa elimu, sina matatizo na mfumo wa elimu katika Tanzania. Elimu ya awali ni miaka miwili, elimu ya msingi miaka saba, elimu ya sekondari miaka minne, elimu ya *High School* miaka miwili na kuendelea sina matatizo na hiyo. Ninachoomba ni kwamba kuwe na maboresho ya mfumo huu ili kuwe na sekondari za Wilaya kwa sababu kwa mfumo wa sasa hivi sekondari zote ni za Kata, hakuna sekondari za Wilaya tena. Mimi nadhani huu ni mfumo wa kizamani. Utatuletea matatizo ya vijana kutochanganyika hata kwenye Wilaya yenewe, utaanza sekondari, katika Kata, huko mbele ya safari kutakuwa na *High School* katika Kata, utaenda Chuo Kikuu mara nyingi katika Mkoa husika huko mbele ya safari, itaturudisha nyuma suala la utaifa. Maboresho ambayo ninayo ni kwamba tuwe na Sekondari za Wilaya ambazo zitachukua watoto kutoka kata zote ili waweze kuchanganyika katika Wilaya husika. Hayo ndiyo maboresho ninayopenda kuipa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iyafanyie kazi. Itatusaidia sana huko mbele ya safari. Zamani *system* ilikuwa ya aina hiyo, lakini kwa wakati huu naona, imevurugika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya pili kuhusu sekondari, natoa mawazo kwamba tuwe na sekondari za Mkoa, kwa sasa hivi hilo wazo halipo. Katika hotuba ya Waziri sikusikia Sekondari za Mikoa. Tuwe na Sekondari za Mkoa ambazo zitachukua vijana waliofanya vizuri katika kila Wilaya ili kuwe na mchanganyiko wa wanafunzi katika Mkoa husika. Hayo ndiyo maboresho napenda kuzungumzia ili tuyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya tatu, tuwe na Sekondari za Kitaifa, hizi sekondari zitachukua vijana au wasichana, kutoka nchi nzima Mikoa yote. Turudi kwenye zile sekondari za watoto wenye vipaji, kwa kufanya hivyo, tutaboresha elimu. Kwa mtindo wa sasa, hizo sekondari ni kama hazipo. Zamani kulikuwa na *Tabora Boys*, kulikuwa na Ilboru, Kibaha, shule ambazo zilikuwa zinachukua wanafunzi kutoka nchi

nzima. Wanafunzi walipata fursa ya kuchanganyika na kujua mila na desturi za wenzao wanaotoka Makabila tofauti. Nadhani hii itatusaidia sana katika kujenga utaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye *University*. *University* sina matatizo na mpangilio wa sasa. *Weakness* ninayoiona katika *University* sasa hivi ni fedha zinazowekwa kwa ajili ya *training*. Zamani ilikuwa inaitwa *Post Graduate Training* au *Staff Development* ni kama imepungua sana. Kinachotokea ni kwamba tunanyang'anyana Walimu katika *University* mpya zinazojengeka sasa hivi. Mimi niko kwenye *University Council of Dar es Salaam*. Malalamiko makubwa yaliyoko pale ni kwamba Walimu wote wazuri wako miaka 55 na kuendelea. Hao hao ndiyo wananyang'anywa kwenda *University of Dodoma*, kwenda Botswana na kwingineko. Kinachotokea ni kwamba wale wanaobaki au ni wale ambao ni vijana mno na hakuna *recruitment program*. Ninachopendekeza ni kwamba *Post Graduate Training* ipewe fedha za kutosha ili tu-*train PhD* wengi zaidi ambao watashirika katika kuboresha elimu katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ratio* ya *PhD Holders* ikilinganishwa na *total population*, ni ndogo sana. Sisi tuko nyuma, Kenya wako mbele, Uganda wako mbele *and of course South Africa* wako mbele sana. Hiyo, ni *index* ya kuonyesha ni kiasi gani tunaweza kwenda kwenye ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Kama *ratio* ya wenye *PhD* ni wachache na *population* ni kubwa ina maana ya kwamba *rate* ya *research*, inayofanyika ni ndogo hasa *Basic And Applied Research*. Kama hatuna hawa watu kwa wingi, tutabaki nyuma *technologically*. Hayo ni maboresha ambayo ninalipenda Wizara iyafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nizungumzie Ngara. Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Ngara. Hapa niwashukuru wapiga kura wa Ngara, kwa kunichagua na labda niwaombe wanichague tena mwaka kesho. Huu ndiyo uwanja wangu wa kujidai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya msingi MMEM imefanyakazi vizuri sana. Shule zote katika Wilaya ya Ngara zimejengwa kwa kiwango kinachoridhisha. Tatizo ni ukosefu wa Walimu. Katika shule nyingi za msingi, Walimu hawatoshi, vitendea kazi havipo. Ninachoomba Wizara ni kwamba isukume idadi ya Walimu wawe wengi katika shule ya msingi ili tuweze kuboresha elimu katika Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofanya ziara kwenye shule za msingi, unakuta Mwalimu mmoja amekaa kwenye shule moja miaka 25. Huyu Mwalimu ameshapata na bibi katika kijiji husika na kinywaji ni *full time* hata shulenii haendi. Nilipouliza kwa nini imekuwa hivyo wakasema gharama za *kum-transfer* kutoka shule moja mpaka shule nyingi ni kubwa mno kiasi cha kwamba Afisa wa Elimu wa Wilaya anashindwa kuwapa *tranfer*. Hii inazorotesha elimu katika Wilaya ya Ngara. Namwomba Afisa Elimu na Waziri mhusika awekeze katika *reshuffling*, kuchanga Walimu ili wasikae mahali pamoja kwa muda mrefu sana kwa sababu wanajisahau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa sekondari. Tumetumia fedha za *TASAF* kwa kujenga sekondari za Kata. Sasa hivi Ngara kuna Sekondari 24. Mwaka 2006, awamu ya

utawala wa Awamu ya Nne, ulipoingia madarakani kulikuwa na shule sita tu. Katika miaka miwili, 2006/2007/2008, tumejenga sekondari 18. Hiyo ni rekodi kubwa. Lakini nilichogundua ni kwamba ilibidi tutumie nguvu ya ziada kuzijenga hizo sekondari. Uzoefu wangu umeonyesha kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Ngara na TAMISEMI walikuwa hawana uwezo wa kusimamia ujenzi wa sekondari. Hii siwezi kumlaumu yeoyote ni kwa sababu walisukumiziwa mzigو ambaо walikuwa hawana uzoefu nao. Kwa hiyo, walisuasua siku za kwanza na imeleta mtafaruku ambaо unaendelea mpaka sasa. Lakini tunaweza kujivuna ya kwamba tumejenga sekondari 18 ila zina matatizo ya Walimu. Nimwombe Mheshimiwa Profesa Maghembe aiangalie Wilaya ya Ngara kuhusu Walimu wa sekondari kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa lazima nizungumzie ya kwamba tumepata *High Schools* mbili, ya Kabanga na Lukole. Nimshukuru Mheshimiwa Mahiza kwa kufuatilia suala hili kwa sababu Ngara tulikuwa hatuna *High School* sasa tuna *High School* mbili ambazo zimeleuliwa katika mwaka mmoja uliopita. Ninachokiomba ni kwamba angalau kila tarafa ipate *High School* ili iwe ni changamoto kwa vijana kuingia kwenye hizo *High School*. Tukipata hiyo, mambo yatakuwa yamenyooka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, niseme hizo *High Schools* ambazo hazijajengwa, zijengwa katika tarafa ya Murusagamba na Tarafa ya Ruhenge. Kwa sasa hivi, tarafa hizo mbili ziko mbali sana na makao makuu ya Wilaya, kuna manung'uniko ya kwamba kuna upendeleo mkubwa kwa sababu shule zote za *High School* ziko karibu sana na Makao Makuu ya Wilaya. Sasa wale ambaо wanakaa mbali na Makao Makuu ya Wilaya wanunung'unika kwamba wamewekwa kando. Kuna mambo mengi yanayohusiana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nawaomba Tarafa za Murusagamba na Tarafa za Rulenge zipewe kipaumbele katika kujenga *High School* na ninaweza kutoa pendekезо ya kwamba Sekondari ya *High School* ambayo itajengwa Murusagamba, ijengwe Murusagamba kwenyewe na siyo karibu na Makao Makuu ya Wilaya. Sekondari nyingine itakayojengwa katika Tarafa ya Rulenge, ijengwe karibu na Rulenge Mji Mdogo ili wawatoe wasiwasi wanaokaa karibu na Rulenge ya kwamba wanaonewa. Kwa sababu hii ni hisia ambayo inajitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Kikwete alipotembelea, aliambiwa maneno mengi sana kuhusu tofauti ya watu wanaokaa karibu na Makao Makuu ya Wilaya na wale ambaо wanakaa mbali na Makao Makuu ya Wilaya. Hii inaleta hisia ya kwamba Ngara imegawanyika katika vipande viwili, ambayo haileti mustakabali wa maelewano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za *Form Five* na *Form Six*, ni chachu ya kuleta maendeleo. Kwanza itailazimisha Serikali kujenga mabweni kwa sababu haiwezekani wanafunzi watoke kwenye Kata moja, itabidi watoke kwenye Wilaya nzima ili tuweze kujaza hizo *High School*. Kwa hiyo, inaleta changamoto na chachu katika kuleta maendeleo. Kingine ni kwamba kuna *mixing effect* kwa sababu vijana katika Kata tofauti

tofauti, inawafanya vijana wachanganyike kwa hiyo waweze kufurahia au kujuua mila na desturi za makabila mengine. Sio rahisi kujaza *High School* kwa khabila moja, haiwezekani! Sio rahisi kujaza *High School* nne kutoka Ngara, wengine watatoka Biharamulo, wengine watatoka Bukoba na hii itakuwa ina faida ya kuleta mchanganyiko wa wanafunzi katika Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana kwa kunisikiliza na naunga mkono hoja. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Banyakwa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali na Mheshimiwa Mohamed Missanga, Alhaj na yeje ajiandae.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mie naomba nitoe mchango wangu kidogo katika Wiraza hii muhimu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba hivi leo watoto wengi ambao wanafika umri wa miaka saba wanayo fursa ya kwenda shule na wengi wao ambao wanafaulu kwenye mitihani yao basi wanaendelea kuingia kwenye shule za sekondari. Hii tunatoa shukrani kwa mpango huu wa MMEM na MMES. Ingawa bado na hasa kwenye shule zetu za sekondari kuna matatizo makubwa lakini tukitupa macho mbele yetu huko naona kuna matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna wimbi kubwa sana la wanafunzi ambao wanamaliza sekondari, wanamaliza Kidato cha Sita, hivi sasa wako katika shule za sekondari wengi sana na wanafunzi hawa wanataka kuendelea na masomo yao katika Vyuo Vikuu vyetu vya Tanzania. Sasa inabidi tuijiweke uzuri ili kuweza kuwa-*absorb* wanafunzi hawa, kuwachukua wanafunzi hawa kuwadahili katika vyuo vyetu vikuu ili kila mmoja ambaye anataka kupata elimu ya juu au anayestahili kupata elimu ya juu, apate elimu ya juu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Chuo Kikuu kikubwa hapa nchini nikitilia maanani kwa udahili wanafunzi ni Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kina wanafunzi wengi sana, kina wanafunzi katika kila Mkoa wa nchi hii tofauti na Vyuo vingine. Lakini wakati tunasomesha vijana wetu, tunahitaji Walimu na kama alivyozungumza Mheshimiwa aliyenitangulia hapa Mheshimiwa Profesa Banyakwa, kuna upungufu mkubwa wa Walimu, Walimu wengi hivi sasa wa Vyuo Vikuu wameshasogea umri, wanaelekea kustaafu na katika hao ndiyo wananyang'anyana, kila Chuo kinataka hapo hapo. Sasa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambacho kinachukua wanafunzi wengi wanaomaliza Kidato cha sita, kinategomea sana Walimu wa muda, *part time Teachers or part time Lecturers* kama vyuo vingine huria katika nchi nyingine, ni chuo kikuu ambacho kina Walimu wengi wa muda, *part time Teachers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu hawa sawa na mfanyakazi yeyote anataka apate stahili yake, malipo yake pale anapomaliza kazi. Walimu hawa wanafanya kazi nzuri sana, wanasomesha wanafunzi wetu, wanasahihisha *practicals*, majaribio haya na wanasahihisha mitihani lakini Mwalimu au mfanyakazi yeyote kama hakupata maslahi yake ipasavyo na kwa wakati mwishowe ataondoka na hilo litakuwa kipigo si kwa chuo peke yake lakini kwa Taifa zima, kwa sababu kama nilivyosema Chuo Kikuu Huria ni chuo ambacho kinadahili wanafunzi wengi zaidi wanaomaliza sekondari katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu wa Vyuo Vikuu Huria vya nchi nyingine kwamba malipo ya hawa Walimu wa muda, *part time Teachers* unawekwa katika sehemu inaitwa *Personal Emoluments (PE)*. Kwa hiyo, wakimaliza wanapata fedha zao, hakuna ugomvi. Lakini hapa kwetu malipo, mishahara ya Walimu hao wa *part time* ipo katika Matumizi ya Kawaida ya kuendesha Chuo (*OC*). Kwa hiyo, inakuwa vigumu kwa chuo kuweza kuwalipa Walimu hawa stahili yao na kwa wakati. Kwa hivyo, hapa pana janga, kuna janga la kwamba hawa Walimu wengi wao kama hawatalipwa wataondoka na kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulipiga kelele hapa hivi hivi na tukambiwa kwamba Wizara inazungumza na Hazina na kwamba Hazina karibu itatoa ufumbuzi wa jambo hili. Lakini hivi leo mwaka umepita, Walimu hawapati stahili zao kwa wakati. Kwa hivyo, tunataka Waziri atueleze je, mustabali wa mambo hayo ukoje, tunakwenda wapi huko mbele? Chuo kikiyumba, ni hasara kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hiyo *OC* yenye inapungua siku hadi siku, hii inafanya kuendesha chuo chenyewe kuwe kugumu. Nitoe mfano, mwaka 2008/2009, chuo kilipata fedha ya *OC* ya shilingi bilioni 1,000,956,966 lakini huko nyuma mwaka 2001/2002, chuo kilipata shilingi bilioni 1,104,000,000 ambazo ni zaidi ya hizi ambazo wamepata katika mwaka 2008/2009 tunakwenda wapi? Chuo kinadahili wanafunzi wengi zaidi, kazi zinazidi lakini fedha ya *OC* inapungua. Tunataka Mheshimiwa Waziri atueleze, kwa nini Chuo hiki hakiongezwi pesa za kuendesha chuo kama ipasavyo ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo hiki sasa hivi kina eneo kubwa sehemu ya Bungo, Kibaha kule kwa ajili ya kujenga Makao Makuu yake. Kinataka kijipe nafasi, kijichanue kiweze kudahili wanafunzi wengi zaidi na ujenzi wa Chuo hicho au Makao Makuu ya kudumu ya chuo gharama yake ni shilingi bilioni 170. Chuo kiko tayari kukopa fedha hizo lakini kipate udhamini wa Serikali kama Vyuo vingine ambavyo vinapata udhamini wa Serikali ili kiweze kujenga Makao Makuu yake hayo katika sehemu ya Kibaha na mkopo unaweza kupatikana katika mabenki au katika mashirika yetu ya fedha kama Serikali ikiweza kutoa udhamini huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu Chuo hiki kina wanafunzi katika kila Mkoa na ikiwa kina wanafunzi katika kila Mkoa, ina maana kinahitaji kuwa na majengo ya kudumu katika Mikoa hii, kiweke vitendea kazi vyake, kiweke vitabu, kiweke kompyuta, kwa sababu wanafunzi katika Mikoa hii wanasoma kwa kutumika kompyuta, *distance*

learning. Sasa ninavyoolewa, chuo kina majengo ya kudumu katika Mikoa mitano tu, Mbeya, Ruvuma, Kilimanjaro, Singida na Iringa. Kwa hivyo, kinahitaji kuwa na majengo ya kudumu katika Mikoa mingine iliyobakia 19 na vile vile chuo hiki kinahitaji kuwa na jengo la kudumu katika Kisiwa cha Pemba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaongelea Pemba kwa sababu natoka Pemba, nina maslahi na matatizo ya wanafunzi wetu nayajua pale. Wanafunzi hawa, jengo hili ambalo sasa hivi chuo kipo hapo, si jengo la chuo, ni jengo la kupanga. Kwa hivyo, hata hawawezi kuweka kompyuta pale. Najua sharti moja la wafadhili wanaoleta kompyuta hizo ni kwamba majengo ya chuo yawe ni majengo yao binafsi siyo ya kupanga. Kwa hiyo, pale katika Chuo Kikuu Huria cha Pemba kuna kompyuta moja na kompyuta hiyo ni ya Uongozi wa Chuo na hata hiyo haifanyi kazi kila siku. Ukienda mara nyingi inaharibika. Wanafunzi wanakosa sehemu ya kujisomea, watasoma viyi jamani na matatizo kama hayo ? Pemba, Chake Chake ambako kiko chuo chenyewe kuna *Internet Café* moja tu *Internet Café* hiyo ukienda ina *speed* ya konokono. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu si hivyo tu, mbali ya *speed* ya konokono, mara nyingi pale wanakuwa na wanafunzi wao ambao wanafundisha kompyuta, wanatoa kozi za *computer literacy*, kwa hiyo wanafunzi hawa wa Chuo Kikuu Huria wanakosa sehemu za kujisomea. Jamani watafutieni majengo ya kudumu wanafunzi wetu wapate kusoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo hiki kimeomba Serikalini kununua au kupewa majengo ya umma, kwa hivyo Serikali ichangamkie. Serikali na Wakuu wa Mikoa, Viongozi wa Mikoa wawasadie ili wapate majengo ya kudumu, wanafunzi wakae wajisomee kwa raha mustarehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine sijui ni kwa nini Wizara inachelewa kuweka miundombinu ya kuvunganisha Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti katika mtandao mmoja. Sijui kwa nini Serikali ina kigugumizi. Kwa nini haitaki kushirikiana na Uongozi wa Vyuo Vikuu hivi? Vyuo Vikuu hivi kuanzia mwaka 1999 vimeunda Umoja wao au *Trust* yao wanaita TENET ambayo inaweza kuunganisha Vyuo Vikuu vyote vya Tanzania pamoja na Taasisi za Utafiti katika mtandao wa kimataifa kupitia *SEACOM* lakini Serikali imelala usingizi fofofoo hata kusaidia haitaki. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo Vikuu hivi 16 hivi sasa wanalipa kwa *local providers* dola 901,254 kwa mwaka, kwa *speed* ya *megabite name per second* lakini ingekuwa wamejiunganisha katika mtandao wa pamoja, wangeweza kulipa dola 750,000 kwa miaka 20, jamani tuna virusi gani sisi ambavyo vinatuzuia kuchangamkia mambo mazuri na faida, kwa nini? Mnatufikisha mahali tunafikiria labda hapa pana harufu harufu za ufisadi, jamani wasaidieni vijana wetu, wanataka kusoma! Wenzetu wa Kenya wamekuja kujifunza kwetu sisi kuhusu *Internet*, leo wameshafungua *KENET* kule, Warwanda wamefungua *RWANET* na wanaendelea, lakini sisi tumelala fofofoo, hatupo na kwa kweli tungkuwa na TENET tungeunganisha na mitandao hii pamoja hata haya mataifa mengine yaliyoko Magharibi yangeweza kununua hizi *services* kwetu na ikawa

faida kwetu sisi, lakini tumelala, wa Kenya watachangamkia, sisi wacha tulale, virusi vimetushika sijui namna gani? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama Wizara inajua kwamba Umoja wa Ulaya (*European Union*) imeahidi kusaidia gharama za kuunganisha vyuo hivi kwa asilimia 75.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Wakati umekwisha!.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, ni kengele ya pili.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Ahsante, naomba kuwasilisha si kuunga mkono, nawasilisha. Ahsante sana. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Tarab kwa mchango wako na leo umekuja na lugha ya mwendo wa konokono. Sasa sijui ni aina gani ya konokono.

Mheshimiwa Missanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Fatuma Mikidadi.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwenye hoja ilio mbele yetu.

Pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote pale Wizarani kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia suala la elimu lakini pia kwa maandalizi mazuri ya bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze hoja rasmi kwanza kwa kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Singida Kusini, kwa kuitekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo, kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi inasema, katika kipindi hiki walau sekondari moja ijengwe katika kila Kata na mimi hapa nataka niipongeze sana CCM kwa kuthubutu kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM isingethubutu kuelekeza hivyo mpaka leo tungekuwa kule kule tulikokuwa miaka iliyopita. Kwa hiyo, pongezi kwa Chama cha Mapinduzi kwa kuthubutu kufanya hivyo na nawapongeza sana wananchi wa Jimbo la Singida Kusini, kwa kuitikia jambo hilo na kujenga Shule za Sekondari za Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitatu iliyopita, kwenye Jimbo langu tulikuwa na sekondari nne tu lakini nafurahi kuwaambia kwa kazi nzuri iliyofanywa na wananchi, sasa tuna sekondari 30 kwa kipindi cha miaka miwili. Lazima niwapongeze sana wananchi wa Jimbo langu la Singida Kusini. Lakini bila kumsahau kumpongeza Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wetu wa Singida, Mheshimiwa Kone, kwa kazi nzuri aliyofanya ya kusimamia na kuhakikisha kwamba suala hilo linafanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanikiwa ujenzi wa sekondari, tunafika mahali sasa tunajenga *High School* au *Form Five and Six* na maelekezo ya Mkoa ni kwamba walau kila Jimbo liwe na *Form Five and Six* na mimi nafurahi kusema kwamba katika shule yetu ya Jimbo la Singida Kusini ya Ikungi tumelenga kujenga *Form Five and Six* na tayari tumeshaanza na taratibu zinafanyika, Wakaguzi wamekuja tumeambiwa yako mambo machache ya kufanya. Nina hakika tutafanya vizuri na kwa muda muafaka ili *Form and Six* haraka iwezekanavyo iweze kuanza. Bado hiyo ni kazi nzuri ambayo imefanywa na wananchi wa Jimbo la Singida Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulinalo ni upungufu wa Walimu na masuala ya maabara. Kazi nzuri iliyofanywa na wananchi lazima iungwe mkono na Serikali kuhakikisha kwamba maabara zipo na vile vile Walimu wapo. Jitihada hizo, tumeelezwa na Mheshimiwa Waziri hapa kuhusu habari ya Walimu lakini nasema bado ni tatizo. Mimi kwenye Jimbo, mahitaji ya Walimu wa sekondari ni 367, waliopo sasa hivi ni Walimu wa sekondari 144, hawajafika hata nusu ya mahitaji ya 367 *only one hundred and forty four*. Unategemea taaluma hapo itaboreka kwa utaratibu gani? Kwa hiyo, tunao upungufu mkubwa sana wa Walimu 223, ndiyo wanaohitajiwa. Niombe sana Mheshimiwa Waziri na wenzake, watuone sisi watu wa Singida. Huko nyuma tulisusua kupata elimu sasa tumeamka. Naomba tafadhali sana tupatiwe Walimu ili jitihada hizi za wananchi ziweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko shule bahati mbaya, hata Walimu wa Serikali hata mmoja hakuna, wako Walimu tu ambao wananchi wameamua kuchanga visenti vyao ili kuwachukua, Walimu wastaifu na *Form Six* ili wawafundishe, wako wawili. Sasa unafunga sekondari Walimu wawili tena Walimu wenyewe wa kuchangiwa na wananchi. Hivi unategemea kutakuwaje na mafanikio? Shule ya Msungua, ni mionganii mwa hizo shule ambazo ninazisema. Juzi nimezungumza na *DEO* na *REO*, naona kama wanaanza kufanya hiyo shughuli. Kwa hiyo, ombi langu hapa ni kwamba kwa kweli tatizo la Walimu liangaliwe ili kusudi tufanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naambiya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina Walimu wa ziada 3,000 au zaidi ya 3,000 wapo kule Zanzibar na hao wangewenza kutusaidia sisi, Tanzania ni moja. Hivi mambo mazuri yakiwa Visiwani hayafai kuja huku Bara? Lazima yatoke Bara tu yaende Visiwani ? Kwa nini mazuri tusiige ? Hivi tunashindwa nini kuchukua Walimu 3,000 wapo hapa Zanzibar hapa, tena Walimu wa ziada?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimecheki na Waziri wa Elimu ambaye ni mwenzetu hapa Mheshimiwa Haroun, amesema ni kweli wapo na sisi tuko tayari kuwaruhusu waje huku. Sasa tatizo liko wapi ? Lakini si hivyo tu naambiya hata Mheshimiwa Rais alishaawahi kutoa maelekezo kwamba Serikali mbili hizi ziangalie uwerekano wa kuchukua wale Walimu kutoka Zanzibar kuwaleta hapa mpaka leo mwaka sijui wa pili, wa tatu, wa nne hakuna kinachofanyika, kuna nini? Ninyi mnataka tuige vitu vyta Afrika Kusini tu, kila jambo Afrika Kusini, Zanzibar hapo wanafanya vizuri na wana Walimu wa ziada tunawaachia kwa sababu ya nini?

MBUNGE FULANI: Hawataki !

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Hawataki, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo juu ya hili kwa sababu ni kweli wapo, Waziri amenihakikishia na ni mwenzetu hapa angekuwepo angeweza kuthibitisha na Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo, sasa upungufu ndiyo tunaousema shule zingine hazina Walimu, kuna nini kushindwa kuwachukua Walimu hawa kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina shule kule inaitwa Mgungira, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshafika, namshukuru sana na nampongeza sana, iko mbali kidogo karibu na mpaka wangu na Mama Ntimizi kule Tabora. Mazingira ya kule ni magumu kidogo. Sasa wanafunzi ambao walikuwa kwenye sekondari ile, wote wameondoka kwa sababu ya mazingira magumu na kwa sababu hakuna bweni, au hakuna mabweni. Wakazi wa pale wengi ni wafugaji na taratibu za wafugaji mnazijua. Kwa hiyo, ombi langu kwa sababu wanafunzi wote wamekimbia mpaka imebidi tuhamishe baadhi ya Walimu kwenye shule zingine, tujengewe mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma Serikali ilishasema kule ambako ni maeneo ya wafugaji yajengwe mabweni, sio hosteli, iko tofauti kati ya hosteli na mabweni. Mimi nazungumzia mabweni, hata kama ni kuchukua baadhi ya wanafunzi kutoka maeneo mengine ili waje pale waweze kujisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze masikitiko yangu kuhusu Baraza la Mitihani. Wote tunajua mwaka 1973, Baraza hili lilianzishwa kwa Sheria Na. 21 na tunajua kama mwaka 1973 mpaka mwaka 1997, Baraza hili limefanya kazi nzuri sana. Matatizo yalianza kutokea mwaka 1998, mtihani ulipovuja nchi nzima na ukafutwa wote, ikatungwa mitihani mipya, hapo ndiyo mwanzo wa matatizo ya lile Baraza la Mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, kwa muda wa miaka miwili, mwaka 1999 mpaka mwaka 2001, Serikali iliamua kuchapisha mitihani Uingereza, mambo yalikwenda vizuri lakini baadaye tukarudi tena, tukasema hapa, wacha tuchapishe sisi wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapakutokea matatizo kwa muda, lakini baada ya kuajiriwa Mtendaji Mpya, yule Katibu Mtendaji aliyeo sasa mwaka 2005, alipokaa miezi karibu 6, 7 akafukuza wafanyakazi 38 na mimi nilieleza hili mbele ya Bunge hapa mwaka 2006, wakafukuzwa kwa madai kwamba Baraza linasafishwa na kwamba mambo ya uvujaji wa mitihani, hayatatokea tena. Sasa wote sisi ni mashahidi, mwaka jana mtihani umevuja ingawa inasemekana kwamba ni mtihani mmoja wa Hisabati, si kweli, mitihani iliyovuja ni mingi, Jiografia, Historia, Kiswahili, Kiingereza yote ilivuja, lakini imewekwa kwamba ni mtihani mmoja tu wa Hisabati, si kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika ni kwamba ilitungwa mitihani ya haraka haraka ikaenezwa katika Mikoa jirani kwa maana ya Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro,

Arusha, ndiyo wakapata mitihani mipyä lakini Mikoa ya mbali kama Kigoma, Mwanza na wapi, wote wale walitumia mitihani ile ile. Kwa hiyo, mwaka jana, kwa taarifa yako, wako waliofanya mitihani iliyotungwa upya lakini wapo waliofanya mitihani ile ile ambayo ilivuja, kwa sababu ilikuwa mbali walishindwa kuirudisha, matokeo yake ndiyo yaliyotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu, tarehe 11 mwezi wa saba, Mkurugenzi huyo huyo amefukuza wafanyakazi 80, wakati ule kafukuza wafanyakazi 38, yeze huyo kazi yake ni kutimua watu. Jamani huu ndiyo Utawala Bora? Kunapotoka matatizo, si tunasemaga mkubwa ndiyo awajibike? Sisi si tumewawajibisha wakubwa hapa? Maskini ndugu yangu, Mheshimiwa Lowassa huyu hapa, amewajibika kama Waziri Mkuu, kwa makosa ambayo si ya kwake. Wako Mawaziri wamejiuzulu hapa, kwa makosa ambayo pengine siyo ya kwao lakini wamechukua *responsibility* kwa sababu ya ukubwa, huyu anashindwa nini kuwajibika, yeze anafukuza watu ambapo sasa wamefikia watu 118 lakini yeze yupo pale pale. Tatizo ni yeze siyo watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema na yeze naye aondoke kwa sababu chombo nyeti kama Baraza la Mitihani, leo unafukuza watu 38, kesho unafukuza watu 80, unaleta watu wapya, sijui wangapi, huo unyeti na usiri wa Baraza la Mitihani unatoka wapi, hauwezi kupatikana. Haya yanatokea ni kwa sababu ya vurugu, hakuna *stability*, watu hawana imani, watu hawana *confidence*, watu hawajui wapo au hawapo kwa sababu ya mtu mmoja tu basi na baadhi ya wakubwa mnalinda, naambiwa analindwa kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwaje, kwa muda mfupi amekuwa ana Wasaidizi, *Deputy Executive Secretaries* sita na wote kawatimua, sasa hivi kabaki mmoja. Hata hao sita kawatimua, ndiyo, majina yao haya hapa. Mmoja anaitwa Mbiku, mwingine anaitwa Hoseno, mwingine Ali Hamed, mwingine Shile Mashauri, mwingine Thobias Oseno, wametimuliwa. Wengine wanafanya kazi miezi sita, wengine mwaka mmoja, wengine sijui miezi mingapi, kawatimua wasaidizi wake wa karibu *Deputy Executive Secretaries*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, akimwona mtu *threat*, anamwondoa ili kusudi nafasi yake isiharibike. Tutakwenda wapi? Watu 118, mara sita, familia ya Kiswahili ni mke na mume na watoto wanne, hao ni karibu watu 700 na ngapi. Sasa huyu anaharibu familia ya watu 700 na ngapi kwa sababu ya kulinda nafasi tu basi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 nilieleza, *no action was taken*, lakini leo nitataka maelezo vinginevyo na mimi nakuja na Hoja Binafsi ya kuunda Tume ya Bunge Kuchunguza Baraza la Mitihani kwa sababu Tume ya kwanza ya mwaka 1998 haikufanikiwa, Tume ya juzi ya mwaka 2008 chini ya Profesa Bazwak, wa Chuo Kikuu, labda kutaja jina nimekosea... (*Makofi*)

MHE. MBUNGE FULANI: Ndio huyo huyo!

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio huyo huyo, haikufanikiwa. Sasa kwa sababu Tume ya Serikali imeshindwa, twende sisi! Nakuja na hoja kwamba Bunge lako Tukufu liunde Tume, tukachunguze Baraza la Mitihani, hawezi kufukuza watu kila siku anavyotaka yeze na anasema wote alioawakuta pale, atawaondoa. Yeye ameshaajiri watu 180, tena habari nyingine ambazo sina uhakika nazo wanasema wote wanatoka kule anakotoka yeze, *180 people employed by her*. Sasa hatufanyi kazi namna hiyo! Hivi kama kila anayekuja anaondoa watu, mbona Mheshimiwa Jakaya hapa amewaacha Mawaziri chungu nzima, hata wengine ambao hawakumuunga mkono, lakini kawaacha. Ndio, si tunajua! Sasa atakuja Rais huyu, ataondoa, atakuja Rais huyu, ataondoa, haiwezekani! Sasa akija Katibu Mtendaji huyu wa Baraza, anaondoa, huyu anaondoa, hatufanyi kazi namna hiyo na unyeti wa Baraza la Mtihani, hauwezi kuwepo. Kama sikupata maelezo ya kweli, nitakuja na hoja ya kuunda Tume ya Bunge, kwa ajili ya jambo hilo. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hapo nitakapopata maelezo, nitakuwa na msimamo, ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hadi leo na kuwa mbele yako, mbele ya Bunge hili Tukufu, nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, kwanza ninapenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, sasa napenda kuweka hoja hii mbele ili niweze kuizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwa kweli kumshukuru, kwanza, Mama Kikwete, ambaye alikuwa mstari wa mbele katika kusaidia mambo mbalimbali katika Mkao wa Lindi katika masuala mazima ya elimu kwa wasichana. Pili Mama Naibu Waziri, Mama Mahiza, vile vile alituhurumia sana alipokuwa mlezi wa Mkao wa Lindi kwa kutusaidia mambo mbalimbali katika kupandisha masuala ya elimu hasa ya sekondari katika Mkao wa Lindi, kwa kuona kwamba kwa kweli tupo nyuma kielimu kutokana na matatizo mbalimbali ambayo Mikoa ya Kusini inayo. Kwa kweli ninapenda kuwashukuru, kwa namna moja au nyingine kwa kweli mmetusaidia sana sana. Hizo ni shukrani za dhati kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho katika shukrani na sio kwa umuhimu, ninawashukuru wananchi wa Mkao wa Lindi, katika Wilaya zake zote, Kilwa, Liwale, Nachingwe, Ruangwa, Lindi Mjini, Lindi Vijijini, kwa kunifikisha hapa nilipo nikawa mtu mbele ya watu. Kwa kweli nawashukuru sana, ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa nizungumzie masuala ya elimu. Wenzangu wengi wamezungumza mengi kuhusu elimu, wengine wamechambua kuanzia juu kwenda chini na wengine wamechambua kuanzia chini kwenda juu. Kwa kweli yote yamezungumziwa, lakini na mimi nitapita humo humo; mimi nitaanza chini kwenda juu, kwanza elimu ya awali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya awali, ni elimu ambayo ni muhimu sana, hata kama wewe ni mzazi, ni muhimu mtoto wako au mjukuu wako umfundishe elimu ya awali. Hata kule kushika peni, akavuruga vuruga tu kalamu, ile ni elimu ya awali kwa sababu unamuandaa mtoto wako kushika kalamu, kuzoea kukaa shulen, kuhesabu, kusoma na kuandika. Kwa hiyo, elimu ya awali ni muhimu sana katika shule. Mimi hili suala la kuwa na elimu ya awali katika kila shule, sasa hivi ni muhimu sana na sio suala la hiari. Tunataka kila ilipokuwa shule ya msingi, ni lazima kuwe na shule ya awali, yaani sasa ni lazima sio hiari. Kwa sababu kuna shule nyingine za msingi hawana shule za awali, sasa hiyo ni lazima kwa sababu ni maandalizi makubwa ya mtoto, kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu. Hayo yalikuwa ni maoni yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya msingi. Wenzangu waliotangulia wamezungumzia sana suala la elimu ya msingi; elimu ya msingi tuna matatizo mengi ya madaftari, madawati, madarasa afadhali yapo lakini kwa mijini. Shule zilizoongezeka ongezeka kidogo, zinaonekana kidogo zina matatizo vijijini, lakini *MMEM* wamejitahidi kujenga shule, ila sasa watoto wanapozidi kukua sasa hivi na wengine wanazaliwa, shule mpya zinahitaji kujengwa zaidi. Lakini bado tuna upungufu ya Walimu na vitabu vya kiada. Kwa mfano, sisi Mkao wa Lindi, tuna upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi 964, kwa sababu tulikuwa tunahitaji Walimu 4,257 waliopo ni 3,293, kwa hiyo, tuna upungufu wa Walimu 964.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la elimu ya sekondari. Baada ya kuanzhishwa elimu za sekondari, tuseme sekondari za kila Kata, ndipo upungufu wa Walimu ulipoanza, vitabu vya kiada, *laboratories*, mabweni na kadhalika. Hapa ndio matatizo yalipoanza kuibuka kwa sababu wanafunzi wamezidi. Sasa tunaomba sana Walimu walioajwa kwamba wataongezwa, kweli waongezwe na hawa wanaoongezwa, tunaomba sana mtusaidie katika Mkao wa Lindi, tafadhali. Kwa sababu katika Mkao wa Lindi, tuna upungufu wa Walimu 741; huo mfano wa Mkao wa Lindi tu, sijui Mkao mwingine. Mkao wetu tu mmoja ina upungufu wa Walimu 741, kwa sababu mahitaji yetu ni Walimu 1,199 waliopo ni Walimu 458. Kwa hiyo, tunaomba tafadhali Mheshimiwa Waziri, utusaidie na sisi Mkao wa Lindi, tuweze kupata Walimu hao wapya ambao wanamaliza chuo. Hiyo ilikuwa ni elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya juu. Hizi sio nyingi, sisi katika Mkao wa Lindi, tunazo shule za elimu ya juu tatu tu, tofauti na Mikoa mingine ambayo kwa kweli wanazo shule nyingi. Sisi tuna shule tatu tu, shule ya Mahiwa, shule ya Liwale na shule ya Lindi Mjini. Kwa hiyo, tunaomba tafadhali, hii shule ya Mbakenyera, Ruangwa, tuliamiwi turekebishe kitu kidogo tu, mtufikirie jamani, tumerekebisha, mje mkague muone tumefikia hatua gani, mtusogeze kidogo angalau na sisi tuweze kupata shule ya nne. Hiyo ilikuwa ni shule ya elimu ya juu, *A-Level*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo, VETA. Huu ndio ugomvi wetu wa kila siku. VETA Lindi jamani, sawa, sisi tumekubali kwamba itatengenezwa, lakini kila nikichungulia, maana ndio njia yangu ya kurudi Dodoma, kila nikizunguka bado. Tafadhalii, 45% ya watu wanaokwenda Dar-es-Salaam kufanya biashara ndogo halafu baadaye wakaitwa, samahani sana kwa kusema hivyo, wakaitwa "Wamachinga", 45% wanatoka Lindi baada ya kumaliza Darasa la Saba, nafikiri ni kwa sababu hawasomi ufundi. Sawa, tuliambiwa twende Mtwara, lakini shule za Sekondari, shule za Darasa la Saba zimeongezeka, baada ya kumaliza Darasa la Saba au *Form Four*, wanakuwa wadogo, hawana pa kwenda. Shule ya VETA peke yake ya Mtwara, haitoshi, wengine wanaachwa nje kwa hiyo wanaamua kwenda Dar-es-Salaam; wanasema potelea zote, wanakimbia wanaenda Dar-es-Salaam. Kwa hiyo, tunaomba Mkoa wa Lindi tuwe na VETA yetu, badala ya kujenga VETA za Wilayani basi wamalizie VETA za kila Mkoa, wamalizie Mkoa wa Lindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea, ukaguzi wa shule. Kwa bahati nzuri Wakaguzi wa Shule wamepatiwa vifaa mbalimbali vya kompyuta, wamepatiwa magari, lakini bado wana matatizo ya mafuta, ingekuwa kidogo wanaongezewa mafuta, hayawatoshi. Si hilo tu, ripoti za Wakaguzi zinapokwenda katika *councils* zetu hazitiliwi maanani. Ripoti zinazokwenda kwa Wakurugenzi, sasa ni nani atawawajibisha Wakaguzi? Hivi kweli zile ripoti zinasomwa zikafuatiliwa? Mbona zinakuwa nyingi au zinawekwa tu stoo? Mimi sioni kama zile ripoti zinafuatiliwa, kwa sababu zinakuwa nyingi halafu zinawekwa tu stoo. Kama ripoti za Wakaguzi zingekuwa zinafuatiliwa na kufanyiwa kazi, kwa kweli mimi nafikiri tungepiga hatua. Kwa sababu Wakaguzi wanafanya kazi nzuri ya kutoa ripoti kwamba hapa panahitajika kitu fulani, lakini ile ripoti kwa vile haifanyiwi kazi basi kila siku anatoa ripoti ile ile. Hakuna vitabu vya kiada, mwezi ujao anatoa ripoti ile ile, hakuna vitabu vya kiada, mwakani anatoa ripoti ile ile, hakuna vitabu vya kiada; mwisho Mkaguzi anaona hakuna maana ya kuandika, anaacha. Kwa hiyo, ripoti za Wakaguzi, zifanyiwe kazi, hilo ndio ombi langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamisho wa Walimu. Mwalimu anapohamishwa kutoka shule hadi shule, pale anapohama inabidi aache taarifa kwamba mimi nimehama, katika *syllabus* yangu, nimeachia kipengele Fulani ili Mwalimu mwingine anayeingia ijulikane basi ameachia wapi. Kwa sababu kuna mtindo Mwalimu anapohama anahama tu; sasa mwingine anayekuja anakuja kuanza sehemu anayotaka na yule Mwalimu anayekuja anafundisha chochote anachotaka, anachokiona yeye ni rahisi kufundisha. Kwa namna hiyo, mtoto hapati zile *skills* ambazo inatakiwa azipate ili mtihani unapokuja aweze kufaulu. Kwa sababu katika mtihani kila stadi wanatoa angalau vitu viwili, sasa yeye kama amejifundisha somo la kujumlisha tu, kwa mfano hesabu, anajifundisha kujumlisha tu mwaka mzima, miaka mitano yote kujumlisha, hajajifundisha kugawanya, kutoa, sijui kufanyaje, yeye amejifundisha kujumlisha tu, kwa kweli mtoto huyo atafeli na hatajua hesabu hata kama akiajiriwa huko ofisini anakokwenda, hatajua hesabu, hatajua kazi yoyote. Hii ndio maana wafanyakazi wetu wengi huko maofisini hawajui mahesabu; akipewa kazi anatoroka anaacha, anakwenda kutafuta ajira nyingine, hapa anaacha anakwenda pengine, kwa sababu hajui *table*, yeye ni kujumlisha tu basi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kwamba tuangalie sana watoto wetu wapate zile stadi maalum, *skills*. Walimu wache maandishi kamili ni wapi wameachia na ni kitu gani wanapaswa sasa wafundishe, kile ambacho bado watoto wale hawajafundishwa. Hiyo inahusu uhamisho kwa Walimu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili Mheshimiwa.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja 100/100. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninapenda kutoa shukrani zangu nyingi sana kwa Waziri wa Elimu, Manaibu wake wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kuchukua nafasi hii kwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Lulindi, walioniamini na kunileta hapa Bungeni ili niweze kuwazungumzia katika matatizo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza na elimu katika Jimbo la Lulindi. Kama wote tunavyojuua, elimu ni msingi wa kila kitu, elimu ndio inayotufanya tuweze kufanya mambo yote. Ni haki yetu, ya wazazi wetu na vijukuu vyetu. Basi nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Lulindi kwa juhudhi zao kubwa wakishirikiana na Halmashauri yao pamoja na mimi Mbunge wao, kuweza kujenga shule za sekondari. Hivi ninavyozungumza katika Jimbo la Lulindi, ambalo lina Kata 14, Kata zote zina shule za sekondari. Hapa ninapenda kuipongeza Wizara ya Elimu kwa juhudhi zao, kwa mchango wao mkubwa, kwa kutuwezesha na kuweza kuzijenga shule hizi za Sekondari. Pia nipende kukishukuru Chama chetu cha Mapinduzi kwa kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi kwa kiwango kikubwa na kwa maana ya Jimbo la Lulindi na kwa maana yangu mimi mwenyewe, ninaweza kusema kwamba tumefikia si chini ya 75% ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Yako mengi tumeyafanya lakini hapa sitapata nafasi ya kuyazungumzia. (*Makofi*)

Mheeshimiwa Mwenyekiti, matatizo. Pamoja na ukweli huo kwamba tumeweza kujenga shule za sekondari katika Jimbo lote la Lulindi na Wilaya ya Masasi kwa ujumla, lakini tuna matatizo yafuatayo; tuna matatizo ya Walimu, matatizo ya maabara, vitendea kazi, nyumba za Walimu na kadhalika. Tusipoyashughulikia yanaweza yakapunguza thamani ya elimu katika nchi yetu na hii itakuwa ni hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa *data* kama ifuatavyio kwa shule za Sekondari za Jimbo la Lulindi na Walimu wake. Shule ya Sekondari ya Mpindimbi yenyе Kidato cha Nne, kuna Walimu wanane tu. Shule ya Makong'ongda yenyе Kidato cha Nne, kuna Walimu wanne tu. Shule ya Namaombwe yenyе Kidato cha Nne, ina Walimu watano tu. Shule ya Namalenga yenyе Kidato cha Nne, ina Walimu watatu tu. Shule ya Mbuyuni yenyе Kidato cha Tatu, ina Walimu watatu tu. Shule ya Lulindi yenyе Kidato cha Nne, ina Walimu watatu tu. Shule ya Mkululu, yenyе Kidato cha Tatu, ina Walimu wawili na huyu mmoja ana matatizo, kwa hiyo maana yake kuna Mwalimu mmoja tu. Shule ya Chiungutwa, yenyе Kidato cha Nne na sasa tunaingia Kidato cha Tano, ina Walimu wanne tu. Shule ya Nanjota, yenyе Kidato cha Nne, ina Walimu wanne. Shule ya Lupaso, yenyе Kidato cha Nne, ina Walimu wanne. Shule ya Marika, yenyе Kidato cha Tatu, ina Walimu watatu. Shule ya Mkundi ambayo imesajiliwa hivi karibuni, bado hatujapata Walimu, vivyo hivyo kwa Sindano na Chiwata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo ndipo tunapokuja kushikwa na butwaa, mwaka jana tuliletewa Walimu 70, Mheshimiwa Naibu Waziri Mwantumu, analifahamu vizuri hilo na wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Kati ya hawa 70, waliokuja kuripoti walikuwa ni 20 tu, wengine wote wakaingia mitini. Mimi mwenyewe kwa juhudzi zangu, nilimletea majina Mheshimiwa Naibu Waziri, miaka miwili, mitatu iliyopita, wakachukue mafunzo ya Ualimu, lakini hivi ninavyosema aliyerudi na kufundisha katika shule zetu hizi ni mmoja tu. Nilikuja hapa nikamuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, wale vijana wangu wako wapi? Wakasema, wamenijibu hivi, hatukuwekeana mkataba na ndio maana tumeamua kwenda katika maeneo mengine. Hii maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba shule zile zibaki bila Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba basi, Wizara ya Elimu, isilione hili kama ni jambo la kawaida; iandae utaratibu mzuri utakaofanya ama utakaosaidia kuwafanya Walimu hawa wanapopelekwa katika shule hizi wasitukimbie. Wenzangu hapa wamezungumza, naomba suala la elimu katika Mikoa ya pembezoni, litiliwe mkazo sana na hili Mheshimiwa Rais, mwenyewe amelizungumzia. Tusipofanya hivyo, tofauti ya elimu itazidi kuwa pana na matokeo yake wingi wa vijana wanaokimbilia Dar-es-Salaam, mkawapa majina haya ambayo wengine hatuyapendi sana, itaongezeka. Tena basi wamejengewa jengo pale linaitwa "Machinga", lakini ukienda pale sidhani kama Wamachinga wenyewe watalipata jengo lile. Naomba sana suala hili litiliwe mkazo, nakuombeni sana; wale ambao wanapangiwa nenda kafundishe sehemu fulani, hasa Mikoa ya Kusini, wanapokimbilia wapewe adhabu. Tusipofanya hivyo, kila siku tutakuwa tunapiga kelele, mtatuona watu wa ajabu lakini huo ndio ukweli, Walimu hawataki kuja kufundisha kule kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie, sisi watu wa Mikoa ile sasa tuna mwamko mkubwa sana wa elimu. Juzi, nilifanya mikutano katika baadhi ya maeneo, wako tayari kufuata utaratibu wa wenzetu wa Rukwa, wajenge nyumba za Walimu na vivutio vingine, kwa hiyo, ninawaomba wasiwe na wasiwasi waje kufundisha Mtwara, waje kufundisha Lulindi, tena kuna korosho nyingi tu kule na korosho ni tamu sana. Huo ni kwa upande wa Walimu katika shule zetu za sekondari, katika Jimbo la Lulindi na Mkoa wetu wa Mtwara kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ninapenda kuzungumzia kitu ambacho wengi wetu hatukizungumzi, lugha ya kufundishia. Hii sio mara yangu ya kwanza kuzungumzia suala hili, ninajua baadhi yetu hawalipendi, lakini huo ndio ukweli, lugha ya kufundishia ni tatizo katika nchi yetu. Ni tatizo kwa sababu bado mpaka hivi sasa tunadhani kwamba Kingereza ndio lugha nzuri ya kufundishia mpaka Chuo Kikuu. Mimi nataka kutoa mifano, mimi nimesoma Urusi nimesoma Kirusi, nimesoma Bulgaria nimesoma Kibulgaria, nimekaa China miaka mitano, elimu yao wanaipata katika Kichina. Kuna kipindi alikuja mawanafunzi kutoka Tanzania, anachukua *Masters*, akaambiwa hivi, wewe umekuja kusoma hapa unataka taaluma ya maji, lakini Profesa mwenye uwezo kiasi hicho hajui Kingereza, wewe kama unataka mtafute kijana ambaye amemaliza Kichina akakutafsirie. Wako vijana China kule wanaomaliza masomo yao hawataki kurudi nyumbani. Akamtafuta akampata, wakati unapofika anakwenda kwa yule Profesa, anaitwa hivyo hivyo Profesa kama tunavyoita sisi tunaozungumza Kingereza, alikuwa anapata elimu nzuri kweli kweli; yule kijana nimerudi hapa ndio Mtaalamu wa Maji kule Kilimanjaro, anatoka Mara. Huo ni mfano wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili, siku moja tulialikwa na Mjeruamani, akatuuliza ninyi Watanzania, hiki Kiswahili mnakitumia mpaka wapi katika elimu? Tukamwambia kadri tunavyokwenda juu tunakiacha, alicheka karibu apasuke mbavi. Akasema ninyi mnafanana na Wa-Hungary, ambao sisi tuliwatawala wakataka kutumia Kijerumani wakajikuta wanakwenda hatua ndogo katika elimu, wakaamua kutumia Ki-Hungary chao, wakapiga hatua kubwa na ndio wale ambao wamekuja kutengeneza maikarusi huku kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni hivi, katika dunia hii hakuna lugha ya elimu, kuna elimu, lugha ni ile ambayo wenyeji wenyeewe wanaielewa. Huwezi kwenda Ufaransa ukamwambia kwamba soma katika Kingereza, hakuelewi, huwezi kwenda Urusi ukamwambia soma katika Kingereza, hakuelewi. Huwezi kwenda Bulgaria ukamwambia soma Kingereza, hakuelewi na ndio hawa wataalamu wanakuja kutufundisha sisi hapa, mimi ninaomba tujiamini katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kabisa, kwa taasisi ile ya taaluma ya kuendeleza lugha ya Kiswahili ilioanzishwa pale Chuo Kikuu. Naomba basi Wizara ya Elimu, kwanza itoe msaada mkubwa kwa Taasisi ile ili iweze kufanya kazi yake vizuri, tufike mahali lugha hii ya Kiswahili tuitumie katika elimu ya juu ili vijana wetu waelewe elimu, wasikariri. Kinachotokea sasa hivi, vijana wetu wanakariri, hawakielewi Kingereza kama nilivyosema mwanzoni, najua wengine hili hamlipendi lakini ukweli utabaki hivyo. Vjana wengi wanakwambia bwana hili somo mimi ungeniambia Kiswahili, ningeweza kulizungumza vizuri. Sasa naiomba Wizara ya Elimu, ile ya kupigapiga mateke mnapoambiwa kwamba tutumie Kiswahili katika elimu, hebu kaeni chini, saidianeni na ile Taasisi ya Chuo Kikuu, itazame uwezekano wa kutumia Kiswahili katika Vyuo Vikuu ili vijana wetu wapate elimu ya kutosha, walete maajabu katika nchi hii; inawezekana, kwanza Kiswahili kina haki.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa kengele ya pili.

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii ya muhimu sana nchini.

Awali ya yote, ninapenda kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo, kwa jitihada kubwa inayozifanya kuweza kufundisha watoto wetu waweze *ku-fit* kwenye karne hii ya 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza Walimu wote ambao wanafundisha kwenye Jimbo langu la Musoma Vijijini, kwa hali ngumu kabisa, kwa kutokuwa na vitendea kazi na kwa kuwa wachache sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizi, ninapenda kujikita kwa suala zima la elimu, ni maoni yangu kwamba kitu fulani kimekwenda potofu, tunapofundisha watoto, tunawafundisha wafanye nini? Nikiwa Jimboni kwangu, huwa napenda sana kuliuliza swali hili kwa wanafunzi, je, mnasoma ili mfanye nini? Wao wanasema tunasoma ili tupate ajira. Nawaambia lakini nani atakupa ajira maana mashirika makubwa tuliyokuwa tunayaendesha kitaifa tumeshayauza na tumewauzia hawa Wazungu ama Wahindi na wao wanaajiri Wahindi ama Wazungu wenzao. Sasa atakayekupa kazi ni nani maana Serikali imejitoa kwenye hizi *commanding post* na waliochukua wao wanatumia lugha za kwao kuendesha viwanda hivi. Yale mabenki yamekwenda kwa Waingereza ama Wahindi, tuliyatoa, sasa ajira nani atampa Mtanzania, hili ni jambo kubwa sana la kulifikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uhai wake Mwalimu, yeye alikuwa anajaribu kusisitiza tuwe na elimu ya kujitegemea, ukiwa vijijini uweze kujitegemea lakini *syllabus* zetu mpaka mijini ni kwamba ukimaliza Chuo Kikuu pengine utapewa kazi kama una bahati na kule kujitegemea hakuko. Napenda tuijulize kabisa, tunaipeleka nchi hii wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *syllabus* ya Waingereza ilikuwa na maana yake, kulikuwa na shule za Serikali na shule za *wa-missionary*, vijana wetu waliokwenda kwenye shule za Serikali ndiyo viongozi waliotuwezesha tukapata uhuru huo. Hawa ndiyo waliotusaidia lakini leo cha kushangaza shule za sekondari hazina heshima tena, zenye heshima ni shule za Kanisa ama shule za watu binafsi, kwa nini Serikali imefanya namna hii? Wenzetu waliokuwa *colonized* kama sisi kwa mfano India mpaka leo shule za heshima ni shule za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina uwezo mkubwa sana wa kuziboresha shule, inao uwezo mkubwa kuliko *private individual*, lakini utakuta hata sisi viongozi tunapenda kuwapeleka watoto wetu *private schools* sio za Serikali, tunakwenda wapi.

Ninadhani kwamba Serikali ina mpango maana ndiyo inayofanya *planning*, tunakuwa na Madaktari wetu pengine 500 mwaka huu mwaka mwingine itakuwa hivyo hivyo, wana-*plan* kwa makusudi na hawa tuliowafundisha waweze kuisaidia Serikali kuendesha kazi lakini sio hivyo leo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za dini zina madhumuni yake ziko pale kwa mwelekeo fulani sio sawasawa na Serikali, shule za *private* pia zina maana yake, lakini shule za Serikali zinafanya nini? Hilo ndiyo swali kubwa lililopo kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeanzisha shule hizi za Kata. Napenda kuchukua nafasi hii kwa kweli kumpongeza Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi nzuri aliyoifanya kuhakikisha kwamba shule ziko kila Kata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwangu pale wakati nakuwa Mbunge zilikuwa shule nne tu za sekondari, lakini leo tuna zaidi ya shule 35 na shule zingine ni nzuri sana, lakini tunapata tena matatizo pale. Hizi shule kwa kuwa hazina dira, hazina *vision* wanakwenda wanafundisha wanafunzi wa aina gani, sayansi hazina na wala hakuna mpango wowote kusaidia kuwezesha vijana wetu wasome sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu hizi zifuatazo; tulipoanza tulikuwa tunasema shule zitakuwa pembeni halafu zile shule nyingi za Kata za vijijini hazina umeme pengine za mijini lakini mpango wa Serikali ni kwamba ifikapo mwaka 2015 lazima kila kijiji kiwe na umeme na kina mawasiliano, ndiyo *plan* ya nchi, sioni tunakwenda huko, tukifanya hivyo basi zile shule za Kata zitakuwa kama *post office*, maana kukiwa na umeme kutakuwa na *internet* kwa shule ya sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya vitabu yamepitwa na wakati, navyoelewa, majirani zetu zimepitwa na wakati, lakini tukisema basi kila shule na kila Kata ina sekondari lakini Walimu hawapo, wa kufundisha sayansi wala wa kufundisha lugha. Ukiona wanavyoongea lugha leo, Kiingereza sio lugha ya Kiingereza wanasema ni Tanzania *English*, lakini pia kuna lugha zingine ambazo ni za muhimu ki-*train* kama vile lugha ya Kifaransa. Wenzetu hapa majirani, ukichukua Rwanda, Burundi wanafundisha lugha zote na kwenye soko la ajira hawana matatizo, sisi Watanzania tukienda kwenye soko hilo tutashindwa kupata ajira kwa sababu lugha yetu ni hii moja eti lugha ya Kiingereza, Kifaransa hatujui, tunafika wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri kwanza kabisa tu-*identify* shule za sekondari, shule ambazo Serikali itapeleka vijana wao ambao hapo mbele watakuwa Madaktari, watakuwa ma-*Engineer*, watakuwa Walimu ili waweze kukidhi mahitaji ya Serikali yale ya wananchi wa kawaida basi wanaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni vigumu ku-*burn* kwa mfano shule yoyote ya *private* ambayo haina vifaa maalum wafungiwe leseni mpaka watakapopata, aidha lazima kuwe na sayansi *lab*, ndiyo wanaweza kupata kibali cha kufungua shule. Hatuwezi kuwa na shule kazi yake ni kuuza elimu, unafanya *profit on education*, hatuwezi kufika hivi, lazima tuwe na *priority* ya kufanya, lazima tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukianza kuona Walimu tulionao, mimi pale kwangu nilijaribu kujenga shule nzuri kabisa, nikawaweka Walimu wakae pale, baada ya miezi miwili wote wakakimbia, kwa sababu mshahara wao ni mdogo sana hauwezi kukidhi mahitaji ya kuweka *bulb* ikivunjika, haiwezekani. Kwa hiyo, Walimu wetu wanashindwa kukaa hata kwenye shule nzuri tunakwenda wapi, kwa elimu ya kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo kile cha *repair and maintenance*, ukiona Wizarani hakuna kabisa fungu ambalo limetengwa kuweza kukarabati shule za zamani, ukiona bajeti ya leo, ukiona *speech* ya Waziri hakuna, je, hivi majengo yakianguka au yakinaka kuanguka ama wakinaka kukarabati watatumia fungu gani kama hakuna fungu lililotengwa kwa ajili hiyo? Jengo kama hili bila shaka kuna *provision* ya kufanya *maintenance* lakini shule zote hizi hazina *provision* ya namna hiyo. Tulikotoka walikuwa nazo, ukienda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hata jiko likiharibika hakuna *repair* na ndio inakuwa *standard* za kila shule za Serikali, tunakwenda wapi? Ninashauri, Wizara ya Elimu itenge kiasi cha fedha za kuweza kukidhi mahitaji ya *repair* na *maintenance*, vinginevyo baada ya miaka 20, hizi shule zote zitakuwa zimepotea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushauri tena lazima tuwe na sehemu ya kuwafundisha watoto wetu angalau tabia njema, maadili. Shule zetu zote hazifundishi maadili lakini sisi ndiyo tunasema kuna mafisadi, mafisadi, hawa vijana wetu tumewafundisha ujisadi ni nini, hatujafanya hivyo! Wenzetu nadhani Waislam wanabahati kweli, wanawapeleka watoto wao kwenye Madrasa kuwafundisha maadili, hizi shule za Kata nani anawafundisha maadili watoto wetu, ni wazazi wao, je, tutafika kule tunakokwenda? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za *kindergarten* zingeweza kufanya hivyo. Nimesikia Mbunge mwenzangu hapa anachangia shule za awali, Wajerumani wanaita *kindergarten*, vijijini hakuna *kindergarten*, mtoto akizaliwa akiwa amefika umri fulani anakwenda moja kwa moja darasa la kwanza, la pili, la tatu, la nne la tano, bila maadili. Wazazi wake wenyewe walikuwa wanamwambia kwa mfano, anayewafundisha maadili ni nani, hakuna sayansi hakuna maadili, kweli tutafika tunakokwenda? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naunga mkono mia kwa mia. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mkono, mchango wako kwa kweli umekuwa ni mahiri, ningependa kukuongeza muda lakini haiwezekani.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza na mimi naungana na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha muda huu, tukiwa katika hali ya usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia masikitiko yangu, napenda kuyakita zaidi kwa Walimu, kwa kweli Walimu wana hali ngumu sana ya maisha ukizingatia mishahara yao haitoshelezi, vitendea kazi na mazingira wanayoishi wakiwa humo mashulenii, kwa

kweli ni magumu. Kuna Walimu wanaishi katika sehemu ambazo hazina hata nyumba, kwa kweli kama utaenda vijijini, utasikitishwa ukiona maisha ya Mwalimu anavyoishi. Wakati mwingine hali ya Mwalimu anashindwa hata na mwanakijiji ambaye hafanyi kazi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iwafikirie Walimu kuwainua kimaisha wawape mshahara ambao utakidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma, watu wengi walipenda kujiunga na Ualimu, kutokana na hadhi waliyokuwa wakipata Walimu, mishahara ilitosheleza na hali ya maisha ilikuwa inaridhisha. Leo watu wanaukwepa Ualimu kutokana na hali ya maisha na ugumu wa maisha walionayo Walimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia kuhusu shule za msingi, shule za msingi zina matatizo ya Walimu na kwa kawaida msingi unapokuwa imara basi huko juu kunakoendelea vile vile kutakuwa imara. Ni sawa sawa na unapojenga nyumba ya ghorofa, ikiwa msingi utakuwa mbaya basi hali kadhalika ile nyumba itakuwa haina msingi ulio bora na hatimaye nyumba ile ya inaweza ikaporomoka kama tunavyoona maghorofa yanayoporomoka katika jiji la Dar es Salaam ambayo yamekosa msingi ulio mzuri. Sasa tutakapomuanda mwanafunzi, kuanzia msingi, tukimpa elimu bora, kwa kweli mwanafunzi huyo mpaka atamaliza elimu yake ya sekondari hadi chuo kikuu anaweza kuwa ni mwanafunzi ambaye amepata elimu iliyo bora. Lakini mwanafunzi tutakapokuwa tumempa elimu ambayo ni duni, kwa kweli mwanafunzi huyo naye vile vile ataendelea hivyo hivyo tu mpaka anamaliza elimu yake atakuwa hajafanikiwa na kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kuhusu jinsi gani Walimu wanajituma lakini pia bado wanaonekana hawafanyi kazi. Kwa kweli Walimu wanapokuwa katika mazingira hayo magumu wanajituma, lakini utakuta wakuu wengine wa Wilaya kama tulivyoshuhudia Bukoba, wanaamuru Walimu wapigwe viboko. Hivi jana nimesoma katika gazeti la majira, Mkuu wa Wilaya fulani ambayo sitaki kuitaja hapa, ameamaru eti Walimu wazomewe kutokana na uzembe. Mimi nasema kuwaita Walimu wazembe, ni kosa sana tena ni kosa la jinai. Mwalimu hawezi kuwa mzembe. Tatizo Mwalimu anaonekana hafanyi kazi kutokana na kwamba hana vitendea kazi, Mwalimu atafundisha wakati hana vitendea kazi, atafundishaje, wakati darasa lina wanafunzi 80, 100 mpaka 120? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida Mwalimu anatakiwa afundishe wanafunzi wasiozidi 40 mpaka 45 sasa wanafunzi 80 au 100 au 120, Mwalimu huyo atakuwa na muda saa ngapi wa kutoa somo lake, atakuwa na muda gani wakuzunguka kuangalia wanafunzi wamefanya vipi kazi aliyoitoa na atakuwa na muda gani wa kusahihisha kazi yao. Sasa mimi nachosema lawama asitupiwe Mwalimu lawama itupiwe Serikali ambayo ina tatizo la pesa kwa ajili ya kujenga madarasa ya kukidhi wanafunzi wasome lakini Mwalimu hana lawama. Mwalimu anafanya kazi yake katika mazingira magumu, ukizingatia Mwalimu huyo huyo ni mlezi kwa sababu mzazi anapomtoa mtoto wake nyumbani utakuta Mwalimu yule anashinda na mtoto yule asubuhi mpaka jioni. Mwalimu anakuwa ni Mwalimu, anakuwa ni mlezi au mzazi na wakati huo huo anakuwa hakimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi nyingi sana huko shulenii, Walimu ndio wanaziamua na mambo mengine mengi. Sasa Mwalimu huyo huyo utakapomweka katika mazingira magumu, kwa kweli una mchanganya na wakati huo huo anapotoka kazini anatakiwa akajitafutie riziki zake na riziki hiyo pengine akaitafute pesa maana hana za kutosheleza. Kwa hiyo, Mwalimu anakuwa anachanganyikiwa jamani, tunaiomba Serikali iwasaidie sana na iwaangalie sana Walimu, ukizingatia wengi wana malimbikizo wanayoyadai kutokana na malimbikizo ya mishahara, wengine wametibiwa hawajalipwa matibabu yao, wengine wanakwenda likizo hawajalipwa likizo zao. Kwa hiyo yote yale yanachangia pia kuleta uduni wa elimu, kwa sababu Mwalimu anaamua afadhali akafanye kazi zake nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine utakuta kuna baadhi ya Wilaya hazina vipaumbele kama tulivoambiwa katika bajeti hii ya mwaka huu kipaumbele cha kwanza ni kilimo kwanza, ni sawa kilimo kwanza, lakini utakuta na Halmashauri zingine pia hazitoi vipaumbele kwa baadhi ya Halmashauri zao. Nikizungumza hivyo nina mfano hai wa Halmashauri yangu ya Jiji la Tanga. Halmashauri ya Jiji la Tanga, katika kutoa vipaumbele safari hii walipokuwa katika bajeti yao kipaumbele chao wamekielekeza kwenye Tanga televisheni. Tanga televisheni, imepewa shilingi milioni 80, lakini elimu imepewa shilingi milioni 25, hebu tuangalie jamani tunakwenda wapi, kama jiji, habari kweli tunazitaka kuzipata lakini hatuna umuhimu huo kuliko elimu. Mwaka uliopita, elimu Tanga ilipewa shilingi milioni 100 na bado wanafunzi kadhaa waliweza kubaki kutokana na uchache wa madarasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanga kweli tunataka habari lakini ziko televisheni nyingi kuna *ITV*, *Star TV*, *TBC*, sasa *Channel Ten* na nyingine nyingi, sasa shilingi milioni 80 inakwenda kupewa Tanga TV. Jamani kama watu wanavyosema Tanga kuna na mimi nasema kunani hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nalopenda kuzungumzia ni wanafunzi wanatokea katika familia zilizo na kipato duni. Napenda kuishukuru Serikali kwa kuwasaidia wale wanafunzi amba wanaishi katika mazingira magumu na wenye kipato duni. Kwa kweli Serikali inawasaidia sana kuwalipia ada, lakini hali kadhalika utakuta katika Halmashauri nyingine wanaolipiwa ada, wengi wao ni watoto wa watu wenye uwezo wale amba hawana uwezo wananyimwa fursa ile ya kulipiwa ada. Kwa hiyo, tunaomba pia Wizara ihakikishe inapitia au Halmashauri inapitia kuhakiki, watoto wanaolipiwa amba wazazi wao wanavipato duni, je, kweli wazazi wao wana vipato duni au tunawasaidia watu amba wanavipato na wale wenye vipato duni hawapati elimu na ukizingatia wakati mwingine wale wenye vipato duni akili zao ni bora zaidi kuliko hao waliotoka kwenye familia amba zina kipato? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michango, kwa kweli mimi kila wakati ninapochangia ninazungumzia kuhusu michango mbalimbali wanayotakiwa wanafunzi walipe ikiwemo maji, mlinzi, michango ya mitihani na kadhalika. Ni sawa kuchangia elimu, tunatakiwa wazazi kama wazazi tuchangia elimu, lakini inapobidi basi mzazi ashirikishwe zaidi kuliko mwanafunzi. Sasa hivi imekuwa ni tabia hasa katika baadhi ya

shule nyingi za Jiji la Tanga, kila wakati watoto wanarudishwa nyumbani kwa kosa mchango wa mlinzi, mchango wa jengo la darasa na michango mingine mingine, uji na kadhalika. Sasa mtoto yule hana makosa, mwenye makosa yale ni mzazi, si bora kumrudisha mtoto Yule!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, mtoto kama hana ada au hana mchango wa aina yoyote, mzazi mhusika aandikiwe barua, aitwe shulen i pale azungumze na Walimu na aweke mkataba kwamba mimi mpaka siku fulani nitaweza kuchangia pesa hiso. Lakini watoto wanarudishwa na matokeo yake utakuta watoto wanazagaa mitaani na ndiyo chanzo cha mimba za utotoni kwa sababu mtoto akifika nyumbani mama anamrudisha arudi shule, akifika shule Mwalimu anamrudisha arudi nyumbani. Sasa naomba kama itawezekana, Wizara iandae *secular* maalum ya kuwaomba Walimu wasiwarudishe wanafunzi kwa kukosa michango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia kuhusu Walimu ambao wanapewa ajira sasa hivi. Kuna baadhi ya Walimu ambao wanaajiriwa, wanachelewa sana kupewa mishahara yao. Kuna Walimu toka mwaka 2008 mpaka leo hawajalipwa mishahara, *arrears* zao. Kwa hiyo, tunachoomba sisi wapewe malimbikizo yale maana hii pia ndiyo kichocheo kikubwa kinachomfanya mtu akatae kazi hii, kwa sababu halipwi kwa wakati na hata huo wakati wenyewe ukifika pesa zake hazipati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumalizia kwa kusema, nachoomba Walimu shulen iwasipewe ukada wa vyama, kwa sababu wanapopewa ukada badala ya kuangalia shughuli za ufundishaji yeye anazama zaidi katika suala zima la Chama fulani. Wakati huo huo utakuta anaweza pia mwanafunzi akishabikia Chama fulani akamrudisha au akamuadhibu kutokana na kushabikia Chama Fulani. Kwa hiyo, tunachoomba, Walimu wahakikishe wanazama zaidi katika masomo au wachague aidha kama anataka ukada yeye abaki kwenye Chama ashughulike na ukada, la hataki ukada aendelee kufundisha ili watoto wetu waweze kupata elimu na elimu iliyo bora zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa yote, napenda pia kusisitiza kwamba Walimu wote wale ambao wanadai malimbikizo yao ambayo hapa mimi nina takwimu inayoonyesha Wilaya zote za Tanzania Bara kuna Walimu wanaodai malimbikizo yao ya mishahara ikiwemo matibabu pamoja na likizo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kama ilivyoahidi basi ihakikishe Walimu hawa wanapewa pesa zao ili waweze kufanya kazi hii kwa ufanisi na watoto wetu waweze kupata elimu ambayo itakidhi ili tuweze kupata wanafunzi ambao watatusaidia. Wakati sisi Tanzania tunasema tunataka kujitahidi kupata wanafunzi wengi katika somo la sayansi, ikiwa hatuna Walimu wa kutosha, ikiwa hatuna maabara, ikiwa hatuna vitendea kazi vingine, kweli tutawatoa wapi wanafunzi ambao watachukua masomo ya sayansi? Kwa hiyo, tunachoomba, tutafute mbinu za kuwalipa Walimu ili waipende kazi yao na waweze kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. JOYCE M. MASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwanza kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza, kumpongeza sana Waziri wetu kwa hotuba yake nzuri sana ambayo ameitoa pamoja na Manaibu wake niwashukuru sana, lakini vilevile pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii. Kwa kweli hotuba yao ni nzuri na kweli nimeifuatilia na mimi nimeipenda nasema ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kabla sijaanza, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza sana mama yetu, Mama Salma Jakaya Kikwete, kwa kazi nzuri anayoifanya kwa *NGO* yake ambayo inaitwa WAMA. Yeye kama Mwenyekiti, kwa kweli anajitahidi na juzi tulikuwa naye Mwanza, Shinyanga na Tabora, anakemea sana mimba za utotonii. Kwa kweli tunachukua nafasi hii kumshukuru na mimi nasema aendelee na kazi hiyo na Mungu amjalie. Nilikuwa sijui maana ya WAMA lakini alivyotutembelea, nimejua. Kwa hiyo, nasema kazi ni nzuri na Mungu amjalie na aendelee kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nichukue nafasi hii nizungumze kuhusu maslahi ya Walimu, Walimu wamekuwa na mgogoro mkubwa wanagoma na wanafanya mambo mengi. Lakini mimi nimejiuliza hivi kwa nini tusiwe na chombo kimoja ambacho kinamhudumia Mwalimu? Walimu wamekuwa wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwalimu lakini zamani tulikuwa wachache. Lakini sasa ni wengi mno, wanahudumiwa na Wizara ya Elimu, Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Utumishi na Wizara ya Fedha na Uchumi. Wizara zote hizo nne Mwalimu lazima azipitie, hivi kwa nini Wizara ya Fedha na Uchumi na Hazina, zisichukue hizo pesa zikapeleka TAMISEMI wakashughulikia hao Walimu moja kwa moja? Ashughulikiwe na Wizara yake ya Elimu na TAMISEMI, Wizara ya Utumishi na Fedha na Uchumi wapumzike waendelee na watumishi wengine, Walimu ni wengi mno. Mbona Wanajeshi wanashughulikiwa na kundi lao wenyewe tu lakini hatujasikia hata siku moja wanagoma? Naomba Waziri akae vizuri afikirie jinsi gani Wizara yake ya Elimu na TAMISEMI pekee itawashughulikia Walimu kwa madai yao yote wanayodai na kila kitu, kuwe na chombo pekee kinachoshughulikia masuala ya Walimu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye michezo. Kilio kina mwenyewe na mwenyewe ni Wizara ya Elimu. Wametangaza kwamba sasa michezo shulenii imeanza lakini mimi naona imeanza kwa nadharia tu, michezo hatuioni kama zamani walivyokuwa wanacheza UMISETA na UMISHUMTA. Mimi nasema naomba Waziri wa Elimu aanze kulia yenyewe na sisi tutaitikia kilio, vipaji hivi vyote vinatoka katika shule za msingi, sekondari na vyuo, sasa kama michezo hakuna mashulenii hivyo vipaji vitatoka wapi? Rais wetu anahangaika kuleta makocha, watafundisha wakina nani wakati vipaji havipo? Tunaomba Waziri wa Elimu aone sasa hii kazi ni yake na atenge fedha nyingi ili watoto wacheze na tuwaone wenye vipaji swaende mbele wafundishwe na makocha wa kimataifa na chuo tunacho kule Malya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu mishahara ya Maafisa Elimu wa Mikoa. Kama huna habari, hapo ulipo Maafisa Elimu wa Mikoa wanapokea mishahara midogo, Maafisa Elimu wa Wilaya wanapokea mishahara mikubwa. Hata ungekuwa wewe, hivi unaweza ukamtuma mtu kazi wakati mwenzako ana mshahara

mkubwa kuliko wewe? Hii yote imetokana na maboresho yaliyofanywa katika miaka ya 2000 iliwaondolea hadhi Maafisa Elimu wa Mikoa na kuwaita Washauri wa Elimu wa Mkoa hivyo kuwafanya wabakie na mishahara midogo. Sasa hata kama yule Afisa Elimu wa Mkoa anakuwa na nung'uniko kwamba yeze anapokea mshahara kidogo lakini Afisa Elimu wa Wilaya anapokea mshahara mkubwa, hivi ina maana gani? Hawana maana kuwa Maafisa Elimu wa Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi namuomba sana Waziri wetu wa Elimu awaangalie sana hawa Maafisa Elimu wa Mikoa kama haiwezekani na vyeo havipo basi wawe Ma-RAS wasaidizi waongezewa mishahara. Afisa Elimu wa Wilaya ana gari na kadhalika lakini Afisa Elimu wa Mkoa hana, hivi kweli unamtumaje kazi mtu kama huyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, tunaomba muwaone hawa Maafisa Elimu wa Mikoa kwamba wana kazi ngumu na sasa hivi ndiyo Walimu wote wameshapelekwa kwenye Halmashauri, kwa hiyo, wao ndiyo wanashughulikia. Tunaomba muwasaidie kwa kuwapa kila kitu kwani huu ni uonevu kwa Maafisa Elimu wa Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie habari ya Idara ya Ukaguzi wa Shule. Naomba hadhi ya Ukaguzi wa Shule sasa irudi kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Kama tunataka elimu iwe kama tunavyotaka basi Wakaguzi wawepo wa kutosha. Katika kitabu hiki nilichosoma, Wakaguzi wa Sekondari wametengwa katika Kanda. Kanda ni kubwa mnao hiyo imeshafeli, mimi naomba yafuatayo; Wakaguzi wawe wa aina mbili, Wakaguzi wa Shule za Msingi wawe wengine na Wakaguzi wa Shule za Sekondari wawe wengine lakini wawe palepale Mkoani siyo kwenye Kanda kwani kwenye kanda ni mbali mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue tu Mkoa wa Shinyanga, tuna shule 255 za Sekondari, hivi kweli hizo Shule za Sekondari huyo Mkaguzi wa Kanda aende Tabora, Kigoma halafu aje kwetu Shinyanga, huo utakuwa kweli ni ukaguzi? Tunaomba Wakaguzi wawe wa kutosha na muwaangalie basi hao Wakaguzi vigezo vyao vikoje na huyo Mkaguzi asiwe anaangalia kwamba mpaka aalikwe ndiyo aende kwenye hiyo shule. Wakaguzi wa zamani walikuwa wanavamia shule, unavamia shule unakwenda darasani, unakaa pembeni unamsikiliza Mwalimu anavyofundisha, unaangalia andalio, unaangalia na madaftari ya watoto. Tunaomba Wakaguzi wasikae maofisini bali waende shulenii waangalie kazi za Walimu zinavyofanyika na ofisi zao ziwe nzuri na wapewe magari isije ikawa Mkaguzi anakwenda na baiskeli jasho linamtoka anafika pale anakuta Mwalimu wa shule ya msingi amepaki gari halafu yeze anakuja na jasho linamtoka, haina maana yoyote. Wapeni magari wafanye kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niingie nyumbani Shinyanga. Naomba nichukue nafasi hii, niwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Shinyanga. Katika Awamu hii ya Nne, mwaka 2006 tulikuwa tuna shule 102 za Sekondari, lakini mwaka 2007 tumejenga shule mpya 117 na kufika 219, mwaka 2008 tumejenga shule 31 tukawa na jumla ya shule 250, mwaka 2009 tukajenga shule tano jumla zimekuwa 255. Naomba

kuchukua nafasi hii, kuishukuru sana Serikali kwa kutusaidia na hasa niwashukuru wananchi wa Shinyanga kwa hali na mali kwa kujenga shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi naomba niwaombe wananchi wa Shinyanga kwamba tumejenga shule nyingi lakini nyumba za Walimu bado tunasuasua. Basi ikifiki muda tunaomba tusaidie tena ili Walimu wetu wakae kwa raha mustarehe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia kuhusu uhaba wa Walimu. Mkoaa wa Shinyanga tuna uhaba wa Walimu lakini mwaka huu tunashukuru kwa shule za msingi tumeletewa Walimu 1,846 lakini kwa masikitiko Manispaa ya Shinyanga tumepewa Walimu 15 tu lakini tunaambiwa Walimu 15 hao warudi. Mimi naomba hawa Walimu 15 wasirudi waendelee kufundisha katika Manispaa ya Shinyanga kwa sababu zifuatazo; kwanza tuna upungufu wa Walimu 331 na hapo hapo tuna Walimu 44 ambao ni wagonjwa. Sasa hao wakirudi itakuwa balaa tupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia kuhusu matibabu ya Walimu nje ya nchi. Namshukuru sana Ndugu yangu Mheshimiwa Margreth A. Mkanga. Mheshimiwa Mkanga amezungumza lakini mimi nina *data* na hizi *data* vijana naomba waje kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mwalimu mmoja wa shule ya msingi anaitwa Richard Yared Mpongo, huyu Mwalimu alikuwa na macho mazuri lakini baadaye macho yale yakapofuka. Sasa baada ya matibabu tarehe 30/12, Muhimbili wakamwambia aende India akatibiwe, amekaa huko mwezi mzima mpaka tarehe 27/1/2005. Lakini wakati alipokuwa huko wenzake wote walikuwa wamepewa dola 500 za kujikimu, lakini yeye akaambiwa atapewa na Mwajiri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa masikitiko na huyo Mwalimu ananisikiliza huko alipo, toka mwaka 2004 mpaka leo huyo Mwalimu hajalipwa hizo pesa. Hivi ananiambia, Mheshimiwa Mbunge hebu nenda kaniulizie ili Spika naye asikie jinsi walemavu tunavyoonewa, ninaonewa kwa sababu sioni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri aniambie huyu Mwalimu Richard Yared Mpongo analipwa na nani ili ajue na aende akadai na ninaomba hizi karatasi kijana aje kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nasema hivi, mimi nilikuwa Mwalimu, najua Walimu wanavyohangaika na ninawapenda sana lakini nataka niwaambie kwamba Waziri ameshasema, Wabunge hapa tunasema mnatusikia, tunawaambia hivi, kugoma hakuna maana, fedha zao zote watalipwa na sisi tutaendelea kuangalia kwamba kweli wanalipwa ila tunasema tunaomba na wenyewe wawafundishe watoto wetu kwa moyo wao wote kwa sababu na wao wasingefundishwa wasingegekuwa Walimu mbona Walimu wa zamani hawakugoma? Kwa hiyo, tunaomba na wenyewe wafanye kazi kama inavyotakiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi, katika Wizara hii, hapo awali kulikuwa na Wizara ambayo ilikuwa inashughulikia shule za msingi na sekondari na nyingine ikawa ya Sayansi na Teknolojia kwa sababu ya vyuo vikuu lakini sasa vimeunganishwa ila tunaona jinsi shule za msingi zilivyo nyingi, shule za sekondari tunazijenga sana, vyuo vikuu vinajengwa mno, vyuo vyaa kawaida vinajenga mno, ninasema, pamoja na kwamba imeunganishwa lakini nashauri hapo baadaye vitengenishwe ili kazi iende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joyce Masunga nakushukuru sana kwa mchango wako mahiri kabisa na ninaomba niseme nimepokea *document* hii na itakabidhiwa kwenye ofisi husika ili iweze kufanyiwa kazi kwa mujibu wa maelezo ambayo umeyatoa hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu ya leo na muda tuliokuwa nao umefikia ukomo, ila naomba tu niseme tutaendelea na uchangiaji huo kesho na mchangiaji wetu wa kwanza kesho atakuwa Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhan Maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nitoe majibu ya mwongozo yaliyowasilishwa leo asubuhi kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7) iliyotumiwa na Mheshimiwa Diana M. Chilolo na Mheshimiwa Naibu Spika alizingatia ufanyaji wa maamuzi ya mwongozo huo kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (4) ambacho kinampa mamlaka Spika ama kutoa maamuzi ya mwongozo ama hoja yoyote wakati huo huo ama kutumia muda mwininge wa ziada ili kuweza kupata majibu sahihi ya mwongozo wowote ambaa utakuwa umewekwa Bungeni.

Sasa baada ya tuko hilo la leo asubuhi, maamuzi ya kikao cha dharura cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika tarehe 23/3/2009 hapa Dodoma katika ukumbi wa Mheshimiwa Spika yalikuwa ni kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa mjadala huu wa Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na kwa kuzingatia hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Diana M. Chilolo Bungeni na kuungwa mkono na takribani Wabunge wote ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo basi, Kamati ya Uongozi imeona iko busara ya kuendelea kufanya majadiliano ya kuhusu hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa muda wa siku mbili. (*Makofi*)

Kwa hiyo, muda wa majadiliano umeongeza kutoka tarehe 23/7/2009 mpaka tarehe 24/7/2009. Kwa hiyo, hoja hiyo itahitimishwa tarehe 24/7/2009 yaani kesho siku ya Ijumaa kipindi cha jioni kwa maana ya kuanzia saa 11.00 jioni kwa kadri ya mwendeleo wa wachangiaji utakavyokuwa.

Mjadala sasa wa bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ambao ulikuwa ufanyike siku ya tarehe 24/7/2009, utaanza rasmi siku ya tarehe 25/7/2009 yaani Jumamosi na siku hiyo ya Jumamosi ratiba itakuwa kama ifuatavyo:-

Bunge litaanza saa tatu asubuhi, litaendelea na kikao kwa mjadala wa Wizara ya Nishati na Madini mpaka saa saba mchana. Siku hiyo ya Jumamosi kwa kuwa tunatazamia kupokea wageni, Wajumbe 50 wa Baraza la Wawakilishi kutoka Zanzibar, kwa hiyo itatupasa kurudi tena Bungeni saa tisa mchana na tutamaliza shughuli hizo saa kumi na moja jioni. Mjadala huo wa Wizara ya Nishati na Madini utaendelea tena siku ya Jumatatu tarehe 27/7/2009 kwa muda wa siku nzima.

Baada ya marekebisho hayo ya kiutendaji ya Bunge na kwa nia njema iliyoonyeshwa na Bunge na kuridhiwa na Kamati ya Uongozi iliyoketi leo tarehe 23/7/2009 basi Kamati hiyo inapenda tena kutoa taarifa kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Spika kuwa kutakuwa na ongezeko la muda wa kikao cha Bunge kwa muda wa siku moja kama ifuatavyo:-

Kutokana na mapendekezo ya kuongeza siku moja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge umesogezwa mbele kwa siku moja ili kukidhi ongezeko la mabadiliko ya Wizara na hivyo mkutano huo sasa utamalizika siku ya Jumamosi tarehe 1/8/2009 saa saba mchana badala ya siku ya Ijumaa tarehe 31/7/2009.

Waheshimiwa Wabunge, ratiba ya mabadiliko haya itagawiwa kwenu wote na naomba niwashukuru sana kwa nia njema ya utendaji kazi bora ndani ya Bunge mliyoonyesha leo na kupelekea hotuba ya leo kuweza kuchukua siku mbili.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo ambayo nilikuwa nayo hapa mezani, niendelee kuwashukuru sana kwa shughuli za leo na sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.44 Usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,
Tarehe 24 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)